# FIKIHI
# KWA MUJIBU WA
# MADHEHEBU TANO

الفقه على المذاهب الخمسة

**(HANAFI, MALIKI, HANBALI, SHAFII NA JA'FARI)**

**Sehemu Ya Kwanza**

**Kimetungwa Na:**
Muhammad Jawad Mughniyyah

**Kimetafsiriwa Na:**
Jopo La Wafasiri

ترجمة

# الفقه على المذاهب الخمسة

العبادات

تأليف

محمّد جواد مغنية

من اللغة العربية إلى اللغة السواحلية

**© Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
AL-ITRAH FOUNDATION

**ISBN:** 978 – 9987 – 17 – 012 – 8

**Kimetungwa Na:**
Muhammad Jawad Mughniyyah

**Kimetafsiriwa Na:**
Jopo La Wafasiri

**Kimehaririwa Na:**
Alhaji Hemedi Lubumba

**Kimesomwa Prufu Na:**
Ramadhani S. K. Shemahimbo

**Kimepitiwa na:**
Al Hajj Mujahid Rashid

**Toleo la Kwanza:** June, 2017
**Nakala:** 1000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania
**Simu:** +255 22 2127555
**Barua Pepe:** alitrah@yahoo.com
**Tovuti:** www.alitrah.info

مكتب شيخ الجامع الأزهر

بسم الله الرحمن الرحيم

نص الفتوى
التى أصدرها السيد صاحب الفضيلة الأستاذ الأكبر
الشيخ محمود شلتوت شيخ الجامع الأزهر
فى شأن جواز التعبد بمذهب الشيعة الامامية

---

قيل لفضيلته :

ان بعض الناس يرى أنه يجب على المسلم لكى تقع عباداته ومعاملاته على وجه صحيح أن يقلد أحد المذاهب الأربعة المعروفة وليس من بينها مذهب الشيعة الامامية ولا الشيعة الزيدية ، فهل توافقون فضيلتكم على هذا الرأى على اطلاقه فتمنعون تقليد مذهب الشيعة الامامية الاثناعشرية مثلا .

فأجاب فضيلته :

١ ـ ان الاسلام لا يوجب على أحد من أتباعه اتباع مذهب معين بل نقول : ان لكل مسلم الحق فى أن يقلد بادئ ذى بدء أى مذهب من المذاهب المنقولة نقلا صحيحا والمدونة أحكامها فى كتبها الخاصة ولمن قلد مذهبا من هذه المذاهب أن ينتقل الى غيره ـ أى مذهب كان ـ ولا حرج عليه فى شئ من ذلك .

٢ ـ ان مذهب الجعفرية المعروف بمذهب الشيعة الامامية الاثناعشرية مذهب يجوز التعبد به شرعا كسائر مذاهب أهل السنة .

فينبغى للمسلمين أن يعرفوا ذلك ، وأن يتخلصوا من العصبية بغير الحق لمذاهب معينة ، فما كان دين الله وما كانت شريعته بتابعة لمذهب ، أو مقصورة على مذهب ، فالكل مجتهدون مقبولون عند الله تعالى يجوز لمن ليس أهلا للنظر والاجتهاد تقليدهم والعمل بما يقررونه فى فقههم ، ولا فرق فى ذلك بين العبادات والمعاملات .

محمود شلتوت

... ... ...

السيد صاحب السماحة العلامة الجليل الاستاذ محمد تقى القمى
السكرتير العام
لجماعة التقريب بين المذاهب الاسلامية

سلام الله عليكم ورحمته أما بعد فيسرنى أن أبعث الى سماحتكم بصورة موقع عليها بامضائى من الفتوى التى أصدرتها فى شأن جواز التعبد بمذهب الشيعة الامامية ، راجيا أن تحفظوها فى سجلات دار التقريب بين المذاهب الاسلامية التى أسهمنا معكم فى تأسيسها ووفقنا الله لتحقيق رسالتها .

والسلام عليكم ورحمة الله

شيخ الجامع الأزهر
محمود شلتوت

# FATWA YA AL-AZHAR KUHUSU SHIA

Ifuatayo ni Fatwa (hukumu ya kidini) ya mmojawapo wa wanazuoni wa ulimwengu wa Sunni anayeheshimiwa sana, Sheikh Mahmud Shaltut, kuhusu Shia. Sheikh Shaltut alikuwa mkuu wa chuo mashuhuri cha kitheolojia cha al-Azhar nchini Misri, moja ya vituo vikuu vinavyotoa masomo ya taaluma ya dini ya madhehebu ya Sunni hapa duniani. Linapaswa kuwa ni jambo la kuvutia kujua kwamba miongo michache iliyopita, kundi la wanazuoni wa Sunni na Shia waliunda kituo hapo al-Ahzar kwa jina la *"Dar al-Taqreeb al-Madhahib al-Islamiyyah"* ambalo tafsiri yake ni "Kituo cha Kuyakurubisha Pamoja Madhehebu Mbalimbali ya Kiislamu"

Lengo la jitihada hizi, kama jina la kituo linavyoashiria, ilikuwa ni kuziba pengo miongoni mwa madhehebu mbalimbali, na kusababisha kuheshimiana kwa pamoja, kuelewa na kutambua michango ya kila madhehebu kwa maendeleo ya maarifa ya sheria za Kiislamu, miongoni mwa wanazuoni wa madhehebu mbalimbali, ili kwamba na wao kwa upande wao wawaongoze wafuasi wao kwa mintarafu ya lengo kuu la umoja, na kushikamana na kamba moja, kama aya ijulikanayo sana ya Qur`ani Tukufu isemayo; "Shikamaneni kwenye Kamba ya Mwenyezi Mungu na msifarikiane," kwa uwazi inavyowataka Waislamu wawe.

Juhudi hii nzito sana hatimaye ilizaa tunda lake kuu wakati Sheikh Shaltut alipotoa tamko rasmi ambalo tafsiri yake imeambatanishwa hapo chini. Pia inapaswa kuwekwa wazi dhahiri kabisa, kwamba msimamo rasmi wa al-Ahzar, kuhusiana na utaratibu wa kufuata madhehebu yoyote, pamoja na madhehebu ya Shia (Shia Imamiyah), haujabadilika tangu Sheikh Shaltut alipotangaza.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 1 2/1/2017 3:51:38 PM

Baadhi ya watu ambao huwafuata wanazuoni bandia nchini Hijaz wangependa kutofautiana; hata hivyo, unachokiona hapo chini ndio mtazamo unaoshikiliwa na wanazuoni wengi sana wa madhehebu ya Sunni, na sio wale tu walioko al-Azhar. Naijulikane kwa wale wanaojitahidi kututenganisha sisi, kwamba juhudi zao sio lolote ila ni bure tu.

Kwa rejelea ya usomaji fungu la maneno "Shia Imamiyyah Ithnaashariyyah" maana yake ni ile Madhehebu ya Maimamu Kumi na Wawili ambayo ina idadi kubwa sana ya wafuasi leo hii. Fungu la maneno "Shia Ithnaashariyyah" hutumika bila ubadilikaji pamoja na "Shia Ja`fariyyah" na "Shia Imamiyyah" katika vitabu mbalimbali. Hayo ni majina tofauti tu kwa madhehebu hiyo hiyo.

"Shia Zaidiyyah" hawa ni wachache miongoni mwa wafuasi wa madhehebu ya Shia, ambao wengi wao wapo nchini Yemen katika sehemu ya Mashariki ya Rasi ya Arabuni. Kwa maelezo ya kina zaidi kuhusu tofauti iliyopo baina ya hawa Zaidiyyah na "Shia Ithnaashariyyah," tafadhali rejea kwenye kitabu kiitwacho "Shi`ite Islam" ambacho kimeandikwa na mwanazuoni mashuhuri wa madhehebu ya Shia, Allamah Tabatabai, na kutarjumiwa na Sayyed Hussen Nasr, na kuchapishwa na chuo kikuu cha *State University of New York Press* (SUNY).

Na kuhusu tamko la Sheikh Shaltut linasomeka kama ifuatavyo:



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 2 2/1/2017 3:51:38 PM

# MAKAO MAKUU YA CHUO KIKUU CHA AL-AZHAR:

Kwa jina la Mwenyezi Mungu,
Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

Maandishi ya Fatwa Iliyotolewa na Mstahiki Sheikh al-Akbar Mahmud Shaltut, Mkuu wa Chuo Kikuu cha al-Azhar, juu ya Ruksa ya Kufuata Madhehebu ya "Shia Imamiyyah."

Mstahiki Sheikh aliulizwa:

Baadhi ya watu huamini kwamba, kwa Mwislamu kuwa na ibada na ushiriki wa kidini sahihi, ni muhimu kufuata mojawapo ya madhehebu manne ambayo ni mashuhuri sana, ambapo, madhehebu ya "Shia Imamiyyah" sio miongoni mwa madhehebu hayo wala "Shia Zaidiyyah." Hivi wewe Mstahiki Sheikh unakubaliana na fikira hiyo, na kwa mfano hata kuweza kuharamisha kufuata madhehebu ya "Shia Imamiyyah Ithnaashariyyah"?

Mstahiki Sheikh akajibu:

**1.** Uislamu haumshurutishi Mwislamu katika kumtaka afuate madhehebu fulani mahsusi. Kwa usahihi zaidi tunasema: kila Mwislamu anayo haki ya kufuata mojawapo ya madhehebu ambayo yameelezewa kwa usahihi na hukumu zake zimekusanywa kwenye vitabu vyake. Na, kila mtu anayefuata mojawapo ya Madhehebu hayo, anaweza kuhamia kwenye madhehebu mengine, na hakutakuwa na kosa kwake kwa kufanya hivyo.

**2.** Madhehebu ya Ja`fari, ambayo pia yanajulikana kama "Shia Imamiyyah Ithnaashariyyah" (yaani Shia wanaofuata Maimam



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 3 2/1/2017 3:51:38 PM

Kumi na Wawili) pia ni madhehebu ambayo ni sahihi kidini kufuatwa katika ibada kama ilivyo kwa madhehebu mengine ya Sunni.

Waislamu lazima wajue hili, na wanapaswa kujiepusha kuwa na chuki isiyo na haki dhidi ya madhehebu mengine yoyote, kwani dini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na Sheria Yake kamwe haikuwekewa mpaka kwa madhehebu yoyote mahsusi. Wanasheria wao (Mujtahiduun) wanakubaliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu, na inaruhusiwa kwa "wasiokuwa Mujtahid kuwafuata wao na kukubaliana na mafundisho yao iwe katika ibada au shughuli (mu'amalaat) zingine.

**Imesainiwa na:**
**Mahmud Shaltut**

Fatwa hiyo hapo juu ilitangazwa mnamo tarehe 6, Julai,1959 kutoka kwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha al-Azhar nchini Misri na baadaye ilichapishwa katika machapisho mengi katika Mashariki ya Kati ambayo ni pamoja na:

**1.** Gazeti la al-Sha`ab (la Misri) toleo la tarehe 7, Julai, 1959.

**2.** Gazeti la al-Kifan la Lebanon, toleo la tarehe 8, Julai,1959.

Sehemu hiyo hapo juu pia inaweza kupatikana katika kitabu kiitwacho "*Inquiries about Islam*," mwandishi wake ni Jawad Chirri, Mkurugenzi wa Islamic Centre of America, 1986 Detroit, Michigan.

Mpendwa Mwislamu:

*Assalam Alaykum Wa Rahmatullah Wa Barakatuhu,*

Hii ni fatwa ambayo Imam mashuhuri, marhum Imam Shaltut, aliyekuwa mkuu wa Chuo Kikuu cha al-Ahzar nchini Misri, aliitoa



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 4 2/1/2017 3:51:38 PM

kuhusu Madhehebu ya Shia. Fatwa hii inafuatiwa na barua ya Imam Shaltut aliyomwandikia mwanazuoni wa Madhehebu ya Shia.

## MAKAO MAKUU YA CHUO KIKUU CHA AL-AZHAR:

Kwa jina la Mwenyezi Mungu,
Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

**Maandishi ya Fatwa Iliyotolewa na Mstahiki Sheikh al-Akbar Mahmud Shaltut, Mkuu wa Chuo Kikuu cha al-Azhar, juu ya Ruhusa ya Kufuata Madhehebu ya "Shia Imamiyyah."**

Mstahiki Sheikh aliulizwa:

Baadhi ya watu huamini kwamba, kwa Mwislamu kuwa na ibada na ushiriki wa kidini sahihi, ni muhimu kufuata mojawapo ya madhehebu manne ambayo ni mashuhuri sana, ambapo, madhehebu ya "Shia Imamiyyah" sio miongoni mwa madhehebu hayo wala "Shia Zaidiyyah." Hivi wewe Mstahiki Sheikh unakubaliana na fikira hiyo, na kwa mfano hata kuweza kuharamisha kufuata madhehebu ya "Shia Imamiyyah Ithnaashariyyah"?

Mstahiki Sheikh akajibu:

**1.** Uislamu haumshurutishi Mwislamu katika kumtaka afuate madhehebu fulani mahsusi. Kwa usahihi zaidi tunasema: kila Mwislamu anayo haki ya kufuata mojawapo ya madhehebu ambayo yameelezewa kwa usahihi na hukumu zake zimekusanywa kwenye vitabu vyake. Na, kila mtu anayefuata mojawapo ya Madhehebu hayo, anaweza kuhamia kwenye madhehebu mengine, na hakutakuwa na kosa kwake kwa kufanya hivyo.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 5 2/1/2017 3:51:38 PM

**2.** Madhehebu ya Ja`fari, ambayo pia yanajulikana kama "Shia Imamiyyah Ithnaashariyyah" (yaani Shia wanaofuata Maimam Kumi na Wawili) pia ni madhehebu ambayo ni sahihi kidini kufuatwa katika ibada kama ilivyo kwa madhehebu mengine ya Sunni.

Waislamu lazima wajue hili, na wanapaswa kujiepusha kuwa na chuki isiyo na haki dhidi ya madhehebu mengine yoyote, kwani dini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na Sheria Yake kamwe haikuwekewa mpaka kwa madhehebu yoyote mahsusi. Wanasheria wao (Mujtahiduun) wanakubaliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu, na inaruhusiwa kwa "wasiokuwa Mujtahid kuwafuata wao na kukubaliana na mafundisho yao iwe katika ibada au shughuli (mu'amalaat) zingine.

**Imesainiwa na:**
**Mahmud Shaltut**



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 6 2/1/2017 3:51:38 PM

Mheshimiwa Allamah Mohammad Taqi al-Qumi:

Katibu Mkuu wa Kamati ya Mapatano ya
Kuyakurubisha Pamoja Madhehebu ya Kiislamu,
(*Jama`at at-Taqrib bain al-Mathahib al-Islamiyah*),

Salamullah Wa Rahmatuh,

Kisha ni fuaraha yangu kukutumia ewe mstahiki nakala ya fatwa hii, yenye saini yangu, ambayo niliitoa kuhusu uruhusiwaji wa kufuata madhehebu ya Shia Imamiyyah, nikiwa na matumaini kwamba utaiweka katika kumbukumbu ya *Jama`at at-Taqrib*, ambayo tulishiriki pamoja nawe katika kuiasisi, na Mwenyezi Mungu Mtukufu atujaalie mafanikio katika ufanikishaji wa misheni yake.

Wassalam Alaykum Wa Rahmatullah,

Imesainiwa na:

Sheikh al-Jaamea al-Azhar,
ahmud Shalut.

**نص فتوى الشيخ شلتوت في التعبد بمذهب الشيعة الإمامية**

أصدرها صاحب الفضيلة الإمام الأكبر الشيخ محمود شلتوت شيخ الجامع الأزهر, فى شأن

جواز التعبد بمذهب الشيعة الإمامية.

قيل لفضيلته:



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 7 2/1/2017 3:51:38 PM

إن بعض الناس يرى أنه يجب على المسلم لكى تقع عباداته ومعاملاته على وجه صحيح أن يقلد أحد المذاهب الأربعة المعروفة وليس من بينها مذهب الشيعة الإمامية ولا الشيعة الزيدية, فهل توافقون فضيلتكم على هذا المبدأ على إطلاقه فتمنعون تقليد مذهب الشيعة الإمامية الاثنا عشرية مثلا:

فأجاب فضيلته:

1. إن الإسلام لا يوجب على أحد من أتباعه إتباع مذهب معين بل نقول إن لكل مسلم الحق فى أن يقلد بادئ ذى بدء أى مذهب من المذاهب المنقولة نقلاً صحيحًا والمدونة أحكامها فى كتبها الخاصة ولمن قلّد مذهبًا من هذه المذاهب أن ينتقل إلى غيره. أى مذهب كان. ولا حرج عليه فى شئ من ذلك.

2. أن مذهب الجعفرية المعروف بمذهب الشيعة الإمامية الاثنا عشرية مذهب يجوز التعبد به شرعًا كسائر مذاهب أهل السنة. فينبغى للمسلمين أن يعرفوا ذلك, وأن يتخلصوا من العصبية بغير الحق لمذاهب معينة, فما كان دين الله وما كانت شريعته بتابعة لمذهب أو مقصورة على مذهب, فالكل مجتهدون مقبولون عند الله تعالى يجوز لمن ليس أهلاً للنظر والاجتهاد تقليدهم والعمل بما يقررونه فى فقههم, ولا فرق فى ذلك بين العبادات والمعاملات.

السيد صاحب السماحة العلامة الجليل الأستاذ محمد تقى القمى:

السكرتير العام لجماعة التقريب بين المذاهب الإسلامية:

سلام عليكم ورحمته, أما بعد فيسرنى أن أبعث إلى سماحتكم بصورة موقع عليها بإمضائى من الفتوى التى أصدرتها فى شأن جواز التعبد بمذهب الشيعة الإمامية راجيًا أن تحفظوها فى سجلات دار التقريب بين المذاهب الإسلامية التى أسهمنا معكم فى تأسيسها ووفقنا الله لتحقيق رسالتها.

والسلام عليكم ورحمة الله.

شيخ الجامع الأزهر

السابع عشر من شهر ربيع الأول 1378هـ

# YALIYOMO

Dibaji........................................................................................
Neno la Mchapishaji .................................................................... 14
Kidokezo ...................................................................................... 15
Utangulizi..................................................................................... 19
Sehemu ya Kwanza:...................................................................... 29
Mambo ya Kiibada........................................................................ 29
**Tohara** ........................................................................................ 29
Maji Halisi .................................................................................... 31
Maji Yaliyotumika......................................................................... 34
Maji yasiyokuwa halisi (*mudhaf*): ............................................... 34
Kulateni......................................................................................... 35
Maji yanayotembea na yaliyotuwama .......................................... 38
Kutoharisha maji yaliyonajisika ................................................... 42
Aina za najisi................................................................................. 44
Hukmu za kwenda haja.................................................................. 49
Vyenye kutwaharisha .................................................................... 50
Yanayowajibisha kutawadha na yanayotengua wudhu................. 53
Lengo la wudhu............................................................................. 57
Mambo yaliyo wajibu katika wudhu............................................. 59
Masharti ya wudhu......................................................................... 64
Kuoga ............................................................................................ 67
Hedhi............................................................................................. 73
Istihadha........................................................................................ 77



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 10 2/1/2017 3:51:39 PM

Damu ya kuzaa (nifasi) .................................................................. 79
Kugusa maiti .............................................................................. 80
Maiti na hukmu zake ...................................................................... 82
*Hanut* - kuipaka maiti karafuumaiti ............................................... 87
Sanda ........................................................................................ 88
Mawalii wa maiti ......................................................................... 91
Kuzika ....................................................................................... 98
Kutayammamu ............................................................................. 101
Hukmu za kutayammamu ............................................................... 109
Kauli za madhehebu katika aya ya kutayammamu ............................ 112
**Swala ...................................................................................... 114**
Kibla ......................................................................................... 121
Viungo ambavyo ni wajibu kuvisitiri, na sehemu ya mwili ambayo ni haramu kuitizama ........................................... 124
Sehemu ya mwili ambayo ni wajibu mtu kuisitiri pindi awapo katika swala ........................................................ 133
Mahali pa kuswalia ....................................................................... 139
Adhana ...................................................................................... 143
Faradhi za swala na nguzo zake ..................................................... 148
Kusahau na kutia shaka katika swala .............................................. 162
Swala ya ijumaa ........................................................................... 168
Swala ya iddi mbili ....................................................................... 172
Swala ya kupatwa kwa mwezi na jua ............................................... 177
Swala ya kuomba mvua ................................................................. 177
Swala ya kulipa ............................................................................ 179
Swala ya jamaa ............................................................................ 182



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 11 2/1/2017 3:51:39 PM

Swala ya msafiri .......... 191
Kukusanya swala mbili .......... 196
Asiyejua hukmu za kukusuru swala, na hukmu ya aliyesahau ... 196
Mambo yanayobatilisha swala .......... 197
**Swaumu .......... 204**
Masharti ya swaumu .......... 209
Vyenye kutengua swaumu .......... 210
Vigawanyo vya swaumu .......... 214
Kuthibiti mwandamo wa mwezi .......... 220
Kuandama kwa mwezi kupitia wanajimu .......... 224
**Zaka .......... 226**
Mali ambazo ni wajibu kuzitolea zaka .......... 230
Zaka ya dhahabu na fedha .......... 235
Zaka ya mali ya biashara .......... 237
Watu wanaostahiki kupewa zaka .......... 239
Zaka ya fitri .......... 246
**Khumsi (fungu la tano) .......... 250**
**Hijja .......... 254**
Tanzuo za kuwa na uwezo .......... 259
Kuweka naibu .......... 262
Umra .......... 267
Aina za hijja .......... 272
Vituo vya kuhirimia (miqat) .......... 275
Kuhirimia .......... 279
Yaliyo haramu kwa aliye ndani ya ihramu .......... 287
Kutufu .......... 300



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 12 2/1/2017 3:51:39 PM

Namna ya kutufu ........ 306
Kusai na kupunguza nywele ........ 314
Kupunguza nywele ........ 319
Kusimama Arafah ........ 323
Kusimama Muzdalifa ........ 329
Mina ........ 334
Jamaratul-Aqabah ........ 335
Wanyama wa kuchinjwa ........ 339
Kati ya makka na mina ........ 352
Sura ya hija ........ 358
Mwezi mwandamo wa dhulhija ........ 362
Historia ya kujengwa haram mbili takatifu ........ 366
**Kumzuru Mtukufu Mtume ﷺ** ........ 366
**Msikiti wa Mtume ﷺ: ........ 369**



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 13 2/1/2017 3:51:39 PM

# DIBAJI

Kitabu hiki ni toleo la Kiswahili la taasisi ya Al Itrah Foundation. Chapisho lake limelenga kukidhi mahitaji ya kiroho ya zama hizi pamoja na Ubongo na fikra zinazokuwa za Muislam. Jitihada kubwa zimefanywa na Taasisi kuweka chapisho hili la Kiswahili katika msingi wa haki na wenye kukubalika katika Uislam.

Unaombwa kwa Taadhima ukisome kitabu hiki katika malengo yaliyokusudiwa. Pia Unaombwa kuwasilisha kwetu maoni yako huru juu ya chapisho letu hili, jambo ambalo tutashukuru sana.

Kutangaza ujumbe wa Uislam ni kazi ambayo inahitaji ushirikiano wetu sote. Taasisi inakuomba kuungana na kushirikiana kama ilivyoagizwa katika aya ya Qur'an: (Surat Saba' 34:46).

Na rehma za Allah ziwe juu yako.

Wako katika Uislam

Al Itrah Foundation

Barua Pepe: alitrah@yahoo.com

SMS: +255 778 300 140



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 14 2/1/2017 3:51:39 PM

# NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako kimetarjumiwa kutoka kitabu cha Kiarabu kwa jina la*,* al-*Fiqh 'ala al- Madhahib al-Khamsah* kilichoandikwa na Sheikh Muhammad Jawad Mughniyyah. Sisi tumekiita, *Fikihi kwa Mujibu wa Madhehebu Tano – Hanafi, Maliki, Shafii, Hanbali na Ja'fari.*

Kitabu hiki huelezea masuala ya kisheria katika matendo ya ibada kama vile swala, saumu, zaka, hija, tohara, mirathi, ndoa, talaka, n.k. kwa mujibu wa madhehebu hizo nne za Kisunni na moja ya Kishia. Alichofanya Sheikh Mughniyyah ni kuelezea tu taratibu za kila madhehebu katika suala husika. Kwa mfano, kutawadha huelezwa jinsi wanavyofanya Hanafi, Maliki, Shafii, Hanbali na Shia Ithnaasharia (Ja'fari); kisha hutoa rejea katika vitabu vyao vya kifikihi basi. Hiki ni kitabu kizuri sana kwa Waislamu wa madhehebu zote kuwa nacho.

Jambo ambalo litamvutia na kumpa mazingatio kila mtafiti ni kuona kwamba licha ya kuwepo hitilafu za kifikihi kati ya madhehebu nne za Kisunni kwa upande mmoja, na madhehebu ya Kishia Ithnaasharia na madhehebu nne za Kisunni wa upande wa pili, lakini karibu katika kila suala la kifikihi katika Shia (Ja'fari), kuna madhehebu mojawapo kati ya hizo nne za Kisunni ambayo inakubaliana na suala *(hukm)* fulani la Kishia na kutofautiana na madhehebu tatu nyinginezo. Hili linamaanisha kwamba Sunni wa madhehebu yoyote anaweza kufuata karibu masuala yote ya kifikihi ya Shia Ithnaasharia bila ya kuwa na wasiwasi wowote, na ndiyo maana aliyekuwa Mufti Mkuu wa al-Azhar, Marehemu Sheikh Mahmoud Shaltut, alitoa fatwa kuruhusu Sunni kufuata fikihi ya madhehebu ya Ja'fari.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 15 2/1/2017 3:51:39 PM

Hiki ni kitabu kikubwa cha rejea ambacho ni kizuri sana kwa wale wanaofaya utafiti wa kisomi. Sisi tumekiona kuwa ni chenye manufaa sana hususan wakati huu ambao kuna propanganda nyingi za ndani na nje za kuwapotosha Waislamu ili wasifikie lengo lao la takwa ambalo ndio lengo kubwa la waumini na kuzitumia tofauti hizi ndogo ndogo kuwagawanya.

Kutokana na ukweli huu, Taasisi yetu ya al-Itrah imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa madhumini yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Hii ni katika kazi kubwa zilizofanywa na Taasisi ya al-Itrah. Tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine kuanzia kwa watarjuma na wengine hadi kufikia kuchapishwa kwa kitabu hiki. Allah Mwenye kujazi awalipe kila la kheri hapa duniani na huko Akhera pia.

**Mchapishaji**
**Al-Itrah Foundation**



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 16 2/1/2017 3:51:39 PM

# KIDOKEZO

Fikihi (Sharia) ya Kiislamu inagawanyika katika vigawo kadhaa. Miongoni mwa hivyo ni: Ibada, mkiwa na jumuisho la Tohara, Swala, Swaumu, Zaka, Khums na Hijja.

Juzuu ya kwanza ya kitabu hiki **'Fikihi kwa Mujibu wa Madhehebu tano'** imekusanya milango hiyo sita, juzuu hii kwa mara ya kwanza kabisa ilichapishwa na kusambazwa na shirika linalojulikana kwa jina la *Darul-Ilmi Lil Malayin* na hatimaye nakala zake zilikwisha haraka bila kutarajiwa, kwa hivyo walirudia kukichapisha kwa mara ya pili na ya tatu na ya nne, na matoleo yote hayo pia nayo yalikwishia njiani bila ya kutosheleza kama vile vile ilivyokuwa kwa chapa ile ya kwanza.

Pia miongoni mwa vigawo vya Fikihi ya Kiislamu ni mambo yanayohusiana na hali binafsi za mtu ikiwa ni jumla ya mambo yanayohusiana na Ndoa, Talaka, Wasia, Mirathi, Wakfu na Zuwio dhidi ya kutumia mali. Kwa hivyo Juzuu ya pili ya kitabu hiki inakusanya milango hii sita, nayo pia ilichapishwa na kusambazwa na *Darul-Ilmi Lil Malayin* na mara hii nakala zake zilikwisha zote kikamilifu, na bado hadi leo hii kitabu hiki kwa Juzuu zake zote mbili, kimeendelea kuhitajika na kutafutwa kama kilivyokuwa pale kilipochapishwa kwa mara ya kwanza.

Na kutokana na mahitaji au maoni ya watu walio na kiu na kitabu hiki, baadhi ya mabwana wakubwa watukufu waliiomba idara inayohusika ikichapishe tena kitabu hiki, lakini mara hii juzuu zake zichanganywe pamoja ili ziwe kama kitabu kimoja ingawa zitabaki kwenye mfumo wake uleule wa kwanza, yaani juzuu ya kwanza ielezee tu mambo ya ibada, na juzuu ya pili nayo kama ilivyokuwa



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 17 2/1/2017 3:51:39 PM

mara ya kwanza, ielezee hali binafsi za mtu. Wachapishaji waliitikia ombi hilo kwa kuwa maudhui ya hizo juzuu zote mbili ni moja, na mtungaji wake ni mmoja, asaa mkusanyo huu ukamrahisisishia kitu msomaji. Na Mwenyezi Mungu (s.w.t.) ndiye mwenye taufiki.

**Mtungaji**



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 18 2/1/2017 3:51:39 PM

# UTANGULIZI

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu,
Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.

**Na rehma na amani zimshukie bwana wetu Muhammad, na Aali zake na Swahaba zake watukufu.**

Imepokewa katika Hadith tukufu kwamba: "Kwa hakika Jibril alishuka kwa Adam, akamwambia: "Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amekupa hiyari uchague kimoja kati ya vitu vitatu hivi: Akili, dini na haya". Adam akasema: "Nachagua akili, kwani ndani ya akili mna haya na dini." Malaika wakasema: "Basi na sisi tuko pamoja na wewe ewe Adam, kwa hakika Mwenyezi Mungu ametuamuru daima tuwe pamoja na akili popote iwapo."

Kutokana na Hadithi hii, tunapata mambo yafuatayo:

**1.** Kwamba kila jambo linalokataliwa na akili, basi si chochote katika dini, na twajifunza kwa Hadith hiyo kwamba kila asiyekuwa na akili basi huwa hana dini wala haya, hata kama anasimama usiku kucha kwa ibada na kufunga mchana kucha, ni kutokana na maelezo ya Hadith hii mwanachuoni mmoja anasema: "Hakika kipimo cha sawa na kilicho cha salama kabisa ambacho twaweza kupambanulia Hadithi ya Mtume na isiyokuwa ya Mtume, ni iwe na ukweli halisi na iwe inatoa nuru inayong'aa. Ama isiyo na ukweli halisi au wa nuru, basi hayo huwa ni maneno ya shetani.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 19 2/1/2017 3:51:39 PM

**2.** Maadamu daima dini haitengani na akili kwa hali yoyote ile iwayo, basi kuufunga mlango wa Ijtihad itakuwa ni sawa au ndiko hasa kuufunga mlango wa dini kwa sababu 'Ijtihad' maana yake ni kuipa akili uhuru wake, na ni kuipa nafasi ya kung'amua matawi ya dini kutokana na misingi yake. Kwa hivyo tunapoinyima akili nafasi ya kufanya kazi yake tutakuwa tumezuia dini. Pia ni kuinyima uhuru dini kwa hukmu hiyo ya kuwapo ulazima wa vitu hivyo viwili kushirikiana pamoja, na kwa neno jingine tunaposema mlango wa Ijtihadi umefungwa basi ni lazima tulazimike kukubali mojawapo ya mambo mawili, hapana la tatu, wala hakuna nafasi ya kukwepa kuangukia katika mojawapo, ima tukubali kuufunga mlango wa dini sawa na tulivyoufunga mlango wa Ijtihadi, au tuseme kuwa akili haikubaliani na hukmu za dini. Na hayo yote mawili yako mbali kabisa na mantiki ya kisharia na hali yenyewe ilivyo.

Ni kuwa 'Msomi' yeyote yule ambaye huwa na chuki binafsi dhidi ya madhehebu yoyote yale yawayo, huwa yuko kwenye hali iliyo mbaya zaidi kuliko hali na ubaya alionao mtu ambaye hakujaliwa kupata elimu, kwa sababu mwanachuoni huyo huwa si mwenye chuki na dini na Uislamu, bali huwa ni mwenye chuki binafsi na mtu binafsi ambaye ndiye mfuasi wa madhehebu husika maadamu akili yake haikuamua kumfuata katika madhehebu yake. Kama ambavyo kuyakhalifu madhehebu fulani, haina maana ya kuukhalifu Uislamu na uhakika wake, bali ni kumkhalifu mwenye madhehebu peke yake, na kwa usahihi kabisa ni kuikhalifu sura ya dhihinia aliyoijenga kuhusu Uislamu. Na kwa vyovyote vile iwavyo, kila mmoja wetu anafahamu fika kwamba katika muhula wa mwanzo wa Uislamu hukukuwa na makundi ya dini wala madhehebu, pindi Uislamu ulipokuwa mweupe na msafi kabisa uliotakasika na kila

doa litialo kasoro, na Waislamu walikuwa juu zaidi kuliko umma wowote mwingine, na vilevile kila mmoja wetu anajua kwa yakini kabisa kwamba madhehebu haya na vikundi vilivyozuka (baada ya Mtukufu Mtume ﷺ kuuaga ulimwengu huu) yamekuwa sababu kubwa iliyowatenganisha Waislamu na kuwaweka mbali mbali na ndiyo sababu pia iliyoweka vizuizi kati yao vilivyowazuia kuwasiliana au kutangamana na kushauriana pamoja ili kuondoleana matatizo yanayoukabili upande wa kila mmoja wao, na wakoloni na maadui wa Uislamu waliitumia fursa hii ya kutengana kwao, kuwakandamiza na kueneza fitina na uchonganishi kati yao. Na wala kamwe wasingeliweza kuingia Mashariki kutoka huko kwao Magharibi, lau wasingeliitumia njia hiyo ya kuwatenganisha na kuwavunja nguvu na uwezo wao kwa kuisambaza chuki ya kimadhehebu kati yao.

Na kwa ajili ya mambo kama haya na mengineyo, ndipo ilipozuka katika akili za viongozi wa kidini wenye nia njema fikra ya kuwaunganisha na kuyakusanya pamoja makundi yote ya Waislamu na kuwafanya wawe na neno moja. Walijishughulisha na dhamira hiyo kwa kila njia, na miongoni mwa njia hizo ni kufunguliwa mlango wa kufanya Ijtihadi, na kutokomeza kabisa ubeberu wa kuwalazimisha Waislamu kufuata madhehebu maalumu.

Na jambo lililo maarufu sana kati ya mafakihi wengi ni kuwa sababu kubwa ya kufungwa kwa mlango wa Ijthadi ni kwamba, eti unapofunguliwa na kuachwa wazi kutazuka fujo na vurugu na aidha vijana wadogo watajikweza na kujiona kuwa ni miongoni mwa wasomi, ambapo watajitwika mambo wasiyoyaweza. Mwishowe ni kuzuka uharibifu na dini kumalizika kabisa. Na hapo wana maana ya kuwa wale wanaodai mlango wa Ijtihad uwe wazi eti wanatibu magonjwa kwa kumuangamiza anayeugua, si kwa kuangamiza ugonjwa.

Haya ndiyo waliyoyaeleza waandishi wa zamani kwenye vitabu vyao, na wakajibiwa na waliofatia bila kufanya uchunguzi na utafiti. Ama mimi nasimama kando peke yangu bila ya kufuata mawazo na fikra za mtu yeyote kati ya hao waliotangulia na waliofuata nyayo zao. Bali naona sababu pekee ya kufungwa kwa mlango wa Ijtihadi ni viongozi wa serikali dhalimu walipohofia kwamba uhuru wa kifikra na mawazo utahatarisha nafasi zao na viti vyao hivyo waliona njia ya pekee ya kuuhami utawala wao ni kuwakata ndimi wasomi wa ngazi zote wasiweze kusema, huku wakisingizia eti wanaihami dini, kama ambavyo imekuwa ni ada yao kumnyang'anya na kumkandamiza kila mtu huru asiyetaka kushirikiana na dola yake katika ufuska na uovu.

Na kitendo cha kutolewa wito wa kufunguliwa mlango wa Ijtihadi baada ya kudhoofika utawala wa kigeni ni dalili iliyo wazi zaidi juu ya ukweli huu, na bado utekelezwaji wake mpaka sasa unategemea uwepo wa uhuru kamili kwa maana yake yote.

Na baada ya yote, ni kwamba kila aina ya kudhalilika mbele za viongozi wenye tamaa ni kujitia kwenye unyonge na utumwa, na mawili hayo tumeishi nayo kwa muda mrefu, na kwamba hivi sasa hapana budi tuishi tukiwa watu huru kwenye fikra zetu, kama vile tunavyoishi tukiwa watu huru kwenye miji yetu, na tuache kabisa mawazo ya kujilazimisha (kinyonge na kitumwa) kufuata madhehebu maalumu au kauli maalumu bali tuwe na moyo wa kujichagulia Ijtihadi za madhehebu yote ambayo yanakubaliana na kuendelea mbele kwa uhai na maisha ya mwanadamu na wepesi wa sharia, na hata kama kule kujiamulia kufuata aina ya madhehebu unayotaka sio kufanya Ijtihadi, lakini ni Tanzuo mmojawapo ya kufanya Ijtihadi.

Kwa msingi huu, msingi wa kujiandaa kuelekea kwenye kituo cha kujiamulia au kujichagulia madhehebu yoyote mtu anayotaka kufuata, ndipo nikaazimia kutunga kitabu hiki, ndani yake nikiwa nimekusanya kwa mukhtasari kauli za madhehebu tano:



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 22 2/1/2017 3:51:40 PM

1. Ja'fari (Shia Itha Asharia)
2. Hanafi
3. Maliki
4. Shafi
5. Hanbali

Yote niliyoyakusanya humu nimeyatoa kutoka kwenye vitabu vyao halisi vinayotegemewa. Kama ambavyo katika kauli za madhehebu ziko zinazolingana na maisha ya kila siku ya wanadamu zinazohakikisha usawa na uadilifu, vilevile mna maneno au kauli zinazolazimu kuzisitiri na kuzipuuza kabisa au kuzitoa maanani, na kwa ajili hiyo na mimi nimezipuuza kauli kama hizo sikuziandika humu, nikiwa na uhakika wa kuwalindia heshima yao mafakihi waliosema maneno hayo na vile vile kuipa Fikihi hadhi na heshima yake.

Na nimeyaandika hayo niliyoyaandika huku nikijaribu kwa kadiri nilivyoweza kufanya yawe rahisi na yenye kueleweka kwa mwanafunzi, na nimejaribu kiasi cha uwezo wangu kufupisha maelezo yangu na nimetumia njia inayofahamika wazi wazi na kwa urahisi. Na kwa kweli njia hii ni kazi ngumu anayokutana nayo kila mwandishi anayenukuu maneno na matamshi ya lugha ya kigeni na kuyaingiza kwenye lugha yake ya asili, kwani mtindo wa utunzi wa zamani na wa sasa ni kama tofauti iliyoko kati ya lugha ya Kiarabu na lugha nyinginezo za kigeni.

Nilipokuwa nikipitapita kwenye maktaba kama ilivyo ada yangu ya kila siku, ilikuwa nikipekua pekua nione vitabu vipya vilivyotolewa na wapiga chapa, na hatimaye humo nilimuona mwanafunzi mmoja ambaye alikuwa ni miongoni mwa wanafunzi wa Kitunisia anayesoma katika Chuo Kikuu cha Lebanon, naye

pia alikuwa akichunguza chunguza na kupekua vitabu. Mara tu alipoona mkononi mwangu nimeshika kitabu *Aliyyun wal Qur'ani* (Ali na Qur'ani) aliniomba akiangalie, na mara aliposoma tangazo la kutolewa kwa kitabu hiki **'Fikihi kwa Mujibu wa Madhehebu tano'** lililokuwa limeandikwa juu ya jalada alifurahi na kutabasamu, akasema: "Sisi tuna haja kubwa sana ya kupata mfano wa kitabu kama hiki." Nikamwambia: "Kwa sababu gani?" Akasema: "Sisi huko kwetu upande wa miji iliyoko upande wa Magharibi tunamfuata Imam Maliki, na ukweli ni kuwa yeye hutia mkazo mkubwa sana katika mas'ala ambayo maimamu wengine huwa wameyalegeza, na sisi ni vijana bado, lakini vyovyote yawavyo maarifa yetu na mielekeo yetu, na vyovyote tuwavyo na dhana (mbaya) na kujazwa tuhuma mbaya, bado hatuko tayari kuuepuka Uislamu, au kutoka nje ya amri zake, lakini wakati huo huo pia hatupendi na wala hatuko tayari kuingia kwenye dhiki, taabu, kuelemewa na kupata uzito katika kuzifuata hukmu zake na kulazimika kudumu kwetu juu ya hukmu hizo, kwa sababu hiyo tunapenda kwamba tunapopatwa na tatizo ambalo utatuzi wake kutoka upande wa Imam Maliki una uzito basi tujuwe pia rai ya Imam mwingine ni ipi kuhusu hukmu hiyo; huenda tukapata ufumbuzi, na hatimaye tutende huku tukiwa na imani kubwa ya kuwa hatujafanya jambo lililoharamishwa. Lakini tu tatizo kubwa kwetu ni kwamba hatuna njia yoyote inayoweza kutuwezesha kujua rai za madhehebu mengine kwa sababu mashekhe wetu hawaelewi au wanajifanya kutoelewa jambo au rai inayomkhalifu Imam Maliki. Na tunaporejea kwenye vitabu vya zamani vilivyotangulia hukutana na vizuizi vilivyoko kati yetu na kufahamu khitilafu iliyopo, hiyo ni kwa sababu ya ugumu wa ibara na kurefushwa mas'ala, hata ikawa hatuwezi kuongokewa na kujua chochote, na bila shaka katika kitabu chako tutapata kila kinachohitajika na kijana ikiwa ni pamoja na wepesi wa maelezo."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 24 2/1/2017 3:51:40 PM

Kwa hakika maneno ya kijana huyu yalinipa moyo sana na yalinishajiisha kuendelea mbele katika kuzitoa Juzuu zilizobaki, na pia alinifanya nisiwe mwenye masikitiko wala majuto juu ya kwenda kinyume na azma yangu ya kwanza (pale nilipoanza kukitunga kitabu hiki), maana hapo mwanzo nilitaka nitaje kwa kila kauli miongoni mwa kauli za madhehebu dalili yake iliyoitegemea katika mas'ala, iwapo ni Aya, au ni riwaya au ni Ijmai, au ni akili au ni kauli ya Swahaba. Lakini nikashauriwa kwamba nifupishe kwa kutaja kauli (zao) peke yake, kwa kuwa kufanya hivyo itakuwa wepesi na rahisi zaidi katika kuwafahamisha watu, hasa ukizingatia kwamba dalili zilizotegemewa na wenye madhehebu hayo hazifahamu ila tu waliokomaa kwenye elimu. Kwa kweli ni kana kwamba kauli hii ilinizindua na kunikumbusha ukweli ambao ulikuwa umejificha nafsini mwangu, nao ni kuwa kwa hakika wengi miongoni mwa watu ambao walisoma elimu ya Fikihi huzipa umuhimu mkubwa zaidi fatwa kuliko wanavyotilia maanani dalili yake na chimbuko la fatwa husika. Ikiwa hali ni hiyo kwa wasomi, vipi hali ilivyo kwa wengineo? Hivyo nikabadili azma yangu ya awali, na nikatosheka kutaja kauli za madhehebu tano na maelezo yake kwa ufupi, nikiacha dalili zao na maelezo yao ya ziada, ila pale tu nilipolazimika nayo kuyajumuisha, ili kitabu hiki kiwe ni cha watu wote, wala kisiwe ni cha kikundi maalumu cha watu.

Pamoja na hayo yote, kwa kweli nilipata ugumu wakati wa kunukuu kwangu, na nilipata pia taabu kubwa ambayo hakuna anayeweza kuijua ila tu yule ambaye alishatunga kitabu. Ni uzito ambao sikuwahi kuupata katika utungaji wangu wa vitabu hata siku moja ndani ya maisha yangu ya uandishi wa vitabu vya maudhui mengineyo. Niliwahi kumsikia mtu akisema: "Kuandika kitabu cha Fikihi ya madhehebu mbali mbali ni rahisi sana kwa sababu ni kunukuu tu maneno basi huwa imetosha." Lakini kusema hivi ni



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 25 2/1/2017 3:51:40 PM

sawa na maneno ya mtu anayesema kuwa: “Vita havina taabu yoyote ila ni kushika silaha na kuingia kwenye mapambano tu basi. Na wala baada ya hivyo hakuna kazi nyingine.”

Hakika bahari ya elimu ya Fikihi ni bahari kuu yenye kina kirefu, kwani kutokana na mas’ala moja tu huzuka Tanzuo na matawi mengi yasiyohesabika, na pia huzuka migongano ya kila tawi kwa mafakihi kupingana katika kauli zao. Aidha, hutokea kupingana na kupatikana hitilafu kati ya mafakihi wa madhehebu moja au mwanachuoni mmoja. Kwa kweli yeyote anayeingia kwenye mas’ala yenye tofauti ambayo wanavyuoni wamepingana au kutofautiana huwa amejiingiza kwenye utata na hupata shida na mashaka makubwa. Sasa vipi itakuwa sahali unapokusudia kuiandika Fikihi nzima mkiwamo ibada zake na miamala yake, tena Fikihi kwa mujibu wa madhehebu zote?

Na kwa ajili ya kuchelea tabu kama hiyo ndio maana viongozi wa ‘Chuo Kikuu cha Azhar’ walipotaka kuweka au kutunga Fikihi kwa mujibu wa madhehebu manne mnamo mwaka 1922 A.D walichagua kamati ya wanavyuoni (mafakihi) wakubwa wa madhehebu hayo manne, kwa shabaha ya kila sheikh wa madhehebu husika aandike mas’ala za madhehebu yake tu. Na pamoja na hivyo kamati hiyo ilishughulikia jambo hilo kwa muda wa miaka mingi, ndipo baada ya miaka mingi wakaweza kukusanya hukmu za Fikihi kwa mujibu wa madhehebu manne, bila ya kuambatanisha na dalili zake, kwa mfumo kama huu unaouona kwenye kitabu hiki.

Pamoja na kufanya juhudi kubwa lakini hata hivyo kimenitaabisha sana katika baadhi ya mas’ala. Nililazimika kufanya upekuzi na kupitia mas’ala hayo katika vitabu vikubwa na vidogo na kwa muda mrefu. Licha ya kwamba nimetumia miaka 33 ya kusoma na kusomesha somo la Fikihi na Misingi yake, ikiwa ni pamoja na kutunga vitabu katika maudhui hizo lakini hata hivyo hazikuniepuka



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 26 2/1/2017 3:51:40 PM

taabu hizo. Ikiwa hivi ndivyo itakuwaje kwa mtu asiyejua chochote katika Fikihi isipokuwa jina lake?!

Kisha ni kwamba Fikihi iliyotungwa kwa mujibu wa madhehebu manne imetaja kila kauli ya madhehebu moja kivyake, kama ilivyo katika vitabu vya wanavyuoni wake, isipokuwa pale tu ambapo wameafikiana rai maimamu wote wanne. Ama kitabu hiki chenyewe kimekusanya yale waliyoafikiana kati ya madhehebu mawili au zaidi katika jumla moja, kwa lengo la kutaka kufupisha na kurahisisha. Na kusema kweli sikupata taabu sana wakati wa kukitunga kitabu hiki kama pale inapotokea nukuu zinapingana na kuna kauli nyingi zenye kupingana kutoka kwa imamu mmoja juu ya mas'ala moja. Kwa mfano kitabu fulani cha madhehebu husika kinanukuu kwamba jambo fulani ni haramu, na kitabu kingine cha madhehebu hayo hayo kinanukuu kuwa jambo hilo linaruhusiwa kisharia, na kitabu cha tatu cha madhehebu hayo hayo kinanukuu kuwa jambo hilo ni makuruhu. Lakini kwa kuwa lengo langu ni kuwarahisishia wasomaji hivyo basi nimeepuka kwa kadiri nilivyoweza kunukuu nukuu zote bali nimetosheka na nukuu ya mtunzi wa zamani zaidi kati ya watunzi wa madhehebu husika, na hasa iwapo mwanachuoni aliyenukuu nukuu hiyo ni mfuasi halisi wa madhehebu ya imam anayemnukuu maneno yake. Na imetokea mara nyingine kwamba nimekuta kuna mas'ala waliyoafikiana Maimamu wanne wa Kisuni lakini mmoja akawa ana kauli mbili katika mas'ala hayo. Moja inaafikiana na Maimamu wale watatu na kauli yake moja inawakhalifu, basi mahali kama hapo mimi nimechagua nukuu ile iliyoafikiana na wenzake na nimeiacha ile iliyowakhalifu kwa sababu ya kujaribu kuepuka na kupunguza utengano.[1]

---

[1] Hebu nikupe mfano wa nilivyofanya katika kunukuu kwangu: wamesema Imamiyya, Shafi, Hanafi na Maliki: Yajuzu kuwapa Zaka (yako) ndugu na jamaa, na imepokewa kutoka kwa Imam Ibn Hanbal riwaya mbili, moja inajuzisha na ya pili inakataza." Hapo mimi niliinuku ile iliyoafikiana na wenzake.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 27 2/1/2017 3:51:40 PM

Ama pale inapotokea nukuu ni ya imamu mmoja peke yake, kila mmoja ana kauli yake katika mas'ala basi mimi hapo nimetaja hitilafu hiyo moja kwa moja. Na imetokea katika maelezo yangu mara nyingi ninapotaja kuhusu madhehebu manne ya Ahlu-Sunna: Shafi, Hanafi, Maliki na Hanbali, natumia neno 'Maimamu wanne' tu bila ya kuwataja majina kila mmoja peke yake.

Ama katika mas'ala yanayohusu Fikihi ya Ja'far ambayo ndiyo inayofuatwa na Shia Imamiyya katika matendo yao, mimi nimenukuu yale ambayo wamekongamana juu yake na kuchagua kauli iliyo mashuhuri katika mambo waliyohitalifiana.

Na mwisho kabisa nanukuu hapa maneno yaliyoandikwa katika utangulizi wa kitabu **'Fikihi kwa mujibu wa madhehebu manne'** ambacho walishirikiana katika kukitunga na kukipanga wanavyuoni saba miongoni mwa wanavyuoni wakubwa wa Azhar, walisema: "Si aibu kupatikana kosa ndani ya kitabu hiki, kwani ukamilifu ni wake Mwenyezi Mungu ndiye asiyekosea. Bali aibu ni kwa yule anayegundua kosa kisha asilikosoe na kuliweka kwenye usawa wake, na pia aibu ni kwa yule anayekosoa kosa bila ya kulitambua kosa lenyewe kiini chake."

Namuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu atuongoze pia sote kwenye haki, na amnufaishe kwa kurasa hizi kila atakaye kunufaika, na shukrani ni zake Mwenyezi Mungu tangu mwanzo na hadi mwisho.

**Muhammad Jawad Mughniya**
**Beirut.**
**1/10/1960**



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 28 2/1/2017 3:51:40 PM

# SEHEMU YA KWANZA:

## MAMBO YA KIIBADA

## TOHARA

Waislamu wameipa tohara umuhimu mkubwa sana. Na wametunga vitabu vinavyoelezea tohara kwa maelezo marefu. Aidha huwafundisha pamoja na kuwazoeza watoto wao kuipa kipaumbele, na pia huisoma na kuifundisha misikitini na katika vyuo vyao. Na maimamu wa Fikihi wameifanya ndio msingi na sharti muhimu la kusihi kwa ibada. Na sitakuwa nimeongeza chumvi nikisema kuwa hakuna dini nyingine yoyote iliyoipa tohara umuhimu mkubwa zaidi kama ilivyo dini ya Uislamu.

Na tohara katika lugha ya Kiarabu ina maana ya usafi; na katika istilahi ya mafakihi (sharia) ni kuondoa *Hadathi* au kuondoa *Khabathi*; na *Khabathi* ni aina yoyote ile ya najisi ya kimada, kama vile damu, mkojo na kinyesi. Na *Hadathi* ni jambo la kimaanawi linalomtokea mwanadamu pindi anapotokewa na jambo ambalo kisharia humzuwia kuswali na huwajibisha kuoga josho la kisharia, kutawadha au kutayammamu.

Na kisharia tohara ya kujitwahirisha kutokana na *Hadathi* haiwezi kutimia ila kwa niya ya kutaka kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu na kutii amri kwa tohara hiyo. Ama kutoharisha mkono, nguo na chombo vinapokuwa vimepatwa na najisi (kunajisika) hakuhitaji niya, hutoharika hata bila niya makhususi, bali ni kwamba hata kama ikitokea nguo iliyonajisika itapeperushwa na upepo na hatimaye



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 29 2/1/2017 3:51:40 PM

ikatumbukia ndani ya maji mengi hapo hutwaharika moja kwa moja. - Na hulazimu kutumika maji katika kujitwahirisha kutokana na *Hadathi* na *Khabathi*, hiyo ni kutokana na kauli ya Mwenyezi Mungu:

وَيُنَزِّلُ عَلَيْكُم مِّنَ ٱلسَّمَآءِ مَآءً لِّيُطَهِّرَكُم بِهِۦ ﴿١١﴾

**"Na akawateremshia maji kutoka mawinguni ili awatwaharishe kwayo," (Suratul-Anfal: 11).**

Na kauli yake Mwenyezi Mungu (s.w.t.):

وَأَنزَلْنَا مِنَ ٱلسَّمَآءِ مَآءً طَهُورًا ﴿٤٨﴾

**"Na tumeyateremsha kutoka mawinguni maji tohara (yanayotwa-hirisha) (Al-Furqan:48).**

Na neno '*twahur'* lina maana ya maji ambayo yenyewe ni tohara na yanatwahirisha kitu kingine; na ilivyo ni kwamba katika maji kuna sifa mbili:

**1.** Maji mengi

**2.** Maji machache.

Pia kuna maji yanayopatikana kwa kukamuliwa kutoka katika baadhi ya matunda au mimea, na maji yaliyochanganywa na kitu kingine, na pia maji yanayobaki kwenye asili yake ile ile ya maji ambayo ni maumbile yake yaliyoumbwa, kwa hiyo mafakihi (wanavyuoni wa Fikihi) waliyagawanya maji katika sehemu mbili:

**1.** Maji Halisi

**2.** Maji Yasiyokuwa halisi.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 30 2/1/2017 3:51:40 PM

# MAJI HALISI

Maji Halisi ni maji yaliyobaki katika asili yake na tabia yake kama yalivyoteremka kutoka mawinguni, au kuchimbuka kutoka ardhini. Kwa namna ambayo husihi kuitwa maji bila ya kuingiliwa na sifa yoyote inayoweza kuyatoa maji kutoka katika jina lake la asili. Na jina hilo 'Maji Halisi' linajumuisha maji ya mvua, maji ya bahari, maji ya mto, maji ya kisima na kila maji yanayobubujika ardhini na yaliyoyeyushwa kutokana na barafu au theluji.

Na bado maji hubaki katika sifa yake ile ya 'Maji Halisi' iwapo yatabadilika kwa njia ambayo ni vigumu kwa maji kujikinga na kitu kilichoibadili sifa yake, kama yaliyobadilika kwa udongo au mchanga, au kwa kukaa muda mrefu au kutokana na majani ya mti yaliyodondoka na kuangukia ndani yake, au kwa kudumbukia ndani yake mabua (au pumba) ya ngano yaliyokauka, au kwa kubadilika sifa yake kutokana na kitu kilichoko kwenye mapitio yake au kwenye makao yake kama chumvi au haluli (kibiriti) na madini mengine mfano wa hayo.

Na wanavyuoni wa Fikihi wa madhehebu zote kwa kauli moja wamekubaliana kuwa 'Maji Halisi' ni tohara na hutwahirisha *Hadathi* na *Khabathi*. Ama kauli iliyopokewa kutoka kwa Abdallah bin Umar ya kusema kuwa alivutiwa zaidi na kutayammamu kuliko kutumia maji ya bahari, hapa kauli ya Mtukufu Mtume isemayo: "Asiyetwahirishwa na bahari, basi pia Mwenyezi Mungu hatomtwahirisha" inamkanya.

# MAJI YALIYOTUMIKA

Pindi inapoondoshwa najisi kutoka mwilini, nguoni au kwenye chombo kwa kutumia Maji Halisi, na yakajitenga yenyewe au kwa



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 31 2/1/2017 3:51:40 PM

kukamuliwa, na mahala palipooshwa, maji hayo yaliyojitenga kwa mafakihi huitwa '*Ghasalah'* au '*Mustaamal* (yaliyotumika)*'*, nayo pia huwa ni najisi, kwa sababu ya kuwa ni machache na yameingiliwa na najisi na hivyo yamenajisika, sawa iwe yamebadilika moja ya sifa zake au hayakubadilika. Na yakiwa hivyo, basi huwa haisihi kutumiwa tena katika kuondoa *Khabathi* wala *Hadathi.*

Na kundi la mafakihi wa madhehebu wamesema kwamba: "Yanapojitenga maji haya kutoka mahala palipokuwa pamenajisika na yakawa yamebadilika kwa najisi, basi nayo huwa najisi. Lakini kama hayakubadilika basi hukmu yake itakuwa ni sawa na hukmu ya mahala palipooshwa, hivyo iwapo mahali hapo pametwaharika basi na maji hayo yatakuwa ni tohara, na iwapo bado pamenajisika, nayo yatakuwa ni najisi.

Hili halisihi isipokuwa pale tutakapoizingatia hali ya mahali hapo kabla ya kumwagiwa maji, je palikuwa katika hali gani; na baada ya maji kupitishwa juu yake pamekuwaje, la sivyo huenda pakatwaharika mahala pale palipomwagiwa maji juu yake, na maji yaliyotoka hapo yakawa ni najisi kwa sababu ya kugusana na najisi.

Na yanapotumiwa kwa kuondolea *Hadathi* tu, maji hayo huendelea kuwa tohara lakini yasiyotwaharisha. Hiyo ni kulingana na kauli iliyo mashuhuri katika madhehebu ya Abu Hanifa, na kauli dhahiri ya Imam Shafi na Ahmad. Na kwa mujibu wa Imam Maliki ni kwamba huendelea kuwa tohara na yanayotwaharisha, hiyo ni kwa mujibu wa moja kati ya nukuu mbili zilizopokewa kutoka kwake (*Al-Mughniy* cha Ibn Qudaamah, Juz. 1, uk. 19) .

Ama Shia Imamiyya (Ithnaasharia) wao wamesema: "Maji yaliyotumiwa katika wudhu na majosho ya Sunna, kama josho la kuomba toba, na josho la kuhudhuria Swala ya Ijumaa, maji hayo ni tohara na pia hutwaharisha *Hadathi* na *Khabathi*, yaani inaruhusiwa



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 32 2/1/2017 3:51:40 PM

kwetu kuoga kwa maji hayo yaliyotumika na pia inaruhusiwa kutawadhia na kuondolea najisi.

Ama maji yaliyotumika katika majosho ya wajibu, kama vile kuoga janaba na hedhi, hapa mafakihi wao wote wameafikiana kwamba yanaondoa *Khabathi*, na wamekhitilafiana kuhusu kutumia maji hayo kuondoa *Hadathi* na kuchukulia wudhu. Baadhi yao wameruhusu na baadhi yao wamekataza.

**Tawi:** Iwapo mwenye janaba atapiga mbizi ndani ya maji machache baada ya kuvitwaharisha viungo vilivyonajisika, na katika kupiga mbizi kwake akawa ametia nia ya kuondoa *Hadathi*, Hanbali wamesema: "Maji hayo aliyopigia mbizi sasa yatakuwa *Mustaamal* (yaliyotumika), na janaba lake halitakuwa limeondoka bali itampasa aoge mara ya pili (kwa maji mengine) ili kuondoa janaba lake.

Ama Shafi na Imamiyya na kadhalika Hanafi wao wamesema: "Maji hayo aliyopiga mbizi ndani yake yatakuwa *Mustaamal (yaliyotumika)* lakini janaba litakuwa limeondoka na wala haitamlazimu kuoga tena kwa mara ya pili. (Tazama *Mughniy* cha Ibn Quddamah Juz. 1, uk. 22 chapa ya tatu, na pia tazama Ibnu Abidin Juz. 1, uk. 140, chapa ya Al-Maymaniyyah).

Watu wa karne ya katikati walikuwa na haja kubwa kabisa na tawi hili na mfano wake miongoni mwa matawi ya Fikihi yaliyoandikwa kwa kirefu katika vitabu vikubwa vya Fikihi, ambapo zama hizo maji yalikuwa ni kitu kilicho ghali na kinachogharimu thamani kubwa ya fedha kama ilivyo kwa petroli siku hizi. Lakini kwa sasa hivi, na hasa baada ya elimu ya kuvuta maji kutoka chini ya ardhi na kuyapeleka katika kila nyumba hadi juu ya mlima, tumewasilisha tawi hili kama zinavyooneshwa athari za kihistoria katika majumba ya kumbukumbu za kale.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 33 2/1/2017 3:51:40 PM

# MAJI YASIYOKUWA HALISI (*MUDHAF*):

Maji yasiyokuwa halisi (*Mudhaf*): Ni maji yaliyokamuliwa kutokana na aina za matunda au mimea, kama vile malimau na maji ya zabibu, au ni yale ambayo yalikuwa halisi kisha yakatiwa kitu kilichoyatoa kutoka katika hali yake ya asili ya kimaumbile. Mfano maji ya maua (marashi –*Rose water),* maji ya aina hii ni tohara lakini hayatwaharishi *Khabathi* (najisi), na hii ni kulingana na itifaki ya madhehebu yote isipokuwa Mahanafi, wao wameruhusu kuondoa najisi kwa kutumia kimiminika chochote kile kisichokuwa mafuta, na isipokuwa maji yaliyobadilika kwa kupikwa, na amewaafiki katika hilo Sayyid Murtadha wa madhehebu ya Imamiyya (Shia Ithnaasharia).

Madhehebu yote pia yameafikiana kuwa si ruhusa kutawadha wala kuoga kwa maji yasiyokuwa halisi (*Mudhaf*) isipokuwa Mahanafi. Imeandikwa katika kitabu *Bidayatul Mujtahid wa Nihayatil Muktaswid* cha Ibnu Rushid uk. 32 chapa ya mwaka 1354 A.H. Na katika kitabu *Majmaunur* uk. 37 kilichochapishwa Istanbul: "Abu Hanifa amesema: 'Inaruhusiwa kutawadha kwa mvinyo (*wine*) uliotayarishwa kwa tende iwapo mtu yuko safarini.'"

Na imeandikwa kama hivyo katika uk. 12, Juz. 1, ya kitabu *Al-Mughniy* cha Ibn Qudamah kwa maneno haya: "Madhehebu ya Abu Hanifa yanaruhusu kutawadha kwa maji yasiyokuwa halisi *(Mudhaf)*."

Na Sheikh Swadduq wa madhehebu ya Shia Imamiyya amesema: "Inasihi kutawadha na kuoga janaba kwa maji ya wardi."

Mahanafi wana dalili yao wanayoitumia kuruhusu kutawadha kwa maji yasiyokuwa halisi, nayo ni Aya ya Mwenyezi Mungu isemayo:



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 34 2/1/2017 3:51:40 PM

فَلَمْ تَجِدُوا مَاءً فَتَيَمَّمُوا صَعِيدًا طَيِّبًا ﴿٦﴾

**"Iwapo hamkupata maji, basi tayammamuni kwa kutumia mchanga ulio tohara." (Al-Maidah:8).**

Wanasema: "Kwa hakika maana ya Aya hii ni kuwa, 'iwapo hamkupata maji halisi wala yasiyokuwa halisi,' hivyo yanapopatikana maji yasiyokuwa halisi si ruhusa kutayammamu. Na ni Aya hiyo hiyo madhehebu mengine wameitumia kuwa dalili yao ya kukataza kutumia maji yasiyokuwa halisi, wamesema: "Kwa hakika tamko **maji** lililotajwa katika Aya tukufu linamaanisha maji halisi peke yake bila kujumuisha maji yasiyokuwa halisi, hivyo maana ya Aya inakuwa: 'Iwapo hamkupata maji halisi basi tayammamuni' na hivyo inakuwa kuwepo kwa maji yasiyokuwa halisi au kutokuwepo kwake ni sawa tu. Na hii ndiyo haki kwa sababu mtu unapoomba maji kutoka kwa mhudumu wa mkahawa au mahali penginepo hawezi kukuletea mvinyo wala maji ya matunda. Na ni jambo linaloeleweka sana kwamba maudhui za Aya zinazoteremka kwa lengo la kuwawekea waja hukmu za sharia huteremka kulingana na ufahamu wa jamii.

Na kutofautiana kwa rai za maimamu wa Fikihi katika tafsiri ya neno maji kwenye Aya hiyo kunatujulisha kuwa ni kama wanavyotofautiana malenga wa fani ya mashairi kuhusu maana ya ubeti wa shairi, na ni kama wanavyotofautiana wanavyuoni wa lugha katika kutafsiri neno la kilugha, hakika ni kutofautiana katika ufahamu na Ijtihadi, si katika misingi na asili.

## KULATENI

Mafakihi na maimamu wa madhehebu yote wamekubaliana kwamba maji yanapobadilika rangi yake au ladha yake, au harufu yake kwa sababu ya kukutana na najisi, huwa yamenajisika, sawa yawe ni



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 35 2/1/2017 3:51:40 PM

mengi au machache, yaliyobubujika kutoka ardhini (maji ya chemchem) au yasiyobubujika kutoka ardhini, sawa yawe ni maji halisi au yasiyokuwa halisi. Lakini yakibadilika kwa kupitiwa na harufu ya najisi bila kukutana nayo, kama pale mzoga utakapokuwa kando mwa maji hayo na upepo ukaichukua harufu yake hadi kwenye maji, basi maji hayo bado yatabaki kuwa ni tohara.

Ama iwapo najisi itachanganyika na maji bila kubadilika moja kati ya sifa hizo tatu, Imam Maliki katika moja ya nukuu iliyopokelewa kutoka kwake amesema: "Maji hayo yatakuwa ni tohara, sawa yawe mengi au machache."

Na mafakihi wa madhehebu mengine wamesema: "Ikiwa maji hayo ni machache basi yatakuwa yamenajisika, na iwapo ni mengi basi ni tohara."

Lakini hata hivyo wametofautiana katika kipimo cha maji mengi, Mashafi na Mahanbali wamesema[2]: "Maji mengi ni yale yanayofikia ujazo wa kulateni kwa kufuata Hadith isemayo: 'Maji yanapofikia ujazo wa kulateni huwa hayaathiriwi na najisi.' Na kulateni ni ratili 500 za Kiiraki. Baadhi ya masheikh wa Azhar walikadiria kiwango cha kulateni kuwa ni matangi 12.

Na Maimamiyya wanasema: "Maji mengi ni yale yanayofikia ujazo wa *Kurr* kwa ushahidi wa Hadith hii: "Maji yanapofikia ujazo wa *Kurr* hayanajisiki na kitu." Na *Kurr* ni ratili 1200 za Kiiraki ambazo katika wingi wake zinalingana na wingi wa matangi 27.

Na Mahanafi wanasema: "Maji mengi ni yale ambayo yamefikia kiasi cha ujazo ambao lau mtu atatingisha pembe moja ya maji hayo, pembe ya pili ya maji hayo haitafikiwa na mtingisho huo."[3]

---

[2] Mahanbali wanasema: "Maji mengi hayanajisiki kwa kukutana na najisi, iwapo najisi hiyo si mkojo au kinyesi, lakini yakutanapo na kimoja kati ya hivyo viwili hunajisika, sawa yawe yamebadilika au la, ila tu iwapo ni kutokana na viwanda vilivyoko njia ya Makka (*Al-Mughni* cha Ibn Quddama Juz. 1).

[3] Zipo kauli nyingi zinazoelezea kipimo cha maji mengi, mbali na zilizotajwa huko juu



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 36 2/1/2017 3:51:41 PM

Na kutokana na maelezo yaliyotangulia inabainika kwamba Mamaliki hawazingatii kulateni wala *Kurr*, kwao wao maji hayana ujazo maalumu, wao mengi na machache ni sawa, hivyo iwapo tu yatabadilika moja ya sifa zake huwa yamenajisika, kama si hivyo hayajanajisika. Katika Maimamiya ameafikiana nao katika hilo Ibn Aqil kwa kufuata ujumla wa Hadith isemayo: "Maji ni tohara, hayanajisiki na kitu ila yanapozidiwa na harufu, ladha au rangi." Lakini Hadith hii ni ya kiujumla (عام *Aa'm*) na Hadith ya *Kurr* ni makhususi خاص) *Khaas*) na Hadith makhususi huwa inaitangulia hadithi ya ujumla.

Mahanafi pia hawakuzingatia kulateni wala *Kurr*, wamezingatia mtingishiko lakini sikupata athari yoyote ya Kitabu au Sunna ikizungumzia hili.

**Tawi**: Mashafi na Maimamiyya wamesema: Vimiminika visivyokuwa maji, kama vile siki na mafuta hunajisika kwa kiasi cha kuguswa tu na najisi, sawa kimiminika hicho kiwe ni kingi au kichache, na kiwe kimebadilika au la. Maneno haya ni kulingana na vile ilivyohukumu misingi ya sharia, kwa sababu kinachofahamika kutokana na kauli ya Mtume ﷺ: "Maji yanapofikia ujazo wa kulateni huwa hayaathiriwi na najisi." ni yale maji halisi.

Na Mahanafi wamesema: "Hukmu ya vimiminika ni sawa na hukmu ya maji halisi katika wingi wake na uchache wake, kichache hunajisika kwa kupatwa na najisi lakini si kingi. Imeelezwa katika *Hashiya* ya Ibnu Abidiin Juz. 1, uk. 130 iliyopigwa chapa na Maymaniyyah: "Hukmu ya vimiminika ni kama ya maji kwa kauli iliyo sahihi zaidi, hata kama mkojo utadondokea ndani ya kinywaji maadamu tu ni kingi hakinajisiki, na hata kama damu ya mguu wake itatiririzikia kwenye kinywaji (maadamu tu ni kingi) hakinajisiki."

---

lakini ziliachwa nje na mafakihi, miongoni mwazo ni: Maji mengi ni kurr 40, na maji mengi ni ndoo mbili kubwa, na nyingine ni ndoo arobaini (40).



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 37 2/1/2017 3:51:41 PM

# MAJI YANAYOTEMBEA NA YALIYOTUWAMA

Yamekhitilafiana madhehebu kuhusu maji yenye kutembea. Wamesema Mahanafi: "Kila maji yatembeayo, sawa yawe mengi au machache, sawa yawe yameungana na chanzo chake au hayakuungana na chanzo chake, hayanajisiki kwa kule tu kukutana na najisi, bali hata kama katika chombo kimoja kutakuwa na maji yaliyonajisika, na katika kingine kuna maji tohara kisha yakamiminwa kutoka juu na hatimaye yakiwa hewani yakachanganyika pamoja kisha yakashuka; yote yatakuwa tohara. Na ni hivyo hivyo ikiwa yatapitishwa ardhini." (Ibn Abdin, Juz. 1, uk. 131).

Hivyo kipimo ni kutembea kwa maji, na kukipatikana kwa aina yoyote ile maji hayo hupewa hukmu ya maji mengi, na kama hayatembei, basi ni machache hata kama ni chemchem, na ni kuanzia hapa ndipo wakahukumu kwamba maji ya mvua kama yatamiminikia kwenye ardhi iliyo na najisi na yakawa hayatembei basi yatabaki kuwa najisi.

Kwa hivyo kwa Mahanafi maji ambayo hayanajisiki kwa kuingiwa na najisi ni aina mbili: **Ya kwanza:** Ni maji yaliyotuwama mahala pamoja ambayo kama utayatingisha upande mmoja hayatatikisika upande wake wa pili. **Ya pili:** Ni maji yanayotembea kwa njia yoyote ile.

Ama maji machache ambayo hayanajisiki kwa kugusana na najisi, ni yale maji yaliyotuwama ambayo kama utayatingisha upande mmoja hayatatikisika upande wake wa pili.

Ama Mashafi, kwao wao hakuna tofauti kati ya maji yanayotembea na yaliyotuwama, wala kati ya maji yanayobubujika kutoka ardhini na mengineyo, bali zingatio lao kubwa ni kwenye wingi wa maji na uchache, ambapo mengi ni yale yaliyofikia ujazo wa kulateni, haya



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 38 2/1/2017 3:51:41 PM

hayanajisiki kwa kuingiwa na najisi, na machache ni yale yasiyofikia ujazo wa kulateni, haya hunajisika kwa kuingiwa na najisi, sawa yawe ni yenye kutembea au kutuwama, sawa yawe yamebubujika kutoka ardhini au hayakububujika. Katika hilo wameshikilia ujumla wa Hadith hii: "Maji yanapofikia ujazo wa kulateni huwa hayaathiriwi na najisi."

Na pia wamesema: "Kama maji yanatembea na ndani yake kuna najisi, itaangaliwa. Iwapo maji hayo yaliyobeba najisi yamefikia ujazo wa kulateni basi maji yote yatakuwa ni tohara lakini kwa sharti yawe hayakubadilika sifa. Na kama maji hayo yaliyobeba najisi hayafikii ujazo wa kulateni, basi yatakuwa ni najisi. Ama yale maji yaliyo juu yake na yaliyo chini yake (ambayo si lile eneo lililobeba najisi) hayo yatakuwa ni tohara.

Na Mashafi walifasiri neno '*Jirya'* kwa maana ya mkondo wa maji uliyopo kwenye pande mbili za kingo za mto kwa mapana. Kwa hiyo kwa Mashafi tofauti iliyopo kati ya maji yanayotembea na yaliyotuwama mahali pamoja, ni kwamba maji yaliyotuwama mahali pamoja huhesabika kuwa ni maji mamoja. Ama yale yanayotembea hata kama yatakuwa yameungana na kuchanganyika pamoja, bado wao huyagawa kwenye mikondo tofauti, kisha kila mkondo huupa hukmu yake tofauti na mkondo mwingine. Hivyo unapokuwa ni mkondo wa maji mengi huwa hayanajisiki kwa kuingiwa na najisi, na iwapo ni mkondo wa maji machache hunajisika kwa kuingiwa na najisi. Hivyo basi, iwapo mkono wako umenajisika halafu ukautwaharisha kwa mmojawapo wa mikondo ya maji yanayotembea, na mkondo huo ukawa haufikii ujazo wa kulateni, si ruhusa kwako kunywa wala kutawadhia maji ya mkondo huo, kwa kuwa ni najisi, na hivyo itakulazimu usubiri mkondo wa pili au ufuate maji yaliyo juu yake au chini yake.

Na hapa inabainika kwamba tofauti iliyopo baina ya rai ya Mashafi na Mahanafi kuhusiana na maji yanayotembea ni kubwa



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 39 2/1/2017 3:51:41 PM

sana. Mahanafi wanaona kutembea kwa maji – hata kama ni machache - ni sababu ya utohara wake, kama unavyoonesha mfano wao wa vyombo viwili vilivyo na maji ndani yake. Kimoja kina maji tohara na cha pili kina maji yaliyonajisika, kwamba maji hayo yaliyonajisika hutwaharika kama tu yatachanganywa kwa mfumo wa kutembea.

Ama Mashafi wao hawatilii maanani utembeaji wa maji. Hata kama ni mto mkubwa kiasi gani na wanaona kuwa kila mkondo una hukumu yenye kujitegemea, hata kama sehemu za maji hayo zitakuwa zimeungana na kuchanganyika pamoja.

Na Mahanbali wanasema: "Maji yaliyotuwama na kusimama mahala pamoja ambayo hayajafikia ujazo wa kulateni hunajisika kwa kule tu kuingiwa na najisi, sawa maji hayo yawe yanabubujika kutoka ardhini au mengineyo. Ama yanayotembea hayanajisiki isipokuwa yanapobadilika moja ya sifa zake, yaani hukmu ya maji hayo ni sawa na maji mengi hata kama hayabubujiki kutoka ardhini." Na kauli yao hii inakaribiana sana na kauli ya Mahanafi.

Ama Mamaliki, tumeshatangulia kusema kwamba, kwao wao maji yaliyo machache hayanajisiki yanapokutana na najisi. Na hawatofautishi kati ya maji yanayotembea na yaliyotuwama mahali pamoja. Na kwa neno jingine ni kwamba wao kama inavyodhihirika, hawazingatii wingi wa maji wala uchache wake, wala utembeaji wake wala kutuwama kwake. Wala hawazingatii aina ya najisi wala kinginecho, bali kipimo kwao ni kule kubadilika kwa sifa za maji kutokana na najisi. Hivyo iwapo yatabadilika moja ya sifa zake kwa sababu ya kuingiwa na najisi hunajisika, na yasipobadilika hubakia kwenye utohara wake, sawa yawe ni maji yenye kububujika kutoka ardhini au mengineyo, sawa yawe mengi au machache.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 40 2/1/2017 3:51:41 PM

Na Maimamiyya wamesema: "Utembeaji wa maji hauna taathira yoyote katika hali yoyote iwayo, bali linalozingatiwa ni kule kuwa yenye kububujika kutoka ardhini au mengi, hivyo iwapo yataungana na maji yanayobubujika kutoka ardhini – hata kama ni kwa matone machache machache - yatapewa hukmu ya maji mengi, yaani hayanajisiki kwa kukutana na najisi, hata kama ni machache na yaliyotuwama, kwa sababu katika kule kuchimbuka kuna nguvu yenye kuyahifadhi na ya asili ya mbubujiko. Na kama hayajaungana na maji yenye kububujika kutoka ardhini kama yana ujazo wa *kurr* hayanajisishwi kwa chochote isipokuwa kama tu yatabadilika moja ya sifa zake. Na kama hayajafikia *kurr* hunajisika kwa kule tu kuingiwa na najisi, sawa yawe ni yaliyotuwama au yanayotembea. Isipokuwa yanapokuwa yanatembea kutoka juu kwenda chini hapo hukmu yake ni kwamba yaliyo juu hayanajisiki. Na hali ni hiyo hiyo najisi inapokutana na yaliyo chini." Hivyo ni kwamba kwa Maimamiyya kutembea kwa maji na kutotembea hukmu yake ni sawa, na inabainika kwamba wao wamejitenga na madhehebu mengine kwa kuzingatia maji yenye kububujika kutoka ardhini kwa kule kuyapa maji yanayobubujika kutoka ardhini hukmu sawa na maji mengi, hata kama machoni mwa watu yataonekana kuwa ni machache.

Isipokuwa mwanachuoni wao mmoja Allamah al-Hilli ndiye aliyejitenga na wenzake, pale alipoacha kuyapa uzito wowote maji yanayobubujika kutoka ardhini, na akatoa hukmu ya kunajisika maji hayo kwa kule tu kugusana na najisi iwapo hayajafikia ujazo wa *Kurr*.

Na maji ya mvua wakati wa kuteremka (kunyesha) kwake kutoka mawinguni, kwa madhehebu ya Maimamiyya ni sawa na yanayobubujika kutoka ardhini (chemchem) na maji mengi, kwa maana ya kwamba hayanajisiki kwa kuguswa na najisi,



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 41 2/1/2017 3:51:41 PM

na hutwaharisha nguo, ardhi, vyombo na vitu vyote vingine vilivyonajisika pale tu inapovinyeshea baada ya kuondoka najisi yenyewe.

## KUTOHARISHA MAJI YALIYONAJISIKA

**1.** Maji yanapokuwa ni machache, hunajisika kwa kuguswa (kuingia) na najisi hata kama hayatabadilika moja ya sifa zake kutokana na najisi hiyo. Mashafi wamesema: "Yanapokusanyika sehemu moja maji yaliyonajisika na kufikia mkusanyiko huo ujazo wa kulateni huwa ni tohara na yenye kutoharisha, hivyo basi kama mtu ana vyombo viwili au vyombo vingi na ndani ya kila chombo kimoja mna maji yaliyonajisika, kisha maji hayo yakakusanywa mahali pamoja, na mkusanyiko wote ukafikia ujazo wa kulateni, katika hali hii maji hayo yanakuwa tohara na yenye kutoharisha." (*Sharhul Muhadhab*, Juz. 1, uk. 136).

Mahanbali na wanazuoni wengi wa Imamiyya wamesema: "Haiwezekani kuyatwaharisha maji machache yaliyonajisika kwa kuyaongeza hadi kufikia ujazo wa kulateni au *Kurri*, sawa hayo yaliyoongezwa yawe ni yaliyonajisika au ni tohara, kwa sababu kuchanganya maji yaliyonajisika kwenye maji mengine yaliyonajisika hakufanyi mjumuiko huo wa maji hayo yaliyochanganywa kutwaharika. Na kadhalika maji machache yaliyo tohara yanapochanganywa na maji yaliyonajisika hunajisika kwa kule tu kugusana na maji yenye najisi, hivyo mtu anapotaka kutwaharisha maji machache yaliyonajisika anapasa kuyaunganisha na *Kurr*. Au na maji yanayobubujika kutoka ardhini (chemchem) kwa mujibu wa madhehebu ya Imamiyya, au na kulateni kwa mujibu wa madhehebu ya Hanbali.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 42 2/1/2017 3:51:41 PM

**2.** Maji Mengi yanapobadilika moja ya sifa zake kutokana na kuingiwa na najisi hunajisika, na hivyo hutoharika kwa kuondoka mabadiliko hayo. Na kwa mujibu wa Mashafi na Mahanbali hayahitaji kuongeza kitu chochote kile. Ama Maimamiyya wao wanasema: "Inapokuwa si maji yanayobubujika kutoka ardhini hayatwahariki kwa kuondoka tu mabadiliko husika, bali baada ya kuondoka mabadiliko hayo hulazimu kuyaongezea maji mengine tohara yenye ujazo wa *Kurr*, au kuyaunganisha na maji ya chemchem au mvua. Ama yakiwa ni maji ya chemchem yanayobubujika kutoka ardhini yenyewe hutoharika kwa kule tu kuondokewa na mabadiliko hata kama ni machache."

Mamaliki wamesema: "Maji yaliyonajisika hutwaharika kwa kuongezewa maji halisi hadi sifa ya najisi iliyokuwamo humo iondoke kabisa."

Na Mahanafi wanasema: "Bila ya shaka maji yaliyonajisika hutwaharika kwa kutembea, hivyo kama ndani ya chombo fulani mna maji yaliyonajisika, halafu yakamwagiwa maji mengine ndani yake mpaka yakaanza kumwagika na kutembea, maji hayo yanatoharika. Na hali ni kama hiyo, kama maji yaliyonajisika yamo ndani ya birika au katika shimo kisha likachimbwa shimo jingine la pili na yakawepo masafa kati ya mashimo hayo mawili ingawa ni mafupi, kisha ukachimbwa mtaro baina yake ukayatiririsha maji kutoka shimo hilo hadi la pili na yakakusanyika humo yote basi hutwaharika. Na kama maji hayo yatanajisika kwa mara ya pili baada ya kukaa humo kwa muda kisha likachimbwa shimo jingine la tatu na akarudia kufanya kama mara ya kwanza, maji hayo yatatwaharika tena, na ni hivyo hivyo bila kuwa na mwisho. Hii ni kuwa maji ambayo wewe ulikuwa umezuiliwa kisheria kuyatumia yalipokuwa yametuwama, unaruhusiwa kuyatumia yanapokuwa yanatembea kwa njia yoyote ile, hata kama ndani yake kulikuwa na



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 43 2/1/2017 3:51:41 PM

mzoga wa mnyama, au yalikojolewa na watu wengi yakiwa chini, na athari yake haijaonekana wakati wa kutembea kwake. Hii ni pamoja na kufahamu kuwa maji hayo hayajaungana na maji ya chemchem yanayobubujika kutoka aridhini." (Ibnu Abidiin Juz. 1, uk. 131).

## AINA ZA NAJISI

**MBWA:**

Ni najisi isipokuwa kwa Maliki, lakini naye alisema: "Chombo kilichotiwa mdomo na mbwa kioshwe mara saba (7), lakini si kwa sababu ya unajisi ila ni kama njia ya kiibada tu."

Mashafi na Mahanbali wamesema: "Kioshwe chombo kilichotiwa mdomo au kunuswa na mbwa mara saba na moja yake iwe ni kwa mchanga."

Maimamiyya wamesema: "Kuosha chombo kilichotiwa mdomo na mbwa ni mara moja tu kwa mchanga kisha mara mbili zifuatie kwa maji matupu."

**Nguruwe:**

Naye hukmu yake ni sawa na ya mbwa katika madhehebu yote isipokuwa kwa Maimamiyya tu peke yao, kwani wao wamewajibisha kuoshwa chombo mara saba kwa maji matupu bila ya kuchanganya na mchanga. Na hukmu hii vile vile inahusika kwa chombo kilichonajisika kwa mzoga wa ndezi naye ni aina ya panya wa nchikavu, ila tu yeye ni mkubwa zaidi.

**Mzoga:**

Wote wameafikiana juu ya unajisi wa mzoga wa mnyama wa bara (si wa bahari) isipokuwa maiti ya mwanaadamu, iwapo mnyama huyo



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 44 2/1/2017 3:51:41 PM

ni miongoni mwa wanyama wenye damu ya kuchupa wakati wa kutoka kwake. Ama kuhusu maiti ya mwanadamu, Mamaliki, Mashafi na Mahanbali wamekubaliana kuwa ni tohara. Na Mahanafi wasema maiti ya mwanadamu ni najisi, lakini hutwaharika kwa kuoshwa. Na ni hivyo hivyo ndivyo wanavyosema Maimamiyya, lakini wao wameweka sharti la kwamba iwe ni maiti ya Mwislamu, hiyo ndiyo inayotwaharika kwa kuoshwa.

**Damu:**

Madhehebu manne yameafikiana juu ya unajisi wa damu isipokuwa damu ya mtu aliyeuawa shahid inapokuwa bado ingali juu ya mwili wake, na damu iliyobaki katika mwili wa mnyama aliyechinjwa, na damu ya samaki, chawa, viroboto na vile vile kunguni.

Ama Maimamiyya wao wamesema: "Ni najisi damu ya kila mnyama ambaye anapochinjwa damu yake hutoka kwa nguvu, sawa awe ni mwanadamu au mwingineo kati ya wanyama, sawa awe ni shahid (mtu aliyeuawa shahidi) au mwingine asiyekuwa shahidi. Na wamesema damu ya mnyama yoyote ambaye anapochinjwa damu yake haitoki kwa nguvu ni tohara, sawa awe ni mnyama wa bara (nchi kavu) au wa baharini. Na kadhalika wamesema kuwa damu iliyobaki katika mwili wa mnyama aliyechinjwa hukmu yake ni tohara.

**Manii:**

Maimamiyya, Mamaliki na Mahanafi wamesema: Manii ya mwanadamu na wanyama wengineo wote ni najisi, lakini hata hivyo Maimamiyya wameyaondoa katika hukmu hiyo manii ya mnyama asiye na damu ya kuchupa anapochinjwa, ambapo wamesema manii yake ni tohara na kadhalika damu yake.

Na Mashafi wamesema: "Manii ya mwanadamu ni tohara, na manii ya kila mnyama ni tohara isipokuwa manii ya mbwa na nguruwe.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 45 2/1/2017 3:51:41 PM

Na Mahanbali wamesema: "Manii ya mwanadamu ni tohara na vile vile manii ya mnyama anayeliwa nyama yake, ama mnyama asiyeliwa nyama yake manii yake ni najisi.

**USAHA:**

Kwa madhehebu yote manne ni najisi, na kwa Maimamiyya ni tohara.

**KINYESI CHA MWANADAMU NA MIKOJO:**

Vyote viwili ni najisi katika madhehebu yote.

**Kinyesi cha mnyama:**

Wanyama wasiyokuwa wanadamu, baadhi yao ni ndege na wengine si ndege, na baadhi yao wanaliwa na wengine hawaliwi. Ama ndege wanaoliwa ni kama vile njiwa na kuku, na wasioliwa ni kama vile kipanga na mwewe (ijapokuwa Imam Malik amewahalalisha kuliwa), na wanyama wanaoliwa ni kama vile ng'ombe na mbuzi. Na wasioliwa ni kama vile mbwa mwitu na paka (ijapokuwa Imam Malik amehalalisha kula nyama zao). Madhehebu yana kauli tofauti kuhusu kinyesi cha wanyama:

Mashafi wamesema: "Kinyesi cha wanyama wote ni najisi (kwa kauli moja), kwa hiyo kinyesi cha njiwa, shorewanda na kuku ni najisi, na kadhalika samadi ya ngamia, mbuzi na ng'ombe ni najisi, na kinyesi cha farasi na nyumbu ni najisi, na kinyesi cha wanyama hao wote na mfano wao ni najisi."

Na Maimamiyya wamesema: Kinyesi cha ndege wote wanaoliwa na wasioliwa ni tohara, na hali ni kama hiyo hiyo kwa wanyama wasiokuwa na damu ya kuchupa wanaoliwa na hata wasioliwa. Ama wale wenye damu ya kuchupa, iwapo ni katika wanyama wanaoliwa



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 46 2/1/2017 3:51:41 PM

kama vile ngamia na mbuzi basi kinyesi chao ni tohara. Na kama ni katika wanyama wasioliwa kama vile dubu na wanaowinda kwa makucha, kinyesi chao ni najisi. Na kila mnyama anayetiliwa shaka ya kuwa analiwa au haliwi kinyesi chake ni tohara.

Na Mahanafi wamesema kinyesi cha wanyama wasiokuwa ndege kama vile ngamia na mbuzi ni najisi. Ama ndege iwapo ni katika wale wanaojisaidia wakiwa angani kama vile njiwa na ndege wengineo kinyesi chao ni tohara. Na kama ni katika wale wanaojisaidia wakiwa ardhini kama vile kuku na bata kinyesi chao ni najisi.

Na Mahanbali na Mashafi wamesema: Kinyesi cha wanyama wanaoliwa ni tohara, ama cha mnyama asiyeliwa mwenye damu inayochupa ni najisi, sawa awe ni ndege au mwingineo.

Na wote kwa pamoja wameafikiana kuwa kinyesi cha mnyama yoyote ambaye kwa kawaida hula kinyesi chake ni najisi.

## KILEO CHA MAJIMAJI:

Ni najisi kwa madhehebu yote, lakini Maimamiyya wameongeza sharti, wamesema kiwe kina asili ya majimaji, wameweka sharti hilo ili kukijumuisha kileo ambacho kimekuwa kikavu kwa sababu nyingine, hivyo hata kama kitaganda na kukauka huendelea kuwa najisi. Na itakuwa bora hapa nikinukuu maneno ya mmoja kati ya watunzi wa Kiimamiyya, amesema: "Wameungana na kukubaliana wanavyuoni wote wa Kisunni na Kishia juu ya unajisi wa pombe isipokuwa kikundi kidogo katika sisi na katika wao."

## Matapishi:

Ni najisi katika madhehebu manne, na kwa Maimamiyya ni tohara.

## Madhii na wadhii:

Ni najisi kwa Mashafi, Maliki na Mahanafi, na vyote viwili ni tohara kwa Maimamiyya. Na Mahanbali wametenganisha kati ya



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 47 2/1/2017 3:51:41 PM

wadhii na madhii ya mnyama anayeliwa na asiyeliwa, wakasema ya mnyama anayeliwa ni tohara na ya mnyama asiyeliwa ni najisi.

**Madhii:** Ni maji membamba na laini ambayo hutoka kwenye tupu ya mbele wakati wa kuchezeana.

**Wadhii:** Ni majimaji mazito ambayo hutoka kwenye tupu ya mbele baada ya kukojoa.

Kama yalivyojitenga madhehebu manne kwa kusema matapishi, madhii na wadhii ni najisi ndivyo walivyojitenga peke yao Maimamiyya mbali na madhehebu mengine kwa kusema kuwa ni najsi jasho linalomtoka mtu mwenye janaba lililotokana na tendo la haramu, ambapo wamesema: "Mtu yeyote mwenye janaba litokanalo na zinaa au ulawiti au kwa kumwingilia mnyama, na au kwa kupiga punyeto, na akatokwa na jasho kabla hajaoga basi jasho lake hilo ni najisi."

**Masalio:** Mahanafi wamesema masalio yaliyoachwa na mbwa na nguruwe ni najisi. Na hivyo ndivyo wasemavyo Mashafi na Mahanbali. Na kadhalika wameafikiana wote juu ya masalio ya maji aliyoyabakisha nyumbu na punda kwamba ni tohara lakini hayatwaharishi. Bali Mahanbali wamesema: "Si ruhusa kutawadha kwa masalio ya maji ya kila mnyama asiyeliwa nyama yake isipokuwa paka peke yake au walio wadogo katika umbo kuliko paka kama vile panya na kicheche."

Na Mahanafi wameyaunganisha katika hukmu ya masalio yaliyoachwa na mbwa na nguruwe masalio ya maji ya mlevi anayokunywa mara tu baada ya kunywa pombe, na masalio ya maji anayokunywa paka mara tu baada ya kumla panya. Na masalio ya wanyama wanaokula nyama, kama vile simba, mbwa mwitu, duma, chui, mbweha na fisi. (Ibnu Abidiin Juz. 1, uk. 156).



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 48 2/1/2017 3:51:41 PM

Na Maimamiyya wamesema: "Masalio ya wanyama walio najisi kama vile mbwa na nguruwe ni najisi. Na masalio ya mnyama aliye tohara ni tohara, sawa awe analiwa au haliwi, yaani masalio ya mnyama yeyote yanafuata hali ya mnyama mwenyewe, kama mnyama huyo ni tohara nayo yatakuwa tohara, na kama ni najisi basi nayo ni najisi."

Na Maliki wamesema: "Masalio ya mbwa na nguruwe ni tohara na inaruhusiwa kutawadha kwa maji hayo na hata kunywa vilevile." (*Al-Mughniy* cha Ibn Quddamah Juz. 1, uk. 47 chapa ya tatu).

## HUKMU ZA KWENDA HAJA

Mashafi, Maliki na Mahanbali wameafikiana kuwa si haramu kuelekea Kibla wala kukipa mgongo wakati wa kujisaidia ndani ya jengo au mwituni kunapokuwapo kitu kinachozuia kati ya mtu na Kibla. Kisha wametofautiana ikiwa mtu anajisaidia mwituni bila ya kuwepo sitara, Mashafi walisema: Si haramu; na hivyo ndivyo wanavyosema Mahanbali. Na Maliki wamesema ni haramu; na Mahanafi wamesema: "Ni makuruhu kwa uzito wa makuruhu iliyo haramu, kuelekea au kukipa mgongo Kibla wakati wa kujisaidia uwapo ndani ya jengo au mwituni." (Kitabu *Fiqh A'lal Madhaahibl Arbaa*, Juz. 1, mlango wa kwenda haja.)

Maimamiyya wamesema: "Ni haramu kuelekea Kibla au kukipa mgongo wakati wa kujisaidia, iwe ni ndani ya jengo au peupe, iwe pana kizuizi au hapana."

Na wote wameafikiana kuwa maji yanayotwaharisha huondoa najisi kutoka kwenye matokeo ya mikojo au mavi. Na madhehebu manne wamesema "Mawe hutosha kutwaharisha sehemu hizo mbili."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 49 2/1/2017 3:51:41 PM

Na Maimamiyya wamesema: "Mawe hayatoshi kutwaharisha matokeo ya mikojo isipokuwa maji pekee, ama mahali panapotokea haja kubwa mtu ana hiyari ima kuosha kwa maji au kupangusa kwa mawe matatu au tambara lililo tohara, kama kinyesi chenyewe hakikusambaa kando ya matokeo yake, na kama si hivyo hapana budi maji yatumike."

Na katika kupangusa kwa kutumia mawe ni lazima ikamilike idadi ya mawe matatu kwa Mashafi na Maimamiyya na Mahanbali hata kama sehemu hiyo itatakata kabla ya jiwe la tatu.

Na Maliki na Mahanafi wamesema: "Hakuna ulazima wa kukamilika idadi maalumu, bali muhimu zaidi ni kutakata mahali palipotokea haja." Kama ambavyo Mahanafi nao wameruhusu kuondoa najisi kutoka katika njia mbili zinazotokea najisi kwa kutumia kimiminiko chochote kilicho tohara kisichokuwa maji.

## VYENYE KUTWAHARISHA

**Maji halisi:** Kwa itifaki ya madhehebu yote haya ni tohara yanayotoharisha.

**Vimiminika visivyokuwa maji**: Vimiminika ambavyo vimekamuliwa kutokana na matunda fulani kama vile siki na maji ya marashi, hivi hutwaharisha kwa Mahanafi peke yao.

**Ardhi**: Hutwaharisha tumbo la unyayo na viatu kwa kutembea juu yake (juu ya ardhi) au kujipangusa kwa hiyo ardhi, lakini kwa Maimamiyya na Mahanafi ni sharti najisi iondoke.

**Jua**: Maimamiyya wamesema: "Jua hutwaharisha ardhi na vitu vinginevyo kati ya vitu visivyohama, kama miti na vilivyoko juu yake ikiwa ni pamoja na matunda na majani. Na vile vile mimea,



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 50 2/1/2017 3:51:41 PM

majumba na vigingi, na hata majamvi na mikeka ambayo ni miongoni mwa vitu ninavyohamishwa isipokuwa mabusati na madawati." Na wameweka sharti kwamba ukaukaji huo utokane na jua tu peke yake bila ya kuingiliwa na upepo.

Mahanafi wamesema: "Kukauka (ukavu) hutwaharisha ardhi na miti, sawa kukauka huko kuwe kumepatikana kutokana na jua au upepo."

Na Mashafi, Maliki na Mahanbali wameafikiana kuwa ardhi haitwahariki kwa jua wala kwa upepo, bali hapana budi imwagiwe maji juu yake, na wametofautiana katika jinsi ya kuitwaharisha.

**Mgeuko:** Nako ni kugeuka uhakika wa kitu fulani hadi kwenye uhakika mwingine, kama vile kugeuka damu ya paa kuwa miski, na kitendo hicho ni miongoni mwa mambo yenye kutoharisha kwa mujibu wa madhehebu yote.

**Moto:** Mahanafi wamesema: "Kuiteketeza najisi kwa moto hutwaharisha, lakini kwa sharti la kuondoka kiini cha najisi." Na pia wamehukumu kuwa tope lililonajisika hutwaharika pindi linapokauka na kuwa udongo mkavu; na pia mafuta yanapokuwa sabuni.

Na Mashafi na Mahanbali wamesema: Moto si katika vinavyotwaharisha, na wamepindukia katika hilo pale waliposema: "Hata jivu la najisi na moshi wake pia ni najisi."

Maliki wamesema: "Jivu la najisi ni tohara na moshi wake ni najisi."

Na Maimamiyya wamesema: "Moto hauna nafasi yoyote katika kutwaharisha, kwa sababu kipimo katika kutwaharisha ni kupatikana mgeuko na mabadiliko, hivyo kama kuni zitageuka na kubadilika kuwa jivu huwa tohara. Na maji yaliyonajisika yakichemshwa basi



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 51 2/1/2017 3:51:41 PM

ule mvuke unaotokana nayo ni tohara. Lakini kuni zinapobadilika na kuwa makaa, na udongo unapofanywa bunguu au chungu, hali ulikuwa umenajisika basi huendelea kuwa ni najisi, kwa sababu ya kutopatikana mgeuko wa tabia.

**Kuitia dawa ngozi:** Mahanafi wamesema: "Kuitia dawa ngozi ya mzoga kunatwaharisha, na kila ngozi iliyonajisika huwa tohara inapotiwa dawa ya ngozi, isipokuwa tu ngozi ya nguruwe. Ama ngozi ya mbwa inapotiwa dawa ya kuondoa vinyamanyama na manyoya huwa tohara inayofaa kusalia juu yake. (*Fiqhu alal Madhahibul Arbaa*, Juz. 1, mlango unaohusu kuondoa najisi.)

Mashafi wamesema: Kuitia dawa ngozi kunatwaharisha ngozi yoyote ile isipokuwa ngozi ya mbwa na nguruwe, hizo hazitwahariki kwa kuzitia dawa ya kusafisha ngozi. Lakini Maimamiyya, Maliki na Mahanbali hawakuhisabu utiaji dawa kwenye ngozi kuwa ni miongoni mwa vitu vinavyotoharisha, isipokuwa ni kwamba Mahanbali wanaruhusu kutumia ngozi iliyotiwa dawa katika matumizi yasiyohusisha kimiminika ambapo huwa haiwezekani najisi kuhama.

**Kupura**: Mahanafi wamesema: Inapopurwa pamba iliyonajisika hutwaharika.

**Kutumia**: Mahanafi wamesema: "Zinaponajisika baadhi ya ngano au mfano wake, na ikatokea zikatumika kwa kuliwa au kutolewa hiba au kwa kuuzwa kwa kiasi kama kile kilichonajisika, basi ngano iliyobaki huwa imetoharika." (*Ibnu Abidiin* Juz. 1, uk. 199).

**Kusugua:** Mahanafi wamesema: Manii hutoharika pindi yanapoondoka kwa kusugua bila kuhitaji maji.

**Kupangusa:** Mahanafi wamesema: Kitu kinapokuwa ni kigumu kisichofyonza maji kama vile chuma, shaba na kioo hutwaharika



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 52 2/1/2017 3:51:41 PM

mahali palipo na najisi kwa kupapangusa tu, bila ya kulazimu kutumia maji.

Na Maimamiya wamesema: "Kuondoa kwa namna yoyote ile iwayo najisi iliyo juu ya mwili wa mnyama hutosha kutwaharisha mwili huo. Ama vyombo, nguo na mwili wa mwanadamu ni lazima vitwaharishwe kwa maji baada ya kuondoka kiini cha najisi."

**Mate**: Mahanafi wanasema; "Linaponajisika titi au vidole hutwahirika vinaponyonywa mara tatu." (*Ibnu Abidiin*, Juz. 1, uk. 215). `

**Kuchemka**: Wamesema Mahanafi: Yanapochemshwa kwa moto mafuta au nyama iliyonajisika huwa tohara. Na baadhi ya wanavyuoni wa Kiimamiyya wamesema: "Zinapochemshwa zabibu mbichi hunajisika, na zinapochemshwa hadi zikapungua theluthi mbili kutokana na huko kuchemshwa hapo hutwaharika."

## YANAYOWAJIBISHA KUTAWADHA NA YANAYOTENGUA WUDHU

### Mkojo, haja kubwa na kutokwa na upepo (ushuzi):

Waislamu wa madhehebu yote wameafikiana kwamba kutokwa na mkojo (kukojoa) na haja kubwa kupitia kwenye njia mbili, na kutokwa na upepo (ushuzi) kupitia mahali pa kawaida, hutengua wudhu.

Ama kutokwa na mdudu, changarawe, damu na usaha hutengua wudhu kwa Mashafi, Mahanafi na Mahanbali. Lakini kutokwa na vitu hivyo hakutengui wudhu kwa Maliki inapokuwa vitu hivyo vimezalika kutoka matumboni mwa mtu, lakini kama mtu amemeza kijiwe kisha kikatoka kupitia njia ya kawaida ya haja, hapo wudhu hutenguka.

Na Maimamiyya wamesema: "Kijiwe au changarawe hakitengui wudhu ila tu kinapotoka hali ya kuwa kimetapakaa (kimechanganyika na) haja."

**Madhii na Wadhii:** Vinatengua wudhu kwa madhehebu manne, lakini kwa Maimamiyya havitengui.

Maliki wamemtoa katika hukmu hiyo mtu ambaye ana ada ya kutokwa na madhii muda wote. Huyu kwao hawajibiki kutawadha yanapomtoka.

**Kutokwa na akili:** Mtu anapotokwa na (fahamu) akili kwa kulewa, wazimu au kuzimia au kwa kifafa wudhu wake hutanguka kwa itifaki ya madhehebu yote.

Ama kulala, Maimamiyya wamesema: "Kunatengua wudhu kunapozidi kiasi cha kuushinda moyo, masikio na macho, kwa namna ambayo aliyelala hatoweza kuwasikia walio kando yake wanaposema au alikuwa akiyasikia maneno yao lakini bila ya kuyafahamu, au kwa kutoweza kumuona yeyote aliye mbele zake kati ya watu, bila ya kutofautisha wakati akiwa amelala alikuwa amelala chali, au kasimama au kakaa chini (kitako).

Na kauli ya Mahanbali inakaribiana sana na kauli hiyo ya Maimamiyya. Nao Mahanafi wamesema: "Mtu aliyetawadha akilala kwa kujinyoosha kiubavu au kwa kuegemea moja ya makalio yake, wudhu wake hutenguka. Na anapolala hali ameketi kwa kujitegemea au hali amesimama au amerukuu au amesujudu wudhu wake hautenguki, hivyo kama mtu atalala ndani ya Swala katika hali yoyote ile ya Swala, wudhu wake hautatenguka hata kama usingizi wake utakuwa mrefu kiasi gani." (*Miizanus Shaaraniy*, mlango unaoeleza sababu za *Hadathi*).

Na Mashafi wamesema: "Matokeo ya upepo yanapokuwa yamebanwa na makalio yake kwa kiasi cha kuwa kama mdomo wa



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 54 2/1/2017 3:51:42 PM

chupa uliofungwa vyema kwa kifuniko, hapo kulala huwa hakutengui wudhu, na inapokuwa ni kinyume cha hivyo wudhu hutenguka.

Nao Mahanafi walitenganisha baina ya usingizi mzito na mwepesi (khafifu) wakasema: "Ikiwa usingizi ni mwepesi hautengui wudhu na hukmu ni hiyo hiyo kwa mtu aliyelala usingizi mzito lakini kwa muda mfupi, kwa sharti kwamba njia ya matokeo ya upepo iwe imefungwa (imezibwa). Lakini anapolala usingizi mzito kwa kipindi kirefu wudhu wake utatenguka, sawa awe kalala kwa njia ambayo njia ya kutokea upepo imezibika au haikuzibika.

**Manii (shahawa):** Hutengua wudhu kwa Mahanafi, Maliki na Mahanbali, lakini kwa Mashafi hayatengui wudhu. Na Shia Imamiyya wamesema: "Manii yanapomtoka mtu humlazimu kuoga tu, bila ya kulazimika kutawadha."

**Kugusana:** Mashafi wamesema: "Mwanamume aliyetawadha akigusana na mwanamke wa kando (ajnabi) bila ya kizuizi (kama nguo) wudhu hutenguka, lakini mwanamke aliyegusa asipokuwa ajinabi kama vile mama au dada hautenguki.

Na Mahanafi wamesema: "Hautenguki wudhu kwa kule tu kugusana, ila yanapotokea mambo mawili kwa pamoja: Kugusana na uume kusimama."

Maimamiyya wamesema kugusana hakuna athari yoyote katika kutengua wudhu, hii ni kuhusu kumgusa mwanamke.

Ama aliyetawadha akiigusa tupu yake ya mbele au tundu ya tupu yake ya nyuma bila ya kizuizi nako hakutengui wudhu wake kwa mujibu wa Maimamiyya na Mahanafi.

Ama Mashafi na Mahanbali wao wamesema: "Kugusa tupu bila ya kizuizi hutengua wudhu moja kwa moja, tena kwa namna yoyote iwayo, iwe ni kwa tumbo la kiganja cha mkono au mgongo wake."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 55 2/1/2017 3:51:42 PM

Ama Maliki wao imepokewa kutoka kwao kuwa wanatofautisha katika kugusa, baina ya kugusa kwa tumbo la kiganja cha mkono, na huko ndiko kunakotengua wudhu, na kugusa kwa mgongo wa kiganja, huko hakutengui. (*Al-Bidayyatu Wan-nihaaya*, cha Ibnu Rushdi – mlango wa vinavyotengua wudhu).

**Kutapika**: Kutapika hutengua wudhu moja kwa moja katika madhehebu ya Mahanbali. Kwa Mahanafi hutengua wudhu pale tu kunapojaa kinywa tele, lakini hakutengui wudhu kwa madhehebu ya Shafi, Imamiyya na Maliki.

**Kutokwa na damu au usaha**: Kutokwa na damu mwilini mahali pasipokuwa tupu ya mbele au ya nyuma, hakutengui wudhu kwa Maimamiyya, Mashafi na Maliki. Ama kwa Mahanafi hutengua wudhu iwapo damu itavuka mahali ilipotokea. Mahanbali nao wamesema: "Damu au usaha vikitoka kwa wingi hutengua wudhu."

**Kucheka kwa ha ha ha:** Hubatilisha Swala kwa ijmai ya Waislamu wote, wala hakutengui wudhu mtu achekapo ndani ya Swala wala nje ya Swala, isipokuwa kwa Mahanafi ndio wanaosema: "Kunapotokea kucheka kwa ha ha ha ndani ya Swala hutengua wudhu, lakini kucheka huko hakutengui wudhu kunapotokea nje ya Swala.

**Kula nyama ya ngamia:** Mtu aliyetawadha akila nyama ya ngamia hutengua wudhu kwa madhehebu ya Mahanafi peke yao.

**Damu ya (ugonjwa) Istihadha -** Amesema mwanachuoni Hilliy katika kitabu kiitwacho '*At-tadhkirah*' naye ni miongoni mwa mafakihi walio wakubwa katika madhehebu ya Imamiyya: "Damu ya Istihadha inapotoka kwa uchache hulazimu kuchukua wudhu, na hivi ndivyo walivyofutu wanavyuoni wetu wote isipokuwa Ibnu Abi Aqil. Na Malik amesema: 'Mwenye damu ya Istihadha halazimiki kutawadha.'"



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 56 2/1/2017 3:51:42 PM

# LENGO LA WUDHU

Mafakihi wamesema: Hadath zimegawanyika katika aina mbili: Hadath ndogo nayo ni ile inayolazimu wudhu peke yake. Na hadath kubwa, nayo imegawanyika katika aina mbili: Ile inayolazimu kuoga tu, na ile inayolazimu kuoga na wudhu pamoja. Yatakuja maelezo yake kwa ufafanuzi hivi punde, na hadath ndogo kwa mujibu wa sharia inamzuwilia mtu kufanya mambo yafuatayo:

**1.** Kusali Swala ya faradhi na ya Sunna kwa itifaki ya madhehebu yote. Ama Maimamiyya hapa walijitenga na madhehebu mengine kwa kuiondoa Swala ya jeneza katika hukmu hiyo. Wakasema hailazimu tohara (wudhu) unapotaka kuswali Swala ya jeneza, lakini ni sunna, kwa sababu Swala ya jeneza ni dua (tu kama dua nyinginezo), si Swala ya kihakika yenye rukuu na sijda. Na maelezo ya Swala yatakuja mahala pake (yaani mahala pa Swala ya jeneza).

**2.** Kutufu: Nako ni kama Swala, si ruhusa kutufu bila ya tohara kwa Maliki, Mashafi, Maimamiyya na Mahanbali, hiyo ni kwa mujibu wa Hadith tukufu: "Kutufu Kaaba ni (kama) Swala.." Mahanafi wamesema: "Inasihi kutufu Kaaba akiwa na hadath japokuwa atakuwa amefanya dhambi."

**3.** Sijda ya kisomo: Tohara ni wajibu kwa madhehebu manne wakati wa kuitekeleza, na ni mustahabu kwa Maimamiyya.

**4.** Kugusa msahafu: Wanavyuoni wa madhehebu yote wameafikiana kwamba haifai kugusa maandishi ya Qur'ani ila kwa tohara, na wamekhitilafiana juu ya mtu mwenye hadath ndogo je anaruhusiwa kuandika Qur'ani na kuisoma kwa sauti au kwa moyo? Na katika kuigusa kwa kizuizi (kama mfano wa nguo



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 57 2/1/2017 3:51:42 PM

au karatasi) na kuibeba ikiwa ni hirizi? Maliki wamesema: "Si ruhusa kugusa wala kuandika Qur'ani wala kugusa jalada lake hata kama ni kwa kizuizi, lakini anaruhusiwa kuisoma kwa sauti na kwa moyo. Kisha Maliki wametofautiana wao wenyewe kuhusu kuibeba ikiwa hirizi.

Mahanbali wamesema: "Inaruhusiwa kuiandika na kuibeba ikiwa ni hirizi kwa sharti la kuwa kwenye kizuizi (sitara).

Mashafi wamesema: "Si ruhusa kugusa jalada lake na hata linapojitenga mbali na msahafu wenyewe, wala si ruhusa kugusa hata mwangikio wake maadamu ingali imeangikwa, hata hivyo inaruhusiwa kuiandika, kuichukua ikiwa ni hirizi, kama ambavyo pia inaruhusiwa kugusa Qur'ani iliyonakishiwa kwenye nguo."

Na Mahanafi wamesema: "Si ruhusa kuiandika (bila ya tohara) wala kuibeba hata kama imeandikwa katika lugha ya kigeni, na inajuzu kuisoma kwa moyo."

Na Maimamiyya wamesema: "Ni haramu kugusa maandishi ya Kiarabu iwapo ni bila ya kizuizi, sawa maandishi hayo yawe katika Qur'ani (mas'hafu) au katika kitu kingine, lakini si haramu kusoma Qur'ani, kuiandika na wala kuibeba ikiwa ni hirizi, wala si haramu kugusa maandishi (ya Qur'ani) yaliyoandikwa kwa lugha isiyokuwa ya Kiarabu, isipokuwa Jina takatifu la Mwenyezi Mungu 'Allah', ni haramu kwa mtu mwenye hadath kuligusa jina hilo katika lugha yoyote ile, na popote liwapo, sawa iwe ni ndani ya Qur'ani au penginepo.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 58 2/1/2017 3:51:42 PM

# MAMBO YALIYO WAJIBU KATIKA WUDHU

## 1. Kutia niya:

Nayo ni kukusudia kufanya kitendo kwa dhamira ya utii na kufuata amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kwa hakika maimamu wa madhehebu yote wameafikiana kwamba niya ni faradhi katika wudhu, na kwamba mahali pake ni wakati wa kufanya kitendo.

Mahanafi wamesema: "Kwa hakika kusihi kwa Swala hakutegemei kutawadha kwa kutia niya, hivyo kama mtu ataoga kwa lengo la kupoza mwili tu, au kwa ajili ya unadhifu na viungo vyake vyote vinavyolazimu kuoshwa katika wudhu vikaenea maji na kisha akaswali, Swala yake itasihi, kwa sababu makusudio ya wudhu ni tohara, na imeshapatikana." Katika hukmu hiyo wameondoa masalio ya maji aliyokunywa punda au mvinyo wa tende, ambapo wamesema katika hali hii niya ni lazima. (Ibnu Abidiin Juz. 1, uk. 76).

## 2. Kuosha uso:

Na makusudio ya kuosha hapa ni kueneza maji juu yake, na mara moja ndiyo wajibu, na mpaka wake wa urefu ni kuanzia mwisho wa nywele za kichwani hadi mwisho wa kidevu. Na Mashafi wamesema: "Yapasa kuosha kilicho chini ya kidevu vilevile." Na mpaka wake kwa upana kwa Maimamiyya na Maliki ni mapana yaliyopo kati ya ncha ya kidole cha katikati na ncha ya kidole gumba. Na kwa madhehebu yaliyobakia ni kuanzia ndewe ya sikio moja hadi ndewe ya sikio la pili.

Na rai ya Maimamiyya ni kwamba yapasa kuanzia sehemu ya juu wakati wa kuosha uso, na kwamba haijuzu kuosha kinyume chake. Na maimamu wa madhehebu manne wamesema: "Lililowajibika ni kuosha uso tu kwa namna yoyote iwavyo, iwe ni kuanzia juu kwenda chini, au kuanzia chini kwenda juu."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 59 2/1/2017 3:51:42 PM

### 3. Kuosha mikono:

Wote wameafikina kuwa kuosha mikono pamoja na kongo zake mbili mara moja ni wajibu.

Maimamiyya waliendelea hadi kusema kuwa: "Inapasa wakati wa kuosha mikono ianzie kwenye kongo za mikono, wakabatilisha kuosha kinyume cha hivyo. Pia waliwajibisha kuanza kuosha mkono wa kulia kabla ya mkono wa kushoto. Madhehebu yaliyobakia yanasema: "Kinachopasa ni kuosha hiyo mikono vyovyote inavyowezekana. Na kuutanguliza mkono wa kulia, na kuanzia vidoleni kupeleka kwenye kongo ni bora zaidi.

### 4. Kupaka kichwa

Mahanbali wamesema: "Katika kupaka kichwani ni lazima kupaka kichwa chote pamoja na masikio mawili; na kwao wao kuosha kwatosheleza badala ya kupaka, kwa sharti tu la kuupitisha mkono juu ya kichwa."

Maliki wamesema: "Inapasa kupaka kichwa chote bila ya masikio."

Na Mashafi wamesema: "Yapasa kupaka sehemu ya kichwa, angalau kwa uchache tu, pia hutosheleza kuosha (kichwa) au kunyunyiza maji juu yake badala ya kupaka.

Maimamiyya wamesema: "Kupaka ni lazima kufanywe katika sehemu ya mbele ya kichwa, na hutosha kunapofanyika kwa uchache sana kwa kiasi ambacho yatosha kuitwa kupaka, na kamwe haijuzu kuosha wala kunyunyiza maji badala ya kupaka, na vilevile katika kupaka waliwajibisha kuwe ni kwa unyevunyevu uliobakia mikononi wakati wa kuosha viungo vya wudhu vilivyotangulia, na kama atachota maji mapya akapaka kwa maji hayo, basi wudhu utabatilika.

Ama madhehebu manne wao wamewajibisha kupaka kwa kutumia maji mapya (*Al-Mughnii* cha Ibnu Quddamah. Kifungu kinachoelezea kupaka kichwa, na *Tadhkirah* cha mwanachuoni Hilly).

Ama kupaka juu ya kilemba, Mahanbali wameruhusu kwa sharti kwamba, sehemu ya kilemba hicho iwe imefikia chini ya taya.

Na Mahanafi, Maliki na Mashafi wamesema: "Yajuzu kupaka juu ya kilemba panapokuwapo na udhuru, ama bila ya udhuru haijuzu." Nao Maimamiyya wamesema: "Haijuzu kwa vyovyote vile kupaka juu ya kilemba kwa ushahidi wa kauli yake Mwenyezi Mungu: 'Na pakeni sehemu katika vichwa vyenu' Na kilemba hakiitwi kichwa."

## 5. Miguu miwili:

Maimamu wa madhehebu manne wamesema inapasa kuosha miguu miwili pamoja na vifundo vyake viwili mara moja.

Na Maimamiyya wamesema: "Wajibu ni kupaka miguu miwili kwa unyevunyevu wa wudhu uliyobakia kwenye mikono, kuanzia juu ya vidole hadi kwenye vifundo, na iwe ni juu ya nyayo mbili (si chini yake). Na kwa madhehebu yote yaswihi kutanguliza mguu wa kushoto kabla ya mguu wa kulia, lakini ni kinyume na ihtiyat kwa Maimamiyya, na ni kuacha iliyo aula na bora zaidi kwa madhehebu manne.

Tofauti ya kupaka ilizuka kutokana na kila mmoja alivyoifahamu Aya ya wudhu ambayo ni Aya ya sita katika Surat Al-Maidah:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِذَا قُمۡتُمۡ إِلَى ٱلصَّلَوٰةِ فَٱغۡسِلُواْ وُجُوهَكُمۡ وَأَيۡدِيَكُمۡ إِلَى ٱلۡمَرَافِقِ وَٱمۡسَحُواْ بِرُءُوسِكُمۡ وَأَرۡجُلَكُمۡ إِلَى ٱلۡكَعۡبَيۡنِ ....."

**"Enyi mlioamini, mnaposimama kwa ajili ya kutaka kuswali, basi osheni nyuzo zenu na mikono yenu hadi kwenye kongo (visuku suku), na pakeni vichwa vyenu na miguu yenu hadi kwenye vifundo viwili." Ambapo Aya hii husomeka kwa '*Khafdhi'* katika (*Arjuli*) na kwa *nasbu*, kwa hiyo wale wanaosema miguu ipakwe badala ya kuoshwa wameifanya '*Arjuli'* (Miguu) ni '*Atfu'* ya '*ru-uusi'* (inaungana na kichwa) na kutosha, na hivyo '*jardi'* (*kasra*) na kulingana na mahala ilipo inakuwa haijuzu kuisoma kwa '*nasbu'* (*fataha*) kwa sababu kila neno '*majruuru'* (lililo na kasra) huwa limetokana na utenda kazi ulioingia uasi kwa kuingiliwa na *harfu jarri* ambazo ni *bee*).**

Na wanaosema kuosha miguu, wana hoja yao ya kusema kwamba: Neno '*arjuli'* (miguu) limeribizwa '*kasra'* kutokana na kuwa jirani ya '*ruusi'* ambayo imelazimika kuingiliwa na '*kasra'* kwa kuingiliwa na '*bee'* na imenasibishwa (katika irabu wanaisema ina fataha) ikiwa na '*atfu'* ya '*aydi'* ya (mikono) ambayo ni fataha (kwa sababu ni *mafuul* ya kuosha). *Fagh-siluu*… nasi twamuachia mtu mwenyewe anayetaka kuujuua uhakika wa Aya hii akaiangalie kwenye tafsiri ya Qur'ani ya Imam Fakhrud-diin Raziy.

Na madhehebu manne yamejuzisha kupaka juu ya 'khoffu' mbili na juu ya soksi badala ya kuosha miguu.

Maimamiyya wamesema: "Haijuzu kupaka juu ya khoffu (aina ya viatu) wala juu ya soksi, kutokana na kauli ya Imam Ali: "Mimi sijali (sitilii maanani) kupaka juu ya khoffu au kupaka juu ya mgongo wa ngamia aliyeko jangwani."

**Mpangilio:**

Nako ni kufuata kama ilivyotaja Qur'ani: Kuanza kuosha uso, kisha mikono miwili, kisha kichwa na mwisho miguu miwili, na kufuata mpangilio ni lazima na sharti la kuswihi kwa wudhu kwa madhehebu ya Maimamiyya, Mashafi na Mahanbali.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 62 2/1/2017 3:51:42 PM

Ama Mahanafi na Maliki wao wamesema si wajibu kutawadha kwa mpangilio, hivyo inaruhusiwa wakati wa kutawadha, kuanzia kuosha miguu miwili na kumalizia usoni.

**KUFUATANISHA:**

Nako ni kufululiza katika kuosha viungo kwa kuosha kiungo cha pili mara tu baada ya kumalizia kuosha kiungo kilichotangulia, na huku kufululiza katika kuosha viungo wakati wa kutawadha ni wajibu kwa Maimamiyya na Mahanbali.

Maimamiyya waliweka sharti la ziada baada ya hilo la kufuatanisha, kuwa kiungo kilichotangulia kuoshwa kisikauke kabla ya kuanza kuosha kiungo kinachofatia, na kama kiungo kilichotangulia kuoshwa kitakauka kabisa kabisa, basi wudhu utabatilika na itabidi kurudia kutawadha tena.

Na Mahanafi na Mashafi wamesema: "Haipasi kufuatanisha katika kutawadha, lakini hata hivyo ni makruhu kutenganisha kati ya kuosha viungo pasipo udhuru wa kufanya hivyo, lakini kama upo udhuru basi karaha huondoka."

Maliki wamesema: Hakuna ulazima wowote wa kufuatanisha isipokuwa pale anapotanabahi mwenye kutawadha, na anapokuwa hajatokewa na jambo lisilokuwa katika hesabu zake, kwa mfano lau yatamwagika maji yake ambayo alikuwa ameyaandaa kwa kutawadhia wakati akiwa anaendelea kutawadha, hivyo basi kama ataosha uso wake, na akasahau kuosha mikono, au yalimalizika maji ambayo yalikuwa yakimtosha kujitwahirisha kulingana na imani yake (ikambidi kutafuta maji mengine hadi viungo vilivyotangulia vikakauka) atakwenda kutafuta maji mengine na ataunga mbele na kuendelea na viungo vilivyobakia, hata kama utapita muda mrefu katika kuyapata maji.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 63 2/1/2017 3:51:42 PM

# MASHARTI YA WUDHU

Wudhu na masharti yake, miongoni mwa masharti ya wudhu ni maji yawe ni halisi na yaliyo tohara na yawe hayakutumika kabla kwa kuondolea najisi au hadath kama tulivyoelezea huko nyuma katika mlango wa uchambuzi wa maji. Na miongoni mwa masharti yake ni kutokuwa na sababu inayozuia kutumia maji kwa maradhi au kuyahitajia sana kwa (uhai wa viumbe watakatifu).

Na miongoni mwake ni utohara wa viungo vya wudhu, na kutokuwapo juu ya mwili kitu kinachozuwia maji kufika kwenye ngozi, na kupatikane wasaa, na hili la wasaa tutalifafanua kirefu katika uchambuzi wa tayammamu, na masharti yote haya au mengi kati ya haya ni mahali penye mwafaka baina ya madhehebu yote.

Na Maimamiyya wana masharti mengine zaidi ya hayo, nayo ni kuwa maji, chombo, mahali panapotiwa maji na mahali pa kutawadhia pawe ni pa halali (mubaha) si pa kunyang'anya, na lau kimoja tu kati ya vitu vilivyotajwa kitakuwa ni cha unyang'anyi wudhu hubatilika; lakini kwa madhehebu mengine wudhu huswihi, lakini anayetawadha hupata dhambi. (*Ibnu Abidiin* Juz. 1, uk. 128 na pia *Sharhul-Muhadh-dhab* Juz. 1, uk. 251).

## SUNNA ZA WUDHU:

Sunna za wudhu ni nyingi mno, miongoni mwazo ni kuanza kuosha viganja vya mikono, kusukutua na kutia maji puani, ila Mahanbali wamewajibisha viungo hivyo.

Pia miongoni mwa Sunna za wudhu ni kupaka masikio mawili, hii kwa Mahanbali ni faradhi. Nao Maimamiyya wakasema: "Haijuzu kupaka masikio."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 64 2/1/2017 3:51:42 PM

Na katika Sunna za wudhu ni kutangulia kupiga mswaki na kuelekea Kibla wakati wa kutawadha, na kuomba dua iliyopokewa (kutoka kwa Mtume baada ya kutawadha), na kuosha viungo vyote mara mbili au tatu kwa madhehebu manne.

Na Maimamiyya wamesema: "Josho la kwanza ni wajibu, la pili ni Sunna, na la tatu ni bidaa (ni uzushi), na anayefanya hivyo kwa kusudi ya kuwa ni sharia basi atapata dhambi, ama iwapo ameosha mara tatu bila ya kukusudia kuwa ni sharia hapati dhambi, lakini wudhu hubatilika kama atapaka kwa maji ya josho hilo la tatu. (*Misbaahul-Faqiih*, cha Agha Ridhaa Al-Hamudaniy); na bado ziko sunna nyingine mbali ya hizo zilizotajwa katika vitabu vilivyoeleza kwa kirefu.

## KUWA NA SHAKA YA TOHARA NA HADATH

Anayekuwa na uhakika wa tohara na kisha akapatwa na shaka ya je alipatwa na hadath au la, basi yu tohara. Na aliye na yakini kuwa alipatwa na hadath na ana shaka na tohara basi ni mwenye hadath kwa mujibu wa kufuata yakini na kutupilia mbali shaka, kanuni itokanayo na Hadith inayosema: "Kabisa haiwezekani kuitangua yakini kwa shaka bali yakini hutanguliwa na yakini."

Na kati ya madhehebu hakuna aliyekhalifu wenzake isipokuwa Maliki ndio waliosema: "Mtu akiwa na yakini na tohara, na akawa na shaka na hadath basi yu tohara," na wala wao hawakutofautisha kati ya hali mbili hizo.

Na inapotokea mtu ana yakini na hadath na tohara, lakini hajui kilichotangulia ni kipi kati ya viwili hivyo ili apate kujengea juu yake, mtu huyo huwa ni mwenye tohara kwa mujibu wa madhehebu ya Mahanafi, na kwa mujibu wa wahakiki miongoni mwa Maimamiyya mtu huyo ni mwenye hadath.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 65 2/1/2017 3:51:42 PM

Na Mashafi na Mahanbali wamesema: "Atashikilia hali iliyo dhidi ya hali iliyotangulia, ikiwa mwanzo alikuwa ni mwenye tohara basi hivi sasa ni mwenye hadath, na kama alikuwa ni mwenye hadath basi hivi sasa ni mwenye tohara."

Na hapa pana kauli ya nne nayo ni kushikilia hali ile ile iliyotangulia na kuhukumu kuwa imeporomoka athari ya hadath na tohara zilizopo, hiyo ni kwa sababu dhana mbili zote zi zenye kulingana, na hivyo zinapingana na zinaanguka zote mbili, na hapo inachukuliwa hali ya kwanza. Na kidini njia iliyo karibu zaidi ya kujitoa shakani ni kurudia kujitwaharisha kwa hali yoyote iwayo, sawa awe anaijua hali iliyotangulia (kabla ya kuzukiwa na shaka) au haijui.

Maimamiyya na Mahanbali wamesema: "Anapopatwa na shaka anayetawadha juu ya kuosha kiungo au kupaka kichwa chake, iwapo bado yumo kwenye matendo ya kutawadha, basi atarudia kwenye kiungo alichokitilia shaka na vinavyofuatia, na kama shaka yake imemzukia baada ya kumaliza kutawadha na kuondoka mahali alipokuwa akitawadha basi hatarudi nyuma bali ataendelea tu, kwa sababu hiyo ni shaka iliyozuka katika ibada baada ya kumaliza.

Na mwanachuoni Al-Hilliy alinakili kauli ya baadhi ya mafakihi wa Kishafi katika kitabu chake '*Tadhkirat'* kuhusu shaka, kuwa wamesema: 'Hakuna tofauti kati ya shaka inayomzukia mtu akiwa yumo ndani ya kitendo au baada ya kumaliza, bali katika hali zote mbili ni wajibu kurudia pale palipozusha shaka kisha aendelee kwenye viungo vinavyofuata."

Na Mahanafi wamesema: "Huchunguzwa kila kiungo kivyake, akipatwa na shaka kabla ya kurukia kiungo kingine atakirudia, kinyume na hivyo hatakirudia. Kwa mfano mtu anayepatwa na shaka katika kuosha uso kabla hajaanza kuosha mkono, atarudia kuosha



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 66 2/1/2017 3:51:42 PM

uso kwanza halafu aendelee kuosha mkono, na kama ameshaanza kuosha mkono basi ataendelea bila ya kugeuka. Na mafakihi wote waliafikiana kuwa, hana hukumu ya shaka mtu ambaye ni mwingi wa shaka, kwa maana ya kwamba mtu mwenye ugonjwa wa wasiwasi shaka yake haizingatiwi. Linalopasa kwake ni kuendelea na amali yake katika hali zote.

## KUOGA

**Majosho ya wajibu yako ya aina kadhaa:**

**1. Janaba**

**2. Hedhi**

**3. Nifasi**

**4. Maiti ya Mwislamu.**

Na mambo haya manne wamekubaliana wote. Ama Mahanbali waliongeza aina ya tano nayo ni kafiri anaposilimu. Na Mashafi na Maimamiyya wamesema: "Kafiri anaposilimu hali ya kuwa ana Janaba humpasa kuoga josho la Janaba, si la Uislamu (la kusilimu), na iwapo hakuwa na Janaba huwa haimpasi kuoga.

Nao Mahanafi wamesema: "Haimpasi kuoga kwa hali yoyote ile, awe ni mwenye janaba au si mwenye janaba." (*Al-Mughny* chaz Ibnu Quddamah Juz. 1, uk. 207).

Na ukiachana na majosho hayo manne ya mwanzo, Maimamiyya wameongeza majosho mengine mawili, hayo ni: Josho la mwenye Istihadha na la mtu aliyemgusa maiti, kwa hakika wao (Maimamiyya) wamewajibisha kuoga kwa mtu aliyegusa maiti baada ya kupoa (kuwa baridi huyo maiti) mwili wake kutokana na kifo, awapo bado hajatwaharishwa kwa kuoshwa.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 67 2/1/2017 3:51:42 PM

Yatakuja huko mbele maelezo yake kwa kirefu, na kutokana na ongezeko hili la Maimamiyya inabainika kwamba idadi ya majosho ya faradhi ni manne kwa Mashafi na Mahanafi na ni matano kwa Mahanbali, na Maliki, na ni sita kwa Maimamiyya.

## KUOGA JANABA:

Janaba ambalo mtu humpasa kuoga hupatikana kwa mambo mawili:

**1.** Kushusha manii usingizini au bila ya kuwa usingizini. Mashafi na Maimamiyya wamesema: "Yanaposhuka manii, hulazimu kuoga bila ya kuwepo kutofautisha kati ya kushuka kwake, iwe ni kwa matamanio au bila ya matamanio." Lakini Mahanafi na Maliki na Mahanbali wamesema: "Haimpasi mtu kuoga ila tu unapopatikana utamu (ladha) wa kutoka manii, ama yanapotoka kwa kupigwa, au kwa ajili ya baridi au kwa maradhi bila ya uhusiano wowote na matamanio hakuna ulazima wa kuoga."

Ama manii yanapotoka kwenye uti wa mgongo au mifupa ya kifua cha mwanamke na yasitoke hadi nje, huwa haipasi kuoga, isipokuwa kwa Mahanbali.

**Tanzuo**: Lau mtu ataamka kutoka usingizini akaona uchepechepe (maji maji) asiouelewa uhakika wake, kuwa ni manii au madhii, Mahanafi wamesema: "Inampasa kuoga." Mashafi na Maimamiyya: "Haimpasi kuoga kwa kuwa ana yakini na utohara, na ana shaka ya hadath."

Mahanbali wamesema: "Iwapo kabla ya kulala kwake alihisi au kuwa na fikra ya kusikia ladha (ya kutoka shahawa) haimpasi kuoga, na kama haukutanguliwa usingizi wake na kitu kinacholazimisha kusikia ladha, basi ataoga kutokana na huo uchepechepe usiofahamika."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 68 2/1/2017 3:51:42 PM

**2.** Ni kugusana tupu mbili, nako ni kuingiza ndani ya tupu ya mwanamke kichwa cha dhakari (sehemu iliyopashwa tohara) au sehemu tu iliyokatwa ya dhakari kuiingiza ndani ya tupu moja kati ya tupu mbili; na wameafikiana kuwa humlazimu kuoga hata kama hakushusha manii. Lakini walikhitilafiana katika masharti yake, na kuhusu je ni kila kuingiza hulazimu kuoga, au ni kuingiza kwa namna maalum ndiko kunakowajibisha kuoga?

Mahanafi wamesema: "Kuoga ni wajibu yanapopatikana masharti yafuatayo, sharti la kwanza: Ni kubaleghe, kama aliye baleghe ndiye aliyefanyiwa kitendo na aliyefanya si baleghe, au aliyefanya kitendo ni baleghe na aliyefanyiwa si baleghe, kuoga (janaba) ni wajibu kwa aliye baleghe tu pekee; na wala si wajibu kwa wote wawili iwapo ni watoto wadogo.

Sharti la pili: Ni kutokuwepo kizuizi kigumu ambacho huzuia kupatikana joto la mahali hapo (utupu).

Sharti la tatu: Ni kuwa, huyo aliyeingiliwa awe ni mwanadamu aliye hai, kwa kuwa si wajibu kuoga kwa kumwingilia mnyama au maiti."

Maimamiyya na Mashafi wamesema: "Kwa hakika kule kuingiza tu dhakari, iwe ameingiza sehemu yote ya kichwa au baadhi yake, hutosha kulazimu kuoga Janaba bila ya kuwepo tofauti kati ya aliye baleghe na mtoto ambaye hajabaleghe, na ni wajibu kuoga kwa wote wawili aliyefanya na aliyefanyiwa, panapokuwa na kizuizi au pasipokuwa na kizuizi, sawa iwe kwa kushikwa kwa nguvu au kwa hiari, sawa aliyeingiliwa alikuwa ni mtu hai au maiti, mnyama au mwanaadamu (yote hukmu yake ni sawa)."

Mahanbali na Maliki wamesema: "Hupasa kuoga kwa wote wawili aliyefanya na aliyefanyiwa iwapo hakuna kizuwizi



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 69 2/1/2017 3:51:42 PM

kinachozuia kuhisi ladha. Bila ya kuwepo tofauti kati ya mwanadamu na mnyama. Na ni sawa aliyeingiliwa alikuwa ni mnyama au maiti."

Ama kuhusu hukmu ya aliye baleghe, Maliki wamesema: "Hupasa kuoga (Janaba) kwa mfanyaji anapokuwa ni mtu Mukallaf (baleghe aliye na akili), ama aliyefanyiwa itategemea na kuingiliwa kwenyewe. Ni wajibu kuoga Janaba kwa aliyeingiliwa iwapo aliyemuingilia alikuwa ni mtu baleghe, lakini kama aliyemuingilia alikuwa ni mtoto ambaye hajabeleghe, basi si wajibu kwake kuoga iwapo yeye aliyeingiliwa hakushusha manii."

Na Mahanbali waliweka sharti la kuwa mwanamume asiwe chini ya umri wa miaka kumi, na mwanamke asiwe chini ya umri wa miaka tisa.

## MAMBO YALIYO HARAMU KWA MWENYE JANABA:

Mwenye kuwajibika kuoga Janaba haruhusiwi (kisheria) kufanya mambo yote yaliyo haramu kwa mwenye hadath ndogo, kama kuswali, kutufu, na kugusa maandishi ya msahafu, na zaidi ya hayo ni haramu kwa mwenye janaba kukaa msikitini. Na wameafikiana wote kwamba si ruhusa kwa mwenye janaba kukaa msikitini. Lakini wamekhitalifiana kuhusu kupita ndani ya msikiti, kama mtu mwenye Janaba ataingia kwa mlango mmoja na kutokea mlango wa pili.

Mahanafi na Maliki wamesema: "Haijuzu kupita ndani ya msikiti isipokuwa kwa dharura peke yake.

Mashafi na Mahanbali wamesema: "Yajuzu kupita, lakini bila ya kukaa (hata kidogo)."

Maimamiyya wamesema: "Haijuzu kukaa (mwenye Janaba) wala kupita ndani ya 'Masjidul Haram' na msikiti wa Mtume, na yajuzu kupita bila ya kukaa katika misikiti mingineyo isiyokuwa



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 70 2/1/2017 3:51:43 PM

hiyo miwili, kutokana na Aya hii ya Qur'ani tukufu katika Sura an-Nisaa (4) Aya 43: "Wala mwenye janaba (haifai kukaa ndani ya msikiti) isipokuwa kwa anayepita tu." (yaani msikalie mahali pa kuswalia ndani) ya msikiti isipokuwa kupita tu. Na katika Aya hiyo imetengwa misikiti miwili iliyotangulia kutajwa kwa dalili maalum (hasa).

Ama kuhusu kusoma Qur'ani kwa mwenye Janaba, Maliki wamesema: "Ni haramu kwa mwenye Janaba kusoma kitu chochote katika Qur'ani ila kwa uchache sana inapokuwa ni kwa dhamira ya kujilinda au kutoa dalili," na kauli yao hii ina karibiana sana na rai ya Mahanbali.

Na Mahanafi wamesema: "Haijuzu kabisa, ila tu anapokuwa huyo mwenye Janaba anafundisha kusoma Qur'ani, ataifundisha neno kwa neno."

Mashafi wamesema: "Ni haramu (kusoma Qur'ani) hata kwa herufi moja, isipokuwa anapotaka kuisoma kwa kusudio la dhikri, kama kupiga Bismillahi wakati wa kula chakula."

Na Maimamiyya wamesema: "Si haramu kwa mwenye Janaba kusoma Qur'ani isipokuwa Sura nne zenye sijda za wajibu, na ni haramu kusoma hata sehemu ndogo ya sura hizo, Sura hizo ni *Iqraa*, *An-Najm*, *Hamiim Saj-dah* na *Alif-lam-miim tanziil*. Na yajuzu kusoma Sura nyingine yoyote isipokuwa hizo. Lakini ni karaha kusoma zaidi ya Aya saba. Na huzidi kuwa makruh zaidi anaposoma zaidi ya Aya sabini.

Na Maimamiyya wameongeza (katika mambo yaliyo haramu kwa mwenye Janaba ni) Swaumu ya mwezi wa Ramadhani na Swaumu ya kulipa kwa ambaye alikosa kufunga mwezi wa Ramadhani, wamesema: "Kunapopambazuka asubuhi kwa aliye na Swaumu hali ya kuwa ni mwenye Janaba, Swaumu yake haiswihi anapokuwa



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 71 2/1/2017 3:51:43 PM

kabaki na janaba makusudi au kwa kusahau. Lakini kama atalala wakati wa mchana au usiku, akaamka hali amejiotea, Swaumu yake haibatiliki; na kwa hukmu hii Maimamiyya wamejitenga peke yao mbali na madhehebu mengine.

## YANAYOPASA KATIKA KUOGA JANABA:

Katika kuoga Janaba kuna ulazima wa mambo kama yale yaliyo wajibu kwenye wudhu, kama maji kuwa halisi na utohara wa maji na mwili, na kutokuwepo kitu juu ya mwili kinachozuia maji kufika kwenye ngozi, kama vile ilivyotangulia kuelezewa kwenye mlango wa wudhu; na pia ni wajibu kutia nia, isipokuwa kwa Mahanafi kwani wao hawakuihisabu nia kuwa ni miongoni mwa masharti ya kuswihi kuoga Janaba.

Na madhehebu manne hayakuwajibisha kuoga janaba kwa namna maalum, bali waliwajibisha kuenea maji mwili mzima kwa njia yoyote iwayo, bila ya tofauti baina ya kuanzia juu kuja chini au kuanzia chini kwenda juu.

Mahanafi wameongeza wajibu wa kusukutua na kutia maji puani, wakasema: "Ni mustahabbu kuanza kwa kuosha kichwa kisha upande wa kuume na mwisho upande wa kushoto."

Na Mashafi na Maliki wamesema: "Huwa ni mustahabbu kuoga Janaba kwa kuanzia sehemu ya juu ya mwili kabla ya kuosha sehemu ya chini, isipokuwa tupu tu, ndiyo mustahabbu zaidi kutanguliza kuiosha kabla ya kuosha kiungo chochote kingine."

Na Mahanbali wamesema: "Ni mustahabbu kuanza kuoga kwa kuosha ubavu wa kulia kabla ya kuosha wa kushoto."

Na Maimamiyya wamegawa josho la Janaba katika aina mbili: "Kuoga kwa mpango, na kwa kupiga mbizi. Kuoga kwa mpango ni

mwenye kuoga kujimwagia maji kidogo kidogo, na katika kuoga kwa namna hii wamelazimisha kuanzia kichwa, kisha upande wa kulia na kumazilia upande wa kushoto. Na lau atageuza mfumo kwa kutanguliza cha nyuma akakiweka mbele au cha mbele akakiweka nyuma, josho hubatilika. Na kuoga kwa kupiga mbizi, ni kuuingiza ndani ya maji mengi mwili wote mzima kwa mpigo (mara) mmoja, na lau sehemu moja ya mwili wake itabaki nje bila ya kuzama ndani ya maji, basi haitosihi kuwa kaoga Janaba."

Kwa mujibu wa madhehebu ya Maimamiyya kuoga janaba hutosheleza wudhu, pale waliposema: "Kila kuoga kunahitajia tena wudhuu, isipokuwa kuoga kwa nia ya kuondoa Janaba."

Na Madhehebu manne hawakutofautisha kati ya josho la janaba na majosho mengine, katika suala la kutototesheleza majosho hayo kutenda jambo linalolazimu wudhu.

## HEDHI

Katika lugha ya (kiarabu) ina maana ya mbubujiko au mchuruziko, na katika istilahi ya mafakihi, ni damu ambayo mwanamke huwa na ada ya kuiona (ikitoka) katika siku maalum, na damu hii ina taathira (ambazo humlazimu mwanamke) kuacha kufanya ibada, na (pia) ndicho kipimo kinachotumika katika kuhisabu muda wa eda ya mtalaka. Nayo kwa kawaida damu hii ya hedhi ina sifa zifuatazo: Huwa nyeusi, au nyekundu ya kuiva, na huwa moto, na hutoka kwa msukumo, na kuna wakati damu hii hutoka ikiwa na sifa nyinginezo mbali na hizi tulizozitaja kulingana na makundi na hali za wanawake.

**Miaka ambamo mwanamke huona hedhi:**

Mafakihi wote wameafikiana kwamba damu anayoiona mwanamke kabla hajafikia umri wa miaka tisa haiwezekani kuwa ni damu ya



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 73 2/1/2017 3:51:43 PM

hedhi, bali huwa ni damu ya ugonjwa. Na hata damu anayoiona mwanamke aliyekata tamaa ya kuiona damu ya hedhi kwa sababu ya kupita zaidi ya umri unaoonekana damu hiyo, vilevile si damu ya hedhi. Na walikhitilafiana katika umri unaokomea damu ya hedhi.

Mahanbali wamesema ni umri wa miaka hamsini. Mahanafi: "Miaka hamsini na mitano." Maliki: "Sabini." Na Mashafi: "Maadamu mwanamke angali hai basi akiwa na umri wowote upo uwezekano wa kuiona damu ya hedhi, ingawa kwa kawaida damu hukatika anapofikia umri wa miaka sitini na miwili."

Na Maimamiyya wamesema: "Damu ya hedhi husita katika umri wa miaka 50 kwa mwanamke asiyekuwa wa Kikuraishi, na pia kwa anayetiliwa shaka kuwa ni Mkuraishi. Ama kwa mwanamke wa Kikuraishi anayejulikana ni miaka sitini.

**MUDA WA HEDHI:**

Mahanafi na Maimamiyya wamesema: "Muda wa damu ya hedhi kwa uchache kabisa ni siku tatu, na wingi wake ni siku kumi, na wakati wowote damu inapotoka chini ya siku tatu au zaidi ya siku kumi hiyo si damu ya hedhi."

Na Mahanbali na Mashafi wamesema: "Uchache wa damu ya hedhi ni mchana mmoja na usiku mmoja (yaani ni saa ishirini na nne). Na wingi wake ni siku kumi na tano."

Na Maliki wamesema: "Wingi wake ni siku kumi na tano kwa mwanamke asiye na mimba, na wala hakuna kiwango cha uchache wake."

Na wote wameafikiana kuwa hakuna kikomo maalum cha wingi wa utohara wake unaotenganisha kati ya hedhi mbili. Ama uchache



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 74 2/1/2017 3:51:43 PM

wake kwa Mahanbali ni siku kumi na tatu na kumi na tano kwa Mahanafi, Mashafi na Maliki.

Wamesema Maimamiyya: "Uchache wa muda wa utohara ulioko baina ya damu mbili za hedhi ni zaidi ya wingi wa muda wa hedhi. (yaani siku kumi)."

**Tawi**: Wametofautiana mafakihi wa madhehebu yote juu ya kukutana pamoja damu ya hedhi na mimba (yaani Mwanamke mwenye mimba kuona damu ya hedhi). Na je damu anayaoiona mwanamke wakati akiwa mjamzito yawezekana ikawa ni damu ya hedhi?

Mashafi, Maliki na wanavyuoni wengi wa Imamiyya wamesema: "Upo uwezekano wa mwanamke mjamzito kuwa na damu ya hedhi." Mahanbali na Mahanafi na Sheikh Al-Mufid wa madhehebu ya Imamiyya wamesema: "Havikutani (haiwezekani) kwa hali yoyote ile."

## HUKMU ZA DAMU YA HEDHI:

Ni haramu kwa mwanamke mwenye damu ya hedhi kwa kila jambo lililo haramu kwa mwenye Janaba, kama kukaa msikitini, na kugusa maandishi ya Qur'ani, na Swaumu na Swala huwa hazikubaliwi katika siku za hedhi lakini humlazimu kukidhi siku zilizompita katika mwezi wa Ramadhani, bila ya kukidhi Swala zilizompita wakati wa hedhi, hiyo ni kulingana na Hadith nyingi zilizopokewa kutoka kwa Mtume, na pia kwa ajili ya kumwepushia taabu ya kurudia Swala ambazo zitakuwa ni nyingi. Na ni Swaumu tu atakidhi kwa kuwa si nyingi.

Na ni haramu kumtaliki mwanamke anapokuwa kwenye hedhi. Lakini hata hivyo kwa mujibu wa Madhehebu manne akimtaliki itasihi, isipokuwa tu mtaliki hupata dhambi. Ama kwa Maimamiyya



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 75 2/1/2017 3:51:43 PM

talaka huwa haisihi anapokuwa alimwingilia au anapokuwa mtaliki yu hadhiri (hakuwa safarini) au mwanamke anapokuwa si mjamzito.

Na husihi talaka (kwa Maimamiyya) ya aliyemo kwenye hedhi, mjamzito na ambaye hakuingiliwa na ambaye mume wake yuko safarini; na maelezo kamili yatakuja kwenye mlango wa talaka Inshallah.

Wote wameafikiana kwamba josho la hedhi halitoshelezi wudhu, na pia kwamba wudhu wa mwenye hedhi na kuoga kwake haviondoi hadath; na vilevile wameafikiana kwamba ni haramu kumwingilia mwanamke aliye kwenye damu ya hedhi.

Ama kuburudika na sehemu zilizo kati ya kitovu na magoti, Maimamiyya na Mahanbali wamesema: "Yajuzu bila ya shaka yoyote, sawa iwe kwa kizuizi au bila ya kizuizi." Na kauli iliyo mashuhuri kwa Maliki ni kuwa haijuzu hata kama ni pamoja na kizuizi. Na Mahanafi na Mashafi wamesema: "Ni haramu kumpapasa pasipo na kizuizi na yajuzu awapo na kizuizi.

Na mafakihi wengi katika Maimamiyya wamesema: "Mwanamume anapozidiwa nguvu na matamanio yake akamwingilia mkewe hali yumo kwenye hedhi, basi italazimu atoe kafara ambayo ni dinari moja (au sawa na thamani hiyo) iwapo alimwingilia mara tu hedhi ilipoanza (mwanzoni mwa hedhi), na atoe nusu yake, iwapo ni katikati ya hedhi, na atoe robo yake iwapo ni mwisho wa hedhi."

Na Mashafi na Maliki wamesema: "Yasunniwa atoe sadaka (anapomwingilia mkewe ndani ya hedhi) lakini si wajibu." Ama mwanamke halazimiki kutoa kafara yoyote kwa itifaki ya madhehebu yote, ijapokuwa hupata dhambi iwapo ameingiliwa kwa kupenda kwake mwenyewe na kuridhika kwake.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 76 2/1/2017 3:51:43 PM

## JINSI YA KUOGA:

Kuoga josho la kujitakasa kwa damu ya hedhi, ni kama kuoga josho la Janaba, kuanzia ulazima wa utohara wa maji anayoogea, na kwamba yawe ni maji halisi, aidha mwili wake uwe tohara, na juu ya mwili pasiwepo kitu kinachoyazuwia maji kufikia mwilini, na kutia nia, na kuanzia kichwani halafu ubavu wa kulia na kisha wa kushoto, hii ni kwa mujibu wa Maimamiyya, na pia kutosheka na kupiga mbizi kwa mara moja (kwa mpigo) ndani ya maji mengi.

Na kwa madhehebu manne ni kuenea maji mwili mzima kwa vyovyote iwavyo kama tulivyotangulia kuonyesha kwenye kuoga janaba bila ya kuwepo tofauti yoyote.

## ISTIHADHA

Istihadha: Katika istilahi ya mafakihi ni damu aionayo mwanamke katika wakati usiokuwa wa damu ya hedhi na nifasi, inapokuwa haiyumkini kuwa ni damu ya hedhi, kwa mfano damu inayotoka baada ya kumalizika muda wa hedhi au iliyo chini ya kiwango cha uchache wa muda wa hedhi, nayo aghalabu huwa ni damu yenye rangi ya njano, baridi tena nyembamba, hutoka kwa mfululizo kinyume na ilivyo damu ya hedhi.

Maimamiyya wameigawanya damu ya istihadha katika vigawanyo vitatu:

**1.** Ndogo, nayo ni ile ambayo wakati inapoitapakaza pamba haiiloweshi yote. Na hukmu yake ni kuwa mwanamke mwenye kiwango hiki cha istihadha abadilishe pamba na atawadhe kwa ajili ya kila Swala anayoswali. Hivi ni kusema haruhusiwi kuswali Swala mbili kwa wudhu mmoja.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 77 2/1/2017 3:51:43 PM

**2.** Istihadha ya kati na kati, nayo ni ambayo huitapakaza pamba yote lakini bila ya kuchuruzika nje ya pamba, na hukmu yake ni kuoga mara moja kwa kila siku kabla ya asubuhi pamoja na kubadilisha pamba na kutawadha kwa ajili ya kila Swala.

**3.** Istihadha kubwa, nayo ni ile inayoilowesha pamba na ikatiririka nje ya pamba, na hukmu yake ni kuoga mara tatu kwa kila siku, kabla ya kuswali Swala ya asubuhi, na josho la pili ataliogа kati ya Adhuhuri na Alasiri, na la tatu kwa ajili ya Isha na Magharibi.

Wengi katika wanavyuoni wa Kiimamiyya wamesema: "Katika hali kama hii hapana budi kwake kubadilisha pamba na kutawadha kwa ajili ya kila Swala kadhalika."

Na kwa kweli madhehebu mengine ya Kiislamu hayakuuzingatia mgawanyo huu, na wala hayakuwajibisha kuoga kwa mwenye Istihadha. Na imeandikwa katika kitabu '*Fiq'hus-Sunna*' cha Sayyid Sabiq uk. 155 chapa ya 1957: "Wala haimpasi kuoga (mwenye istihadha) kwa ajili ya Swala yoyote anayotaka kuswali, wala haimpasi kuoga wakati wowote miongoni mwa nyakati isipokuwa mara moja tu, napo ni pale inapokatika damu yake ya hedhi, ikiwa na maana ya kuwa, kuoga kunapasa kwa ajili ya kuondoa hedhi si kwa ajili ya istihadha, na ni maneno haya haya wameyasema jamhuri ya wanavyuoni waliotangulia na waliofuata nyuma."

Na kwa kauli za madhehebu yote manne ni kwamba istihadha haizuwii chochote miongoni mwa mambo yaliyokatazwa kwa mwenye hedhi, kama vile kusoma Qur'ani, kugusa msahafu, kuingia msikitini, kukaa Itikafu, kutufu, kuingiliwa kinyumba na mengineyo yasiyokuwa hayo ambayo tumetangulia kuyataja huko nyuma kwa kirefu katika mlango wa uchambuzi wa mambo ambayo ni haramu kwa mwenye hadath kubwa. Tazama kitabu (*Al-Fiq-hi alal*



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 78 2/1/2017 3:51:43 PM

*Madhahibal Ar-baa*, Juz. 1, *Mabhath ul istihadha*).

Na Maimamiyya wamesema: "Istihadha chache ni sawa na hadath ndogo, hivyo mwenye nayo si halali kwake kufanya chochote miongoni mwa mambo ambayo hulazimu wudhu isipokuwa baada ya kutawadha; na istihadha ya kati na kubwa zote mbili zina uzito wa hadath kubwa, nazo huzuwia kila jambo linalokatazwa kutendwa na mwenye hadath kubwa. Nazo humwajibisha kuoga, kwa kuwa ni sawa na hedhi maadamu walio nazo hawawezi kutekeleza mambo yaliyo wajibu juu yao, na ni hadi hapo watakapofikiwa na hukmu ya tohara ndipo watakapotekeleza ya wajibu juu yao, ambapo huhalalishiwa Swala, kuingia msikitini na kutufu.

Na kuoga ili kujitwahirisha kutokana na istihadha, kwa Maimamiyya ni sawa na kuoga kutokana na hedhi bila ya tofauti yoyote.

## DAMU YA KUZAA (NIFASI)

Maimamiyya na Maliki wamesema: "Damu ya nifasi ni ile inayosukumwa na nyumba ya uzazi kutokana na sababu ya kuzaa, nayo hutoka wakati mwanamke anapokuwa katika hali ya kujifungua au baada ya kujifungua, na si kabla ya kujifungua."

Mahanbali wamesema: "Nifasi ni damu inayoshuka pamoja na mtoto atokapo tumboni wakati mwanamke anajifungua, na baada ya kujifungua, na siku mbili au tatu kabla ya kujifungua ikiandamana na ishara za kujifungua."

Mashafi wamesema: "Nifasi ni damu inayomtoka mwanamke baada ya kuzaa, haitoki pamoja na mtoto wala kabla ya kuzaa."

Mahanafi wamesema: "Nifasi ni damu inayotoka baada ya kuzaa



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 79 2/1/2017 3:51:43 PM

au pale wanapotoka zaidi ya mtoto mmoja; ama damu inayotoka kabla ya kuzaa au inayotoka wakati wa kutoka mtoto mmoja, basi hiyo si damu ya nifasi."

Mwanamke mjamzito anapojifungua na asiione damu wakati wa kujifungua hulazimika kuoga kwa madhehebu ya Mashafi, Mahanafi na Maliki. Lakini kwa Immamiya na Mahanbali haipasi kuoga.

Na mafakihi wa madhehebu yote wamekubaliana kwamba uchache wa damu ya nifasi hauna muda maalum. Ama wingi wake kauli iliyo mashuhuri kwa Maimamiyya ni siku kumi. Na kwa Mahanafi na Mahanbali ni siku arobaini. Na kwa Mashafi na Maliki ni siku sitini. Ama anapozaliwa mtoto kupitia njia isiyokuwa ya kawaida kwa sababu ya kupasuliwa au mfano wa huo, hiyo si damu ya nifasi, lakini hata hivyo mwenye kukaa eda ya talaka hukatika (humalizika) eda yake kwa  kutoka kwa mtoto kwa njia yoyote iwayo.

Na damu ya nifasi iko kwenye hukmu moja na damu ya hedhi katika kutoswihi Swala, Swaumu na kupasa kukidhi Swaumu bila ya kukidhi Swala, na uharamu wa kuingiliwa kinyumba juu ya mwanamke na mume pia. Vilevile kugusa maandishi ya Qur'ani na kukaa msikitini au kuingia msikitini kulingana na ikhtilafu za madhehebu walivyohitilafiana (juu ya jambo hilo). Na kutoswihi talaka kwa madhehebu ya Imamiyya, na hukmu nyingi nyingine mbali ya hizo.

Ama namna ya jinsi ya kuoga mwenye damu ya nifasi ni sawa kabisa na kuoga kwa mwenye hedhi bila ya tofauti yoyote.

## KUGUSA MAITI

Mtu anapoigusa maiti ya mwanaadamu, je hulazimu juu yake kuoga au halazimiki?

Madhehebu manne wamesema: "Kugusa maiti hakusababishi hadath kubwa wala ndogo, kwa maana ya kwamba hakuwajibishi kuoga wala wudhu, bali yasunniwa kuoga kwa aliyemuosha maiti lakini si kutokana na kumgusa maiti."

Wengi katika Maimamiyya wamesema: "Hupasa kuoga kwa aliyegusa maiti lakini kwa sharti ya kuwa baridi huyo maiti (mwili wa mtu hubaridika anapokufa baada ya kupita muda mchache na katika hali hiyo ndipo unapolazimika kuoga umgusapo), na kwa sharti kwamba awe amemgusa kabla hajaoshwa kisheria, lakini linapotokea tendo la kumgusa maiti kabla hajapoa, au baada ya kuoshwa kwa mujibu wa sharia, basi hakutamlazimu kufanya chochote."

Na wala (Maimamiyya) hawakutofautisha katika wajibu wa kuoga baina ya kumgusa maiti Mwislamu na kafiri, wala kati ya mkubwa na mdogo, hata kama ni kitoto kilichotimiza miezi minne tumboini mwa mama yake. Na ni sawa iwe kugusa huko kumetokea kutokana na kupenda kwa mgusaji au alilazimika kumgusa (kwa sababu fulani). Alikuwa huyo aliyemgusa maiti ni mtoto au ni mtu mzima, alikuwa ni mtu mwenye akili zake au alikuwa ni mwendawazimu. Bali ni wajibu kuoga kwa mwendawazimu aliyemgusa maiti baada ya kupona wendawazimu wake, na kwa mtoto mdogo baada ya kubaleghe.

Maimamiyya wamewajibisha kuoga hata kwa kugusa kipande kilichokatwa kutoka kwa mtu aliye hai au maiti iwapo kilikuwa kimeambatana na mfupa. Hivi ni kusema, lau mtu atagusa kidole kilichokatwa kutoka mwilini kwa mtu aliye hai itampasa kuoga, na hukmu ni kama hiyo hiyo lau ataligusa jino lililotengana na maiti. Na kadhalika ni wajibu kuoga anapoligusa jino lililong'oka kutoka kwa mtu aliye hai iwapo tu limeng'oka na vijinyama nyama, na lakini si wajibu kuoga iwapo ni jino kavu bila ya vijinyama.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 81 2/1/2017 3:51:43 PM

Lakini pamoja na kuwa Maimamiyya wamewajibisha kuoga kwa kumgusa maiti hata hivyo ni lazima ieleweke kwamba, kwa hakika wao wameiweka hukmu ya kumgusa maiti kwenye ngazi ya hadath ndogo. Kwa maana ya kuwa kugusa maiti humzuwilia mtu kufanya matendo ambayo hushurutisha wudhu peke yake, bila ya matendo yanayomshurutisha mtu kuoga, kwa hiyo aliyegusa maiti hujuzu kwake kuingia msikitini na kukaa ndani yake, na kusoma Qur'ani. Ama namna ya kuoga josho la kugusa maiti ni sawa na namna ya kuoga josho la Janaba.

## MAITI NA HUKMU ZAKE

Hapa maneno yanagawanyika sehemu kadhaa:

**Sehemu ya kwanza:** Inahusu *Ihtidhar*, na *Ihtidhar* ni kumwelekeza (mtu anayekaribia kufa) upande wa Kibla. Na mafakihi wamekhitilafiana kuhusu jinsi na namna ya kumwelekeza upande huo. Maimamiyya na Mashafi wamesema: "Ni kumlaza mtu anayekaribia kukata roho juu ya maungo yake (kumlaza chali), na kuyafanya matumbo ya nyayo zake yaelekee Kibla, kwa namna ambayo lau atakalishwa angalielekea Kibla (kwa uso wake)."

Ama Maliki, Mahanbali na Mahanafi wamesema: "Ni kulazwa maiti kwa upande wa ubavu wake wa kulia (kuume) na uso wake uelekee Kibla, kama anavyolazwa wakati anapozikwa."

Na kama ambavyo wamekhitilafiana katika jinsi ya kumwelekeza maiti upande wa Kibla, vile vile walikhitilafiana juu ya wajibu wa kitendo hicho. Mafakihi wa madhehebu manne na kundi (dogo) katika Maimamiyya wamesema: "Kumwelekeza maiti upande wa Kibla ni Sunna tu na sio wajibu." Na wengi katika mafakihi wa Maimamiyya wamesema kwamba ni wajibu wa kutoshelezana, kama ilivyo katika



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 82 2/1/2017 3:51:43 PM

kumuosha na kumkafini. Na imeandikwa kwenye kitabu *'Misbahul faqiih'* cha Maimamiyya kwamba: "Wajibu wa kumwelekeza maiti upande wa Kibla unahusika kwa wote mkubwa na mdogo pia."

Na ningependa ieleweke hapa kuwa kila moja miongoni mwa mambo ambayo ni wajibu kumtendea maiti yatakayofuata, yana daraja ya wajibu wa kutoshelezana, yaani wanapoyatekeleza baadhi ya watu, huporomoka wajibu huo kwa waliobaki, na wanapoacha wote kutekeleza, wote hupata dhambi na ni wote wataulizwa mbele za Mwenyezi Mungu.

**Sehemu ya pili: Kumwosha maiti:** Na hapa pana masaili yafuatayo: Wote wamekubaliana kwamba 'Shahid' naye ni mtu aliyeuawa katika vita vya kupigana na makafiri, haoshwi.[4] Na wamekubaliana kuwa asiyekuwa Mwislamu haijuzu kumuosha, isipokuwa Mashafi ndio waliosema kuwa yajuzu kumuosha.

Na vilevile wamekubaliana kwamba mtoto aliyeavywa ambaye hajafikisha umri wa miezi minne ndani ya tumbo la mama yake, haoshwi. Kisha wametofautiana pale anapokuwa amefikisha umri wa miezi minne tumboni mwa mamake. Maimamiyya na Mahanbali wamesema: "Ni lazima aoshwe."

Mahanafi wamesema: "Kama atatoka na kudhihiri akiwa hai kisha akafariki, au alizaliwa akiwa maiti lakini amekamilika umbo, ataoshwa, lakini ikiwa ni kinyume cha hivyo basi hataoshwa."

Na Maliki wamesema: "Haipasi kumuosha mtoto aliyeavywa ila tu anapokuwa katika hali ambayo ingewezekana kuishi kulingana na maelezo ya wataalamu watakaposema kwamba: "Mtoto kama huyu huweza kuishi uhai wa kawaida."

---

[4] Hanafiyya wamesema: "Shahid ni kila mtu alieuawa kwa njia ya dhuluma, ni sawa awe aliuawa kwenye vita au alivamiwa na mwivi au genge la maharamia (chinja chinja). Na walishurutisha juu ya kutomuosha kwamba iwe imethibitika hakuwa na hadath kubwa."

Mashafi wamesema: "Iwapo atatoka baada ya kupitisha miezi sita (tumboni) basi ataoshwa, na iwapo ni chini ya miezi sita lakini akawa amekamilika umbo pia ataoshwa, na iwapo hakuwa amekamilika umbo lakini ikathibitika kwamba alikuwa hai (ingawa muda mchache tu) ataoshwa, la kama alikuwa kinyume cha hivyo haoshwi."

**Tanzuo**: Vinapotoweka sehemu ya viungo kutoka katika mwili wa maiti kwa ajili ya maradhi, kuteketea au kwa kuliwa na mnyama, na jambo lolote lile linaloweza kupoteza sehemu ya viungo vya mwili wa mwanadamu. Je ni wajibu kuoshwa sehemu ya mwili wa maiti iliyobaki?

Mahanafi wamesema: "Haipasi kuoshwa isipokuwa inapopatikana sehemu kubwa zaidi ya mwili (kuliko sehemu iliyotoweka) au nusu yake ikiwa pamoja na kichwa."

Maliki: "Ni wajibu kuuosha inapopatikana theluthi mbili katika mwili wa maiti."

Na Mahanbali na pia Mashafi wamesema: "Huoshwa hata kama sehemu iliyobaki ni ndogo kiasi gani."

Maimamiyya wamesema: "Kinapopatikana kipande cha mwili wa maiti huchunguzwa iwapo kama kilichopatikana ni sehemu ya kifua, au kifua kamili mkiwamo pamoja na sehemu inayokaa moyo basi hukmu yake huwa ni sawa na hukmu ya maiti kamili, kwa kupasa kuoshwa, kukafiniwa na hata kuswaliwa. Na kama kipande cha mwili kilichopatikana hakikuungana na kifua au sehemu ya kifua, kama ndani yake mna mfupa kitaoshwa, kifungwe ndani ya kitambaa, kizikwe, na kama kipande kilichopatikana hakina mfupa, hufungwa fungwa kitambaani na kuzikwa bila ya kuoshwa."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 84 2/1/2017 3:51:43 PM

## MWOSHAJI:

Ni wajibu kuwa katika jinsi moja kati ya mwoshaji na mwoshwa, yaani waume waoshwe na waume, na wanawake waoshwe na wanawake. Maimamiyya, Mashafi, Maliki na Mahanbali wamejuzisha mume amuoshe mkewe, na mke amuoshe mumewe. Ila Mahanafi, wao wamesema: "Mume hapasi kumuosha mkewe kwa sababu huwa ameshatoka chini ya hifadhi yake kutokana na kifo. Ama mke ana haki ya kumuosha mumewe kwa sababu huwa yumo katika eda ya kufiwa na mume, kwa maana ya kuwa umke huwa ungalipo bado katika haki yake (mwanamke) na (eda) huwa bado inaendeleza haki na daraja ya mke."

Lakini anapomtaliki kisha akafa, kama alimtaliki talaka *bayyina* (isiyoweza kurejeana naye) mke hatamuosha mume, hii inatokana na itifaki ya mafakihi wa madhehebu yote. Na kama alimuacha kwa talaka rejea (*raj-iya*), Maimamiyya wamejuzisha kuoshana, kwa mmoja kumuosha mwenza wake. Na Mahanafi na Mahanbali wamesema: "Mke atamuosha mume, lakini mume hana haki ya kumuosha mke." Na Maliki na Mashafi wamesema: "Hapana haki ya mke kumuosha mume wala mume kumuosha mke." Nao wala hawakutofautisha kati ya talaka *bayyina* na talaka rejea (*raj'iya)*.

Na Maimamiyya wamejuzisha kwa mwanamke kumuosha mtoto wa kiume kama mtoto huyo umri wake si zaidi ya miaka mitatu. Na pia wamejuzisha kwa mwanamume kumuosha mtoto wa kike kama umri wake haujavuka miaka mitatu.

Na Mahanafi wamesema: "Hujuzu kumuosha hadi miaka minne."

Mahanbali wamesema: "Hujuzu kumuosha kabla ya umri wa miaka saba."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 85 2/1/2017 3:51:43 PM

Maliki wamesema: "Mwanamke anaruhusiwa kumuosha mtoto wa kiume wa umri wa miaka minane, na mwanamume anaruhusiwa kumuosha msichana wa miaka miwili na miezi minane."

**JINSI YA KUMUOSHA MAITI:**

Maimamiyya wamesema: "Ni wajibu aoshwe kwa majosho matatu: La mwanzo, aoshwe kwa maji yaliyotiwa majani machache ya mkunazi. La pili, aoshwe kwa maji yaliyotiwa karafuumaiti. La tatu, aoshwe kwa maji safi matupu yasiyochanganywa na kitu chochote. Na muoshaji aanze kwa kumuosha kichwa, kisha upande wa ubavu wa kuume, na kisha upande wa kushoto."

Na mafakihi wa madhehebu manne wamesema: "Linalopasa ni josho moja tu la maji yasiyochanganywa chochote, na majosho mawili yanayofuatiwa ni Sunna (yapendekeza tu si lazima) wala hakuna masharti ya kumwosha kwa namna maalum, huswihi kumuosha kwa vyovyote iwavyo, kama ilivyo katika kuoga janaba. Na wala si lazima kwa madhehebu manne kuchanganya majani ya mkunazi wala karafuumaiti bali ni Sunna tu katika maji ya mwisho anayooshewa maiti kutiwa karufuu maiti au aina yoyote ya manukato."

Na yashartiwa katika kuswihi kumuosha maiti muoshaji atie nia, na maji yawe halisi na yawe ni tohara, na kuiondoa najisi iliyoko juu ya mwili wa maiti, na kutokuwepo juu ya mwili wa maiti kitu chochote kinachozuia maji kufika kwenye mwili wa maiti (ngozi).

Maimamiyya wamesema: "Ni makruhu kumuosha maiti kwa maji moto."

Mahanafi wamesema: "Maji moto ni bora zaidi kumuoshea maiti." Mahanbali, Maliki na Mashafi wamesema:: "Maji ya baridi ndiyo mustahabbu kumuoshea maiti."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 86 2/1/2017 3:51:43 PM

Na wameafikiana wote kwa ujumla kwamba mtu aliyekufa akiwa ndani ya ihram ya Hijja maji ya kumuoshea hayatiwi karafuumaiti, na pia wameafikiana kwamba ni lazima atengwe na kila aina za manukato.

Ni inapokuwa vigumu kumuosha, pengine kwa kukosa maji ya kumuoshea, au kwa sababu ya kuteketea kwa moto, au kwa kumomonyoka nyama za mwili, basi tayammamu husimama mahali pake (badala ya kumuosha) kwa itifaki ya maimamu wa madhehebu yote. Ama jinsi ya kumtayamamisha, ni sawa na anavyotayammamu mtu aliye hai. Na maelezo kwa ubainifu zaidi yatafuata katika mlango wa tayammamu.

Na kundi katika wanavyuoni wa Maimamiyya wamesema: "Hupasa kumtayamamisha maiti mara tatu: Ya kwanza: Iwe ni badala ya josho la maji yaliyochanganywa na majani ya mkunazi. Na tayammamu ya pili ni badala ya maji yaliyotiwa karafuumaiti, na ya tatu iwe ni badala ya maji masafi." Ama walio wahakiki kati yao (Maimamiyya) wamesema: "Inatosha tayammamu moja."

## *HANUT* - KUIPAKA MAITI KARAFUUMAITI

***Hanut*** **-** ni kuvipaka karafuumaiti ya unga viungo vya sijda vya maiti baada ya kumwosha, na viungo vyenyewe ni paji la uso, mikono miwili, ambayo hupakwa matumbo ya viganja viwili, magoti na vidole gumba vya miguu.

Maimamiyya wamewajibisha kumpaka maiti kwa mfumo huu, kinyume na madhehebu mengine, kisha wao hawakutofautisha kati ya mkubwa na mdogo hata kitoto kilichozaliwa kabla ya siku za kuzaliwa (kipomoko), wala hawakutofautisha kati ya mume na mke, na hawakumtenga na wajibu huo ila mtu aliyefia ndani ya ihramu ya



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 87 2/1/2017 3:51:43 PM

Hijja peke yake, na ukiachana na viungo saba vya sijida wameongeza pia pua katika hali ya Sunna.

## SANDA

Sanda ni wajibu katika madhehebu zote, na maimamu wanne wamesema: "Katika sanda wajibu ni nguo moja tu inayouenea mwili mzima wa maiti, na Sunna ni vipande vitatu vya nguo."

Na Maimamiyya wamesema: "Vipande vitatu ni wajibu na wala si Sunna, cha kwanza ni shuka ndogo iliyofanana na kikoi, kwa kuwa huanzia kiunoni hadi kwenye magoti, na cha pili ni kanzu ambayo huanzia mabegani hadi katikati ya miundi (ugoko). Na cha tatu ni shuka kubwa inayoufunika mwili mzima wa maiti."

Na yashurutiwa katika sanda, mambo yaleyale yaliyo sharti katika sitara iliyo wajibu pindi mtu anapotaka kuswali, kama vile utohara, uhalali na isiwe ni hariri au inayotokana na mnyama asiyeliwa nyama yake, wala isiwe ya dhahabu, sawa iwe ya mume au mke, na masharti mengineyo yasiyokuwa hayo ambayo yataelezwa kikamilifu mahali pake.

Na sanda ya mwanamke ni wajibu uliyo juu ya mumewe awapo ni mwenye uwezo, hiyo ni kwa mujibu wa madhehebu ya Imamiyya, Shafi na Hanafi.

Nao Maliki na Mahanbali wamesema: "Halazimiki mume kumkafini mkewe hata kama mke ni fukara, na gharama ya sanda ya wajibu na mambo mengineyo ya maiti, huchukuliwa kutoka kwenye mali iliyowachwa na marehemu - kwa asiyekuwa mke - kabla ya kulipa deni, kutekeleza wasia, na kuchukua mirathi, isipokuwa chombo ambacho kina haki ya rehani."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 88 2/1/2017 3:51:44 PM

## ANAPOFARIKI FUKARA:

Maimamu wa madhehebu manne na kundi miongoni mwa Maimamiyya wamesema: "Iwapo marehemu hakuacha mali ambayo ingewezesha kupatikana sanda, basi mwenye wajibu wa kutoa sanda yake ni yule ambaye kisharia alikuwa na wajibu wa kumtunza maiti huyo wakati wa uhai wake (*kafilu*). Na kama marehemu huyo hakuwa na mtu wa kumtunza kisharia, au aliyekuwa na wajibu wa kumtunza naye ni fukara, basi sanda yake itachukuliwa kutoka katika '*Baitul mali*' ya Waislamu, au kutoka kwenye Zaka kama itawezekana, la haikupatikana, basi utakuwa ni wajibu wa Waislamu wote walio na uwezo wa kufanikisha kupatikana."

Na kundi jingine miongoni mwa Maimamiyya wamesema: "Mtu anapofariki hali ya kuwa hana mali aliyoiacha na wala hakuwa na mlezi wake, huwa si wajibu kwa yeyote kugharamia sanda yake, kwa kuwa lililo wajibu ni kufanya tendo la kumvisha sanda si kutoa mali, hivyo basi kutoa mali ya kumkafini maiti katika hali hiyo ni mustahabu katika mlango wa kutenda wema na ihsani, na kama hatapatikana mtu mwema wa kuigharamia sanda yake, basi atazikwa tupu, bila ya sanda."

## SWALA YA MTU ALIYEKUFA SHAHIDI:

Madhehebu yote yameafikiana kuwa ni lazima kumswalia kila maiti Mwislamu na watoto wao pia, bila ya kuwepo tofauti yoyote kati ya madhehebu. Na madhehebu yote yameafikiana kwamba haiswihi Swala ila baada ya kumuosha na kumvisha sanda. Na kwamba Shahidi haoshwi wala havishwi sanda, bali huzikwa na nguo zake alizofia; na Mashafi wametoa hiyari ya kuchagua ima azikwe na nguo zake, au zivuliwe na avishwe sanda.

Kisha wamekhitilafiana kuhusu kumswalia Swala ya maiti. Mashafi wamesema: "Haswaliwi." Na hiyo ndiyo kauli ya Maliki



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 89 2/1/2017 3:51:44 PM

na pia Mahanbali. Ama Maimamiyya na Mahanafi wamesema: "Ni wajibu kumswalia kama ilivyo wajibu kuwaswalia maiti wengineo."

## SWALA YA MTOTO MDOGO:

Wamekhitilafiana kuhusu Swala ya mtoto mdogo, Mashafi na Maliki wamesema: "Huwa ni wajibu kumswalia iwapo alilia baada ya kuzaliwa ingawa ni kwa yowe moja tu. Ikiwa na maana kwamba, hukmu ya Swala hapa ni sawa na hukmu ya mirathi (urithi)." Na Mahanbali na Mahanafi wamesema: "Huswaliwa iwapo atatimiza miezi minne tumboni mwa mama yake."

Na Maimamiyya wamesema: "Si wajibu kuziswalia maiti za watoto wa Kiislamu isipokuwa wanapofikia umri wa miaka sita, na ni Sunna tu kuwaswalia walio chini ya umri huo."

Swala ya maiti asiyekuwepo 'Swala ya ghaibu':

Maimamiyya, Maliki na Mahanafi wamesema: "Katika hali yoyote ile iwayo, haijuzu kumswalia maiti aliye mbali au asiyekuwa mbele za wanaomswalia, na wametoa dalili kwamba Mtume ﷺ na Maswahaba zake hawakuwa na kawaida ya kufanya hivyo, na lau kama Mtume ﷺ na Maswahaba zake wangekuwa wakifanya hivyo basi jambo hilo lingeenea na lingekuwa mashuhuri sana miongoni mwa watu. Na kwamba kumwelekeza maiti Kibla na kuhudhuria mbele ya jeneza yule mwenye kumswalia, ni miongoni mwa masharti ya lazima.

Mahanbali na Mashafi wamesema: "Yajuzu kumswalia maiti aliye mbali, na dalili yao ni kuwa Mtume ﷺ alimswalia Najashiy (wa Ethiophia ya sasa) Swala ya maiti (akiwa mbali naye) pale habari za kifo chake zilipomfikia. Na wakajibiwa kuwa bila ya shaka yoyote tendo hilo lilikuwa ni katika jumla ya matendo yaliyomuhusu Mtume ﷺ peke yake au ilikuwa ni Swala maalum kwa ajili ya



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 90 2/1/2017 3:51:44 PM

Najashiy peke yake. Na ndio maana haikutokea tena kwa Mtume ﷺ kuswali Swala kama hiyo kwa mwingine pamoja na kuwa alipata habari au aliwajua wengi waliokufa miongoni mwa Maswahaba zake wakubwa, ambao walifia mbali na mahali alipokuwa Mtume ﷺ (lakini hakuna aliyemswalia).

## MAWALII WA MAITI

Maimamiyya wamesema: Mambo yote yaliyo ya wajibu ambayo hufungamana na mambo ya mazishi ya mtu (aliyekufa) ili kuyafanya yaswihi ni lazima yaidhinishwe na walii wa maiti, bila ya kutofautisha kati ya kumuosha na kumkafini, au kumhaniti (kumpaka karafuumaiti) na kumswalia, na yeyote atakayefanya moja tu miongoni mwa mambo hayo bila ya kuidhinishwa na walii wake kwa njia yoyote ile, tendo hilo hubatilika na hubidi kulirudia tena (baada ya kupata idhini ya walii). Hii ina maana kwamba ima walii atekeleze mambo hayo yeye mwenyewe au amruhusu mtu mwingine ayatekeleze kwa idhini yake. Lakini (walii) atakapokataa kuyafanya yeye mwenyewe na kukataa kutoa idhini kwa mtu mwingine kuyafanya, basi nguvu yake kama walii huporomoka.

Na kwa Maimamiyya mume ndiye anayetangulia katika uwalii kabla ya ndugu yeyote kuhusiana na mkewe, na mawalii wengineo wasiokuwa mume (wa mwanamke aliyekufa) hufuata katika uwalii kulingana na daraja zao kama ilivyo katika urithi.

Daraja ya kwanza ni mababa na watoto, ambao huwatangulia mawalii wa daraja ya pili, ambao ni ndugu na mababu, na warithi wa daraja ya pili huwatangulia warithi wa daraja ya tatu ambao ni maamu (ndugu za baba) na wajomba. Na baba ndiye walii aliye na haki zaidi kuliko mawalii wengine wa daraja ya kwanza. Na babu



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 91 2/1/2017 3:51:44 PM

ndiye mwenye haki zaidi kuliko ndugu katika daraja ya pili, na kama katika daraja husika hakuna wanaume basi uwalii utageukia kwa wanawake, na pindi ndugu au maamu au wajomba wanapokuwa zaidi ya mmoja, basi utekelezaji utahitaji idhini ya wote.

Ama madhehebu manne wao hawakugusia chochote kuhusu walii, si katika kukataza wala kuidhinisha katika mambo yanayohusu kumuosha maiti na kumvisha sanda, jambo ambalo linamaanisha kuwa idhini ya walii katika mambo yanayotendewa maiti haina uzito wowote kwao wao. Wao wamezungumzia mtu aliye bora na haki zaidi katika kumswalia maiti, Mahanafi wamesema: "Wanaotangulia katika Swala ya maiti wanafuatana kwa daraja hizi: Sultani, kisha naibu wake, kisha ni kadhi, kisha kiongozi wa serikali, kisha ni Imamu aliye hai kama ni mbora kuliko walii wa maiti, kisha ni walii wa maiti, kisha utafuata mpangilio ulivyo katika uwalii wa ndoa (yaani udugu wa kuumeni tu).

Na Mashafi wamesema: "Husimama (kumswalia maiti) baba yake, kisha mwana wa maiti, kisha ndugu yake wa baba na mama mmoja, kisha ndugu yake wa baba tu, ni hivyo hivyo kama ilivyo katika taratibu za mirathi."

Na Maliki wamesema: "Mwenye haki zaidi ya kumswalia maiti ni yule aliyeusiwa na maiti mwenyewe ili aipate baraka ya wema wake, kisha ni khalifa, kisha ni mwanawe, kisha ni mwana wa mwanawe, kisha ni baba, kisha ni kaka, kisha ni mwana wa kaka, kisha ni babu, kisha ni ami na itaendelea hivyo hadi mwisho."

Na Mahanbali wamesema: "Mtu mwadilifu aliyeusiwa ndio mwenye haki zaidi, kisha ni mtawala, kisha ni naibu wake, kisha ni baba, kisha ni mwana, kisha atamswalia ndugu yake wa karibu zaidi, kisha ni anayefuata kwa ukaribu, kama ilivyo katika urithi."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 92 2/1/2017 3:51:44 PM

(*Fiqhu alal madh-hibil Arbaa* mlango unaoeleza mwenye haki zaidi ya kumswalia maiti).

## WANAPOFANANA MWISLAMU NA ASIYEKUWA MWISLAMU:

Anapopatikana maiti asiyejulikana kwa dhati na uhakika kuwa ni Mwislamu au si Mwislamu, kama alipatikana kwenye mtaa unaoishi Waislamu basi hukmu yake ni Mwislamu, la ni kinyume na hivyo basi aliyemuona halazimiki kumfanyia lolote miongoni mwa mambo anayofanyiwa Mwislamu, kwa sababu ya kuwa na shaka na asili ya taklifu. Na wanapochanganyika maiti wa Kiislamu na wasiokuwa Waislamu na ikawa vigumu kuwapambanua, Mahanbali wamesema: "Kila mmoja ataswaliwa kwa nia ya kuwa ni Mwislamu." Na Mahanafi wamesema: "Ni kuwa wazingatiwe walio wengi, kama Waislamu ndio walio wengi basi wataswaliwa wote, na kama Waislamu ni wachache basi wataachwa wote."

## NAMNA YA SWALA YA MAITI:

Maiti huwekwa katika kulazwa chali, na mwenye kumswalia atasimama nyuma ya jeneza si mbali nalo bali alikaribie sana.[5] Akielekea Kibla, na kichwa cha maiti kiwe upande wa kuumeni mwa anayemswalia, na wala baina ya maiti na anayemswalia pasiwepo kizuizi cha ukuta wala chenginecho, na anayemswalia aswali kwa kusimama isipokuwa kwa udhuru wa kisharia, kisha anuwie, apige takbira mara nne.

Maliki wamesema: "Yapasa kuomba dua baada ya kila takbira miongoni mwa takbira hizo nne, na kwa kifupi chake ni kusema anayeswali: "*Allahuma Ighfir Lihadhal Mayyit* (ewe Mola Wangu mghufirie maiti huyu)".

[5] Mashafi wamejuzisha kumswalia maiti aliyebebwa juu ya mnyama au mikononi mwa watu au juu ya mabega yao. Na hiyo ndiyo kauli ya Maliki.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 93 2/1/2017 3:51:44 PM

Na ikiwa maiti ni mtoto mdogo basi atawaombea wazazi wake, na baada ya takbira ya nne atatoa salam. Na hatanyanyua mikono yake isipokuwa kwenye takbira ya kwanza. Na kwa mujibu huu inatosheleza sura ifuatayo:

**1.** *Allahu Akbar, Allahumma Ighfir Lihadhal Mayyit* (Mungu ni mkuuu, ewe Mola Wangu mghufirie maiti huyu).

**2.** *Allahu Akbar Allahumma Irhamhu Warhamna* (Mungu ni mkuu, ewe Mola Wangu, mrehemu (maiti) huyu na uturehemu na sisi pia).

**3.** *Allahu Akbar, Allahumma Tub Alayhi Waalayna* (Mungu ni mkuu, Mola Wangu, mtakabalie toba maiti huyu na ututakabalie na sisi pia).

**4.** *Allahu Akbar, Allahumma Askinhu Fasiha Jinanika* (Mungu ni mkuu, ewe Mola Wangu, mpe maiti makazi yaliyo makunjuufu katika pepo yako). Assalamu Alaykum (Amani ya Mungu iwe juu yenu).

Mahanafi wamesema: Husifiwa Mwenyezi Mungu baada ya takbira ya kwanza, na kuswaliwa Mtume baada ya takbira ya pili. Na aombe dua baada ya takbira ya tatu. Na atoe salam baada ya takbira ya nne. Na wala kamwe asiinue mikono yake isipokuwa katika takbira ya kwanza. Na yatosha kwa mfano kama huu unaofuata:

**1.** *Allahu Akbar, Subhanallah walahulhamdu* (Mungu ni mkuu, ameepukana na mawi, Mwenyezi Mungu, na ni zake Yeye sifa njema).

**2.** *Allahu Akbar, Allahumma Swali Ala Muhammad* (Mungu ni mkuu, ewe Mola Mswalie Muhammad).



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 94 2/1/2017 3:51:44 PM

**3.** *Allahu Akbar, Allahumma Irham Hadhal Mayyit* (Mungu ni mkuu, ewe Mola Wangu mrehemu maiti huyu).

**4.** *Allahu Akbar, Assalam Alaikum Warahmatullah, Assalam Alaykum Warahmatullah*. (Mungu ni mkuu, amani na rehma za Mwenyezi Mungu ziwe juu yenu. Amani na rehma za Mwenyezi Mungu ziwe juu yenu).

Na Mashafi na pia Mahanbali wamesema: Baada ya Takbira ya kwanza husomwa Suratul-Fatiha (Alhamdu), na baada ya Takbira ya pili huswaliwa Mtume, na baada ya takbira ya tatu humuombea maiti, na baada ya takbira ya nne ni kutoa salam, na inatakiwa anayeswali ainue mikono yake katika takbira zote, na hivyo yatosha kwa kusema:

**1.** *Allahu Akbar*. Kisha asome Alhamdu.

**2.** *Allahu Akbar, Allahumma Swali Ala Muhammadin*.

**3.** *Allhu Akbar, Allahumma Irhamna Waiyyahu* (Mungu ni mkuu, ewe Mola wangu twakuomba uturehemu sisi na maiti huyu).

**4.** *Allahu Akbar, Assalam Alaykum Warahmatullah*…

Na Maimamiyya wamesema: Katika Swala ya maiti ni wajibu takbira tano, sawa na idadi ya Swala tano za faradhi za kila siku, na anayeswali ataleta shahada mbili baada ya takbira ya kwanza, na atamswalia Mtume baada ya takbira ya pili. Na atawaombea waumini waume na wanawake baada ya takbira ya tatu, na atamuombea dua maiti baada ya takbira ya nne, na kama anayeswaliwa ni mtoto mdogo wataombewa wazazi wake, na hakuna kinachosomwa baada ya takbira ya tano. Na inapendeza (ni Sunna) ainue mikono yake baada ya kila takbira, na uchache unaopasa katika Swala ya maiti ni kama ifuatavyo:

**1.** *Allahu Akbar, Ash'hadu An'lailaha Ilallahu* (Mungu ni mkuu, nashuhudia kwamba hakuna Mola wa haki isipokuwa Allah). *Waanna Muhammadan Rasulullah* (Na hakika Muhammad ni Mjumbe wa Allah).

**2.** *Allahu Akbar, Allahumma Swalli Ala Muhammad Waalihi* (Mungu ni mkuu, ewe Mola Wangu mswalie Muhammad na watu wa nyumbani kwake).

**3.** *Allahu Akbar, Allahumma Ighfir Lilmuminiina Walmuminat* (Mungu ni mkuu, ewe Mola waghofirie (dhambi zao) walio-amini wanaume na wanawake).

**4.** *Allahu Akbar, Allahumma Ighfir Lihadhal Mayyit* (Mungu ni mkuu, ewe Mola Wangu mghofirie maiti huyu (dhambi zake).

**5.** *Allahu Akbar* (Mungu ni mkuu).

Tumeleta namna hizi kwa ufupi ili kuwafahamisha vipengele vya chini kabisa vya wajibu, vinginevyo ni kwamba kila madhehebu yana dua zake zilizopokewa kwa urefu zikiwa zimetajwa mahali pake hasa panapohusika.

Na madhehebu manne yameshurutisha kwamba ili Swala ya maiti iswihi, hapana budi anayeswali awe yuko tohara na awe amejisitiri tupu kikamilifu kama ilivyo katika Swala za faradhi.

Maimamiyya wamesema: "Swala ya Maiti haina masharti ya kuwa tohara wala kujisitiri tupu, ila hayo ni mambo mawili (kuwa tohara na kujisitiri tupu) ambayo yanapendeza tu. Kwa sababu Swala ya maiti si Swala hasa ya hakika, bali ni dua tu, na ndio maana Imam anayeswalisha Swala ya jeneza hana jukumu lolote analolibeba kuhusiana na kisomo chake badala ya maamuma.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 96 2/1/2017 3:51:44 PM

Na hapa imetubainikia sote kwamba madhehebu manne yanawajibisha takbira nne katika Swala ya maiti, na kwamba Maimamiyya wamewajibisha takbira tano.

Imam Ja'far as-Sadiq ﷺ amesema: "Mwenyezi Mungu amefaradhisha Swala tano, akajaalia katika Swala ya maiti kila takbira ni sawa na Swala moja ya faradhi."

Na amesema tena: "Mtume ﷺ alikuwa akipiga takbira tano katika Swala ya jeneza kwa kila mtu aliyekuwa akimswalia. Na pindi Mwenyezi Mungu alipomkataza kuwaswalia wanafiki alipiga takbira tano kwa asiyekuwa mnafiki, akimuombea dua baada ya takbira ya nne, na alikuwa akitoa takbira nne anapomswalia mnafiki bila kumuombea chochote."

## MAHALI PANAPOSWALIWA SWALA YA MAITI:

Mashafi wamesema: "Ni Sunna Swala ya maiti kuswaliwa msikitini."

Mahanafi wamesema: "Ni makruhu."

Maimamiyya na Mahanbali wamesema: "Ni vyema kuswaliwa msikitini iwapo hapana hofu ya kuutapakaza msikiti kwa najisi."

## WAKATI WA KUSWALIWA SWALA YA MAITI:

Mashafi na Maimamiyya wamesema: "Swala ya maiti huswaliwa wakati wowote." Maliki, Mahanbali na Mahanafi wamesema: "Maiti haswaliwi wakati jua linapochomoza, na wakati jua linapogeuka upande wa Magharibi (mara tu baada ya saa sita mchana) na wakati linapotua."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 97 2/1/2017 3:51:44 PM

# KUZIKA

Wameafikiana kwa pamoja kwamba haijuzu kumuweka maiti juu ya uso wa ardhi na kumjengea bila ya kumchimbia kaburi, na hata kama atakuwa ndani ya sanduku, isipokuwa kwa dharura, na kwamba lililo wajibu ni kumweka ndani ya shimo (la kaburi) ambalo litahifadhi mwili wa maiti usionekane wala kutokeza harufu yake. Na maiti alazwe kwa ubavu wake wa kulia hali ya kuelekezwa Kibla. Na kichwa chake kielekezwe upande wa Magharibi na miguu yake upande wa Mashariki.

Na Maliki wamesema: "Kwa hakika kumlaza maiti katika hali hiyo ni Sunna tu (iliyopendekezwa) na wala si wajibu."

Maimamiyya wamesema: "Na mwanamke alazwe katika mwanandani na mumewe au mmojawapo miongoni mwa maharimu wake (mwanamume asiyeweza kumuoa) miongoni mwa watu ambao walikuwa ni halali kumtazama yeye wakati wa uhai wake, au alazwe na wanawake; na kama hakupatikana mumewe wala mtu aliye maharimu wake wala mwanamke, basi alazwe na wanaume maajinabi (wa kando) wanaoaminika kwa wema wao."

Mahanbali na Mahanafi wamesema: "Mume hukmu yake kwa mwanamke aliyekufa ni hukmu ya mwanamume ajinabi (wa kando) kwa kuwa hifadhi ya ndoa huwa imekatika kati yao kwa kifo hicho."

Na imeandikwa katika kitabu *Al-Wajiiz* cha Ghazal ambaye ni mfuasi wa madhehebu ya Shafi kwamba: "Maiti hawekwi kaburini isipokuwa na mwanamume, na kama maiti husika ni mwanamke basi mumewe au maharimu wake ndiye atakayetawalia jambo hilo. Kama akikosekana, basi ni mtumwa wake ndiye atakayetawalia. Wakikosekana basi ni mwanamume aliyehasiwa, la kama hakuna



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 98 2/1/2017 3:51:44 PM

mtu kama huyo basi wapatikane katika ndugu zake, pia nao wakikosekana basi wamlaze wanaume wa kando."

Hii ina maana kwamba katika jambo hili mwanamume ajinabi (wa kando) ni bora kuliko mwanamke.

Kutupwa maiti baharini:

Anapokufa mtu ndani ya meli au jahazi mbali na ufukwe, kama itawezekana kuchelewesha maziko hadi akazikwe ardhini itakuwa ni wajibu kufanya hivyo, na ikihofiwa kwamba ataoza, basi ataoshwa, avishwe sanda na aswaliwe, kisha atiwe ndani ya sanduku lililofungwa vyema, au ndani ya pipa linalofunika kichwa chake, lisindikwe vyema kisha litupwe baharini, na kama haiwezekani basi maiti itatiwa uzito kwa chuma au jiwe kisha itupwe baharini.

Na inavyoelekea wazi ni kwamba mafakihi walilisemea tawi hili katika fatwa zao na mfano wake, katika nyakati ambazo hakukuwako na nyenzo za kitaalamu zinazoweza kuhifadhi maiti muda mrefu bila kuoza. Lakini kwa vile sasa kuna vifaa aina kadhaa na nyenzo ambazo zinawezesha kumhifadhi maiti asioze, kama vile kumtia ndani ya jokofu au kutumia baadhi ya mbinu ambazo huhifadhi mwili wake bila kuharibika, basi ni wajibu acheleweshwe hata kama itabidi kusubiri muda mrefu kiasi gani.

## KULITANDAZA KABURI:

Mafakihi wa madhehebu yote wameafikiana kwamba ni Sunna kulitandaza kaburi baada ya kwishamzika maiti, ambapo ilithibiti kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa alilitandaza kaburi la mwanawe Ibrahim, na hii ndio kauli ya Mashafi na Maimamiyya.

Mahanafi, Mahanbali na Maliki wamesema: "Kuliinua kaburi ndio bora kwa sasa hivi, si kwa sababu nyingine yoyote ila ni kwa

kuwa siku hizi kulitandaza kaburi imekuwa nembo na ada ya baadhi ya mataifa (yasiyokuwa ya Kiislamu)."

## KULIFUKUA KABURI:

Wote wamekubaliana kwamba ni haramu kufukua kaburi, sawa maiti husika awe ni mtoto au mtu mzima, timamu wa akili au mwendawazimu, isipokuwa pale itakapojulikana kwa hakika kabisa maiti imekwisha na kugeuka mchaga, au kama kulifukua ni kwa maslahi ya maiti, kama pale itakapodhihiri kwamba kaburi lipo kwenye mapitio ya maji wakati wa mvua inyeshapo, au ufukwe wa mto, au maiti alizikwa kwenye ardhi iliyoporwa kutoka kwa mwenyewe kutokana na uadui, au kwa kutojua au kwa kusahau, na mmiliki halali amekataa kusamehe au kuchukua kitu badala yake, au alipozikwa alivishwa sanda isiyofaa kisharia, au alizikwa pamoja na mali ambayo ina thamani kubwa, sawa mali hiyo iwe ni yake au ni ya mtu mwingine.

Na mafakihi wamekhitilafiana kuhusu ruhusa ya kulifukua kaburi awapo maiti alizikwa bila ya kuoshwa, au alioshwa kwa namna isiyo ya kisharia. Mahanafi na baadhi ya mafakihi wa Imamiyya wamesema: "Haijuzu kufukua, kwa sababu maiti huwa mwili wake umeshaoza na kumomonyoka viungo."

Ama Mahanbali, Mashafi, Maliki na wengi katika mafakihi wa Imamiyya wamesema: "Hufukuliwa, huoshwa na huswaliwa kama hawatahofia kuwa ameoza." Na baadhi ya Maimamiyya wameongeza kusema kwamba: "Vilevile inajuzu kumfukua kwa sababu ya kutaka kupata uthibitisho fulani kwa kuuona mwili wa maiti."

# KUTAYAMMAMU

Kutayammamu kuna sababu zake zinazomfanya mtu awe na ruhusa kisharia ya kutayammamu, na kuna vitu maalumu vinavyotumika katika kutayammamu, na kuna namna maalumu ya kutayammamu, na kuna hukmu zake ambazo ni lazima ziambatane nako.

## SABABU ZINAZOPELEKEA KUTAYAMMAMU:

Wametofautiana (mafakihi wa madhehebu) juu ya mtu asiye safarini mwenye swiha kamili, je anaruhusiwa kutayammamu iwapo atakosa maji? Kwa maana ya kwamba je huko kuyakosa maji ni sababu ya kutayammamu kwa msafiri na mgonjwa tu, au ni sababu ya kutayammamu katika hali zote, hata kama yuko kwake hayuko safarini?

Abu Hanifa alisema: "Mkaazi wa mji aliye na siha kamili haruhusiwi kutayammamu wala halazimiki kuswali anapoyakosa maji." (*Kitabul- Al-Bidayatu Wan-Nihayah* cha Ibni Rushdi, Juz. 1, uk. 63 chapa ya mwaka 1935. Na kitabu *A-Mughni* cha Ibnu Qudamah, Juz. 1, uk. 234 chapa ya tatu).

Na alitoa dalili kwa Aya ya sita katika Sura al-Maidah isemayo: "Na mkiwa wagonjwa au mko safarini, au mmoja wenu ametoka chooni, au mmewaingilia wanawake (kinyumba) na msiyapate maji, basi tayammamuni." Hivyo dalili ya Aya hii iko wazi kabisa kwamba kule kuyakosa tu maji haiwi sababu ya kutosheleza kutayammamu maadamu mtu huyo hayuko safarini wala si mgonjwa. Na ikiwa tayammamu imefungika kwa msafiri au mgoinjwa tu, katika hali hii, asiye safarini mwenye siha njema si wajibu kwake kuswali (anapokosa maji), kwa sababu huwa amekosa twahara, na hakuna Swala isipokuwa kwa twahara.

Na madhehebu yote yaliyobaki yamewafikiana kwamba anayekosa maji hupaswa kutayammamu na kuswali, sawa mtu huyo



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 101 2/1/2017 3:51:44 PM

awe yuko safarini au mjini kwake, mzima au mgonjwa. Na hukmu hii inatokana na Hadith iliyoenea na mashuhuri sana *mutawatir* kwa wote: "Kwa hakika mchanga ulio tohara humtwahirisha Mwislamu hata kama ameyakosa maji kwa muda wa miaka kumi."

Na safari iliyotajwa kwenye Aya wameitolea hoja ya kuwa imetajwa katika matokeo ya '*aghlab'* (jambo lenye kutokea zaidi), kama ilivyo ni kwamba katika safari za zamani mara nyingi ilikuwa anayesafiri hukumbana na jambo hili la kukosa maji.

Kama lingetimia jambo hili lililonakiliwa kutoka kwa Abu Hanifa (kwamba mkaazi wa mji si wajibu kuswali kwa kutayammamu anapoyakosa maji) basi msafiri na mgonjwa watakuwa kwenye hali mbaya zaidi kuliko mkaazi wa mji aliye mzima, kwani Swala ni wajibu juu yao (msafiri na mgonjwa) hali ya kuwa si wajibu kwa mkaazi wa mji.

Mashafi na Mahanbali wamesema: "Yanapopatikana maji yasiyotosha kujitwahirisha kikamilifu, basi itampasa atumie maji hayo kwa kuosha sehemu inayotosha maji hayo, kisha atayammamu katika viungo vilivyokosa kuoshwa kwa maji, na kama ana maji ambayo yanatosha kuoshea uso tu, aoshe huo uso kisha atayammamu."

Na Madhehebu yaliyobakia yamesema: "Kuyapata maji yasiyotosha kutawadhia ni sawa na kuyakosa kabisa na huwa hakuna jingine linalopasa kwa mtu aliye na maji hayo yasiyotosha isipokuwa kutayammamu tu."

Na vyovyote iwavyo, katika nyakati zetu za leo, suala zima la kuyakosa maji halina nafasi ya kujadiliwa kwa kirefu, kwa sababu maji yamejaa na humfikia kila mtu mahali alipo, na kila mahali maji hupatikana na bila tatizo, iwe safarini au mjini. Na kama mafakihi wamerefusha maneno kuhusu wajibu wa kutafuta maji, kiwango cha urefu wa eneo la kutafutia maji hayo, au kuhusu wakati atakapokuwa



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 102 2/1/2017 3:51:44 PM

anahofia juu ya nafasi yake (kuingia hatarini), au anapohofia kupoteza mali yake na heshima yake dhidi ya wezi au wanyama washambuliao, au pindi atakapoyapata ndani ya kisima hali ya kuwa hana ndoo ya kuchotea, au anapolazimika kutoa thamani kubwa kuliko bei ya kawaida anapotaka kuyanunua, na mengineo mengi, kwa kweli ni kwa kuwa huko nyuma wasafiri walikuwa wakipata tabu kubwa sana katika njia ya kuyapata maji.[6]

## MADHARA YA KIAFYA:

Mafakihi wa madhehebu yote wameafikiana kuwa miongoni mwa sababu zinazomruhusu mtu kutayammamu ni kutokea madhara ya kiafya iwapo mtu atatumia maji, hata kama ni kwa dhana tu. Kwa hiyo mtu yeyote anapohofia kwamba kama atatumia maji huwenda akapatwa na madhara katika siha yake au maradhi yatazidi au yatachukua muda mrefu kupoa, au yatakuwa vigumu kupona, hapo ataacha kujitwahirisha kwa kutumia maji na hivyo atajitwahirisha kwa udongo.

**Tanzuo**: Kama wakati utakuwa finyu kiasi cha kutoweza kutumia maji, kama pale atakapoamka asubuhi kutoka usingizini ilihali wakati wa Swala ya Alfajiri umebaki mchache sana kiasi kwamba lau atajitwahirisha na maji, basi Swala ya faradhi ataiswali nje ya wakati na kuwa kadha, lakini kama atatayammamu basi ataiswali ndani ya wakati wake. Katika hali hii je ni wajibu juu yake kutayammamu au kujitwahirisha kwa maji?

Maliki na Maimamiyya wamesema: "Atatayammamu na kuswali, kisha atairudia Swala hiyo." Na Mashafi wamesema: "Haijuzu mtu

[6] Kwa kweli mas'ala hii bado ina nguvu na ni muhimu sana kwetu Afrika, hasa Afrika Mashariki, kwani maeneo mengi ya vijijini bado yangali yateseka kwa ukosefu wa maji, sawa iwe nyumbani au safarini, na hivyo kuna umuhimu wa kuendelea kuzidurusu na kuzielewa vilivyo mas'ala za Tayammamu – Mhariri wa Toleo la Kiswahili.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 103 2/1/2017 3:51:44 PM

kutayammamu yanapopatikana maji katika hali yoyote iwayo." Na Mahanbali wametofautisha kati ya kuwa safarini na nyumbani, wakasema: "Litokeapo jambo kama hilo wakati mtu awapo yuko safarini basi atatayammamu na aswali na hatairudia Swala. Ama linapomtokea hilo akiwa yuko nyumbani haruhusiwi kutayammamu kabisa."

Na Mahanafi wamesema: "Katika hali kama hii mtu huruhusiwa kutayammamu kwa kuswali Swala ya Sunna ya wakati maalum, kama vile Sunna zinazoswaliwa baada ya Swala ya Adhuhuri na Magharibi, ama katika Swala ya faradhi hairuhusiwi kutayammamu wakati ambapo maji yanapatikana hata kama wakati uliobaki ni mchache kiasi gani bali atatawadha na aswali kadha. Na kama atatayammamu na aiswali Swala ndani ya wakati itambidi arudie kuiswali Swala hiyo nje ya wakati."

## KINACHOTUMIKA KATIKA KUTAYAMMAMU:

Wameafikiana juu ya wajibu wa kutayammamu kwa mchanga ulio tohara kufuatana na kauli yake Mwenyezi Mungu aliposema: "Tayammamuni kwa mchanga  ulio safi." Na Kwa maneno ya Hadith tukufu ya Mtume ﷺ "Iliumbwa ardhi hali ya kuwa ni mahali pa kuswalia na kujitoharishia." Na neno '*twayyib'* lililotajwa ndani ya Aya lina maana ya tohara, nalo lina maana ya kitu ambacho hakijapatwa na najisi.

Kisha mafakihi wamekhitilafiana katika maana ya neno *swaiid.* Mahanafi na kundi la mafakihi wa Imamiyya neno hilo walilielewa kwa maana ya uso wa ardhi, kwa hivyo walisema kuwa yajuzu kutayammamu kwa mchanga, changarawe, hata jiwe, kisha wamekataza kutumia madini katika kutayammamu, kama vile chokaa, chumvi, zeri (arsenic) na vitu  vingine kama hivyo.

Na Mashafi neno hilo walilifahamu kwa maana ya udongo na mchanga, hivyo wamewajibisha kutayammamu kwa vitu viwili hivyo tu kama vina vumbi, na hawakujawizisha kutayammamu kwa jiwe.

Na Mahanbali walilifahamu kwa maana ya mchanga tu. Kwao haijuzu kutayammamu kwa changarawe wala jiwe. Na hili ndilo walilosema mafakihi wengi wa Imamiyya, lakini hata hivyo wao wameruhusu kutayammamu kwa udongo wa changarawe na hata jiwe wakati wa dharura.

Na Maliki neno hilo *Swaiid* walilipanua kwa maana ya udongo, mchanga, changarawe, jabali (jiwe), theluji na madini madamu tu hayajahamishwa kutoka kwenye makao yake ya asili, isipokuwa dhahabu, fedha na lulu, wao hawakujuzisha kutayammamu kwa vitu hivyo vyovyote iwavyo.

## NAMNA YA KUTAYAMMAMU:

Mafakihi wote wameafikiana kuwa kutayammamu hakuswihi bila ya kutia niya, hadi Mahanafi wakasema: "Niya ni sharti katika kutayammamu, na si sharti katika kutawadha." Na kutayammamu kwao wao kunaondoa Hadath kama ulivyo wudhu na kuoga, na kwa ajili hiyo wamejuzisha kwa anayetayammamu anuwie kwa huko kutayammamu kuondoa hadath kama anavyonuwia kuhalalisha Swala.

Na madhehebu yaliyobaki yamesema: "Hakika huko kutayammamu kunahalalisha tu, na wala hakuondoi hadathi, kwa hivyo inamlazimu mwenye kutayammamu anuwie kwa tayammamu hiyo kuhalalisha jambo linaloshamritiwa twahara, wala asinuwie kuondoa hadath; lakini baadhi ya Maimamiyya wamesema: "Yajuzu kutia niya ya kuondoa hadathi pamoja na kuelewa kwamba

kutayammamu hakuondoi hadath, kwa kuwa niya ya kuondoa haiachani na niya ya kuhalalisha.

Na njia iliyo bora inayokusanya pamoja kauli hizi ni mwenye kutayammamu kukusudia na kutia niya ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kutekeleza jambo linalohusu kutayammamu kwake, sawa iwe kutayammamu kwake kulifungamana na jambo hilo tangu mwanzo wake au kulitokana na kuingiliwa na jambo analotaka kulifanya, kama vile Swala na mfano wake miongoni mwa malengo ya tayammamu.

Na kama walivyotofautiana katika neno '*swaiid'* (mchanga) ndivyo walivyotofautiana kuhusu '*aydiy'* (mikono) na uso katika Aya tukufu ya Qur'ani. Mafakihi wa madhehebu manne na Ibnu Babawayhi wa madhehebu ya Imamiyya wamesema: "Kilichokusudiwa katika neno '*wajhi'* ni uso mzima, na pia zikiwamo ndani yake ndevu, na katika mikono miwili ni viganja viwili na kongo mbili pamoja na vifundo viwili. Hii ina maana ya kwamba ulio mpaka katika kutayammamu ndio huo huo ulio mpaka wa wudhu. Kwa hivyo anayetayammamu atapiga mapigo mawili juu ya mchanga kisha pigo la kwanza atapaka juu ya uso wote, na la pili atapaka mikono miwili kuanzia ncha za vidole hadi kwenye vifundo.

Nao Maliki na Mahanbali wakasema: "Kwa hakika huko kupangusa hadi mwisho wa viganja vya mikono ni faradhi, na kufikisha kwenye kifundo ni Sunna."

Maimamiyya wamesema: "Kilichokusudiwa katika neno '*wajhi'* ni baadhi ya uso tu, si wote, kwa sababu ile herufi '*bee'* iliyoko kwenye kauli yake Mwenyezi Mungu '*Famsahuu bi wujuuhikum'* huelewesha sehemu au baadhi. Dalili juu ya hilo ni kuwa imeingia kwa mtendewa ('*maf-uul*'), hivyo basi kama haitakuwa ni ya kuonesha sehemu itakuwa ni ya nyongeza, kwa kuwa neno '*imsahuu'* lenyewe



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 106 2/1/2017 3:51:44 PM

tu peke yake linahitaji mtendewa, na asili yake hasa ni kutohitaji nyongeza."[7]

Na waliweka mpaka wa chini kabisa wa eneo la uso linalopaswa kupakwa (kupangusa), kuwa ni kuanzia mwisho wa maoteo ya nywele za kichwa hadi kwenye ncha ya juu ya pua, na ndani yake mkiwemo paji la uso na mashavu mawili.

Na wamesema linalokusudiwa katika neno '*yadayn'* (mikono miwili), ni viganja viwili vya mikono tu. Kwa sababu neno '*yadun'* katika lugha ya kiarabu husemwa kwa maana nyingi, mojawapo ni kiganja cha mkono pekee, na maana hii ndio iliyo dhahiri zaidi kuliko zote zinazotumika katika neno hilo; tazama kitabu *Al-bidaayatu Wan-Nihayah* cha Ibnu Rushdi Juz. 1, Uk. 66.

Na maneno hayo yanaungwa na kuongeza nguvu na dalili hii. Unaposema umepoa mkono wangu, au nimelifanya hilo kwa mkono wangu. Hapo hautafahamika mkono mzima ila tu kiganja cha mkono peke yake. Na juu ya hoja hii ndio maana kutayammamu katika madhehebu ya Imamiyya kunatumika kwa kufuata sura au mfano huu unaofuata:

Anayetayammamu atapiga viganja vyake ardhini na atapaka uso wake kuanzia maoteo ya nywele za kichwani na ncha ya juu ya pua, kisha atapiga juu ya ardhi kwa mara ya pili na atapaka mgongo mzima wa kiganja cha mkono wa kulia kwa kutumia kiganja cha mkono wa kushoto, na mgongo wa kiganja cha kushoto akitumia kiganja cha mkono kulia.

Na Maimamiyya wamewajibisha kufuata utaratibu katika kutayammamu (kutayammamu kwa kufuata mpango), kwa namna ambayo lau mwenye kutayammamu atatanguliza mikono miwili

[7] Kuelewa vizuri uchambuzi huu yahitaji kurejea kwa wataalamu wa Kanuni za Lugha ya Kiarabu – Mhariri wa Toleo la Kiswahili.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 107 2/1/2017 3:51:44 PM

kabla hajapaka uso basi kutayammamu kwake kutabatilika, na vilevile wamewajibisha kuanza sehemu ya juu kuja sehemu ya chini, na lau atatayammamu kwa njia ya kuanzia chini kwenda juu tayammamu yake itabatilika. Na wengi katika mafakihi wa Maimamiyya wamewajibisha kupiga juu ya ardhi kwa viganja wakati wa kutayammamu, kwa maana ya kuwa anayetayammamu lau ataviweka pole pole viganja vyake juu ya ardhi bila ya kupiga basi tayammamu yake itabatilika.

Na Mahanafi wamesema: "Lau uso wa mtu utapatwa na vumbi kisha akaweka mkono wake juu ya uso wake, kisha akapangusa, itatosheleza bila ya kuhitajika kupiga juu ya ardhi."

Na mafakihi wote wameafikinana kuwa utohara wa viungo vya kutayammamu ni sharti la kuswihi kwa tayammamu, sawa kiungo hicho kiwe ni kile kinachopaka au kinachopakwa. Na vile vile utohara wa mchanga anaoutumia katika tayammamu, aidha wamewafikiana juu ya wajibu wa kuivua pete wakati wa kutayammamu, na kuwa haitoshi kuizungusha kama ilivyo katika wudhu.

Kisha wamekhitilafiana kuhusu wajibu wa kufuatanisha, Maliki na Maimamiyya wamesema kwamba ni wajibu kufuatanisha kati ya viungo, na kama atatenganisha kati ya viungo kwa muda ambao utaondoa hali ya kufuatanisha au mfuatano basi kutaibatilisha tayammamu.

Na Mahanbali wamesema: "Ni wajibu kufuatanisha na kufuata mpangilio wa kutayammamu katika viungo inapokuwa kutayammamu huko kumetokana na hadath ndogo, ama kama ni kutokana na hadath kubwa basi huwa hapana ulazima wa kufuatanisha wala kutayammamu kwa mpangilio (taratibu)."

Na Mashafi wamesema: "Ni wajibu kufanya kufuata mpangilio, na wala si wajibu kufuatanisha."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 108 2/1/2017 3:51:45 PM

Na Mahanafi wamesema: "Si wajibu yote mawili: Kufuata mpangilio wala kufuatanisha."

## HUKMU ZA KUTAYAMMAMU

Na hapo kuna masuala kadhaa:

**1.** Wote wameafikiana kwamba haijuzu kutayammamu kwa ajili ya kutaka kuswali, kabla wakati wa Swala haujaingia, isipokuwa Mahanafi peke yao ndio waliosema huswihi kutayammamu kabla ya kuingia wakati wa Swala.

Maimamiyya wamesema: "Kama mtu atatayammamu kabla ya wakati wa Swala haujaingia, kwa ajili ya lengo ambalo ni moja ya mambo ambayo tayammamu inaruhusiwa kwa ajili yake, kisha wakati wa Swala ukaingia hali tayammamu yake haijatenguka, basi hujuzu kwake kuswali kwa tayammamu hiyo hiyo."

Na Maimamiyya na vilevile Mahanafi wamejuzisha kuzikusanya Swala mbili pamoja kwa tayammamu moja.

Na Mashafi na Maliki wamesema: "Haijuzu kuunganisha kati ya Swala mbili za faradhi kwa tayammamu moja."

Na Mahanbali wamesema: "Ipo ruhusa ya kuzikusanya Swala mbili za faradhi kwa tayammamu moja lakini zinapokuwa ni za kulipa, ama kama ni za kutekeleza ndani ya nyakati zake haijuzu."

**2.** Baada ya kuhakikika tayammamu ya mtu kwa njia yake iliyowekwa na sharia, kisharia aliyetayammamu huwa anahukumiwa kuwa ni tohara sawa na aliyejitoharisha kwa maji, na huwa halali kwake kila jambo linalohalalishwa kwa mwenye wudhu na aliyeoga josho la wajibu. Na hutenguliwa na kila



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 109 2/1/2017 3:51:45 PM

jambo linalotengua twahara miongoni mwa hadath kubwa na ndogo, na pia kwa kuondoka udhuru wa kuyakosa maji au kupoa ugonjwa uliokuwa tishio katika kutumia maji.

**3.** Kama yapatikana maji baada ya kutayammamu na kabla ya kuingia kwenye Swala hapo tayammamu hubatilika kwa makubaliano ya mafakihi wa madhehebu yote. Na kama atapata maji hali ya kuwa yumo ndani ya Swala baadhi ya wanavyuoni wa Imamiyya wamesema: "Kama yalipatikana maji kabla hajarukuu katika rakaa ya kwanza basi tayammamu na Swala yake vitabatilika. Na kama yamepatikana baada ya kurukuu basi ataendelea na Swala yake hadi mwisho, na Swala yake itakuwa sahihi." Na Mashafi, Maliki na Hanbali katika moja ya mapokezi yake mawili, na kundi katika baadhi ya Maimamiyya, wamesema: "Anapokwisha kupiga takbira ya kuingia kwenye Swala basi na aendelee na Swala yake tu wala asigeuke kokote, na Swala yake itaswihi, kwa kauli ya Mwenyezi Mungu (s.w.t.) "Wala msibatilishe amali zenu." (47:33). Na Mahanafi wamesema: "Swala hubatilika."

Na kama udhuru wa kutayammamu utaondoka baada ya kuwa mtu ameshamaliza Swala, hata kama wakati ulibaki wa Swala aliyoiswali ni wa kutosha, haimlazimu kuirudia Swala hiyo kwa mara ya pili. Hii ni kwa Ijimai ya madhehebu yote.

**4.** Kama mwenye janaba atatayammamu badala ya kuoga, kisha akazukiwa na hadathi ndogo na mara akayapata maji ambayo yanatosha wudhu peke yake, je, itampasa kutawadha kisha atayammamu mara ya pili badala ya kuoga? Maliki na wanavyuoni wengi wa Imamiyya wamesema: "Atatayammamu badala ya kuoga." Na Mashafi, Mahanafi, Mahanbali na kundi miongoni mwa Maimamiyyah wamesema: "Atatawadha tu, kwa sababu

kule kutayammamu alikotayammamu kulikuwa ni kwa ajili ya kuondoa janaba, kisha utohara wake umetenguka kwa hadath isiyokuwa janaba, kwa hiyo hawezi kuwa na janaba tena bila kupatwa na sababu inayomfanya kuwa na janaba bali atakuwa amepatwa na hadath ndogo tu.

**5.** Mahanbali wameenda kinyume na madhehebu mengine yote kwa kuzingatia kwamba pia tayammamu hufanywa badala ya najisi iliyopo juu ya mwili. Tazama kitabu *Fiqh Alal Madhahibil Arbaa* mlango unaotafiti nguzo za tayammamu.

**6.** Mtu anapokosa twahara mbili (ya maji na ya udongo) kama pale mtu anapokuwa amefungiwa mahali pasipokuwa na maji wala mchanga wa kutayammamu, au pale anapokuwa na maradhi ambayo yanamzuwia kutawadha na kutayammamu, na asimpate wa kumtawadhisha wala wa kumtayamamisha, je katika hali hiyo ni wajibu kwake kuswali bila tohara? Na kama Swala kwake ni wajibu na akawa ameswali, je itambidi kuirudia Swala hiyo pindi atakapoweza kujitwahirisha?

Maliki wamesema: "Wajibu wa Swala huporomoka, hatatekeleza ndani ya wakati wake, wala hatalipa."

Mahanafi na Mashafi wamesema: "Wajibu wa Swala hauporomoki, si kwa kutekeleza ndani ya wakati wake, wala kwa kulipa." Na maana ya kutekeleza hapa, kwa Mahanafi, ni kwamba itamlazimu ajishabihishe na wenye kuswali. Na maana ya kutekeleza kwa Mashafi, ni kuswali Swala kwa uhakika; unapoondoka udhuru basi atairudia kwa namna yake inavyotakiwa na sharia.

Na wengi katika mafakihi wa Kiimamiyya wamesema: "Si wajibu kwake kutekeleza ndani ya wakati, bali ni wajibu kwake kulipa."

Mahanbali wamesema: “Ni wajibu kwake kutekeleza ndani ya wakati, na si wajibu kwake kulipa.”

## KAULI ZA MADHEHEBU KATIKA AYA YA KUTAYAMMAMU

Imetubainikia bayana hitilafu za madhehebu ambazo tumetangulia kuzitaja huko nyuma, kama vile hitilafu yao katika maji yasiyokuwa halisi na vinavyotengua wudhu. Na katika tayammamu, hitilafu kubwa ya madhehebu za Kiislamu zinapatikana katika Aya hii ya kutayammamu:

”..... وَإِن كُنتُم مَّرْضَىٰٓ أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَآءَ أَحَدٌ مِّنكُم مِّنَ ٱلْغَآئِطِ أَوْ لَٰمَسْتُمُ ٱلنِّسَآءَ فَلَمْ تَجِدُوا۟ مَآءً فَتَيَمَّمُوا۟ صَعِيدًا طَيِّبًا فَٱمْسَحُوا۟ بِوُجُوهِكُمْ وَأَيْدِيكُم مِّنْهُ ......“

**“Na mnapokuwa wagonjwa au mnapokuwa safarini, au mmoja wenu amekwenda (kidhi) haja kubwa, au mkawagusa wanawake na msipate maji basi tayammamuni kwa (kutumia) mchanga ulio tohara mpake sehemu za nyuso zenu…..” (5:6).**

Mafakihi wamekhitilafiana kuhusu ni nani mwenye wajibu wa kutayammamu kwa kuyakosa maji, je, ni mgonjwa na aliye safarini tu, au hukmu hii inaenea kwao wote akiwemo pia mtu mzima aliye hadhiri mjini?

Na je, makusudio ya kugusa mwanamke ni kumwingilia hasa, au ni kumgusa tu kwa mkono? Na je, makusudio ya maji, ni maji halisi tu au ni pamoja na maji yasiyokuwa halisi? Na je, makusudio ya udongo ni mchanga maalum au ni kila ardhi ikiwamo mchanga, vichangarawe na hata jabali? Na je, makusudio ya uso ni uso wote au ni sehemu yake tu? Na je, makusudio ya mkono ni mkono au ni kiganja tu cha mkono au ni kiganja pamoja na muundi wa mkono?



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 112 2/1/2017 3:51:45 PM

Na sasa tutakuletea kwa ufupi kauli za mafakihi zilizotangulia:

**1.** Abu Hanifa amesema: "Mkazi wa mji aliye mzima (asiye mgonjwa) ambaye anaweza kupata maji, si ruhusa kwake kutayammamu, na huwa hana Swala anapotayammamu, kwa sababu Aya hiyo ilimruhusu mtu kutayammamu kwa kuyakosa maji, hasa kwa mgonjwa na aliye safarini.

**2.** Madhehebu yaliyobaki yanasema: "Kwa hakika kumgusa mwanamke ajina (wa kando) kwa mkono kikamilifu kabisa ni sawa na kwenda haja (choo), kunatengua wudhu." Ama Maimamiyya wao wanasema: "Kumwingilia mwanamke tu ndiko kunakotangua wudhu, si kimgusa kwa mkono."

**3.** Mahanafi wamesema: "Kwa hakika maana ya Aya: 'Iwapo hamkupata maji basi tayammamuni' ni maji yoyote yawayo, yawe ni maji halisi au yasiyokuwa halisi." Ama madhehebu yaliyobakia yanasema: "Hakika tamko la maji katika Aya hii ni maji halisi peke yake bila ya kuyahusisha maji yasiyokuwa halisi.

**4.** Mahanafi na kundi katika Maimamiyya wanasema: "Makusudio ya udongo katika Aya ya tayammamu ni mchanga, changarawe na jiwe." Mashafi wanasema: "Ni udongo na mchanga tu." Mahanbali nao wanasema "Ni mchanga peke yake." Nao Maliki wanasema: "Inajumuisha udongo, changarawe, mchanga, jiwe, theluji na madini." Madhehebu manne yamesema: "Makusudio ya uso katika Aya hii ni uso wote." Maimamiyya wamesema: "Ni sehemu tu ya uso."

**5.** Madhehebu manne yamesema: "Makusudio ya mikono katika Aya hiyo ni viganja viwili, viwiko pamoja na kongo mbili." Maimamiyya wamesema: "Ni viganja viwili peke yake."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 113 2/1/2017 3:51:45 PM

Basi iwapo kutofautiana kwao kunajulisha juu ya jambo lolote bila shaka si zaidi ya kwamba tofauti hiyo ni ya ganda (ya juu tu) si ya kiini hasa. Na itakuwa ni ya kitamko tu si ya maana hasa, nayo ni sawa na hitilafu ya kilugha kwa wataalamu wa fani hiyo katika kueleza maana ya tamko (neno). Na vile vile ni sawa na hitilafu ya malenga katika kufahamu maana ya ubeti wa shairi. Na ni kwa namna hii tunaona kwamba mafakihi wa madhehebu moja wanatofautiana kikamilifu katika mas'ala moja. Kama wanavyotofautiana wanavyuoni wa madhehebu tofauti.

# SWALA

Swala zimegawanyika sehemu mbili, Swala za faradhi na Swala za Sunna. Swala zilizo muhimu zaidi kuliko zote ni Swala tano za kila siku. Waislamu wote katika madhehebu yao yote wameafikiana kuwa yeyote anayekanusha wajibu wa Swala, au kutia shaka katika kuwa kwake wajibu, huyo huwa si Mwislamu. Hata kama katamka shahada, kwani Swala ni miongoni mwa nguzo za Uislamu. Na wajibu wake umethibiti kwa dharura katika dini, na wala Swala si jambo linalohitaji uchunguzi na *Ijtihadi*, wala taklidi au kuuliza juu ya wajibu wake.

Ama kuhusu hukmu ya mwenye kuacha Swala, mafakihi wa madhehebu wamekhitilafiana kuhusu mwenye kaiacha Swala kwa uvivu tu, au kwa kuipuza pamoja na kuwa anaamini kwamba kuswali ni wajibu. Mashafi, Maliki na Mahanbali wamesema: "Huyo huuliwa." Mahanafi wamesema: "Hufungwa maisha, hadi anapoamua kuswali."

Maimamiyya wamesema: "Yeyote anayeacha tendo la wajibu kama Swala, Zaka, Khumsii, Hijja, na Swaumu hutiwa adabu kwa



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 114 2/1/2017 3:51:45 PM

adhabu ambayo ataamua hakimu (wa Kiislamu). Akianza kutekeleza wajibu huu basi ataachwa, na kama hakusikia atatiwa adabu (ataadhibiwa) kwa mara ya pili, akitubia ataachwa. Laa hakutubia ataadhibiwa kwa mara ya tatu, na akizidi kuendelea na kukataa kutekeleza basi atauliwa katika mara ya nne. (*Kashiful Ghitwaa* kitabu cha Sheikh mkuu Uk. 79 chapa ya mwaka wa 1317 A.H).

## SWALA ZA SUNNA:

Swala za Sunna ziko za aina nyingi, miongoni mwazo ni Sunna zinazofuatana na Swala za faradhi za kila siku, na mafakihi wa madhehebu wamekhitilafiana kuhusu idadi ya rakaa zake. Mashafi wamesema: "Ni rakaa kumi na moja: Mbili kabla ya Swala ya Alfajiri, na mbili kabla ya Swala ya Adhuhuri na rakaa mbili baada ya Swala ya Adhuhuri, mbili baada ya Swala ya Magharibi, na mbili baada ya Swala ya Isha, na rakaa moja ya witiri."

Mahanbali wamesema: "Ni rakaa kumi: Mbili kabla ya Swala ya Adhuhuri, mbili baada ya Swala ya Adhuhuri, mbili baada ya Swala ya Magharibi, na mbili baada ya Swala ya Isha, na mbili kabla ya Swala ya Alfajiri."

Maliki wamesema: "Hizi Swala za Sunna zinazofuatana na Swala za faradhi, zenyewe hazina kiwango maalum kilichowekwa au idadi maalum, lakini ni bora mtu aswali rakaa nne kabla ya Swala ya Adhuhuri, na rakaa sita baada ya Swala ya Magharibi."

Na Mahanafi wamesema: "Swala za Sunna zinazofuatana na Swala za faradhi, zenyewe zimegawanyika vigawanyo viwili, Sunna (*masnuun*) na zilizopendekezwa (*manduubu*),[8] na Swala za Sunna

[8] Wanavyuoni wa kihanafiyya wana istilahi zao kuhusiana na mambo ambayo ni wajibu kuyafanya ambayo haijuzu kuacha kuyafanya. Nayo kwa wao yapo katika



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 115 2/1/2017 3:51:45 PM

*(masnuun)* ni tano: Rakaa mbili kabla ya Swala ya Alfajiri, na rakaa nne kabla ya Swala ya Adhuhuri, na rakaa mbili baada ya Swala ya Adhuhuri katika siku isiyokuwa Ijumaa, na rakaa mbili baada ya Swala ya Magharibi, na rakaa mbili baada ya Swala ya Isha.

Na zilizopendekezwa (*mandubu*) ni nne: Rakaa nne kabla ya Swala ya Alasiri, na akipenda mtu anaweza akaswali rakaa mbili tu. Na rakaa sita baada ya Swala ya Magharibi, na rakaa nne kabla na baada ya Swala ya Isha."

Na Maimamiyya wanasema: "Swala za Sunna zinazofuatana na Swala za faradhi za kila siku ni rakaa thelathini na nne (34): Nane kabla ya Swala ya Adhuhuri, na rakaa nane kabla ya Swala ya Alasiri, na rakaa nne baada ya Swala ya Magharibi, na rakaa mbili baada ya Swala ya Isha ambazo huswaliwa kwa kukaa, ambapo zitahesabiwa kuwa ni rakaa moja, nazo huitwa *Watirah*, na rakaa nane za Swala ya usiku (*Tahajjudi*), na rakaa mbili zinazoitwa *Shufa*, na rakaa moja ya *witri*,[9] na rakaa mbili za Swala ya Alfajiri.

---

vigawanyo viwili. Faradhi inapothibiti kwa dalili ya mkato kama vile kitabu (cha Qur'ani) Sunna, *Mutawatir* (jambo lililozoweleka kati ya wanavyuoni wote,) na *Ijmaa* (kongamano la wanavyuoni wa Kiislamu). Na ni wajibu linapodhihiri jambo kwa dalili ya dhana tu, kama vile *qiyasi* (kwa kutumia akili tu bila ya ushahidi maalum), na Hadith iliyopokewa kutoka kwa Mtume ﷺ na mtu mmoja peke yake. Na ambayo yafaa kufanya pia yanagawanyika sehemu mbili: Zilosunniwa nayo ni ambayo ameyakokoteza Mtume na makhalifa viongozi, na *mandubu* (yaliyopendekezwa) aliyoyaamrisha Mtume ﷺ yafanywe lakini hakukokoteza, na ambayo yapasa kuyaacha na hayajuzu kuyafanya, iwapo yathibiti kukatazwa kwake kutokana na dalili ya moja kwa moja (ya mkato) basi ni haramu, na iwapo itathubutu basi ni haramu. Na iwapo itathubutu kukatazwa kwake kwa dalili ya dhana tu basi huwa ni makuruhu ya haramu kufanya.

[9] Swala ya witiri katika madhehebu ya Imam Hanafi ni rakaa tatu kwa kutumia salam moja, na wakati wake kulingana na madhehebu yao ni tangu kuzama mawingu mekundu hadi inapoingia alfajiri. Na madhehebu ya Imam Hanbali na Shafi wamesema: "Uchache wa Swala ya witiri ni rakaa moja na wingi wake ni rakaa kumi na moja, na wakati ni baada ya Swala ya Isha." Na madhehebu ya Imam Hanbali yamesema: "Witiri ni rakaa moja tu."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 116 2/1/2017 3:51:45 PM

## WAKATI WA ADHUHURI NA ALASIRI:

Mafakihi wote huanza nyakati za Swala kwa kuanza kutaja wakati wa Swala ya Adhuhuri, kwa kuwa ndiyo Swala ya mwanzo kufaradhishwa, na kisha ikafuatia Swala ya Alasiri kisha Magharibi kisha ya Isha kisha Swala ya Asubuhi kulingana na mpangilio wa Swala ulivyo. Swala tano zilifaradhishwa huko Makka mnamo usiku wa Miraji baada ya kupita miaka tisa tangu kutumilizwa Mtume ﷺ. Na wanaoelezea hivyo husema kwamba: Ushahidi ni hii Aya ya 78 katika Suratul Israa isemayo: "Simamisha Swala linapopinduka jua mpaka giza la usiku, na Qur'ani ya Alfajiri; hakika Qur'ani ya Alfajiri imekuwa ni yenye kushuhudiwa." Aya hiyo bila ya shaka imepambanua Swala zote tano na kuiweka kila moja mahali pake.

Na mafakihi wote wamekubaliana kuwa haijuzu kuiswali Swala yoyote ya faradhi kabla ya wakati wake haujaingia, na pia walikubaliana kwamba mara tu jua linapopinduka huwa wakati wa Adhuhuri umeingia lakini walitofautiana katika vipimo vya wakati huu wa Adhuhuri na ni hadi wakati gani huwa ndio mwisho wake.

Maimamiyya wamesema: "Wakati makhususi wa Adhuhuri ni mara tu jua linapopindukia upande wa pili mpaka kiasi cha kuweza kuitekeleza Swala hiyo, na wakati makhususi wa Alasiri ni mwisho wa mchana kwa muda wa kutosha kuitekelza Swala hiyo, na wakati uliopo kati ya nyakati hizo mbili (mwanzo wa mchana na mwisho wa mchana) ni wakati wa kushirikiana kati ya Swala hizo mbili, na ni kuanzia hapa ndipo Maimamiyya waliposema kwamba inajuzu kuzikutanisha Swala mbili hizo katika wakati huo ambao zinashirikiana Swala hizo mbili.[10] Na wakati unapokuwa finyu kiasi

[10] Wako mafakihi miongoni mwa ulamaa wa madhehebu manne waliowafiki rai ya Maimamiyya ya kuzikutanisha Swala mbili za faradhi katika wakati mmoja hali ya kuwa mtu yuko mjini kwao asiyekuwemo safarini, na hata Sheikh Ahmad As-Sadiq Al-Ghumari alitunga kitabu juu ya jambo hilo alichokitilia *'Izaalatul khatwar Am Man Jamm'aa Baynas Swalatayni Fil Hadhwari'.*



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 117 2/1/2017 3:51:45 PM

cha kutoweza kuziswali Swala zote mbili bali umebaki wa kutosha Swala ya Adhuhuri pekee, basi hapo ataitanguliza Swala ya Alasiri kabla ya Swala Adhuhuri, ataiswali kwa nia ya kuitekeleza ndani ya wakati wake, halafu ataswali Adhuhuri nje ya wakati kwa nia ya kulipa."

Na mafakihi wa madhehebu manne wamesema: "Wakati wa Adhuhuri huanzia tangu jua linapopinduka hadi kivuli cha kila kitu kinapokuwa mfano wa kitu chenyewe, na kinapozidi hapo basi wakati wa Adhuhuri huwa umeshatoweka."

Lakini Mashafi na Maliki wamesema: "Kikomo au mpaka huu unategemea na kuhusika na mtu aliye na wasaa. Ama kwa mtu aliyepindwa na wakati basi wakati wa Adhuhuri huendelea hadi baada ya kivuli kinapozidi mfano wa kila kitu."

Maimamiyya wamesema: "Kurefuka kivuli na kuwa mfano wa kitu chenyewe, huo huwa ni wakati wa fadhila wa Swala ya Adhuhuri, na kivuli kinapokuwa mara mbili ya kitu basi huwa ni wakati wa fadhila wa Swala ya Alasiri."

Na Mahanafi pamoja na Mashafi wamesema: "Wakati wa Alasiri huanza tangu pale kivuli cha kitu kinapozidi urefu wa kitu chenyewe, hadi jua linapotua."

Na Maliki wamesema: "Alasiri ina nyakati mbili, kwanza ni wakati wa hiyari, na pili ni wa ulazima, huo wa kwanza huanzia tangu pale kivuli cha kitu kinapozidi urefu wa kitu chenyewe hadi jua linapokuwa rangi ya manjano, na wakati wa pili huanzia tangu jua linapokuwa rangi ya njano hadi linapotua."

Na Mahanbali wamesema: "Mtu yeyote anayeichelewesha Swala ya Alasiri hadi kivuli kinapozidi urefu wa kitu chenyewe zaidi ya mara mbili Swala yake huwa ni ya kutelekeza (si ya kulipa) na



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 118 2/1/2017 3:51:45 PM

wakati huo huendelea hadi jua linapotua. Lakini mwenye kuswali wakati huo wa kukaribia jua kutua hupata dhambi." Na mahali hapa Mahanbali wamejitenga na madhehebu yaliyobaki.

## WAKATI WA SWALA ZA MAGHARIBI NA ISHA:

Mashafi na Mahanbali (hii ni kulingana na rai za maimamu wawili Shafi na Hanbali) wamesema: "Huanza wakati wa Swala ya Magharibi mara tu baada ya kutoweka mduara wa jua, na humalizika mara tu yanapotoweka mawingu mekundu baada ya jua kutua, ambayo huonekana katika upande wa Magharibi."

Nao Maliki wamesema: "Wakati wa Swala ya Magharibi ni mdogo mno, unaanzia tangu jua linapotua kwa kadiri ya muda unaotosha kuiswali Swala hiyo pamoja na kutekeleza matendo yanayoitangulia na masharti yake, kama vile kujitwahirisha na kuadhini, na hairuhusiwi kuichelewesha kwa makusudi hadi ikatoka nje ya wakati huo, ama palipo na udhuru (wa kisharia) basi wakati wa Swala hii huendelea kudumu hadi alfajiri inapoingia."

Na huko kutokujuzu kuichelewesha Swala ya Magharibi nje kidogo ya mwanzo wa wakati wake, ni jambo walilojitenga peke yao na madhehebu yaliyobaki.

Na Maimamiyya wamesema: "Wakati mahususi wa Swala ya Magharibi ni tangu mara tu jua linapotua[11] kwa kiasi cha kuitelekeza

[11] Kwa Imamiyya Magharibi huthibiti baada tu ya kutoweka mduara wa jua kikamilifu sawa na ilivyo katika madhehebu manne. Lakini wao Imamiyya wamesema kutoweka kwa jua hakuwezi kuthibitishwa na kuhakikishwa kwa kule kutoweka tu mduara wa jua machoni, bali ni kwa kutoweka mawingu mekundu ya upande wa Mashariki kwa kiasi cha urefu wa kimo cha mtu, kwani Mashariki huwa juu ya Magharibi, na kwa hivyo ule wekundu wa Mashariki huwa unatokana na mwangaza wa jua, na kadiri jua linavyodidimia chini wakati wa kutua, ndivyo ule wekundu wa Mashariki huzidi kupanda juu. Ama haya madai ya kuwa Shia hawafuturu katika mwezi wa Ramadhani mpaka pale nyota zitakapochomoza mbinguni, ni madai yasiyo na msingi wowote. Bali ukweli wao wenyewe Shia wamelikanusha hilo katika vitabu vyao vya fikihi, na wamemjibu



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 119 2/1/2017 3:51:45 PM

Swala hiyo, na wakati maalum wa Swala ya Isha ni mwishoni mwa nusu ya kwanza ya usiku kwa kiasi cha muda wa kuitekeleza Swala hiyo. Na wakati ulioko kati ya nyakati hizo mbili ni wakati ambao unazishirikisha Swala mbili, ya Magharibi na Isha. Na kwa ajili hiyo ndipo (Shia) walipojuzisha kukusanya Swala hizo mbili katika wakati unaozishirikisha faradhi hizo mbili.

Na hukmu hii ni kwa ajili ya mtu anayependa na kuamua kufanya hivyo, ama kwa mtu aliyepatwa na dharura ya kupitiwa na usingizi au kusahau basi wakati wa Swala mbili hizo huendelea hadi alfajiri, ambapo Swala ya Isha huhusika na mwisho wa usiku kwa kiasi tu cha muda wa kuweza kuitekeleza, na Swala ya Magharibi huanzia mwanzoni mwa nusu ya pili ya usiku kwa kiasi tu cha muda wa kuweza kuitekeleza.

## WAKATI WA SWALA YA ASUBUHI:

Wakati wa Swala ya Asubuhi ni tangu kuingia alfajiri ya kweli hadi jua linapochomoza, hii ni kwa itifaki ya mafakihi wote, isipokuwa Maliki tu, wao wanasema: "Swala ya Asubuhi ina nyakati mbili; wakati wa kujiamulia nao ni tangu alfajiri inapoingia hadi pale watu wanapotambua sura. Na wakati wa kulazimu, ambao ni tangu watu wanapotambua sura hadi kuchomoza kwa jua."

---

mwenye kudai hayo, kwamba hizo nyota kuna wakati hudhihiri kabla ya jua halijatua na wakati mwingine huchomoza wakati wa kuzama kwa jua, na kuna wakati huchomoza baada ya Magharibi kuingia. Na kwamba ni maluun mwana wa maluun yeyote yule anayeichelewesha Swala ya Magharibi hadi nyota zinapozagaa. Wamesema hivi pale walipowajibu "Khatwabiyyah' wafuasi wa Abul-Khatwab aliyedai maneno hayo. Nao ni miongoni mwa kundi ovu. Na Alhamdulilah kweli umedhihiri. Na siku moja Imam as-Sadiq aliambiwa: "Watu wa Iraq wanaichelewesha Swala ya Magharibi hadi nyota zinapoenea." Akasema: "Tendo hilo hufanywa au linatokana na mafundisho ya adui wa Mwenyezi Mungu Abul-Khatwab."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 120 2/1/2017 3:51:45 PM

# KIBLA

Madhehebu yote yameafikiana kuwa al-Kaaba yenyewe ndio Kibla cha mtu aliye karibu ambaye anaiona. Ama kuhusu mtu aliye mbali asiyeiona wametofautiana rai: Mahanafi, Maliki, Mahanbali na kundi katika Maimamiyya wamesema: "Kwa hakika Kibla cha mtu aliye mbali na al-Kaaba ni upande ule iliyopo al-Kaaba na si al-Kaaba yenyewe."

Mashafi na wengi miongoni mwa Maimamiyya wamesema: "Ni wajibu kuielekea al-Kaaba yenyewe kwa mtu aliye mbali na aliye karibu, kwa uzito mmoja bila ya kutofautinana kati yao. Inapowezekana kupatikana utambuzi wa kuielekea al-Kaaba yenyewe basi ni wajibu kufanya hivyo, la haiwezekani basi hapo ndipo dhana itatosheleza. Na ukweli ni kuwa aliye mbali hawezi kuitimiza kauli hii kwa hali yoyote iwayo, kwani huko ni kujikalifu kwa jambo lililo muhali kulifikia maadamu dunia yetu ina umbo duara kama mpira. Kwa hivyo basi hapa tunaweza tukaamua kwamba Kibla cha mtu aliye mbali ni upande ulioko al-Kaaba na si al-Kaaba yenyewe.

## ASIYETAMBUA KIBLA KIKO WAPI:

Asiyejua Kibla ni upande gani, inampasa afanye bidii ya kuchunguza mpaka apate yakini au dhana kwamba Kibla kipo upande fulani, na kama hakupata utambuzi wa hakika wala wa kudhani, wanavyuoni wa madhehebu manne wamesema: "Ataswali kuelekea upande wowote anaotaka, na Swala yake itaswihi wala haitalazimu kuirudia." Na hivyo ndivyo linavyosema kundi miongoni mwa Maimamiyya, isipokuwa Mashafi tu ndio wamewajibisha kurudia.

Na wengi katika mafakihi wa Maimamiyya wamesema: "Mtu huyo ataswali akizielekea pembe zote nne kwa ajili ya kutekeleza



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 121 2/1/2017 3:51:45 PM

amri ya Swala, na kutaka kuufikia uhakika. Na kama wakati hautoshi kuiswali Swala yake kwa kuelekea pande nne, au hawezi kuswali kwa kuelekea pande nne, basi atatosheka na Swala alizokwisha swali akielekea baadhi ya pande anazoweza.[12]

**Tanzuo**: Mtu anaposwali bila ya kusibu Kibla kilipo, kisha likambainikia kosa lake, Maimamiyya wanasema: "Linapodhihiri kosa na mtu bado yumo ndani ya Swala, na amekengeuka kutoka upande wa Kibla kwa kuelekea baina ya upande wa kulia na kushoto, hatarudia sehemu ya Swala aliyoiswali bali ataendelea na sehemu ya Swala iliyobaki kwa kuelekea mwelekeo sahihi. Na kama itambainikia kwamba kaswali ilihali kaelekea Mashariki au Magharibi au Kaskazini, kwa maana ya kuwa alikipa mgongo Kibla, basi Swala yake itabatilika na italazimu aianze upya. Na atakapogundua kosa kama hilo baada ya kumaliza Swala na akawa bado yumo ndani ya wakati wa Swala hiyo, atairudia, na hatairudia kama wakati umeshatoweka."

Na baadhi ya Maimamiyya wamesema: "Halazimiki kuirudia Swala hiyo awapo ndani ya wakati wala nje ya wakati iwapo amekengeuka kidogo kutoka upande wa Kibla, na atairudia Swala hiyo iwapo yumo ndani ya wakati wa Swala hiyo atakapogundua

---

[12] Imekuja amri hiyo katika Surat al-Baqarah, ya kwamba tuzielekeze nyuso zetu upande ulioko Masjidul Haraam, **"Basi ulekee uso wako upande ulioko msikiti wa Haram." (Al-Baqara:144).** Na katika Aya ya 115 katika Sura hiyo hiyo imekuja amri isemayo tuelekee upande wowote tupendao: **"Na ni ya Mwenyezi Mungu Mashariki na Magharibi basi kokote mnakoelekea mtakuta radhi ya Mwenyezi Mungu." (Al-Baqarah:115).** Watu wengine wamesema: "Hapo hapana iliyofuta wala iliyofutwa. Wala hapana iliyo *khas*, wala *a'mm*. Na njia ya kuzikusanya pamoja Aya mbili hizo ni kuwa iliyo maalum kwa mtu aliyejua Kibla kilipo, basi itamlazimu yeye kuelekea hapo, na ndivyo ilivyofahamika katika hiyo Aya ya kwanza. Na Aya ya pili yamhusu mtu aliyechanganyikiwa ambaye haelewi kabisa Kibla kilipo, na hukmu yake ni kuwa aswali hali ya kuelekea upande wowote anaotaka, na fikra hii ndiyo iliyo karibu kueleweka na kuifuata.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 122 2/1/2017 3:51:45 PM

kwamba ameiswali Swala hiyo kwa kukipa mgongo Kibla, na wala hatairudia iwapo amegundua baada ya wakati kutoweka."

Mahanafi na Mahanbali wamesema: "Anapojibidisha na kujitahidi katika kutafuta Kibla, na akawa hakufaulu kwa kuipata pande yoyote, na akaswali kuelekea upande wowote ule, kisha baadaye likamdhihirikia kosa lake, ikiwa bado angali ndani ya Swala basi atageukia upande alio na yakini nao kwamba ndiko Kibla iliko, au alio na asilimia kubwa kuwa ndiko Kibla kiliko. Na kama alipogundua kosa hilo alikuwa ameshamaliza Swala basi hatalazimika kufanya chochote na Swala yake itakuwa imeswihi."

Mashafi wamesema: "Iwapo litabainika kosa kwa njia ya hakika na yakini atawajibika kurudia Swala, na kama kosa litabainika kwa dhana tu basi Swala itakuwa sahihi bila ya kuweko tofauti ya kuwa alibainikiwa akiwa ndani ya Swala au baada ya kumaliza."

Ama kwa aliyeacha kufanya juhudi ya kutafuta Kibla kisha ikambainikia kwamba ameswibu Kibla, basi Swala yake itakuwa batili kwa mujibu wa Maliki na Mahanbali. Na Swala huwa ni sahihi kwa Mahanafi na Maimamiyya iwapo aliswali bila ya kutia shaka kwa namna ambayo ilipokuwa akiswali alikuwa ana hakika kwamba ameelekea Kibla, kwa maana ya kuwa katika hali hii nia yake ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu imeswihi, kama walivyosema Maimamiyya.

# VIUNGO AMBAVYO NI WAJIBU KUVISITIRI, NA SEHEMU YA MWILI AMBAYO NI HARAMU KUITIZAMA

Maudhui haya ni miongoni mwa maudhui ambayo ndani yake zinachimbuka hukmu nyingi, miongoni mwazo ni kuainisha eneo la mwili ambalo mtu mukallaf (baleghe) ni wajibu kwake kulisitiri. Na miongoni mwazo ni kuainisha eneo la mwili wa mtu mwingine ambalo ni haramu mtu kulitizama. Na miongoni mwazo ni kueleza tofauti kati ya maharimu wa nasabu au wa ukwe na wasiokuwa maharimu. Na miongoni mwazo ni kueleza hukmu ya kumtazama mtu wa jinsia yake au wa jinsia tofauti kati ya mwanamke na mwanamume. Na miongoni mwazo ni kutofautisha kati ya kugusa na kutazama au jambo jingine miongoni mwa mambo ambayo tutagusia hukmu zake katika vipengele vifuatavyo:

## MTU KUJIANGALIA TUPU YAKE:

**1.** Wametofautiana mafakihi wa madhehebu kuhusiana na mtu kujisitiri tupu yake dhidi yake mwenyewe, na je, ni haramu mtu kujifunua tupu anapokuwa peke yake pasipo na mtazamaji mwingine? Mahanafi na Mahanbali wamesema: "Kama ambavyo haijuzu kwa mtu mukallaf kuifichua tupu yake mahali palipo na mtu asiyefaa kumuona uchi wake, hukmu ni hiyo hiyo haifai kuifunua anapokuwa mahali peke yake isipokuwa kwa dharura, kama ya kwenda haja au kuoga."

Na Maliki na Mashafi wamesema: "Si haramu bali ni makruhu tu, isipokuwa wakati wa dharura."

Maimamiyya nao wanasema: "Si haramu wala si makruhu inapokuwa hapana awezaye kumuona."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 124 2/1/2017 3:51:45 PM

Ila jambo la kushangaza ni hii kauli ya Ibnu Abi Layla, ambayo anamkataza mtu kuoga uchi (tuputupu) kwa kuwa ati katika maji kuna chenye kuishi humo. (*Majmuu* sherehe ya *Muhadhab* Juz. 2, Uk. 197).

**MWANAMKE NA MAHARIMU:**

**2.** Mafakihi wa madhehebu wamekhitilafiana kuhusu sehemu ya mwili ambayo ni wajibu kwa mwanamke kujisitiri anapokuwa na maharimu zake wanaume mbali na mumewe, na awapo na mtu wa jinsia yake miongoni mwa wanawake wa Kiislamu.[13] Na kwa kauli nyingine ni upi mpaka wa uchi katika mwili wa mwanamke mbele ya mwanamke mwenzake, na ni upi mbele ya aliye maharimu wake kwa nasaba au ukwe?

Mahanafi na Mashafi wamesema: "Katika hali hii mwanamke (wa Kiislamu) ni wajibu juu yake kujisitiri sehemu iliyoko kati ya kitovu na magoti."

Maliki na Mahanbali wamesema: "Mwanamke awapo kati ya wanawake hutakiwa kujisitiri kati ya kitovu na magoti, na awapo mbele ya maharimu zake wanaume ni lazima ajisitiri mwili wake wote ila pembe tu kama vile kichwa na viganja vya mikono miwili."

Na wengi katika Maimamiyya wamesema: "Humpasa kuzisitiri tupu mbili tu anapokuwa mbele ya wanawake wenzake na maharimu

[13] Aya ya 31 katika Suratun Nuur imebainisha wanawake ambao yajuzu kwa mwanamke kujikashifu miili yao mbele zao na ikataja miongoni mwao kundi hili (*Nisaaihinna*) maana yake wanawake wa Kiislamu, bila ya shaka Aya hii imewakataza kujiachilia sehemu ya miili yao mbele za wanawake wasiokuwa Waislamu. Na hapo Shafiiyya, Malikiyya na Hanafiyya walikuchukulia kukatazwa huku, kuwa ni kukataza kwa kuharamisha. Na kundi kubwa la Imamiyya na Hanbaliyya wamesema: "Hapana tofauti kati ya mwanamke wa Kiislamu na asiyekuwa wa Kiislamu," kama ambavyo kwa Imamiyya ni makruh tu, kwa sababu mwanamke huyo atakwenda msifiya mume wake jinsi alivyomuona yule mwanamke wa Kiislamu umbo lake lilivyo.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 125 2/1/2017 3:51:45 PM

zake, ama kusitiri zaidi ya hapo ni bora zaidi na siyo lazima isipokuwa inapohofiwa kuzuka fitina."

## MWANAMKE NA AJINABI (MTU WA KANDO):

**3.** Sehemu ambazo ni lazima mwanamke ajisitiri anapokuwa mbele ya wanaume wa kando, hapa bila ya shaka mafakihi wa madhehebu yote wameafikiana kuwa ni mwili wake wote, kwani mwili wake wote ni tupu awapo mahali kama hapo, isipokuwa uso na viganja viwili vya mikono. Hii ni kwa mujibu wa Aya ya 31 katika Suratun Nur; **"Wala wasionyeshe uzuri wao, isipokuwa unaodhihirika. Na waangushe shungi zao juu ya vifua vyao."**

Inavyoeleweka hapa ni kuwa makusudio ya neno *Az-zinatu* kwa dhahiri ni uso na viganja viwili vya mikono. Ama neno *Khimar* (mtandio) ni nguo inayokifunika kichwa si ya kufunika (kuziba) uso. Na neno *Jayb* lina maana ya kifua, na bila ya shaka wanawake waliamrishwa wafunike vichwa vyao na mitandio yao waishushe hadi vifuani mwao.

Ama Aya ya 59 katika Suratul-Ahzaab isemayo: **"Ewe Nabii! Waambie wake zako na wake za waumini, wajiteremshie jalbab zao. Hilo ni karibu zaidi kuweza kujulikana wasiudhiwe. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu."** Kwa hakika ilivyo hapa neno *Jalbab* halina maana ya Hijab ya kufunika uso bali ni rinda (gauni) na nguo.

## TUPU YA MWANAMUME:

**4.** Mafakihi wametofautiana kuhusu mipaka ya tupu ya mwenye kutazama na anayetazamwa miongoni mwa wanaume, kwa

maana ya sehemu ya mwili ambayo ni wajibu kwa mwanaume kuisitiri yeye mwenyewe, na sehemu ya mwili ya mwanaume ambayo ni wajibu mtu kutoitazama.

Mahanafi na Mahanbali wamesema: "Mwanamume ni wajibu kwake kusitiri sehemu iliyoko kati ya kitovu na magoti, awapo mbele ya asiyekuwa mkewe, na ni halali kwa mwenginewe, sawa awe mwanamume au mwanamke, maharimu wake au asiyekuwa maharimu wake, kutazama sehemu zisizokuwa hizo katika mwili wa mwanamume ikiwa hapahofiwi kuzuka fitina."

Maliki na Mashafi wamesema: "Tupu ya mwanamume iko katika hali mbili; moja inawahusu wanamume wenzake na wanawake ambao ni maharimu wake. Na nyingine inahusu wanawake ajinabi (wa kando). Ama kuhusu hali ya kwanza, ni wajibu mwanamume ajisitiri sehemu iliyoko kati ya kitovu na magoti peke yake. Na kuhusu hali ya pili, mwili wote wa mwanamume huwa ni tupu, ambapo huwa ni haramu kwa mwanamke ajinabi (wa kando) kumtazama mwanamume huyo." Isipokuwa Maliki wao wamevua katika hukumu hiyo pembe za mwili (kama vile mikono na miguu) wakati panapokuwa na usalama wa kutotokea matamanio.

Na Mashafi wamesema: "Ni haramu moja kwa moja kumtazama sehemu yoyote ya mwili." (*Al-fiqhu Alal Madhabil Arbaa,* Juz. ya kwanza mlango unaozungumzia kujisitiri tupu).

Ama Maimamiyya wao wametofautisha baina ya lililo wajibu kwa mwenye kutazama, na lililo wajibu kwa mwenye kutazamwa, wakasema: "Si wajibu kwa mwanamume kujisitiri zaidi ya tupu ya mbele na ya nyuma tu, lakini ni wajibu kwa wanawake ajinabi (wa kando) kutotazama sehemu nyinginezo za mwili zisizokuwa uso na viganja vya mikono."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 127 2/1/2017 3:51:46 PM

Na rai hii ya Maimamiyya inatudhihirishia kwamba ni ruhusa kwa mwanamume kutazama sehemu za mwili wa mwanamume mwenzake na pia mwili wa mwanamke aliye maharimu wake, isipokuwa tupu ya mbele na ya nyuma tu, iwapo ni bila matamanio. Na vilevile mwanamke anaruhusiwa kuutazama mwili wa mwanamke mwenzake, au wa mwanamume ambaye ni maharimu wake, isipokuwa tupu mbili, iwapo ni bila matamanio.

## MTOTO MDOGO:

**5.** Kuhusu tupu ya mtoto mdogo, Mahanbali wamesema: "Hakuna tupu iliyo haramu kuiangalia kwa mtoto ambaye bado hajafikia umri wa miaka saba. Ipo ruhusa ya kugusa mwili wake wote na pia kuutazama. Na kwa mtoto aliyezidi miaka saba lakini hajafikisha miaka tisa, basi tupu yake ni uchi wa mbele na nyuma awapo ni mwanamume, na awapo ni mwanamke ni mwili wake wote awapo yuko mbele ya wanaume ajinabi (wa kando)."

Mahanafi wamesema: "Hakuna uchi kwa mtoto mwenye umri wa miaka minne na chini yake, na unapozidi umri wa miaka minne basi tupu yake ni mbele na nyuma tu, maadamu hajajua matamanio. Anapofikia makamu ya kutamani, basi hukmu yake itakuwa sawa na hukmu ya mabalehe bila ya kutofautisha kati ya mwanamume na mwanamke."

Na Maliki wamesema: "Yajuzu kwa mwanamke kumwangalia na kumgusa mtoto wa kiume hadi anapofikia umri wa miaka minane, na anaruhusiwa kumtazama bila kumgusa hadi atakapofikia umri wa miaka kumi na miwili, na atakapozidi zaidi ya umri huo basi hukmu yake huwa ni sawa na mwanamume mtu mzima. Na mwanamume anaruhusiwa kumtazama na hata kumgusa binti wa umri wa miaka

miwili na miezi minane, na anaruhusiwa kumtazama bila ya kumgusa hadi atakapofikia umri wa miaka minne."

Mashafi wamesema: "Uchi wa mtoto anayekaribia kubalehe ni sawa na uchi wa mtu balehe. Ama ambaye hajakaribia kubalehe au hawezi kuelezea kitu barabara, basi hana uchi kisharia. Na kama atakuwa hodari wa kuelezea tupu kwa matamanio basi hukmu yake ni kama aliye balehe. Ama mtoto wa kike ambaye hajakaribia kuvunja ungo kama atakuwa anatamanika basi ni kama balehe, la si hivyo, basi hapana chochote, lakini hata hivyo huwa haramu kumtazama tupu yake kwa mtu asiyekuwa mlezi wake."

Maimamiyya wamesema: "Ni wajibu kujisitiri tupu mbele ya mtoto ambaye anaweza kukielezea vyema kitu anachokiona. Ama ambaye hamudu kueleza kitu vyema basi hapa si wajibu kujisitiri mbele yake, maana yeye muda huo huwa ni sawa na hayawani (mnyama). Hili linahusu wajibu wa kujisitiri mbele yake. Ama kuhusu ruhusa ya kutazama uchi wake, Sheikh Ja'far katika kitabu chake *Kashful Ghitaa*, amesema: "Si wajibu kuyazuia macho kutazama tupu ya mtoto ambaye hajafikia umri wa miaka mitano, lakini haijuzu kabisa ikiwa ni kwa matamanio." Na imenibainikia mimi kutokana na Hadith za Ahlulbayti kwamba kutazama kunaruhusiwa hadi anapofikia umri wa miaka sita, na si mitano.

## SAUTI YA MWANAMKE:

**6.** Mafakihi wa madhehehebu yote wamekubaliana kwamba sauti ya mwanamke ajinabi (wa kando) si uchi isipokuwa pale tu panapopatikana matamanio au panapohofiwa kuzuka fitina. Mwenye kitabu *Jawahir* amelithibitisha hilo mwanzoni mwa mlango wa ndoa, kwa kusema kuwa dalili yake ni mwenendo unaoendelea katika miji na zama zote, na dalili nyingine ni ile



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 129 2/1/2017 3:51:46 PM

khutba ya Bibi Zahra na binti zake, na kitendo cha wanawake kuzungumza na Mtume, Maimamu na wanavyuoni kwa njia ambayo haiyumkini kuidhibiti wala kuichukulia kuwa ni kwa dharura. Na pia ni kile kitendo cha wanawake kusimamisha matanga na harusi kati ya wanaume tangu nyakati za kale. Na pia kitendo cha kuzungumza jinsi hizo mbili (mke na mume) mahali pa kazi, na kwa kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema kuwaambia wake za Mtume: **"Wala msilegeze sauti mnaposema,"** hapo bila shaka Mungu alikataza namna maalum ya sauti na kuilegeza.

## NI RANGI SI UMBO:

**7.** Mafakihi wameafikiana lililo wajibu ni kusitiri rangi ya mwili na wala si umbo, (tazama hashia ya mwandishi isemayo): Kama rangi ya sitara (nguo) ni sawa na rangi ya ngozi ya mwili kwa namna ambayo haitawezekana kuipambanua nguo na rangi ya mwili, kama ilivyo katika soksi au glovu, basi kupatikana chenye kusitiri na kutopatikana kwake muda huo huwa ni sawa.

## KATI YA KUTAZAMA NA KUGUSA:

**8.** Kila kinachojuzu kukigusa pia hujuzu kukitazama. Na kila kilicho haramu kukigusa ni haramu kukitazama. Hii ni kwa itifaki ya madhehebu yote, kwani kugusa kuna nguvu zaidi na ndiko kunakotia uchu zaidi kuliko kutazama, na hakuna mwanachuoni yeyote miongoni mwa mafakihi wa madhehebu aliyedai kuwa kuna mwambatano wa hukmu kati ya kujuzu kutazama na kujuzu kugusa, hivyo mwanamume hujuzu kwake kuuangalia uso wa mwanamke wa kando na viganja vyake viwili vya mikono, lakini papo hapo haijuzu kwake kumgusa isipokuwa



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 130 2/1/2017 3:51:46 PM

kwa dharura, kama wakati wa kumtibu mgonjwa (ikiwa hakuna jinsi) na wakati wa kumwokoa anayekufa maji. Na imepokewa Hadith kutoka kwa Imamu Ja'far as-Sadiq isemayo: "Je iko ruhusa kwa mwanamume na mwanamke wasiokuwa maharibu kupeana mkono?" Akasema: "Hakuna ruhusa, isipokuwa kwa nyuma ya nguo."

Mahanafi walitenganisha hukmu ya kumpa mkono mwanamke mkongwe (mzee sana) kama ilivyoandikwa katika kitabu cha Ibnu Abidin Juz. ya kwanza Uk. 284 kwamba. "Si ruhusa kumgusa msichana uso wake na viganja vyake, na hata panapokuwa na tumaini la kutozuka matamanio. Ama mkongwe asiyetamanika basi hapana ubaya kumpa mkono na kuugusa mkono wake kama kuna tumaini la kutozuka matamanio."

Maimamiyya na Mahanafi wamejuzisha kuugusa mwili wa maharimu pasipo matamanio wala ladha (uchu), na Mashafi wamekataza kumgusa yeyote anayeruhusiwa kumtazama miongoni mwa maharimu zake, hadi kwao wao si ruhusa kwa mwanamume kugusa tumbo la mama yake wala mgongo wake, wala asimkande muundi wake na nyayo zake, wala asimbusu uso wake. Vilevile kwao wao si ruhusa kwa mwanamume kumwamuru binti yake wala dada yake amkande mguu wake. (Tazama *Tadhkiratul Al-Laamatil Hulliy* Juz. 2, mwanzoni mwa mlango wa *zawaji*).

## KATI YA KUTAZAMA NA KUFUNUA:

**9.** Maimamiyya wamesema: "Hapana mwambatano wa hukmu kati ya kujuzu kufunua nguo kutoka mwilini na kujuzu kutazama sehemu hiyo iliyofunuliwa, hivyo kwao (Maimamiyya) yajuzu kwa mwanamume kuzivua nguo zake zote kasoro tupu mbili tu, hata hivyo huwa haijuzu kwa mwanamke ajinabi (wa

kando) kumwangalia." Na mimi sijaona katika vitabu nilivyonavyo vya madhehebu manne, licha ya wingi wake, aliyesema hivyo.

**AJUZA:**

**10.** Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَٱلْقَوَٰعِدُ مِنَ ٱلنِّسَآءِ ٱلَّٰتِى لَا يَرْجُونَ نِكَاحًا فَلَيْسَ عَلَيْهِنَّ جُنَاحٌ أَن يَضَعْنَ ثِيَابَهُنَّ غَيْرَ
مُتَبَرِّجَٰتٍۭ بِزِينَةٍ ۖ وَأَن يَسْتَعْفِفْنَ خَيْرٌ لَّهُنَّ ۗ وَٱللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٦٠﴾

**"Na wanawake watu wazima (vikongwe) ambao hawatumaini kuolewa, basi si vibaya kwao kuvua (baadhi) ya nguo zao. Lakini bila ya kuonyesha mapambo yao. Na wakijizuilia (bila ya kuvua) nguo zao ni bora kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, (na) Mwenye kujua." (An-Nur:60).**

Aya hii tukufu inatufundisha kuwa wanawake wakongwe ambao hawana tamaa ya kuolewa hakuna kosa juu yao kutokana na uzee wao kuziacha wazi nyuso zao na baadhi ya sehemu ya nywele zao na miili yao na sehemu nyenginezo ambazo kwa kawaida huwa wamezowea kuziacha wazi. Na Hadithi iliyopokewa kutoka kwa Ahlul Bait inaongeza dalili juu ya jambo hilo kwamba, ni sharti kuwa isiwe kuvua baadhi ya nguo zao ni kwa lengo la mtindo wa kujionyesha mapambo ya miili yao, bali ruhusa hiyo ipo wanapokuwa wanatoka kwa ajili ya kushughulikia haja zao za muhimu, pamoja na kuwepo ruhusa hiyo, lakini hata hivyo kujisitiri ni bora zaidi juu yao.[14]

Hapa yataka ieleweke kuwa pamoja na kuwepo ruhusa kama hiyo lakini inaondolewa inapokuwa inaweza kumwingiza katika kufanya jambo lililoharamishwa, kwa sababu mwanamke hata

[14] *Jawaahir* mwanzoni mwa mlango wa ndoa.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 132 2/1/2017 3:51:46 PM

anapofikia umri mkubwa kiasi gani bado huendelea kuwa sehemu ya kuweza kufanya kitendo cha ndoa. Na ruhusa aliyoipata ni kutokana na kule kuchukuliwa kuwa yeye ni sawa na mtoto mdogo hadhaniwi kwamba anaweza kuwa na uchu au kutamani tendo kama hilo. Basi iwapo itapatikana uhakika wa kuwa na matamanio ya kimaumbile, hukmu hiyo inageuka mara moja na kuwa yuko sawa sawa na msichana kihukmu.

Uislamu umelegeza masharti hayo kwa wanawake watu wazima mno na ukayatilia mkazo kwa msichana. Lakini hivi sasa mambo yako kinyume na ilivyoamuru Qur'ani tukufu ambapo leo hii tunaona kutangatanga na kuonyesha uzuri wa mapambo ya mwili kwa wasichana likiwa ndilo jambo la kawaida na kina mama watu wazima ndio wanaojisitiri na kujihifadhi. Hii ina maana kuwa tumelegezea katika jambo alilolitilia mkazo Mwenyezi Mungu na kutilia mkazo jambo alilolilegeza.

## SEHEMU YA MWILI AMBAYO NI WAJIBU MTU KUISITIRI PINDI AWAPO KATIKA SWALA

Mafakihi wote wameafikiana kuwa ni wajibu kwa mwanamume na mwanamke, wanapokuwa katika Swala, kuisitiri sehemu ile ambayo ni wajibu kwa mtu kuisitiri anapokuwa mbele ya watu ajinabi (wa kando) pale awapo nje ya Swala. Kisha wakatofautiana kuhusu sehemu iliyozidi hapo, kwa maana je, ni wajibu pia kwa mwanamke kujisitiri uso na viganja vya mikono, au sehemu yake pindi anapokuwa katika Swala, pamoja na kuwa si wajibu kwake kufanya hivyo nje ya Swala? Na je, ni wajibu kwa mwanamume kujisitiri zaidi ya sehemu iliyoko kati ya kitovu na magoti wakati awapo ndani ya Swala,



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 133 2/1/2017 3:51:46 PM

pamoja na kuwa si wajibu kwake kufanya hivyo anapokuwa nje ya Swala?

Mahanafi wamesema: "Mwanamke anapokuwa ndani ya Swala hulazimika kujisitiri sehemu ya maungo ya viganja vyake vya mikono na pia matumbo ya nyayo za miguu, na mwanamume ni juu yake ajisitiri juu zaidi ya sehemu iliyo kati ya kitovu na magoti."

Mashafi na Maliki wamesema: "Inajuzu kwa mwanamke awapo katika Swala kuuacha wazi uso wake, viganja vyake vya mikono, nje yake na ndani yake." Mahanbali wamesema: "Haijuzu kwa mwanamke awapo katika Swala kujiacha wazi isipokuwa uso peke yake."

Maimamiyya wamesema: "Ni wajibu kwa wote wawili mwanamume na mwanamke wakiwa ndani ya Swala kujisitiri kila sehemu ambayo ni wajibu kujisitiri anapokuwa nje ya Swala. Na kama pana watu wa kando wanaoweza kumtazama, basi mwanamke anaruhusiwa kujifunua uso wake kwa kadiri ambayo huiosha wakati wa kutawadha na viganja viwili hadi kwenye viwiko, na nyayo mbili, nje yake na ndani yake, hadi mwanzo wa miundi. Na ni wajibu kwa mwanamume ajisitiri tupu zake, na bora zaidi ni kujisitiri sehemu iliyo kati ya kitovu na magoti."

## MASHARTI YA CHENYE KUSITIRI KATIKA SWALA:

Vyenye kusitiri vina masharti ambayo hapana budi yatimie panapokuwa na uwezo wa kuyatekeleza na wakati wa kujiamulia, nayo ni:

## TOHARA:

**1.** Utohara wa nguo anazojisitiri mtu na mwili ni shariti katika masharti ya kuswihi Swala. Hiyo ni kwa maafikiano ya mafak-



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 134 2/1/2017 3:51:46 PM

ihi wote, isipokuwa kila madhehebu miongoni mwa madhehebu za Kiislamu imetenga vitu vyake vinavyosamehewa katika Swala kulingana na maelezo yanayofuata:

Maimamiyya wamesema: "Husamehewa (katika Swala) damu ya jeraha (kidonda) na usaha, iwe ni nyingi au chache, nguoni na mwilini, inapokuwa kuiondoa kwake kutasababisha taabu kubwa (kama imekuwa vigumu kuiondoa), na damu kidogo iliyo ndogo zaidi kuliko dirhamu iwapo ni ya huyo mtu anayeswali au mwinginewe, kwa sharti ya kuwa damu hiyo iwe iko mahali pamoja haikutawanyika. Na wala isiwe inatokana na damu tatu: Hedhi, nifasi na istihadha, na wala isiwe inatokana na damu ya mnyama ambaye ni najisi kama vile mbwa na nguruwe, wala damu ya mzoga.

Vilevile husamehewa katika najisi iwapo katika kile kisichotimiza Swala, kama vile mkanda kofia, soksi, viatu, pete na kikuku, na pia kitu kinachobebeka kama kisu na karatasi ya pesa (noti). Na pia nguo ya mlezi wa mtoto mchanga, sawa awe ni mama mzazi au mwenginewe, kwa sharti aifue mara moja kila siku, tena iwe inakuwa vigumu kuibadilisha, na kadhalika kwao (Maimamiyya) husamehewa kila najisi iwayo nguoni au mwilini wakati wa dharura."

Maliki wamesema: "Husamehewa najisi ya mtu mwenye ugonjwa wa kutokwa na mkojo, na mwenye maradhi ya kutokwa na haja kubwa, na mwenye maradhi ya kutokwa na majimaji sehemu ya makalio, na najisi inayompata mlezi mwilini mwake au nguoni mwake kutoka kwa mtoto anayemlea kama vile mkojo na kinyesi, na najisi inayoingia nguoni mwa mchinjaji, marasharasha yanayoruka kutoka mahali panapoogewa, na yanayompata twabibu anayeponya vidonda, na damu hata kama ni ya nguruwe (husamehewa), kwa sharti isiwe inazidi uduara wa dirham, na damu itokayo kwenye majipu, na choo cha viroboto." Na vitu vyenginevyo visivyokuwa hivi ambavyo tumeviacha kwa kuwa si sana kutokea ila mara chache tu.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 135 2/1/2017 3:51:46 PM

Mahanafi wamesema: "Husamehewa katika najisi iwapo ni kadiri ya kipimo cha dirhamu, sawa iwe ni damu au chenginecho, na kinyesi cha paka au panya katika hali ya dharura, na marasharasha ya mkojo yanapokuwa ni mepesi sawa na ncha ya sindano, na damu inayomrukia mchinjaji kwa dharura, na mchanga wa barabarani hata kama umechanganyika na najisi kwa wingi ikiwa hakitaonekana kiini cha najisi." Na hivyo husamehewa kwao wao najisi iliyo nyepesi, kama mkojo wa mnyama anayeliwa nyama yake iwapo utaswibu robo ya nguo au chini ya robo ya mwili.

Mashafi wamesema: "Husamehewa aina yoyote ya najisi inapokuwa kidogo ambayo haionekani, na mchanga wa barabarani uliochanganyikana na najisi nyepesi, na choo cha wadudu waishio ndani ya matunda na jibini, na najisi ya majimaji ambayo huongezwa kwenye madawa na kwenye harufu ya uturi, na kinyesi cha ndege na nywele chache zinazotokana na wanyama wasiokuwa mbwa na nguruwe." Na nyinginezo ambazo zimetajwa katika vitabu vilivyoelezea masiala haya kwa kirefu.

Mahanbali wamesema: "Husamehewa katika damu na usaha viwapo ni vyepesi, na vumbi la mchanga wa barabarani ambao upo uhakika wa unajisi wake, na najisi inayoliswibu jicho la mwanaadamu na ni dhiki kuiosha."

## KUVAA HARIRI:

**2.** Mafakihi wa madhehebu yote wameafikiana kuwa kuvaa hariri na dhahabu kumeharamishwa kwa wanaume wanapokuwa ndani ya Swala au nje ya Swala; na inaruhusiwa kwa wanawake. Hii ni kulingana na Hadith ya Mtume ﷺ: 'Zimeharamishwa nguo za hariri na dhahabu kwa wanaume wa umati wangu, na zimehalishwa kwa wanawake wao."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 136 2/1/2017 3:51:46 PM

Na kutokana na Hadith hii ndipo Maimamiyya waliposema: "Haiswihi Swala kwa mwanamume aliyevaa hariri halisi, wala kwa kuvaa nguo iliyotomelewa kwa dhahabu, sawa iwe ni mkanda, kofia au soksi, hata pete pia si ruhusa." Kisha walijuzisha kuvaa hariri na kuswali na nguo hiyo kwa ajili ya maradhi au anapokuwa vitani.

Na Mashafi wamesema: "Mtu anaposwali hali ya kuwa amevaa hariri au akasujudu juu ya nguo ya hariri huwa anafanya jambo la haramu, lakini hata hivyo Swala yake huwa swahihi. (Amesema hivyo An- Nawawiy katika *Sharhul Muhadhab,* Juz. 3, uk. 179).

Mimi sijapata kauli inayoeleweka ya madhehebu mengine yaliyobaki ambayo inaelezea kinaganaga juu ya kuswihi Swala au kutoswihi anaposwali mtu hali amevaa hariri, lakini hata hivyo Mahanafi, na vilevile Mahanbali katika mojawapo ya riwaya mbili, wamewaafiki Mashafi kuhusu kaida jumuishi, isemayo kuwa inapokuwa katazo lililotolewa halikutolewa kwa ajili ya Swala wala halirudii kwenye Swala, kama ilivyokatazwa kupora (kunyang'anya), basi katika hali hii Swala huwa ni swahihi lakini huyo mukallaf huwa ametenda kitendo kilichoharamishwa, na papo hapo ametekeleza kitendo cha wajibu, na kwa hivyo basi Swala ile aliyoiswali akiwa amevaa hariri huwa ni swahihi.

Na mwenye kitabu *Al-Fikhu Ala Madhahibil Arbaa* amenukuu kauli ya itifaki kati ya madhehebu kwamba aliyelazimika kwa dharura kuswali na nguo ya hariri, Swala yake huswihi na halazimiki kuirudia tena.

## UHALALI WA NGUO ANAZOVAA MTU WAKATI WA KUSWALI:

**3.** Maimamiyya wameweka sharti kuwa nguo anazovaa mtu wakati anaposwali ni lazima ziwe ni za halali, na lau ataswali



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 137 2/1/2017 3:51:46 PM

na nguo alizozipata kwa njia ya kunyang'anya, basi Swala yake huwa batili iwapo anajua kuwa nguo hizo ni za kunyang'anya. Na hii pia ndiyo kauli ya Ahmad bin Hanbal katika moja ya riwaya zilizopokewa kutoka kwake.

Na mafakihi wa madhehebu yaliyobaki wamesema kwamba huswihi Swala inayoswaliwa na nguo za kunyang'anya, maana katazo hilo halikuhusu Swala, hata lizuie kuswihi kwake. Ama Imamiyya wao wametilia mkazo suala la nguo za kunyang'anya hadi baadhi yao wamefikia kusema: "Lau kama mtu ataswali na nguo ambayo ndani yake mna uzi mmoja tu wa kunyang'anya, au akawa amebeba kisu au dirhamu au kitu chochote cha kunyang'anya, basi Swala yake haiswihi." Lakini hata hivyo wamesema: "Anaposwali mtu na nguo za kunyang'anya bila ya kujua au kwa kusahau basi Swala itaswihi."

## NGOZI YA MNYAMA ALISIYELIWA NYAMA YAKE:

**4.** Maimamiyya wamejitenga peke yao kwa kauli yao kuwa, haiswihi Swala inayoswaliwa katika ngozi ya mnyama asiyeliwa nyama yake hata inapotiwa dawa ya kusafisha ngozi, wala Swala haiswihi katika nywele zake wala sufi zake, manyoya yake wala mabaki yake kama vile mate yake na jasho lake maadamu tu ni majimaji, na lau unywele mmoja tu kutoka mwilini mwa paka au mwingine mfano wake utaangukia juu ya nguo ya mtu anayeswali, naye akaendelea na Swala yake baada ya kuwa ameshauona basi Swala yake itabatilika.

Kisha wameengua katika hukmu hiyo mshumaa na asali, damu ya kunguni, chawa na viroboto na walio kundini mwao kati ya wadudu wasiokuwa na nyama. Kama walivyoengua nywele za mwanadamu, jasho lake na nyute zake (udenda). Wakasema tena hutokea kubatilika



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 138 2/1/2017 3:51:46 PM

kwa Swala iwapo nguo iliyomsitiri mwenye kuswali ina sehemu ya mnyama mfu, sawa awe ni yule anayeliwa nyama yake au haliwi, mwenye damu ya kuchururuzika au la, anayedaghibiwa ngozi au asiyedabighiwa.

**Tawi**: Ikiwa hakuna budi ila mtu kujisitiri kwa nguo iliyonajisiwa kwa najisi isiyosamehewa, kwa kiasi cha kufungika kati ya mambo mawili, ima aswali na nguo hiyo iliyonajisika au aswali uchi? Atafanya nini?

Mahanbali wamesema: "Aswali na nguo hizo zilizonajisika kisha itamlazimu kuirudia Swala hiyo." Maliki wamesema na kundi kubwa katika Maimamiyya: "Ataswali na hiyo nguo iliyonajisika wala haitamlazimu kuirudia Swala hiyo." Mahanafi na Mashafi wamesema: "Ataswali uchi, wala haifai kuvaa nguo iliyonajisika awapo ndani ya Swala."

# MAHALI PA KUSWALIA

## MAHALI PALIPONYANG'ANYWA:

Maimamiyya wamefikia kusema kuwa Swala inayoswaliwa mahali paliponyang'anywa hubatilika, na vilevile inayoswaliwa hali anayeswali amevaa nguo za kupora kwa kuhiari bila ya kulazimika huku akijua kwamba nguo hizo ni za kunyang'anya. Na wasiokuwa wao wamesema: "Swala huswihi, na anayeswali hupata dhambi, kwa maana ya kuwa katazo la kupora halikuihusu Swala (kwa hiyo Swala huswihi na hapo hapo hupata dhambi ya kupora), bali dhambi au katazo hilo lilihusu matumizi ya nguo kama hizo, ni kama kuswali na nguo ya kunyang'anya.

Ni umbali ulioje uliopo kati ya madhehebu hayo manne yanayoiswihisha Swala ya mnyang'anyi anayoiswali hali anatumia



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 139 2/1/2017 3:51:46 PM

mali ya kunyang'anya, na kauli ya Zaydiyya isemayo kwamba Swala ya mmiliki halali haisihi maadamu milki yake ingali mikononi mwa mtu mwingine, hiyo ni kutokana na katazo la kutumia vitu vilivyoporwa.

Na kauli ya Maimamiyya iko kati ya hizo mbili, ambapo wameswihisha Swala ya mmiliki halali na ya mtu aliyepewa idhini, na wakaibatilisha Swala ya mporaji na ya mtu aliyeswali bila ya idhini ya mmiliki halali. Kisha Maimamiyya wamejuzisha kuswali katika ardhi kubwa ambazo ni vigumu au haiwezekani watu kujiepusha nazo, hata isipopatikana idhini kutoka kwa mwenye miliki hiyo.

## UTOHARA WA MAHALI PA KUSWALIA:

Wamesema mafakihi wa madhehebu manne: "Mahali pa kuswalia ni sharti pawe tohara kutokana na najisi zenye kuhama na zisizokuwa za kuhama, yaani za majimaji au zilizo kavu."

Mashafi wametilia mkazo zaidi kwa kusema: "Ni wajibu kiwe tohara chochote kile ambacho kinagusana na mwili au nguo za anayeswali, hivyo kama atagusana na ukuta wenye najisi au nguo iliyo na najisi, au atashika najisi, au kamba ambayo baadhi ya sehemu yake imo kwenye najisi, basi Swala yake itabatilika."

Mahanafi wao wametosheka na utohara wa mahali pa kutosha nyayo mbili na anapoweka kipaji cha uso peke yake. Na Maimamiyya wameweka sharti kwamba mahali anapoweka paji lake la uso peke yake ndipo pawe tohara. Ama najisi isiyokuwa mahali hapo haibatilishi Swala kwa sharti kwamba, najisi hiyo isihame hadi kuufikia mwili wa anayeswali au nguo zake.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 140 2/1/2017 3:51:46 PM

## KUSWALI JUU YA MNYAMA:

Mahanafi na Maimamiyya wameweka sharti kwamba ni wajibu mahali pa kuswalia pawe ni penye kutulia, hivyo kwao wao haifai kuswali juu ya mnyama wala juu ya bembea na sehemu nyingine mfano wa hizo isipokuwa kwa dharura, kwani mwenye udhuru huswali kulingana na uwezo wake.

Mashafi, Maliki na Mahanbali wamesema: "Huswihi Swala juu ya mnyama wakati wa amani na uwezo, iwapo ataiswali kikamilifu na kutekeleza masharti yake."

## KUSWALI NDANI YA AL-KAABA:

Maimamiyya, Mashafi na Mahanafi wamesema: "Hujuzu kuswali ndani ya Al-Kaaba, sawa iwe ni Swala ya faradhi au ya Sunna." Maliki na Mahanbali wamesema: "Ndani ya Al-Kaaba hujuzu kuswali Swala ya Sunna tu wala haijuzu kuswali Swala ya faradhi."

## MWANAMKE KUSWALI KANDO YA MWANAMUME:

Wamesema kundi katika Maimamiyya: "Anaposwali mwanamume na mwanamke mahali pamoja, na mwanamke akawa ndiye aliyemtangulia mwanamume, au wapo sawa ilihali kati yao hakuna kizuizi au umbali wa dhiraa kumi za mkono, Swala ya aliyeanza kabla ya mwenzake haitabatilika, bali haitaswihi ya wa pili, na kama wataanza pamoja kwa wakati mmoja basi wote wawili Swala zao hubatilika."

Mahanafi wamesema: "Anapotangulia mwanamke au akawa yuko sawasawa na mwanamume basi Swala ya mwanamume na mwanamke hubatilika maadamu tu mahali pao wanaposwalia ni pamoja, na hapana kizuizi cha kadiri ya dhiraa moja kinachotenganisha



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 141 2/1/2017 3:51:46 PM

kati yao, na mwanamke mwenyewe si wa kutamanika, na wala asilingane naye sawa kwa muundi wala bega, na wala isiwe ni katika Swala ya jeneza, na Swala yenyewe iwe ni yenye kuwashirikisha wote, kama kuwa huyo mwanamke ni maamuma wa mwanamume au wote wawili wanamfuata Imamu mmoja."

Mashafi, Mahanbali na wengi katika Maimamiyya wamesema: "Swala huswihi, licha ya kuwa ni makruhu."

## MAHALI PA KUWEKA PAJI LA USO WAKATI WA KUSUJUDU:

Mafakihi wote wamekubaliana kuwa mahali panapowekwa paji la uso wakati wa kusujudu ni lazima pawe ni penye kutulia, na wala pasiwe pameinuka kuliko mahali pa magoti mawili, mwinuko wa kupita kawaida, kisha wametofautiana katika kitu kinachoswihi kusujudu juu yake.

Maimamiyya wamesema: "Haifai kusujudu isipokuwa juu ya ardhi, au kilichozalika ardhini katika vitu visivyoliwa wala visivyovaliwa, anayeswali haruhusiwi kusujudu juu ya sufi, pamba, madini na wala juu ya kitu kilichoota juu ya maji, kwa sababu maji si ardhi." Na wameruhusu mtu kusujudu juu ya karatasi, kwa kuwa malighafi yake imetokana na mmea wa ardhini, na madhehebu yao imetoa dalili ya kuwa kusujudu ni ibada ya kisheria ambayo ni lazima utekelezaji wake uambatane na nususi ya kisheria.

Na mafakihi wote wamekongamana juu ya kuswihi kusujudu juu ya ardhi na kilichotokana na ardhi, na hapa kwa ufupi tutatosheka na kauli ya Mtume ﷺ: "Haitimu Swala ya mmoja wenu mpaka atawadhe kama alivyoamuru Mwenyezi Mungu, kisha asujudu kwa kutuliza paji la uso wake ardhini." Na kauli yake: "Imeumbwa ardhi kuwa ni mahali pa kusujudu na ni yenye kutwahirisha." Na Khabbab



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 142 2/1/2017 3:51:46 PM

alisema: "Tulimlalamikia Mtume wa Mungu ﷺ joto la ardhi wakati wa kiangazi linavyounguza mapaji yetu ya nyuso (tunaposujudu), wala Mtume hakuyasikiliza." Hivyo basi kama kungekuwa na uwezekano wa kusujudu juu ya tandiko wasingelilalamika.

Kisha Maimamiyya wamejuzisha kusujudu juu ya pamba na katani palipo na dharura.

Na mafakihi wa madhehebu manne wamesema: "Inajuzu kusujudu juu ya kila aina ya kitu, hata juu ya mkia wa kilemba na juu ya duara la kilemba kwa sharti kiwe tohara tu." Bali Mahanafi wamejuzisha juu ya kiganja cha mkono, lakini ni makuruhu.

# ADHANA

Mwadhini:

Neno *Adhana,* katika lugha (ya Kiarabu), lina maana ya tangazo, na katika istilahi ya Sharia ni tangazo linalowajulisha watu kuingia kwa wakati wa Swala, kwa kutumia matamko maalum. Sharia ya Adhana iliwekwa katika mwaka wa mwanzo wa Hijra ya Mtume ﷺ huko Madina. Na namna ya kuwekwa kwake kwa Shia ni kwamba Jibril alishuka kwa Mtume kutoka kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t.) akamletea hiyo Adhana. Na kwa Sunni ni kwamba Abdilahi bin Zayd alimuona mtu ndotoni alipokuwa amelala akamfundisha kuadhini, akaenda kumweleza Mtume ﷺ ndoto yake, Mtume akakubali na hatimaye akaiweka Adhana.

## ADHANA NI SUNNAH:

Mahanafi, Mashafi na Maimamiyya wamesema: "Kuadhini ni Sunna iliyosisitizwa."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 143 2/1/2017 3:51:46 PM

Mahanbali wamesema: "Adhana ni faradhi ya kutosheleza katika kijiji na mijini, kwa ajili ya Swala tano za faradhi, kwa wanaume wawapo kwao, si safarini."

Maliki wamesema: "Ni wajibu wa kutosheleza katika mji ambao huswaliwa Swala ya Ijumaa, iwapo watu wote wa mji huo wataacha kuadhini basi watapigwa vita juu ya kosa hilo la kuacha kuadhini."

## HAIJUZU KUADHINI KWA AJILI YA MAMBO KADHAA:

Mahanbali wamesema: "Haijuzu kuadhini kwa ajili ya Swala ya jeneza, Swala ya Sunna wala Swala ya nadhiri." Maliki wamesema: "Haijuzu kuadhini kwa ajili ya Swala ya Sunna, wala iliyopita na Swala ya jeneza." Mahanafi wamesema: "Haijuzu kuadhini kwa ajili ya Swala ya maiti, Swala ya Iddi mbili, Swala ya kupatwa jua na Swala ya kuomba mvua, katika Swala ya tarawehe wala Swala yoyote miongoni mwa Swala za Sunna." Mashafi wamesema: "Haijuzu kuadhini kwa ajili ya Swala ya jeneza wala za Sunna."

Maimamiyya wamesema: "Sharia ya Adhana inahusu Swala tano za kila siku pekee, na hupendekezwa kuadhini katika Swala hizo, iwe ni ndani ya wakati wa Swala anayotaka kuiswali au wakati wa kulipa, iwe ni jamaa au mtu mmoja, awe safarini au mjini kwake, kwa wanawake na wanaume, wala haijuzu kuadhini kwa ajili ya Swala nyingine yoyote, sawa iwe ni ya Sunna au ya wajibu, bali mwadhini hutakiwa kusema katika Swala ya kupatwa kwa jua na Swala ya Iddi mbili: '*Aswalah'* mara tatu.

## MASHARTI YA ADHANA:

Mafakihi wa madhehebu yote wamepatana kuwa ni katika masharti ya Adhana kufuatanisha maneno ya Adhana na kufuata mpangilio kati ya vipengele vya Adhana, na mwadhini awe ni mwanamume



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 144 2/1/2017 3:51:47 PM

Mwislamu,[15] na mwenye akili timamu, na pia huswihi Adhana kutoka kwa mwadhini mtoto mtambuzi. Pia wote wamekubaliana kwamba si sharti kwa mwenye kuadhini kuwa tohara, kisha walikhitilafiana katika mambo yasiyokuwa hayo.

Mahanafi na Mashafi wamesema: "Yaswihi kuadhini bila ya kutia nia." Na madhehebu yaliyobaki yamesema, haiswihi bila ya kunuia. Mahanbali wamesema: "Hujuzu kuadhini kwa lugha isiyokuwa ya kiarabu."

Maliki, Mahanafi na Mashafi wamesema: "Haijuzu kwa Mwarabu kuadhini kwa lugha isiyokuwa ya Kiarabu, na hujuzu kwa asiyekuwa mwarabu kuadhini kwa lugha yake mwenyewe anapokuwa anataka kuswali peke yake na kwa jamaa wasiokuwa Waarabu."

Maimamiyya wamesema: "Haijuzu kuadhini kabla ya kuingia wakati wa Swala ya faradhi isipokuwa Swala ya Alfajiri." Mashafi, Maliki, Mahanbali na wengi katika Maimamiyya wamesema: "Inajuzu mwadhini kutanguliza Adhana ya kujulisha watu kuwa kumepambazuka kabla ya wakati wa Swala ya Alfajiri haujaingia." Mahanafi wamelikataa hilo, na hawakutofautisha kati ya Swala ya Alfajiri au nyengineyo, na ndio bora zaidi.

## NAMNA YA KUADHINI:

*Allahu Akbar,* mara nne kwa madhehebu yote isipokuwa Maliki, wao wamesema atasema mara mbili.

*Ashhadu Anlailaha Ilallah,* mara mbili kwa madhehebu yote.

[15] Imamiyya wamesema: "Yasunniwa kwa mwanamke anapotaka kuswali aadhini lakini si kwa lengo la kutangaza, kama ambavyo imependekezwa kuadhiniwa katika Swala ya jamaa ya wanawake, mmoja wao aadhini kisha akimu, lakini waume wasimsikie sauti yake." Na kwa Maimamu wanne wanasema: "Yapendeza kwao wao kukimu tu, na kuandini ni makruh."

*Ashhadu Anna Muhammadan Rasululah,* mara mbili kwa wote.

*Hayya Alas-Swalah,* mara mbili kwa wote.

*Hayya Alal-Falah,* mara mbili kwa wote.

*Hayya Alaa Khayril -Amal,* mara mbili, kwa Maimamiyya tu.

*Allahu Akbar,* mara mbili kwao wote.

*Lailaha Ilallah,* mara moja kwa madhehebu manne, na mara mbili kwa Maimamiyya.

Maliki na Mashafi wamejuzisha kuirudia (kuikariri) mara mbili, lakini hiyo ya pili itakuwa ni Sunna. Maana yake ni kuwa, Adhana huwa haibatiliki kwa kutosheka kuadhini mara moja, ni kama wanavyosema Shia Imamiyya, na huko huitwa *Iadah* (kurudia tena).

Mwenye kitabu *Al-Fiqh Alal-Madhahab Arbaa* amenukuu itifaki ya madhehebu manne juu ya kufanya *tathwib,* nako ni kuongeza maneno *'As-swalatu Khayrun Minan Nawm'* mara mbili baada ya kusema *Hayya Alal-Falah,* na Maimamiyya wamekataza jambo hilo.[16]

## KUKIMU SWALA:

Yasunniwa kukimu Swala kwa wanaume na wanawake, katika Swala za faradhi za kila siku, na hufuatiwa Swala ya faradhi moja kwa moja mara tu baada ya kukimu. Na hukmu yake ni kama hukmu

[16] Ibnu Rushd amesema katika kitabu *Bidayatul Mujtahid* Jz. 1, uk. 103, chapa ya 1985: "Wengine walisema: 'Hapana ruhusa ya kusema *As-swallatu khayrum minan nawm*, kwani maneno hayo si katika maneno ya adhana iliyosunniwa. Na hivyo ndivyo alivyosema Shafi, na sababu ya kutofautiana ni kuwa je, maneno haya yalisemwa wakati wa Mtume ﷺ au yalisemwa wakati wa Khalifa Umar? Na katika kitabu *Al-Mughni* cha Ibnu Quddamah Juz. 1, uk. 408, chapa ya tatu amesema: "Amesema Is'haq: Kitu hiki kimezuliwa na watu." Na Abu Isa amesema: Hii ni *Tathwiib* ambayo walichukia (na kuikataa) wanavyuoni, na ndiyo ile ambayo Abdallah bin Umar alitoka msikitini mara tu alipoisikia."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 146 2/1/2017 3:51:47 PM

ya Adhana katika kufuatanisha, kufuata mpangilio katika vipengele vyake na kuyatamka maneno yake kwa lugha ya Kiarabu, na mfano wa hukmu hizo.

Na hii ndio namna ya kukimu:

*Allahu Akbar,* mara mbili kwa madhehebu yote isipokuwa Mahanafi ambao hapa waliifanya mara nne.

*Ashhadu Anlailaha Ilallah,* mara moja kwa Mashafi na Maliki na Mahanbali, na mara mbili kwa Mahanafi na Maimamiyya.

*Ashhadu Anna Muhammadan Rasululah,* mara moja kwa Mashafi na Maliki na Mahanbali, na mara mbili kwa Mahanafi na Maimamiyya.

*Hayya Alas-Swalah,* mara moja kwa Mashafi, Maliki na Mahanbali. Na ni mara mbili kwa Mahanafi na Maimamiyya.

*Hayya Alal-Falah,* mara moja kwa Mashafi, Maliki na Mahanbali. Na ni mara mbili kwa Mahanafi na Maimamiyya.

*Hayya Alaa Khayril -Amal,* mara mbili kwa Maimamiyya peke yao.

*Qad Qaamatis-Swalah,* mara mbili kwa wote isipokuwa kwa Maliki tu, kwao ni mara moja.

*Allahu Akbar,* mara moja kwa wote.

*Lailaha Ilallah,* mara moja kwa wote.

Na kundi katika Maimamiyya limesema: "Yajuzu kwa msafiri na mwenye haraka kutosheka na mara moja katika kila kifungu wakati wa kukimu, na katika kuadhini kadhalika."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 147 2/1/2017 3:51:47 PM

# FARADHI ZA SWALA NA NGUZO ZAKE

Kuswihi kwa Swala kunahitaji utohara kutokana na hadath na khabathi, kuingia kwa wakati, kuelekea Kibla na kupatikana chenye kuusitiri mwili, na hapana budi mtu ahakikishe kwamba mambo haya yametimia kabla hajaingia kwenye Swala. Na mambo haya huitwa *Masharti* (mambo ambayo bila ya hayo Swala haiswihi). Na maneno kuhusu masharti tumetangulia kuyataja kwa kifupi. Na Swala pia ina nguzo na faradhi ambazo zinafungamana nayo, mambo hayo hutekelezwa moja kwa moja wakati wa kutekeleza tendo la Swala, na nguzo hizo ni nyingi:

## KWANZA, KUTIA NIA:

**1.** Madhehebu yamekhitilafiana mahali hapa, bali hata mafakihi wa madhehebu moja pia wamekhitilafiana wenyewe kwa wenyewe kuhusu lile ambalo ni wajibu mwenye kuswali kulinuwia, wanasema; Je, ni wajibu mtu anuie kwa kutaja Swala anayotaka kuiswali, kwa mfano – anuie kwa kusema hii ni Adhuhuri au Alasiri, na kuitaja kuwa ni faradhi au ni Sunna, na kuwa ni Swala yenye rakaa kamili au ni ya kukusuru, na anaiswali akiwa yumo ndani ya wakati au analipa, na mengine yasiyokuwa hayo.

Na uhakika wa nia ni kama tulivyotangulia kueleza katika mlango wa wudhu, ni ibara inayoelezea kusudio la kitendo kwa msukumo wa kumtii Mungu na kufuata amri yake. Ama *kuleta uainisho* (kutaja jina la Swala) na kukusudia kuitaja kwamba ni ya faradhi au ni ya Sunna, ni ya kutekeleza ndani ya wakati au ni kulipa, kitu hicho hutokea chenyewe kulingana na dhamira na nia yake (hata bila ya kutaja), hivyo ikiwa tangu mwanzoni alikuwa amekusudia



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 148 2/1/2017 3:51:47 PM

kuswali Swala ya Sunna na akaiswali kwa kusudio hilo basi huwa ni ya Sunna, na kama amekusudia Swala ya faradhi ya Adhuhuri au Alasiri basi huwa kama alivyokusudia vivyo hivyo. Na kama hakukusudia chochote katika Swala yake, basi huwa si chochote Swala yake hiyo, kwa sababu kila kitendo kinachotendwa na mtu mwenye akili yake ni lazima kinaambatana na lengo au dhamira hakiwezi kuwa nje ya hivyo, ni sawa awe ametamka kusudio lake kwa lafdhi maalum au la, sawa awe amejielekeza kwenye kusudio lake au la, na kwa ajili hiyo ndipo mafakihi wote walipokubaliana kuwa haitakiwi kuitamka nia. Kama ilivyo ni muhali sana kulingana na ada ya mwanadamu aikusudie Swala ya faradhi huku anaswali Swala ya Sunna tena hasa anapokuwa ni mjuzi ajuaye tofauti iliyopo kati ya Swala hizo.

Na kwa vyovyote vile iwavyo, maneno yanayohusu kuitamka nia na vigawanyo vyake au kufanya uainisho hayakuwepo wala hayakujulikana baina ya viongozi wa kale ambao waliweka misingi ya dini na sharia zake, na itakuwa vyema hapa tunukuu maneno ya wanavyuoni wawili wakubwa, mmoja kutoka kwa mafakihi wa kisunni naye ni Ibnul Qayyim, na wa pili kutoka kwa Maimamiyya, naye ni Sayyid Muhammad mwenye kitabu *Al-Madaarik*.

Huyo wa mwanzo amesema katika kitabu *Zaadul Maad* kama ilivyo kwenye Juzuu ya kwanza ya kitabu *Al-Mughni* cha Ibnu Qud'damah: "Mtume ﷺ alikuwa anaposimama kwenye Swala akisema: *Allah Akbar* hakuwa akisema chochote kabla ya tamko hilo, wala hata mara moja hakusikika akiitamka nia kabisa, wala hakuwa akisema: *Uswaliy kadha kadha mustaqbilal Qiblata Arbaa Rakaati Imaaman,* wala *Maamuman,* wala hakuwa akisema: *Adaan* wala *Fardhul Waqt,* na hii ni miongoni mwa uzushi uliosambaa tu hakuna yeyote aliyenukuu kutoka kwa Mtume ﷺ kuswihi kwa jambo hilo kwa Hadith iliyo na sanadi swahihi wala dhaifu, wala hakuna hata



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 149 2/1/2017 3:51:47 PM

mmoja katika tabiina aliyesema kuwa hiyo ni bidaa njema, wala hata maimamu wanne hakuna mmoja kati yao aliyesema hivyo."

Na wa pili amesema katika kitabu *Madarikul Ahkam* – mlango unaoelezea kutia nia, mwanzo wa Swala: "Inavyoeleweka katika dalili za kisheria ni kuwepo usahili (kutokuwa na uzito) katika kuitamka nia, na kwa hakika kabisa linalozingatiwa katika hiyo nia ni kukusudia kufanya kitendo maalumu katika hali ya kumtii Mwenyezi Mungu (s.w.t.), na kadiri hii ni jambo asiloliepuka timamu wa akili mwenye kujielekeza katika kutekeleza ibada. Na ni kuanzia hapa ndipo baadhi ya wanavyuoni watukufu wakasema: 'Kama Mungu angeweka wajibu wa watu kuswali au kufanya ibada nyingineyo pasi na nia basi ingekuwa ni amri iliyo juu ya uwezo *wa* mwanaadamu.' Naye Shahid katika kitabu *Ad-Dhikraa* amesema: 'Waliotangulia katika wanavyuoni wetu walikuwa hawataji nia katika vitabu vyao, bali walikuwa wakisema: 'La awali linalolazimu katika wajibu wa wudhu ni kuosha uso, na la mwanzo katika wajibu wa Swala ni takbira ya kufungulia Swala.' Ni kama hoja yake ni kwamba ile kadri inayohitajika katika nia ni jambo asiloweza kuliepuka mwanadamu, na ile inayozidi si wajibu. Na katika yanayounga mkono hilo ni kuwa nia haikutokea kutajwa peke yake kuwa ni sehemu katika ibada. Na bila shaka zimeshapokewa Hadith zinazoelezea jinsi alivyokuwa akitawadha Mtume ﷺ, alivyokuwa akioga au kuyatammamu, bila kutaja nia."

## TAKBIRA YA KUHIRIMIA SWALA:

Swala yoyote haitimii bila ya takbira ya kuhirimia Swala. Na iliitwa kwa jina hilo kutokana na kauli ya Mtume ﷺ aliposema: "Ufunguo wa Swala ni kujitwahirisha, na kuhirimia kwake ni kupiga takbira, na hitimisho lake ni kutoa salam." Maana yake ni kuwa kwa takbira hiyo huwa ni haramu kwake kusema maneno yaliyo nje ya Swala



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 150 2/1/2017 3:51:47 PM

na kila kitendo ambacho hakihusiani na Swala. Na kwa kutoa salam humaanisha kujiacha huru na kujihalalishia yote aliyokuwa amejiharamishia kuyatenda mara tu alipopiga takbira.

Na jinsi rasmi ya kuitamka takbira ni kusema: '*Allahu Akbar',* kamwe haijuzu kusema visivyokuwa hivyo kwa Maimamiyya, Maliki na Mahanbali. Na Mashafi wamesema: "Yajuzu kusema '*Allahu Akbar'* au '*Allahu al Akbar'* ikiwa ni kuongeza *Alifu* na *Lam* katika tamko *Akbar* ikawa *al Akbar*. Mahanafi nao wamesema yajuzu kusema neno lolote ambalo lina maana yanayofanana na hayo ya *Allahu Akbar,* kama kusema: *Allahu Aadhamu* na *Allahul Ajallu.*

Kisha wameafikiana kuwa ni lazima takbira hiyo itamkwe kwa lugha ya kiarabu, isipokuwa Mahanafi tu, hata kama anayeswali si Mwarabu, na kama atashindwa basi ajifunze, na kama atashindwa kujifunza basi ataifasiri kwa lugha yake.

Mahanafi wamesema: "Inaswihi kuitamka takbira hiyo kwa lugha yoyote ile mtu anayotaka hata kama anaijua lugha ya Kiarabu."

Pia wameafikiana kuwa ina sharti kama zile zinazoshartiwa katika Swala, kuanzia kuwa tohara, kuelekea Kibla, kujisitiri tupu na mengineyo, na ailete hiyo takbira katika hali ya kusimama na kutulia vyema pasipo na dharura, na aitamke kwa sauti ya kuweza kuisikia yeye mwenyewe, au ya kadiri ya kusikika iwapo ana uziwi masikioni mwake, na alitangulize jina takatifu *Allahu* kabla ya neno *Akbar*, lau atafanya kinyume chake akasema *Akbar Allahu* haitoswihi kuwa ni takbira ya kuhirimia.

**2.** Wameafikiana kuwa kusimama wima katika Swala ya faradhi ni wajibu kuanzia anapopiga takbira hadi anapoporomoka kurukuu. Na hapa katika kusimama ni wajibu iwe ni kusimama katika hali ya kunyooka, kwa kutulizana na pia bila kuegemea.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 151 2/1/2017 3:51:47 PM

Haijuzu kwa mtu anayeswali kusimama ilihali kaegemea kitu anapokuwa anaweza kusimama wima, kama hawezi kusimama basi aswali ilihali ameketi, na akishindwa kuketi ataswali ilihali kalalia ubavu wa kuume, kama anavyolazwa maiti ndani ya mwanandani akiwa ameelekea Kibla kwa sehemu ya mbele ya mwili wake, na hii ni kwa mafakihi wa madhehebu yote isipokuwa Mahanafi, kwani wao wamesema: "Anayeshindwa kuswali ilihali kaketi ataswali ilihali kalala chali kwa mgongo wake, kisha aelekee Kibla kwa miguu yake ili kuwe kuinama kwake katika rukuu na kusujudu kwake ni (kama) kaelekea Kibla, (yaani lau atainuka kurukuu basi angekuwa ameelekea Kibla)."

Na anaposhindwa mtu kuswali huku ameulalia ubavu wake wa kuume, Maimamiyya, Mashafi na Mahanbali wamesema: "Ataswali akiwa amelala chali akitumia kichwa chake katika kuashiria rukuu na sijda; na anaposhindwa kuinama kwa kichwa atatumia nyusi zake."

Mahanafi wamesema: "Anapofikia hali hiyo basi wajibu wa Swala huporomoka toka kwake, lakini hulazimika kulipa pindi atakapopona na kuondoka kilichokuwa kizuizi."

Maliki wamesema: "Mfano wa mgonjwa kama huyu wajibu wa Swala huporomoka toka kwake wala halazimiki kulipa."

Maimamiyya, Mashafi na Mahanbali wamesema: "Kwa hakika Swala haiporomoki kwa hali yoyote iwayo, kama atashindwa kutekeleza kwa kope basi ataihudhurisha Swala moyoni mwake, na atautingisha ulimi wake kwa dhikiri (kumtaja Mungu) na kusoma. Kama atashindwa kuutingisha ulimi wake, basi atapitishia moyoni mwake madamu akili yake iko sawa na thabiti (hajarukwa na akili), kwa ujumla Swala ni wajibu kwa anayeweza na hata aliyezidiwa kamwe haiachiki kwa kutokewa na hali yoyote iwayo, bali anatakiwa



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 152 2/1/2017 3:51:47 PM

aiswali kila mukallaf (mtu baleghe) kufuatana na uwezo wake. Kuanzia kusimama hadi kwenye kukaa, na kuanzia kwenye kuswali kwa kuihudhuria moyoni hadi kwenye kuihudhurisha akilini."

Na mwenye kuswali atahama kutoka hali moja hadi nyingine muda inapopatikana sababu ya kufanya hivyo. Na lau mtu mwenye uwezo ataswali kwa kusimama kisha likamtokea jambo fulani linalomzuia kuswali ilihali kasimama, au aliyekuwa amezidiwa anaswali kwa kuketi, kisha akiwa ndani ya Swala uwezo ukamrudia, basi ataungisha hiyo aliyoanza kuiswali na hii ya sasa na ataitimiza kulingana na uwezo wake alio nao. Hivyo basi kama mtu ataswali rakaa ya kwanza kwa kusimama kisha akazidiwa, atakamilisha Swala yake kwa kukaa, na kama anaswali kwa kukaa kisha uwezo wa kusimama ukamrudia, ataitimiza Swala yake kwa kusimama.

## KISOMO:

**3.** Mafakihi wa madhehebu yote wamekhitilafiana kuhusu, je ni wajibu kusoma Sura *Alhamdu* (*Al-Fatiha*) katika kila rakaa, au ni wajibu katika rakaa mbili za mwanzo tu, au ni wajibu katika rakaa nne?

Na je Bismillahi ni sehemu ya kila Sura ya Qur'ani ambayo haina budi kuisoma, au yajuzu kuiacha?

Na je, kila panapodhihirishwa na panaposomwa kimoyoni ni wajibu iwe hivyo, au ni pendekezo tu?

Na je ni wajibu kusoma Sura nyingineyo baada ya kusoma *Alhamdu* katika rakaa mbili za mwanzo au si wajibu?

Na je, tasbihi inaweza ikawa badala ya Sura?

Na je, kufunga mikono juu ya kifua au chini ya kifua ni Sunna au ni haramu? Na mengineyo.

Mahanafi wamesema: "Hapana ulazima wa kusomwa *Alhamdu* tu katika Swala za faradhi, bali chochote kinachosomwa kutoka katika Qur'ani hutosheleza kufuatana na kauli yake Mwenyezi Mungu: "Basi someni kiasi kilicho sahali (kwenu kukisoma) katika Qur'ani." (*Bidayatul mujtahid*, Juz. ya kwanza Uk. 122, na pia kitabu *Mizanus Sha'araniy* katika mlango unaoelezea namna ya Swala). Na kwa vyovyote vile kusoma Qur'ani ni wajibu katika rakaa mbili tu za kwanza, ama katika rakaa ya tatu ya Swala ya Maghribi na mbili za mwisho katika Adhuhuri, Alasiri na Isha, mtu huruhusiwa kusoma anapopenda mwenyewe, akipenda kusoma tasbihi atasoma na akipenda kunyamaza kimya atanyamaza. (An-Nawawiy katika kitabu *Sharhul Muhaddhab* Juzuu ya tatu, Uk. 361).

Na yajuzu kuacha kupiga Bismillahi, kwani Bismillah si sehemu katika Sura. Aidha kudhihirisha kisomo kwa sauti si Sunna, na kusoma moyoni pia si Sunna bali kusoma kwa kudhihirisha na kusoma kwa moyo, mtu anayeswali peke yake ana hiyari kujiamulia, akipenda atasoma kwa sauti anayoisikia yeye mwenyewe tu, na akipenda atatoa sauti inayosikika na mwenginewe, na akipenda ataificha sauti kabisa. Na katika Swala hakuna kunuti isipokuwa katika Swala ya witiri tu.

Ama kufunga mikono ni Sunna tu wala si wajibu, na iliyo bora kwa mtu ni kuweka tumbo la kiganja chake cha mkono wa kushoto chini ya kitovu chake, hiyo ni kwa mwanamume, ama kwa mwanamke aiweke mikono yake juu ya kifua chake."

Mashafi wamesema: "Ni wajibu kusoma Alhamdu katika kila rakaa pasi na kutofautisha kati ya rakaa mbili za mwanzo na rakaa nyinginezo, wala baina ya Swala ya wajibu na ya Sunna. Na Bismillahi ni sehemu ya Sura kwa hivyo haiachwi kwa hali yoyote ile. Na mtu atasoma kwa sauti katika Swala za Alfajiri, Maghribi na Isha, ama zinginezo hatosoma kwa sauti.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 154 2/1/2017 3:51:47 PM

Na yasunniwa kuleta kunuti katika Swala ya asubuhi, mahali pake maalum ni baada ya kuinua kichwa kutoka kwenye rukuu ya rakaa ya pili. Na pia yasunniwa kusoma Sura nyingineyo baada ya Alhamdu katika rakaa mbili za mwanzo peke yake.

Ama kufunga mikono si lazima, ni Sunna kwa mwanamume na mwanamke, na ilivyo bora katika kufunga mikono ni kuliweka tumbo la kiganja cha mkono wake wa kulia juu ya maungo ya kiganja cha kushoto, iwe ni chini ya kifua juu ya kitovu sehemu inayofuatia upande wa ubavu wa kushoto."

Maliki wamesema: "Pana wajibu wa kusoma *Alhamdu* katika kila rakaa bila ya tofauti yoyote baina ya rakaa, iwe ni za mwanzo au za mwisho, ziwe ni za Swala za faradhi au Sunna", kama ilivyotangulia katika maelezo ya Mashafi. "Na yapendekezwa kusoma Sura nyingine baada ya *Alhamdu* katika rakaa mbili za mwanzo. Na bismillahi si sehemu ya Sura bali yapendekezwa kuiacha kwa mara moja. Na yapendekezwa kusoma kwa sauti inayosikika katika Swala ya asubuhi na katika rakaa mbili za mwanzo za Swala ya Magharibi na Isha. Na kuleta kunuti ni katika Swala ya Asubuhi peke yake. Ama kufunga mikono inajuzu lakini yasunniwa kuachilia mikomo katika Swala za faradhi."

Mahanbali wamesema: "Ni wajibu kusoma Alhamdu katika kila rakaa, na yapendekezwa kusoma Sura nyingineyo baada yake katika raka mbili za mwanzo, na kudhihirisha kisomo katika Swala ya asubuhi na katika rakaa mbili za mwanzo za Swala ya Magharibi na Isha. Na Bismillah ni sehemu katika Sura lakini iwe kimoyomoyo isisomwe kwa sauti, na kunuti huwa katika Swala ya witiri tu haileti katika Swala nyinginezo. Ama kufunga mikono ni Sunna kwa mwanamume na mwanamke, na ubora ni kuweka tumbo la kiganja chake cha mkono wa kulia juu ya kiganja chake cha kushoto na aviweke chini ya kitovu."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 155 2/1/2017 3:51:47 PM

Imetubainikia kuwa *at-takatuf* ambako mafakihi wa kisunni wanakutaja kwa maana ya kufunga mikono katika Swala, na mafakihi wa kishia wanakutaja kwa maana ya kusitiri, hakuna hata madhehebu moja ya kisunni iliyosema kuwa kufanya hivyo ni wajibu.

Na Maimamiyya wamesema: "Kusoma *Alhamdu* kunahusika katika rakaa mbili za mwanzo za kila Swala, wala hakuna inayotosheleza hapo ila hiyo peke yake, wala si wajibu kuisoma katika rakaa ya tatu ya Magharibi na rakaa mbili za mwisho katika Swala ya rakaa nne, bali ipo ruhusa kwa mtu kujiamulia kati ya *Alhamdu* na kuleta tasbihi, nayo ni anayeswali kusema: *Subhanallah, Walhamdulilah, Walailaha ilahlah, Wallahu Akbar* mara tatu, na pia mara moja hutosha.

Na ni lazima kusoma Sura nzima katika rakaa mbili za mwanzo (baada ya *Alhamdu*). Na Bismillahi ni sehemu katika Sura, haijuzu kuiacha kwa hali yoyote. Na ni wajibu kudhihirisha kisomo pekee bila ya kudhihirisha jinginelo miongoni mwa dhikri katika Swala ya asubuhi, na katika rakaa mbili za mwanzo za Magharibi na Isha, na ni wajibu kusoma kwa kuficha katika Swala ya Adhuhuri na Alasiri isipokuwa Bismillahi, kwani hii yapendekezwa idhihirishwe katika rakaa mbili za mwanzo za Swala hizo, na pia katika rakaa ya tatu ya Magharibi na rakaa mbili za mwisho za Swala ya Isha. Na yasunniwa kusoma kunuti katika Swala zote tano, na mahali pake ni katika rakaa ya pili baada ya kumaliza kusoma Sura na kabla ya kurukuu. Na uchache wa kusoma kwa sauti ni kiasi cha kusikia mtu aliye karibu naye, na upeo wa kuificha sauti ni kiasi cha kujisikia mwenyewe."

Na kulingana na madhehebu yote hakuna pa kudhihirisha sauti kwa mwanamke, wala kusoma kwa kuficha zaidi ya kujisikia



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 156 2/1/2017 3:51:47 PM

mwenyewe. Na anayeswali akidhihirisha mahali pasipokuwa pa kudhihirisha kwa makusudi basi Swala yake itabatilika, na itakuwa swahihi kama alifanya hivyo kwa kutojua au kwa kusahau.

Maimamiyya wameendelea kusema: "Ni haramu kutoa kauli ya kusema *Amin*, na Swala hubatilika kwa kusema neno hilo, sawa awe peke yake, ni Imamu au ni maamuma, kwani tamko hilo ni katika maneno ya watu na haisihi kuingiza maneno ya watu ndani ya Swala."

Na madhehebu manne yamekongamana juu ya kuwa neno hilo ni Sunna kwa kupitia Hadith iliyopokewa kutoka kwa Abu Huraira aliyosema kwamba Mtume ﷺ amesema: "Imamu anaposema *Ghayril Maghdhubi Alayhim Waladdhwahliin*, basi nanyi semeni, *Amin*." Maimamiyya wamekataa kusihi kwa Hadith hii.

Na wengi katika Maimamiyya wameendelea kusema kwamba huko kufunga mikono ndani ya Swala kunaibatilisha, kwa ajili ya kukosekana nususi, na baadhi yao wakasema: "Kufunga mikono ndani ya Swala ni haramu, na anayefanya hivyo hupata dhambi lakini Swala yake haibatiliki." Na kundi la tatu likasema ni makruhu tu (inachukiza) lakini si haramu.

**KURUKUU:**

**4.** Mafakihi wote wameafikiana kuwa kurukuu ni wajibu, lakini wametofautiana kuhusu kadiri ya wajibu katika kurukuu, na kuhusu kujituliza ndani ya rukuu, kwa maana ya kutulizana na kutuwama viungo vyote muda wa kurukuu. Mahanafi wamesema: "Kinachopasa katika rukuu ni kuinama tu vyovyote inavyowafiki kuinama wala haipasi kujituliza."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 157 2/1/2017 3:51:47 PM

Madhehebu yaliyobakia yanasema kwamba katika rukuu ni wajibu kuinama hadi viganja vya mwenye kuswali viyafikie magoti yake, na ni wajibu kujituliza ndani ya rukuu.

Mashafi, Mahanafi na Maliki wamesema: "Si wajibu kuleta dhikri kwenye rukuu bali yasunniwa anayeswali aseme: S*ubhana Rabbiyal Adhimi."*

Na Maimamiyya na pia Mahanbali wamesema: "Tasbihi ni wajibu katika rukuu; na kuitamka kwake kwa Mahanbali ni *Subhana Rabbiyal Adhimi*. Na kwa Maimamiyya ni *Subhana Rabbiyal Adhimi wa Bihamdihi*, au *Subhanallah* mara tatu. Na yapendekezwa kwa Maimamiyya anayeswali baada ya tasbihi aongeze kumswalia Mtume na Ahli zake, aseme: *Allahumma Swalli Ala Muhmmad Waali Muhammad*."

Mahanafi wamesema: "Si wajibu kusimama wima kutoka kwenye rukuu, bali yajuzu kwake kukishusha kichwa chake hadi kwenye sijda bila ya kusimama wima, lakini kufanya hivyo ni makruhu."

Mafakihi wa madhehebu yaliyobaki wamesema: "Ni wajibu kuinuka na kusimama wima kwa kunyooka sawa sawa, na yasunniwa kuleta *Tasmii* kwa kusema: *Samiallahu Liman Hamidah*." Na Maimamiyya wamewajibisha kujituliza na kutulia wakati wa kisimamo hiki.

## KUSUJUDU

**5.** Wameafikiana kuwa kusujudu ni wajibu iwe mara mbili katika kila rakaa, kisha wakakhitilafiana katika kiwango chake, je, ni wajibu kusujudu kuwe ni kwa viungo saba kamili au kwa baadhi tu ya viungo? Na viungo saba hivyo ni: Paji la uso, viganja viwili vya mikono, magoti mawili na magumba mawili ya miguuni.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 158 2/1/2017 3:51:47 PM

Maliki, Mashafi na Mahanafi wamesema: "Wajibu ni kusujudu kwa paji la uso tu, ama viungo vilivyobaki ni Sunna."

Maimamiyya wamesema: "Wajibu ni kusujudu kwa viungo vyote saba vya sijda." Na hiyo ndiyo kauli ya Mahanbali isipokuwa wao waliongeza na pua, hivyo kufanya idadi ya viungo vya sijda kuwa vinane.

Na tofauti iliyopo kati yao kuhusiana na tasbihi na kujituliza kwenye sijda ni kama tofauti ileile iliyoko kwenye kurukuu, Yule aliyewajibisha vitu viwili hivyo kwenye rukuu pia aliviwajibisha vitu hivyo hapa.

Mahanafi wamesema: "Si wajibu kukaa kati ya sijda mbili," na madhehebu yaliyobaki yamesema: "Ni wajibu."

## *TASHAHHUD* (KUKAA *TAHIYYATU*):

**6.** *Tashahhud* katika Swala imegawanyika katika sehemu mbili: Ya kwanza ni ile ya baada ya rakaa mbili za Magharibi, Isha, Adhuhuri na Alasiri, hii haina kutoa salam. Na ya pili ni ile ambayo hufuatiwa na kutoa salam, sawa iwe katika Swala ya rakaa mbili, tatu au nne.

Maimamiyya na Mahanbali wamesema: "Kwa hakika *tahiyatu* ya kwanza ni wajibu." Na madhehebu yaliyobaki yamesema ni Sunna tu, kamwe si wajibu.

Ama *tahiyyatu* ya mwisho, Mashafi, Maimamiyya na Mahanbali wamesema: "Ni wajibu." Na Maliki na Mahanafi wamesema: "Ni Sunna tu na wala si wajibu." (kitabu *Bidayatul Mujtahi*d Juz. ya kwanza Uk. 125).



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 159 2/1/2017 3:51:47 PM

## TAMKO LA *TASHAHHUD* KATIKA MADHEHEBU YOTE:

Mahanafi wanasoma hivi: A*ttahiyatu lillahi waswalawatu wattwayy-ibaatu, was salamu alayka ayyuha nnabiyyu warahmatullahi wa barakatuhu. Assalam alayna waala ibadilllahis swalihina. Ash'hadu an lailaha ilallah, Waash'hadu anna Muhammadan abduhu wa ra-suluhu*.

Maliki husoma hivi: *"Attahiyatu lilahi, Az zakiyyatu lilahi, atwayyibaatu Aswallawatu lillahi, Assalam alayka ayyuhan nabiyu wa rahmatullahi wa barakatuhu. Assallamu alayna wa ala ibaadilllahi swalihiina. Ash'hadu an lailaha ilallah, wahdahu la shariika lahu, wa ash'hadu anna Muhammadan abduhu wa rasuluhu."*

Mashafi husoma hivi: *Attahiyatu mubarakatu swalawatu ttwayyiibaatu lillahi, Assalam alayka ayyuhanabiyyu warahmatullahi wa barakatuhu, Assalam alayna waala ibaadilllahi swalihiina. Ash'hadu anlailaha ilallah, wa ash'hadu anna (Sayyidana) Muhammadan rasuluhu."*

Mahanbali husoma: "*Attahiyatu lilahi waswalawatu wattwayyibatu. Assalamu alayka ayyyuhannabiyyu warahmatullahi wabarakatuhu, Assalam alayna waala ibadilllahis swalihiina. Ash'hadu an lailaha ilallah wahdahu laa shariika lah, waash'hadu anna Muhammadan abduhu wa rasuluh. Allahuma swali ala Muhammad ...*

Maimamiyya: "*Ash'hadu anlailaha illallah wahdahu laa sharika lah, waash'hadu anna Muhammadan abduhu warasuluh. Allahuma swali ala Muhammadin wa aali Muhammad ..."*



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 160 2/1/2017 3:51:48 PM

**KUTOA SALAM:**

**7.** Mashafi, Maliki na Mahanbali wamesema: “Kutoa salam (ya kumaliza Swala) ni wajibu.” Mahanafi wamesema: “Kutoa salam si wajibu.” (*Bidayatul Mujtahid* Juz. ya kwanza Uk. 126).

Maimamiyya wamekhitilafiana, kundi moja limesema kutoa salam ni wajibu na wengine wamesema ni Sunna. Na katika waliosema ni Sunna ni Sheikh Mufid, Sheikh Tusi na Allamah Hilli. Na namna ya kuitamka kwake kwa madhehebu manne ni kwa namna moja nayo ni: *Assalam alaykum wa rahmatullah*. Mahanbali wamesema: “Ni faradhi kutoa salam mara mbili (kulia na kushoto).” Na waliobaki wamesema: “Faradhi ni mara moja tu nayo hutosha.”

Ama Maimamiyya wamesema: “Kutoa salam kuna matamshi aina mbili, ya kwanza ni: *Assalam alayna waala ibaadilahis swalihiina,* na ya pili ni *Assalam alaykum warahmatulah wabarakatu*, na iliyo wajibu ni moja kati ya hizo mbili, mtu anaposoma tamko la kwanza basi hilo la pili huwa ni Sunna. Na kama atasoma la pili basi atakomea hapo. Ama *Assalamu alayka ayyuhan nabiyyu wa rahmatulahi wa barakaatuhu* si chochote katika salam, bali ni Sunna inayopendekezwa baada ya *tashahud*.

**MPANGILIO:**

**8.** Ni wajibu kutekeleza kwa mpangilio vifungu vya Swala, kwa kutanguliza takbira ya kuhirimia kabla ya kusoma *Alhamdu* na kisomo kabla ya kurukuu, na kurukuu kabla ya kusujudu, na kuendelea vivyo hivyo hadi mwisho.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 161 2/1/2017 3:51:48 PM

**KUFUATANISHA**

**9.** Ni wajibu kufuatanisha na kufululiza kati ya vifungu vya Swala, na kati ya vipengele vya vifungu vya Swala, kwa kuanza mara moja kusoma baada tu ya takbira ya kuhirimia Swala, bila ya kutenganisha (kwa kuacha mwanya hata kidogo), na kurukuu baada tu ya kisomo, hivyo hivyo hadi mwisho. Vilevile haruhusiwi mtu kutenganisha kati ya Aya, matamko na herufi."

# KUSAHAU NA KUTIA SHAKA KATIKA SWALA

Mafakihi wa madhehebu yote wameafikiana kuwa mtu anapoacha kitu katika vitu vilivyo wajibu katika Swala kwa makusudi basi Swala yake itabatilika, na kwamba atakayeacha kwa kusahau basi hulazimika kuziba pengo hilo kwa kusujudu sijda ya kusahau kama ilivyo katika maelezo ya madhehebu yanayofuata:

Mahanafi wamesema: "Kwa hakika kusujudu sijda ya kusahau namna yake ni kusujudu mara mbili kisha aketi kwa ajili ya *tashahhud* na atoe salam, pia alete Swala ya kumswalia Mtume na aombe dua. Na mahali pa sijda hii ni baada ya kutoa salam, kwa sharti kuwa pawe pana wakati wa kutosha, hivyo mtu atakapokuwa amesahau katika Swala ya asubuhi – kwa mfano – na jua likachomoza kabla hajasujudu sijda ya kusahau, basi sijda hiyo huporomoka kutoka kwake.

Ama sababu za kusujudu sijda ya kusahau ni pale mwenye kuswali anapoacha wajibu, au kuongeza kitu miongoni mwa nguzo za Swala, kama rukuu na sijda. Na kama atasahau mara nyingi basi



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 162 2/1/2017 3:51:48 PM

zitatosha sijda mbili, kwa sababu hairuhusiwi kukariri, na kama atasahau ndani ya sijda ya kusahau hatawajibika kusujudu tena sijda ya kusahau. (kitabu *Majmaul an har* Juz. ya kwanza, mlango wa *Sujuudis sahwi*)."

Maliki wamesema: "Namna ya sijda ya kusahau ni sijda mbili, na atakaa *tashahhud* baada ya kusujudu sijda hizo mbili bila ya kusoma dua wala kumswalia Mtume ﷺ; ama mahali pa kufanyika sijda hizi mbili ataangalia kwanza, kama ni ya kupunguza peke yake au ni ya kuzidisha na kupunguza kwa pamoja, hapo atasujudu kabla ya kutoa salam. Na kama ni ya kuongeza tu ataileta baada ya kutoa salam. Vile vile atachunguza sababu zilizowajibisha sijda hiyo ya kusahau, kama kusahau kulifanyika kwa kupunguza, na hicho kilichoachwa kilikuwa ni kitendo cha Sunna basi atasujudu sijda ya kusahau, lakini kama kilichoachwa ni kitendo cha faradhi za Swala basi hatalazimika kusujudu sijda ya kusahau, bali itakuwa hapana budi aitimize sehemu aliyoiwacha. Na kama kusahau ni kwa kuongeza kama vile kuongeza rukuu moja au mbili, au rakaa moja au mbili, hapo hulazimika kusujudu sijda ya kusahau."

Mahanbali wamesema: "Hujuzu kusujudu sijda ya kusahau kabla ya kutoa salam na pia baada ya kutoa salam, na namna yake ni kusujudu mara mbili, kuketi tashahud na kutoa salam. Na sababu yake ni kuzidisha, kupunguza na kutia shaka, na mfano wa kuzidisha ni mtu azidishe katika kusimama au kukaa, basi anayekaa mahali pa kusimama au akasimama mahali pa kukaa atasujudu sijda ya kusahau." Ama katika kupunguza hapo pana kitendo chake maalum katika madhehebu yao, nacho ni kama atakumbuka kabla hajaingia katika kisomo cha rakaa inayofuatia, itampasa atekeleze kitendo hicho alichokisahau kisha atasujudu sijda ya kusahau, na kama hatakumbuka isipokuwa baada ya kisomo cha rakaa inayofuatia, basi



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 163 2/1/2017 3:51:48 PM

ataiachilia mbali hiyo iliyopita na hiyo ya pili itasimama sehemu yake na atasujudu sijda ya kusahau.

Na mfano wa hilo ni huu: Anaposahau kurukuu hali ya kuwa yuko kwenye rakaa ya kwanza kisha akakumbuka baada ya kusujudu, hapo ataleta rukuu kwanza kisha arudie kusujudu. Na kama atakumbuka baada ya kuingia kwenye rakaa ya pili na kuanza kisomo; ataipuuza rakaa ile ya kwanza yote (ataitoa kwenye hesabu) kisha ya pili ndiyo itakuwa ni ya kwanza.

Ama shaka ambayo huwajibisha kuleta sijda ya kusahau, mfano wake ni pale anapopatwa na shaka ya kuacha rukuu au kuhusu idadi ya rakaa, hapo atafuata iliyo yakini na alete kile alichokitilia shaka, kisha aitimize Swala yake na hatimaye asujudu sijda ya kusahau, na inatosha kwake kusujudu sijda mbili tu kwa kusahau kwake kote kulikotokea, hata kama kunakowajibisha sijda ya kusahau kumetokea mara ngapi. Kwao wao Mahanbali hakuna kusujudu sijda ya kusahau kwa mtu ambaye ni mwingi wa kusahau (yaani ambaye ana ugonjwa wa kusahau).

Mashafi wamesema: "Mahali pa kusujudu sijda ya kusahau ni baada ya tashahhud na kumswalia Mtume na kabla ya kutoa salam. Ama namna yake ilivyo ni kama ilivyotangulia katika madhehebu yaliyotangulia. Na sababu yake ni kuacha Sunna iliyosisitizwa, au kuzidisha maneno machache au kuisoma Alhamdu mahali pasipokuwa pake kwa kusahau, au kumfuata mtu ambaye katika Swala yake kuna upungufu, au anapopatwa na shaka kuhusu idadi ya rakaa au anapoacha sehemu maalum (muhimu katika Swala)."

Ama Maimamiyya wao wametofautisha kati ya hukmu ya shaka na hukmu ya kusahau, wakasema: "Shaka inayotokea baada ya kumaliza Swala haizingatiwi, pia shaka ya maamuma kuhusu idadi ya rakaa iwapo Imamu amedhibiti idadi yake, na pia shaka ya imamu



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 164 2/1/2017 3:51:48 PM

kuhusu idadi ya rakaa iwapo maamuma amedhibiti idadi yake, hapo kila mmoja atarudi mahali alipopakumbuka mwenzake.

Wala haizingatiwi shaka ya mtu aliye mwingi wa kutia shaka, wala haizingatiwi shaka inayotokea katika kitendo miongoni mwa vitendo vya Swala baada ya kuingia katika kitendo kinachofuata, hivyo kama mtu atapatwa na shaka ya kuisoma Sura Alhamdu wakati ameshaanza kusoma Sura nyingine, au akapatwa na shaka ya kuisoma Sura wakati akiwa katika rukuu, au akapatwa na shaka ya kurukuu wakati akiwa ndani ya sijda,  hapo ataendelea tu na Swala yake wala hataizingatia shaka yake. Ama anapopatwa na shaka kabla ya kuingia katika kitendo kinachofuata, hapo ni wajibu kuwahi kuileta sehemu aliyoitilia shaka; hivyo anayepatwa na shaka katika kuisoma Alhamdu, na ikawa ni kabla hajaanza kusoma Sura nyingine, ataisoma Alhamdu kwanza, na hivyo hivyo anapopatwa na shaka ya kusoma Sura kabla hajarukuu, ataisoma Sura kwanza ndipo arukuu.

Ama sijda ya kusahau hufanywa kutokana na kila kuzidisha au kupunguza, isipokuwa atakapodhihirisha kisomo mahali pa kuficha, au atakapoficha mahali pa kudhihirisha, kwani hilo haliwajibishi chochote. Na isipokuwa nguzo za Swala kwani kuzidisha nguzo za Swala au kupunguza hubatilisha Swala kwa hali yoyote iwayo, sawa tendo hilo liwe limetokea kwa kusahau au kwa makusudi."

Na nguzo kwao ni tano: Kutia nia, kupiga takbira ya kuhirimia Swala, kusimama, kurukuu na jumuiko la sijda mbili katika rakaa moja. Na sehemu yoyote iliyoachwa katika Swala kwa sababu ya kusahau si wajibu kuilipa baada ya Swala kwisha isipokuwa sijda na tashahhud, ambapo ni hayo mawili tu ndio wajibu kulipa, hivyo hakuna jingine ambalo ni wajibu kulipa miongoni mwa sehemu zilizosahauliwa katika Swala. Atalipa sehemu mbili hizo baada ya Swala, kisha atasujudu sijda mbili za kusahau.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 165 2/1/2017 3:51:48 PM

Na namna ya kusujudu sijda ya kusahau ni hivi: Atasujudu sijda mbili na katika kusujudu kwake atasema *Bismilahi wabillahi, Allahuma swali ala Muhammadin wa aali Muhammad.* kisha atakaa tashahud na atoe salam.

Na ni wajibu kuleta sijda za kusahau kwa idadi sawa ya makosa yanayolazimu sijda ya kusahau yaliyofanyika, na kwao hana wajibu wa kusujudu sijda ya kusahau mtu ambaye ni mwingi wa kusahau, wala mtu halazimiki kusujudu sijda ya kusahau anaposahau katika sijda ya kusahau.

## KUWA NA SHAKA NA IDADI YA RAKAA:

Mashafi, Maliki na Mahanbali wamesema: "Mtu anapokuwa na shaka na idadi ya rakaa alizoswali, akawa hajui ni rakaa ngapi ameswali, atajengea kwenye uyakini, nao ni uchache wa rakaa, kisha ataendelea na rakaa zinazotimiza Swala."

Mahanafi wamesema: "Iwapo shaka yake ndani ya Swala ni ya mara ya kwanza kabisa katika maisha yake ya kuswali, basi atairudia Swala tangu mwanzo; na kama alikwishawahi kabla ya hapo kupatwa na shaka ndani ya Swala, atazingatia na kufikiri kidogo kisha atafanya kulingana na dhana yake yenye nguvu inavyomwambia, na kama shaka itaendelea basi atajengea juu ya uchache wa rakaa, ili kupata yakini.

Maimamiyya wamesema: "Iwapo mtu imempata shaka katika Swala ya rakaa mbili kama Swala ya Asubuhi, Swala ya msafiri, Swala ya Ijumaa, Swala ya Idd mbili au Swala ya kupatwa kwa jua, au katika Swala ya Magharibi au katika rakaa mbili za mwanzo katika Swala ya Isha, Adhuhuri na Alasiri, Swala hiyo itabatilika na itabidi aianze upya toka mwanzo. Ama akipatwa na shaka kuhusu rakaa mbili za mwisho katika Swala ya rakaa nne, basi

ataswali Swala ya *Ihtiyat* (ya kujitoa shaka) baada ya kutimiza Swala na kabla hajafanya kitendo kinachokatazwa kutendwa ndani ya Swala, na mfano wake ni kama pale mtu atakapokuwa na shaka kati ya rakaa mbili na tatu baada ya kuwa ameshakamilisha sijda mbili, basi hapo atachukulia kuwa ni rakaa ya tatu, kisha atimize Swala yake. Baadaye ataswali Swala ya *Ihtiyat* ambayo ni rakaa mbili zinazoswaliwa kwa kukaa au rakaa moja ya kusimama. Na atakapokuwa na shaka kati ya tatu na nne atachukulia kuwa ni ya nne, aikamilishe Swala yake na aihifadhi kwa rakaa moja atakayoiswali kwa kusimama au rakaa mbili atakazoziswali kwa kukaa. Na atakapokuwa na shaka kati ya mbili na nne atachukulia kuwa ni ya nne, kisha ataswali rakaa mbili (za *ihtiyat*) kwa kusimama. Na atakapokuwa na shaka kati ya mbili na tatu na nne, atachukulia kuwa ni ya nne, kisha ataswali rakaa mbili (za *ihtiyat*) kwa kusimama na rakaa mbili kwa kukaa.

Na hili walilielezea kwamba ni njia mojawapo ya kuhifadhi uhakika wa Swala, na kujitenga na ama kupunguza rakaa au kuzidisha, na makusudio yao hapa yanaeleweka wazi kwa mfano huu: Anayetia shaka kati ya rakaa tatu au nne akachukulia kuwa ni rakaa nne kisha akaleta rakaa hiyo iliyo pekee baada ya kumaliza Swala yake. Kama itakuwa Swala yake ilikuwa imetimia basi hiyo rakaa yake aliyoswali itakuwa ni Sunna, na kama Swala yake ilikuwa pungufu basi rakaa hiyo itatimiza Swala yake. Na vyovyote ilivyo na inavyokuwa, Swala hii ya *ihtiyat* kwa mfumo huo ni katika Swala ambayo wamejitenga nayo Maimamiyya peke yao.

Na tendo la Swala hii kwa Maimamiyya linakomea katika Swala za faradhi tu, na kwa maalum inahusika na Swala ya Dhuhri na Asri na Isha. Ama katika Swala za Sunna anayeswali ana hiari ya kuchukulia katika uchache wa rakaa au wingi wake isipokuwa iwapo ni ziada inayoharibu Swala. Kama kutia shaka katika rakaa

mbili au tatu pamoja na kuelewa kwamba Swala ya Sunna ina rakaa mbili, basi katika hali kama hii atachukulia kwa uchache wa rakaa, na ubora ni kujenga yakini moja kwa moja katika uchache wa rakaa katika Swala hizo za Sunna.

Na kama atatia shaka katika idadi ya rakaa za Swala ya *Ihtiyat* basi atachukulia wingi wa rakaa isipokuwa kama wingi huo unabatilisha Swala, hapo ndipo atajengea katika uchache. Na baadhi ya Maimamiyya wamesema: "Atahiari baina ya kujengea kwenye uchache au wingi."

## SWALA YA IJUMAA

Waislamu wote wamekongamana kuwa Swala ya Ijumaa ni wajibu. Hiyo ni kutokana na kauli yake Mwenyezi Mungu:

"يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِذَا نُودِيَ لِلصَّلَوٰةِ مِن يَوۡمِ ٱلۡجُمُعَةِ فَٱسۡعَوۡاْ إِلَىٰ ذِكۡرِ ٱللَّهِ وَذَرُواْ ٱلۡبَيۡعَۚ ....."

**"Enyi (watu) mlioamini, ikinadiwa Swala siku ya Ijumaa nendeni upesi kwenye dhikiri ya Mwenyezi Mungu na wacheni biashara (zenu) …" (Suratul Jumu'ah; 62:9).**

Pia ni kutokana na Hadithi nyingi zilizo katika daraja ya *mutawatir* katika upande wa Sunni na Shia. Kisha wamekhitilafiana kuhusu je yasharitiwa katika wajibu wake ulazima wa kupatikana sultani au naibu wake, au ni wajibu katika hali yoyote ile?

Mahanafi na Maimamiyya wamesema: "Ni sharti awepo Sultani au naibu wake, na anapokosekana Sultani au naibu wake basi wajibu wa Ijumaa huondoka." Na Maimamiyya wameongeza sharti la uadilifu wa Sultani, kwa maana Sultani huyo awe ni mwadilifu,



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 168 2/1/2017 3:51:48 PM

la sivyo basi kupatikana kwake kutakuwa sawa na kukosekana kwake. Mahanafi wametosheka na kupatikana Sultani hata kama si mwadilifu.

Ama Mashafi, Maliki na Mahanbali wao hawakulipa uzito suala hilo la kupatikana Sultani. Na wengi katika Maimamiyya wamesema: "Asipopatikana Sultani wala naibu wake lakini akapatikana fakihi mwadilifu hapo patakuwa na hiari baina ya watu kuswali Ijumaa na Adhuhuri, japokuwa la uzito zaidi ni Swala ya Ijumaa."[17]

## MASHARTI YAKE:

Mafakihi wameafikiana kuwa yasharitiwa katika Swala ya Ijumaa kila linaloshartiwa katika Swala nyinginezo, kama vile tohara, kujisitiri tupu na kuelekea Kibla, na kwamba wakati wake ni tangu mwanzo wa kupinduka kwa jua hadi kinapokuwa kivuli cha kitu sawa na kitu husika, na kwamba huswaliwa msikitini na mahali penginepo, isipokuwa Maliki, wao wamesema kuwa haiswihi ila msikitini peke yake.

Pia wameafikiana kwamba hiyo Swala ya Ijumaa ni wajibu kwa wanaume tu, si kwa wanawake, na kwamba anayeswali Swala ya Ijumaa si wajibu kwake kuswali Adhuhuri, na si wajibu kwa kipofu. Na kwamba haiswihi ila iwe ni ya jamaa. Na wamekhitilafiana kuhusu idadi maalum ya wanaounda jamaa, Maliki wamesema: "Uchache wa jamaa inayotimiza Ijumaa ni watu kumi na mbili (12) mbali na Imamu." Maimamiyya wamesema: "Ni watu wanne mbali na Imamu." Mashafi na Mahanbali wamesema: "Ni watu arobaini

[17] Amesema Shahidi wa pili katika kitabu *Lumma'a* Juz ya kwanza mlango wa Swala, kifungu cha sita: 'kwa hakika kupasa kwa Swala ya Ijumaa katika hali ya kughibu Imamu ni jambo lililo dhahiri kwa wanavyuoni wengi … Na lau si sababu ya madai ya kongamano (Ijmaa) la wanavyuoni juu ya kutopasa kabisa kabisa kupasa kwa Swala ya Ijumaa katika hali hiyo, basi kauli ya kupasa kwake ingelikuwa na nguvu. Kwa hiyo hakuna la zaidi kuliko kuhiari kati ya Ijumaa na Adhuhuri pamoja na kuipa nguvu Ijumaa.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 169 2/1/2017 3:51:48 PM

(40) pamoja na imamu." Mahanafi wamesema: "Ni watu watano." Na baadhi yao wamesema ni watu saba.

Pia waliafikiana kwamba kwa mtu ambaye ni wajibu kwake kuswali swala ya Ijumaa haijuzu kwake kusafiri baada ya kupinduka jua kabla ya kuswali, anapokuwa amekamilisha masharti ya Ijumaa, isipokuwa Mahanafi wao wamesema yajuzu.

## KUSOMA KHUTBA MBILI:

Wamekubaliana kwamba (kusoma) khutba mbili katika Swala ya Ijumaa ni sharti la kutimia kwa Swala ya Ijumaa, na kuwa mahali pa khutba hizo ni kabla ya Swala tena iwe ni ndani ya wakati wa Swala si kabla ya wakati wa Swala haujaingia. Kisha wamekhitilafiana kuhusu wajibu wa kuzisoma kwa kusimama wima. Maimamiyya, Mashafi na Maliki wamesema: "Ni wajibu." Mahanafi na Mahanbali wamesema: "Si wajibu."

Ama jinsi ya kuzisoma, Mahanafi wamesema: "Hupatikana uhakika wa khutba kwa uchache wa maneno ambayo yumkini kuwa ukumbusho, hivyo lau atasema mwenye kuhutubu: *Alhamdulilah*, (shukrani ni zake Mwenyezi Mungu) au *Astaghafirullah* (namuomba msamaha Mwenyezi Mungu), itatosha. Lakini ni makruhu kuifupisha khutba kiasi kama hicho."

Mashafi wamesema: "Hapana budi katika khutba zote mbili zianzwe kwa neno: *Alhamdulillah*, na kumswalia (kumtakia rehma) Mtume ﷺ na kuusia kumcha Mwenyezi Mungu na kusoma Aya katika Qur'ani katika mojawapo ya khutba hizo mbili kwa uchache. Na kuisoma Aya hiyo katika khutba ya kwanza ni bora zaidi, na kuwaombea dua Waumini katika khutba ya pili."

Maliki wamesema: "Hujuzu kusoma chochote kinachotosha kuitwa khutba kijamii, kwa sharti tu iwe imejumuisha kuhadharisha



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 170 2/1/2017 3:51:48 PM

na kubashiri." Mahanbali wamesema: "Haina budi khutba ianze kwa kumuhimidi Mwenyezi Mungu (*Alhamdulilah)* na kumswalia Mtume ﷺ na kusoma Aya kutoka katika Qur'ani na kuusia kumcha Mwenyezi Mungu."

Maimamiyya wamesema: "Ni wajibu katika kila khutba kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumsifu kwa sifa njema, kumswalia Mtume ﷺ na Ahli zake, kutoa mawaidha (kuwaidhisha) na kusoma kitu kutoka katika Qur'ani. Na katika Khutba ya pili khatibu afanye wingi katika kuomba msamaha na kuwaombea dua waumini waume na wanawake." Maimamiyya na Mashafi wamesema: "Ni wajibu khatibu atenganishe kati ya khutba mbili hizo kwa kuketi kitako chepesi (kifupi)." Maliki na Mahanafi wamesema: "Si wajibu bali ni Sunna."

Mahanbali wamesema: "Katika kuhutubu ni sharti atumie lugha ya kiarabu kama ana uwezo wa kufanya hivyo." Mashafi wamesema: "Kama anaowakhutubia ni Waarabu basi italazimu atumie lugha ya Kiarabu. Ama kama anaowahutubia si Waarabu, basi ni juu yake kuwahutubia kwa lugha yao, na hata kama anaijua vyema lugha ya Kiarabu."

Maliki wamesema: "Ni wajibu ahutubu kwa lugha ya Kiarabu hata kama watu anaowasomea khutba hawaielewi lugha ya kiarabu. Na kama kati yao hapatikani mtu anayeijua vyema lugha ya kiarabu basi Swala ya Ijumaa huporomoka (huwa si wajibu tena)." Mahanafi na Maimamiyya wamesema: "Lugha ya kiarabu si sharti katika khutba ya Ijumaa."

## NAMNA YA KUSWALI SWALA YA IJUMAA:

Swala ya Ijumaa ni rakaa mbili kama Swala ya Asubuhi, Mashafi na Maimamiyya wamesema: "Yasunniwa Imamu anayeswalisha Swa-



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 171 2/1/2017 3:51:48 PM

la hiyo katika rakaa ya kwanza, baada ya kusoma Alhamdu asome *Suratul Jumaa,* na katika rakaa ya pili asome *Suratul Munafiqun*." Maliki wamesema: "Katika rakaa ya kwanza husomwa *Suratul Jumaa,* na katika rakaa ya pili *Alghaashiy*a." Mahanafi wamesema: "Ni makruhu sana kuchagua na kuhusisha Sura maalumu."

## SWALA YA IDDI MBILI

Wamehitilafiana kuhusu Swala ya Idd mbili, ya al-Fitri na al-Udhuha, kuwa je Swala mbili hizi ni wajibu au ni Sunna?

Maimamiyya na Mahanafi wamesema: "Ni faradhi ya kila mmoja (*ainiy)* kwa masharti ya Swala ya Ijumaa. Lakini kama yatakosekana masharti yote au sehemu tu ya masharti hayo basi wajibu huo huondoka. Hiyo ni kwa mujibu wa pande zote mbili, isipokuwa Maimamiyya wao wamesema: "Yanapokosekana masharti ya wajibu basi itaswaliwa kwa njia ya Sunna, ima kwa jamaa au kila mtu peke yake, sawa awe mtu huyo yuko safarini au mjini kwake."

Mahanbali wamesema: "Ni faradhi ya kutosheleza (*kifaya*)."Mashafi na Maliki wamesema: "Swala za Iddi mbili ni Sunna iliyokokotezwa (*muakadah*)."

Wakati wa kuswali Swala ya Iddi mbili kwa Maimamiyya na Mashafi ni tangu kuchomoza kwa jua hadi linapokengeuka. Na kwa Mahanbali ni tangu jua linapoinuka juu kadiri ya mpini wa mkuki hadi wakati linapokengeuka (baada ya saa sita mchana).

Maimamiyya wamesema: "Kwenye Swala ya Idd ni wajibu kusomwa khutba mbili kamili kama ilivyo katika Swala ya Ijumaa." Na madhehebu yaliyobaki yamesema kwamba: "Kusoma khutba za Iddi ni Sunna." Kisha wamekubaliana kuwa khutba mbili hizo

husomwa baada ya Swala, kinyume na Swala ya Ijumaa, kwani katika Swala ya Ijumaa hizo husomwa kabla ya Swala.

Maimamiyya wamesema na pia Mashafi: "Swala ya Iddi huswihi inaposwaliwa kwa jamaa au mtu mmoja mmoja." Na madhehebu yaliyobakia yamesema: "Swala ya Iddi ni wajibu iswaliwe kwa jamaa."

Ama jinsi ya kuiswali katika madhehebu yote ni rakaa mbili kwa mfumo huu ufuatao.

**Mahanafi**: Atatia nia, kisha apige takbira ya kuhirmia Swala, kisha atamtukuza Mwenyezi Mungu kwa kumsifu kwa sifa njema, na baadaye atapiga takbira tatu, atanyamaza baada ya kila takbira moja, kwa kiwango cha kupiga takbira tatu, na hapana ubaya kusema: *Subhanallah Walhamdulillah Walailahailallah Wallahu Akbar,* kisha asome *Suratul Fatiha* na Sura nyingineyo. Halafu atarukuu na kusujudu. Na aanze rakaa ya pili kwa kusoma *Suratul Fatiha* na Sura nyingineyo, baadaye apige takbira tatu, arukuu na kusujudu, na amalize Swala.

**Mashafi:** Anayeswali atapiga takbira ya kuhirimia Swala, kisha ataomba dua ya kufungulia Swala.[18] Kisha apige takbira saba, aseme kwa sauti ya kimoyo baada ya kila takbira mbili: *Subhanallah, Walhamdulillahi, Walailahailallah, Wallahu Akbar,* kisha atapiga *Audhubillahi* asome *Suratul Fatiha* na *Suratu Qaaf*, arukuu, asujudu kisha asimame kwa ajili ya rakaa ya pili, apige takbira ya kusimama kwa ajili ya rakaa hiyo ya pili. Akishasimama ataongeza takbira tano kwa kuzitenganisha kila takbira mbili kwa kusoma: *Subhanallah, Walhamdulillahi, Walailahailallah, Wallahu Akbar*. Kisha asome *Suratul Fatiha* na *Suratul Iqtarabat* na amalize Swala yake.

[18] Dua ya kufungulia Swala kwa Ahlil Sunna ni kusema: *Subhanakallahumma Wabihamdika watabaraka Ismuka Wataala Jadduka wala Ilaha Ghyruka.*

**Mahanbali:** Anayeswali atasoma dua ya kufungulia Swala, kisha atapiga takbira sita na kati ya kila takbira mbili aseme kimoyomoyo (kwa siri): *Allahu Akbar Kabiiran Walhamdulilahi Kathiran Wasubhaballahi Bukratan Waaswilah, Waswalallahu Alaa Muhammad Waalihi Wasallim Taslima.* Kisha apige Audhubillah, asome Bismillahi, asome Alhamdu na sura *Sabbihisima Rabikal Aala*, kisha atimize rakaa ya kwanza na asimame kwa rakaa ya pili. Akishasimama apige takbira tano mbali na takbira ya kisimamo, na aseme kati ya kila takbira mbili kama alivyosema katika rakaa iliyotangulia. Kisha apige Bismillahi, asome Alhamdu na Sura Al-*Ghashiya*, arukuu na atimize Swala yake.

**Maliki:** Anayeswali apige takbira ya kuhirimia Swala, kisha apige takbira sita, asome Alhamdu na *Suratul Aala*, arukuu, asujudu, na asimame kwa ajili ya rakaa ya pili, apige takbira tano, kisha atasoma Alhamdu na Sura  *Ash shamsu* au nyingine, kisha atimize Swala yake.

**Maimamiyya:** Anayeswali atahirimia kwa takbira ya kuhirimia Swala, asome Alhamdu na Sura nyingine, kisha atapiga takbira tano na baada ya kila takbira atakunuti, kisha atarukuu na asujudu. Atakaposimama kwa ajili ya rakaa ya pili atasoma Alhamdu na Sura nyingine, atapiga takbira nne, atakunuti baada ya kila takbira, kisha atarukuu na kutimiza Swala yake.

## SWALA YA KUPATWA KWA MWEZI NA JUA

Mafakihi wa madhehebu manne wamesema: “Swala ya kupatwa kwa jua na mwezi ni Sunna iliyokokotezwa, si Swala za wajibu.” Maimamiyya wamesema: “Ni faradhi ya lazima juu ya kila mukallafu (*Ainiy*).”

Kwa Mahanafi haina jinsi maalum bali huswaliwa rakaa mbili kama ilivyo katika Swala za Sunna za kawaida kila rakaa ikiwa na



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 174 2/1/2017 3:51:48 PM

kisimamo kimoja na rukuu moja. Na anayeswali ataswali Swala hiyo kwa rakaa mbili, na akipenda ataswali rakaa nne au hata zaidi.

Ama jinsi inavyoswaliwa kwa Mahanbali, Mashafi na Maliki, ni kwamba katika kila rakaa moja mna kusimama mara mbili na rukuu mbili. Atapiga takbira kisha asome Alhamdu na Sura nyingine kisha atarukuu. Kisha atasimama tena asome Alhamdu na Sura nyingine kisha atarukuu na asujudu, baada ya hapo atasimama kwa rakaa ya pili, afanye kama alivyofanya katika rakaa ya kwanza, na atatimiza Swala yake. Na pia hujuzu kuswali rakaa mbili kwa mfumo wa Swala za Sunna za kawaida.

Na kwa muwafaka wa mafakihi wa madhehebu yote, Swala hiyo huswihi inaposwaliwa kwa jamaa au kila mtu peke yake. Kisha Mahanafi wakaitofautisha Swala ya kupatwa kwa mwezi kwa kusema kwamba, katika Swala hiyo hapana sharia ya kuswaliwa kwa jamaa, bali huswaliwa na kila mtu peke yake ndani ya majumba yao.

Ama kuhusu wakati wa kuswaliwa kwa Swala hiyo, kongamano la mafakihi limeafikiana kuwa Swala hiyo huswaliwa tangu jua au mwezi unapoanza kupatwa hadi unaporejea katika hali yake kwa ukamilifu. Lakini Maliki wao wanasema: "Wakati wa Swala hiyo huanza tangu jua linapoinuka juu kiasi cha mkuki hadi linapokengeuka."

Mahanafi na Maliki wamesema: "Husunniwa kuswali rakaa mbili wakati wa majanga, kama vile tetemeko la ardhi, kimbunga, kunapofunga giza, kunapozuka maradhi mabaya na kila panapozuka jambo linalotia hofu."

Mahanbali wamesema: "Haisuniwi kuswali Swala ya Sunna katika mambo hayo yote isipokuwa kunapotokea tetemeko la ardhi peke yake."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 175 2/1/2017 3:51:48 PM

Wameafikiana mafakihi wote kuwa Swala hii haina Adhana (kuadhini) wala Iqamah (kukimu Swala) bali kwa Maimamiyya mtu mwenye kunadi atanadi kwa kusema: *As-Swalah,* atakariri neno hilo mara tatu. Na kwa madhehebu mengine atasema: *Asswalatu al-Jamiah*.

Maimamiyya wamesema: "Kwa hakika kupatwa kwa jua, kupatwa kwa mwezi, kunapotokea tetemeko la ardhi, kunapozuka jambo lolote lile linalosababisha hofu kutoka mbinguni, kama vile kutokea giza lisilo la kawaida, wekundu mwingi, upepo mkali (kimbunga) au maafa menginyeyo, basi kila moja kati ya mambo haya na yaliyo ya mfano wake huwa ni sababu inayowajibisha Swala kama hiyo kwa kila mtu.

Na kama itatokea kuswaliwa kwa jamaa, basi Imamu atabeba jukumu la kisomo cha Maamuma yeye binafsi kama ilivyo katika Swala tano za faradhi za kila siku. Ama wakati unaoswaliwa Swala ya kupatwa kwa jua na kupatwa kwa mwezi, ni tangu mara tu baada ya kupatwa hadi hali hiyo inapoondoka, kama tulivyotangulia kusema, na mtu ambaye hakuwahi kuiswali katika wakati huo basi ataiswali kwa kulipa.

Ama Swala ya tetemeko la ardhi na Swala nyinginezo miongoni mwa Swala zenye kuswaliwa kutokana na ishara zenye kuleta hofu, hizo hazina nyakati maalum, bali ni wajibu kuharakisha kuiswali mara tu linapotokea jambo lenyewe, na kama mtu hatowahi kuiswali wakati huo, basi ataiswali wakati mwingine kwa kutekeza na si kwa kulipa, katika muda wa umri wake.

Ama namna ya kuiswali ni kama ifuatavyo: Anayeswali atapiga takbira ya kuhirimia Swala, kisha atasoma Alhamdu na Sura halafu atarukuu, atainua kichwa chake asome tena Alhamdu na Sura kisha atarukuu, atafanya hivyo hadi zitimie rukuu tano, baada ya kumaliza rukuu ya tano atasujudu sijda mbili. Akimaliza atasimama kuanza



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 176 2/1/2017 3:51:48 PM

rakaa ya pili, asome Alhamdu na Sura kisha arukuu, ataendelea vivyo hivyo hadi rukuu ya tano katika rakaa hiyo ya pili, kisha atasujudu sijda mbili, akae tashahudi (asome tashahud) na atoe salaam. Hapo jumla itakuwa ni rukuu kumi, sijda mbili baada ya rukuu ya tano katika rakaa ya kwanza, na sijda mbili baada ya rukuu ya tano katika rakaa ya pili.

## SWALA YA KUOMBA MVUA

Swala hii ya kuomba mvua imethibiti katika kitabu (Qur'ani) na Sunna na katika kongamano la wanavyuoni wanaotegemewa. Amesema Mwenyezi Mungu (s.w.t.):

﴿وَإِذِ ٱسۡتَسۡقَىٰ مُوسَىٰ لِقَوۡمِهِۦ فَقُلۡنَا ٱضۡرِب بِّعَصَاكَ ٱلۡحَجَرَۖ ..... "

**"Na (kumbukeni) Musa alipoomba maji kwa ajili ya watu wake …" (Al-Baqarah; 2:60).**

Na mahali pengine amesema:

فَقُلۡتُ ٱسۡتَغۡفِرُواْ رَبَّكُمۡ إِنَّهُۥ كَانَ غَفَّارٗا ١٠ يُرۡسِلِ ٱلسَّمَآءَ عَلَيۡكُم مِّدۡرَارٗا ١١

**"Nikawaambia, ombeni msamaha kwa Mola Wenu. Hakika Yeye ni Mwingi wa (kutoa) msamaha. Atakuleteeni mawingu yanyeshayo mvua nyingi." (Nuh:10-11).**

Na katika Hadith imepokewa kwamba kuna wakati watu wa Madina walipatwa na ukame, wakati Mtume ﷺ akiwa katikati ya khutba (ya Ijumaa), mara alisimama mtu mmoja akasema: "Ewe Mtume wa Mungu, mimea na wanawake wanaangamia, basi muombe Mwenyezi Mungu atunyeshee mvua." Mtume



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 177 2/1/2017 3:51:49 PM

wa Mungu ﷺ akanyoosha mikono yake juu akaomba. Anas amesema: "Wakati huo mbingu ilikuwa safi kama kioo (chupa), upepo ukaanza kuvuma kisha ukaanza kusuka mawingu (hadi) yakakusanyika, na mbingu ikatiririsha kheri zake, tukatoka huku tukitembea ndani ya maji mpaka tukafika majumbani kwetu. Mvua iliendelea kunyesha hadi ikafika siku ya Ijumaa nyingine. Mtu yule yule akasimama tena akasema: 'Ewe Mtume wa Mungu, majumba yanavunjika, na usafiri umekatika, basi muombe Mwenyezi aizuie.' Mtume ﷺ akatabasamu kisha akasema: 'Mvua hii iwe ya neema kwetu wala isiwe ya adhabu juu yetu.' Nikatazama juu mbinguni nikaona kumetokea kitu kilichozunguka pembe zote za Madina kama taji."

Ama sababu inayosababisha kuswaliwa Swala hii ni kutokea ukame, uhaba wa mvua na kukauka kwa mito. Na mafakihi wa madhehebu yote wameafikiana kuwa kama baada ya Swala hiyo kuswaliwa mvua itachelewa kunyesha, inapendekezwa irudiwe tena na tena, na ni bora watu wafunge kwa muda wa siku tatu; kisha watu watoke kwa miguu, wakiwa wanyenyekevu wenye kujidhalilisha kwa Mola wao, wakiwa pamoja nao wanawake, watoto, wazee, vikongwe na wanyama, kwenda kuomba, ili kwa kufanya hivyo iwe ni sababu inayovutia kushushwa kwa rehema za Mwenyezi Mungu.

Wameafikiana kuwa Swala hii huswaliwa kwa jamaa na pia mtu mmoja mmoja, na kwamba haina kuadhini wala kukimu, pia wameafikiana kuwa yapendeza Imamu awahutubie watu baada ya kuswali.

Ama namna ya kuswali Swala hii, wameafikiana kuwa ina rakaa mbili ambazo huswaliwa kama inavyoswaliwa Swala ya Iddi, hii ni kulingana na rai za madhehebu matatu mbali na Maliki na Mahanafi,



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 178 2/1/2017 3:51:49 PM

wao wamesema: "Yenyewe ni kama Swala ya Iddi isipokuwa hii Swala haipigwi takbira zile za ziada zilizoko kwenye Swala ya Iddi."

Maimamiyya wamesema: "Husuniwa kukunuti baada ya kila takbira kwa kuomba dua ambazo zina madhumuni ya kuhurumiwa na kuomba rehema na kunyeshelezewa mvua."

Madhehebu manne yamesema: "Hakika mfano wa dua hizo huombwa na khatibu baada ya Swala kumalizika ndani ya khutba yake, haifai kuomba ndani ya Swala."

## SWALA YA KULIPA

Mafakihi wa madhehebu yote wameafikiana kuwa anayepitwa na Swala ya faradhi ni lazima juu yake kuilipa, sawa iwe imempita kwa kuiacha makusudi, kusahau, kwa ujinga au kwa kulala. Na kwamba mwanamke mwenye damu ya hedhi na nifasi halipi Swala hata kama bado ungalipo wakati wa kufanya hivyo, kwani wajibu wa Swala kwa wanawake hao wawili umeporomoka moja kwa moja. Na kama si wajibu kwao kuiswali ndani ya wakati wake basi pia si wajibu kwao kuilipa.

Wamekhitilafiana kuhusu mwendawazimu, aliyezimia na mlevi.

Mahanafi wamesema: "Ni wajibu kulipa Swala kwa mtu aliyepotewa na akili kwa kutumia kilevi kilichoharamishwa kama vile pombe na mfano wake. Ama mwenye kuzimia na mwendawazimu, wajibu wa Swala huporomoka kwao kwa masharti mawili, la kwanza ni kuendelea kuzimia kwake au wazimu wake kwa muda zaidi ya nyakati za Swala tano, ama kukiendelea kwa muda wa nyakati za Swala tano au chini kidogo, atalipa. Pili, asirudiwe na akili au kutokwa na uwendawazimu ndani ya wakati wa Swala, kama atarudisha fahamu ndani ya wakati wa Swala na asiswali, basi itakuwa wajibu kwake kulipa."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 179 2/1/2017 3:51:49 PM

Maliki wamesema: "Mwendawazimu na aliyezimia wanawajibika kulipa Swala (wanaporudiwa na fahamu). Ama mlevi kama atakuwa amelewa kwa kitu kilichoharamishwa basi italazimu kulipa, na kama alilewa kwa kitu kilicho halali kama mtu aliyekunywa mtindi akalewa, basi huyo hatalipa."

Mahanbali wamesema: "Aliyezimia na mlevi aliyekunywa kitu kilichoharamishwa ni wajibu kwake kulipa, lakini mwenye wazimu si wajibu kwake kulipa."

Mashafi wamesema: "Mwenye wazimu, kama wazimu wake utadumu kipindi kizima cha Swala, hatalipa, na vilevile aliyezimia na mlevi kama huko kuzimia na kulewa hakutokani na wao wenyewe, la sivyo ni wajibu kwao wote wawili kulipa."

Maimamiyya wamesema: "Kulipa Swala ni wajibu kwa kila mnywaji ulevi, sawa awe alitumia ilihali akijua kwamba ni kileo, au hakujua, alihiyari kunywa, alilazimishwa au ilikuwa hapana budi anywe, ni wajibu kwake kulipa. Ama mwendawazimu na aliyepoteza fahamu kwa kuzimia si wajibu juu yao kulipa."

## NAMNA YA KULIPA SWALA:

Mahanafi wamesema: "Anayepitwa na Swala ya faradhi ni wajibu kwake kuilipa vilevile kama ilivyokuwa wajibu kwake kuiswali kabla ya kupitwa na Swala husika, pasi na kugeuza wala kubadili chochote, hivyo mtu ambaye ana dhima ya Swala kamili, na sasa anataka kuilipa ilihali yeye yupo safarini, atailipa kamili. Na mtu ambaye ana dhima ya Swala ya kukusuru, na anataka kuilipa ilihali yuko mjini kwake, atailipa kwa kukusuru. Na hukmu ni hiyo hiyo kuhusu kudhihirisha na kusoma kwa siri, kwa namna ya kuwa, kama atalipa Swala ya Isha au Magharibi wakati wa mchana basi atadhihirisha kisomo, na kama atalipa Swala ya Adhuhuri au Alasiri wakati wa usiku atasoma kwa siri." Na hii pia ndiyo kauli ya Shia Imamiyya.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 180 2/1/2017 3:51:49 PM

Mahanbali na Mashafi wamesema: "Mtu anayetaka kulipa Swala ya kukusuru iliyompita, kama atakuwa yuko safarini basi atailipa kwa kukusuru kama ilivyompita, na kama atakuwa yuko mjini kwake itampasa kulipa Swala hiyo ya kukusuru iliyompita, kwa kuswali Swala kamili bila ya kukusuru."

Ama kuhusu kusoma kwa siri na kudhihirisha, Mashafi wamesema: "Anayelipa Swala ya Adhuhuri wakati wa usiku itampasa juu yake kudhihirisha, na anayelipa Swala ya Magharibi mchana itambidi asome kwa siri."

Mahanbali wamesema: "Swala zote za kulipa ni wajibu ziswaliwe kwa siri, sawa ziwe ni za siri au za kudhihirisha kisomo, awe anazilipa wakati wa usiku au mchana, isipokuwa kama anayelipa ni imamu, na Swala anayolipa ni ya kudhihirisha, na analipa wakati wa usiku."

Na mafakihi wa madhehebu yote wameafikiana isipokuwa Mashafi tu, kuwa ni wajibu kufuata mpangilio katika Swala za kulipa, kwa kukidhi iliyotangulia kabla ya ile iliyo mbele, hivyo kama itampita Swala ya Magharibi na Isha, basi ataswali Swala ya Magharibi kabla ya Isha, kama hali ilivyo zinaposwaliwa katika nyakati zake.

Mashafi wao wamesema: "Kufuata mpangilio katika Swala zilizotoka katika nyakati zake ni Sunna tu wala si lazima. Kwa hivyo anayeswali Isha kabla ya Magharibi Swala yake huswihi."

## UNAIBU KATIKA IBADA:

Mafakihi wote wameafikiana kuwa haisihi kuweka naibu katika ibada ya Swaumu na Swala kwa niaba ya watu walio hai, katika hali yoyote ile iwayo, sawa huyo aliyewekewa naibu awe ana uwezo wa kutekeleza au hana.

Maimamiyya wamesema: "Inaswihi kuweka naibu katika ibada mbili hizo kwa niaba ya waliokufa." Na madhehebu mengine yamesema: "Haiswihi kumweka naibu kwa niaba ya aliyekufa kama isivyofaa kwa walio hai."

Na wameafikiana kwamba kuweka naibu katika ibada ya Hijja inajuzu kwa niaba ya walio hai, anapokuwa huyo anayefanyiwa Hijja kwa niaba ni mtu asiyejiweza, na pia hujuzu kwa niaba ya waliokufa kwa njia ya awla, isipokuwa Maliki wao wamesema: "Hakuna athari yoyote inayothibitisha unaibu wa badala ya watu walio hai, au wa badala ya watu waliokufa."

Kisha Maimamiyya wakawa peke yao katika kusema kuwa: "Ni wajibu juu ya mtoto kumlipia baba yake kile kilichompita katika Swala na Swaumu." Lakini wakatofautiana wenyewe kwa wenyewe. Wako kati yao waliosema ni wajibu mtoto alipe ibada zote za baba yake zilizompia hata kama alifanya makusudi kuziacha. Na wako waliosema: "Atalipa ibada ambazo zilimpita baba yake kwa udhuru pekee, kama vile maradhi na mfano wake." Na wengine wamesema: "Hatalipiwa isipokuwa ibada ambazo zilimpita wakati wa maradhi yake aliyofia." Na wengine wakaongeza kuwa mtoto hulipa ibada zilizompita mama yake kama anavyolipa zilizompita baba yake."

## SWALA YA JAMAA

Waislamu wote kwa pamoja wanakubaliana kuwa Swala ya jamaa ni katika nembo za Uislamu, na ni alama yake, na bila shaka Mtume ﷺ alidumu katika kuisimamisha (kuiendeleza) Swala ya jamaa, kisha Makhalifa na Maimamu wakaiendeleza baada ya kufa kwake. Lakini mafakihi wamekhitilafiana kuhusu; Je, Swala ya jamaa ni wajibu au Sunna?



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 182 2/1/2017 3:51:49 PM

Mahanbali wamesema: "Swala ya jamaa ni wajibu kwa kila mmoja (*aini*) awapo ana uwezo wa kufanya hivyo, lakini anapoiacha akaswali peke yake, atapata dhambi na Swala yake itaswihi."

Maimamiyya, Mahanafi, Maliki na wengi katika mafakihi wa madhehebu ya Shafi wamesema: "Si wajibu wa kila mmoja (*aini*) wala si wajibu wa pamoja (*kifaya)*, bali yasunniwa na ni Sunna iliyohimizwa tu."

Maimamiyya wamesema: "Ni sharia kuswali jamaa katika Swala za faradhi (za wajibu), wala hakuna Swala ya jamaa katika Swala za Sunna isipokuwa Swala ya kuomba mvua na ya Iddi mbili yanapokosekana masharti." Madhehebu manne yanasema: "Husunniwa jamaa katika Swala za wajibu na za Sunna."

## MASHARTI YAKE:

Ili Swala ya jamaa iswihi ni sharti yatimie masharti yafuatayo:

**1.** Uislamu, hii ni kwa itifaki ya wanavyuoni

**2.** Utimamu wa akili, na hii pia wanavyuoni wameafikiana.

Uadilifu wa Imamu, hii ni kauli ya Maimamiyya, Maliki na Mahanbali katika moja ya riwaya zao mbili zilizopekewa kutoka kwa Ahmad bin Hanbal. Maimamiyya wamesema dalili ya hilo ni kauli ya Mtume ﷺ aliposema: "Mwanamke asiwe Imamu wa mwanamume, wala muovu asiwe Imamu wa muumin." Na pia ni Ijmai ya Ahlulbayt, na kwamba uimamu wa Swala ya jamaa huhusisha uongozi, na muovu hafai kuwa kiongozi. Lakini wamesema: "Iwapo mtu atamwamini mtu mwingine, na hivyo akaswali nyuma yake, kisha ikambainikia kuwa mtu huyo ni muovu (fasiki), si wajibu kwake kuirudia Swala hiyo."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 183 2/1/2017 3:51:49 PM

**1.** Kuwa mwanamume: Haiswihi kwa mwanamke kuwa Imamu wa wanaume, na huswihi mwanamke kuwa imamu wa wanawake wenzake. Hii ni kwa mujibu wa mafakihi wa madhehebu yote isipokuwa Maliki, wao wamesema: "Mwanamke haruhusiwi kuwa Imamu hata kwa wanawake wenzake."

**2.** Kubalehe, ni sharti la uimamu kwa madhehebu ya Maliki, Mahanafi na Mahanbali. Ama Mashafi wao wamesema: "Inaswihi kumfuata katika Swala mtoto mtambuzi." Na Maimamiyya wana kauli mbili, ya kwanza inasema kubalehe ni sharti la uimamu. Na ya pili inasema: "Huswihi uimamu wa kijana mtambuzi aliye karibu na kubalehe."

**3.** Idadi ya wanaoswali jamaa. Wameafikiana kuwa kwa uchache kabisa idadi inayotimiza Swala ya jamaa - mbali na Ijumaa - ni watu wawili, Imamu na maamuma.

**1.** Kwa madhehebu yote, katika kusimama kwao, maamuma asimtangulie Imamu, isipokuwa Maliki wanasema: "Swala ya maamuma haibatiliki hata kama atamtangulia Imamu wake."

**2.** Kuwa mahali pamoja na pasiwepo pazia au kizuizi kinachotenganisha kati yao. Maimamiyya wamesema: "Haijuzu kwa maamuma kuwa mbali na Imamu kwa umbali usiokuwa wa kawaida, isipokuwa kama tu safu za maamuma zimeungana. Wala haijuzu Swala ya jamaa kama patakuwepo kizuizi kinachomzuwia maamuma mwanamume kumuona Imamu wake au kumuona mtu anayemshuhudia Imamu katika wanaomfuata Imamu huyo, isipokuwa wanawake, ambapo yaswihi kwa mwanamke kumfuata mwanamume pamoja na kuwepo kizuizi, iwapo kizuizi hicho hakimtatizi katika kuvifuata vitendo vya Imamu anayemfuata."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 184 2/1/2017 3:51:49 PM

Mashafi wamesema: "Hakuna kinachozuwia kuswihi kwa Swala ya maamuma panapokuwa kati ya Imamu na maamuma pana umbali wa dhiraa mia tatu (300), kwa sharti tu pasiwepo kati yao kizuizi."

Mahanafi wamesema: "Anaposwali mtu ndani ya nyumba yake kwa kumfuata Imamu anayeswali msikitini, kama nyumba yake itakuwa imeshikamana na msikiti kwa namna ambayo hakuna kinachotenganisha kati yake isipokuwa ukuta peke yake, basi Swala yake itaswihi, kama huyo maamuma hatashindwa kujua hali ya Imamu anayemfuata. Ama kama nyumba yake imetengana na msikiti kwa kuwepo njia au mto kati yake, basi Swala yake haitaswihi kwa kumfuata Imamu huyo."

Maliki wamesema: "Kutofautiana mahali alipo Imamu na Maamuma hakuzuii Swala kuswihi, kama patakuwepo kizuizi kinachowatenganisha Imamu na maamuma kwa kuwepo njia, mto au ukuta basi Swala inaswihi madamu tu maamuma atakuwa ana makini ya kudhibiti barabara vitendo vya Imamu."

**3.** Hapana budi kwa maamuma kukusudia (kutia) nia ya kumfuata imamu, kwa itifaki ya mafakihi wote.

**4.** Swala ya Imamu na maamuma iwe ni moja. Wameafikiana kuwa haiswihi mmoja kumfuata mwingine iwapo zinatofautiana Swala mbili (ya imamu na maamuma) katika nguzo na vitendo, kama pale mmoja anapokuwa katika Swala za kila siku za faradhi na mwingine katika Swala ya jeneza, au Swala ya Idd. Wametofautiana katika mambo mengine, Mahanafi wamesema: "Haiswihi mwenye kuswali Swala ya Adhuhuri kumfuata anayeswali Swala ya Alasiri, au anayeswali kwa kulipa kumfuata mtu anayeswali ndani ya wakati, na kinyume chake. Na ndivyo wasemavyo Maliki." Maimamiyya na



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 185 2/1/2017 3:51:49 PM

Mashafi wamesema: "Huswihi Swala katika hali hizo zote." Mahanbali wamesema: "Haiswihi Swala ya Adhuhuri ya mtu anayemfuata mtu anayeswali Swala ya Alasiri, wala kinyume chake, lakini huswihi Swala ya Adhuhuri ya kulipa nyuma ya mtu anayeswali Adhuhuri ya kutekeleza ndani ya wakati."

**5.** Usomaji mzuri (wa Qur'ani), haifai kwa mtu anayesoma vyema Qur'ani kumfuata mtu asiyeisoma vyema, hii ni kwa itifaki ya wanavyuoni, na anapomfuata basi Swala ya huyo anayefuata itabatilika, hii ni kwa mujibu wa madhehebu yote, isipokuwa Mahanafi wao wamesema: "Swala ya wote wawili hubatilika." Nao wana hoja yao waliyoielekea, kwani mtu ambaye hajui kusoma na asiye na uwezo wa kufanya hivyo ni wajibu kwake kuswali nyuma ya mwenye uwezo wa kusoma vizuri, kwa namna ambayo itamwezesha kuitekeleza Swala yake kwa kisomo kilicho sahihi ingawa ni kupitia kwa jamaa, wala hapana ruhusa ya kuswali peke yake.

## KUFUATA:

Mafakihi wameafikiana kuwa mtu aliyetawadha anaweza kumfuata mtu aliyetayammamu, na kwamba ni juu ya maamuma kumfuata Imamu wake katika kusoma dhikri zinazotajwa katika Swala, kama vile kusema: *Subhana Rabbiyal adhimi,* na *Subhana Rabbiyal Aala* na *Samialllahu Liman hamidah.* Kisha wamekhitilafiana kuhusu wajibu wa kumfuata Imamu wake katika kisomo.

Mashafi wamesema: "Maamuma atamfuata Imamu katika Swala za siri, si katika zile za dhahiri, na katika kila rakaa maamuma huwajibika kusoma Alhamdu."

Mahanafi wamesema: "Haruhusiwi kumfuata Imamu katika Swala za siri wala za kudhihirisha, bali imepokewa kutoka kwa



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 186 2/1/2017 3:51:49 PM

Imamu Abu Hanifa mwenyewe kuwa maamuma kusoma nyuma ya Imamu wake ni kufanya maasi (ni kuasi).” (An Nawawiy *Sharhul Muhaddhab* Juzuu ya 3, uk. 355).”

Maliki wamesema: “Maamuma hutakiwa kusoma nyuma ya Imamu katika Swala za kusoma kwa siri, wala hatakiwi kusoma katika Swala za kudhihirisha.”

Maimamiyya wamesema: “Kwa hakika kisomo kwa maamuma si wajibu katika rakaa mbili za mwanzo, bali ni wajibu katika rakaa ya tatu ya Magharibi na mbili za mwisho katika Swala ya Adhuhuri, Alasiri na Isha.”

Na mafakihi wote wameafikiana kuwa ni wajibu kwa maamuma kumfuata Imamu wake kwa vitendo, lakini wametofautiana kuhusu maana ya kufuata vitendo vyenyewe. Maimamiyya wamesema: “Maana ya kufuata ni kutotangulia kitendo cha maamuma kabla ya Imamu, wala asichelewe sana kumfuata Imamu wake, hapana budi avikutanishe vitendo vyake na vya Imamu au achelewe kidogo tu.”

Mahanafi wamesema: “Kufuata hupatikana kwa kuvikutanisha vitendo, na maamuma kumaliza kitendo chake anapomaliza Imamu moja kwa moja bila ya kuchelewa, kama maamuma atarukuu baada ya Imamu wake kuinua kichwa chake kutoka kwenye rukuu na kabla hajainama kwenda kwenye kusujudu basi yeye kwa hakika atakuwa amemfuata Imamu wake kwenye rukuu.”

Maliki wamesema: “Maana ya kufuata ni kuwa kitendo cha maamuma kifanyike baada tu ya kitendo cha Imamu, asimtangulie wala asiende naye sawa, wala asichelewe kumfuata kuchelewa kuliko kukubwa sana, bali iwe ni kwa kiasi kwamba maamuma atarukuu kabla Imamu wake bado hajainua kichwa chake kutoka kwenye rukuu.”



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 187 2/1/2017 3:51:49 PM

Mahanbali wamesema: "Kufuata kuna maana ya maamuma kutomtangulia Imamu wake katika kitendo miongoni mwa vitendo vya Swala, wala asichelewe kumfuata kwa chochote katika hivyo vitendo, kwa maana ya kuwa maamuma asirukuu baada ya Imamu kumaliza rukuu, wala Imamu asimalize kurukuu kabla maamuma hajaanza kurukuu."

## ALIYETANGULIWA NA IMAMU KATIKA SWALA:

Anapokuja mtu kuswali baada ya kuwa Imamu ameshaanza kuswali, na pia kumtangulia kwa rakaa moja au zaidi, mafakihi wote wa madhehebu manne wameafikiana kuwa, mtu huyo atanuia Swala ya jamaa na aendelee na Swala yake. Lakini je hapo alipomkuta Imamu, atapafanya kuwa mwanzo wa Swala yake au atapafanya mwisho wa Swala yake? Kwa mfano kama mtu atamkuta Imamu yumo katika rakaa ya mwisho ya Swala ya Magharibi, akaiswali rakaa hiyo pamoja na Imamu, zitabaki juu yake rakaa mbili ambazo hana budi aziswali. Lakini je, hiyo rakaa ya tatu aliyokuta Imamu akiendelea nayo, naye akaungana naye, itakuwa kwa maamuma huyo ni ya tatu kama ilivyo kwa Imamu wake, ambapo zile rakaa mbili zilizobaki zitakuwa ni za kwanza? Au hiyo rakaa ya tatu aliyokuta Imamu akiendelea nayo, naye akaungana naye, ndiyo itakuwa ya kwanza kwa maamuna huyo, ambapo kisha ataendelea na rakaa ya pili na ya tatu?

Maliki, Mahanafi na Mahanbali wamesema: "Kwa hakika pale anapopakuta maamuma katika Swala ya Imamu wake huwa ndipo panapokuwa mwisho wa Swala ya maamuma, hivyo basi kama mtu ataipata rakaa ya mwisho ya Magharibi pamoja na Imamu, ataihesabu kuwa ni rakaa yake ya mwisho vile vile sawa na ilivyo kwa Imamu, kisha baada ya Imamu kutoa salam yeye atainuka na kuleta rakaa ambapo atasoma Alhamdu na Sura. Atasoma tashahud, kisha ataleta rakaa nyingine ambapo atasoma Alhamdu na Sura



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 188 2/1/2017 3:51:49 PM

nyingine. Na kwa neno jingine ni kwamba ataswali kama hivyo kwa kutanguliza rakaa ya tatu kabla ya zile mbili za kwanza, ile rakaa moja aliyoiswali pamoja na Imamu itakuwa ndio mwisho wa Swala yake, na zile alizoswali baada ya Imam kutoa salaam ndio mwanzo wa Swala yake."

Maimamiyya na Mashafi wamesema: "Sehemu ambayo maamuma humkuta Imamu akiendelea nayo huwa ndio mwanzo wa Swala yake, na si mwisho, hivyo kama mtu ataipata rakaa moja ya Maghrib na akaiswali pamoja na Imamu, basi yeye ataihisabu kuwa ni ya kwanza, kisha atainuka aswali ya pili aketi kitako kusoma tashahud baada yake, kisha ataswali rakaa ya tatu na itakuwa ndiyo mwisho wa Swala yake."

## MWENYE HAKI ZAIDI YA KUWA IMAMU:

Mahanafi wamesema: "Inapokusanyika idadi kubwa ya watu kwa ajili ya kutaka kuswali basi atatangulia mbele katika kuwaswalisha, mtu ambaye anazijua hukmu za Swala zaidi kuliko wote. Kama hakupatikana, basi aliye hodari zaidi katika kusoma Qur'ani, kama hakupatikana, basi awaswalishe yule aliyejihifadhi zaidi na mambo machafu, kama hakupatikana, basi awaswalishe aliyewatangulia katika kusilimu, kama hakupatikana, basi awaswalishe aliye mtu mzima wao, pia kama hakupatikana, basi awaswalishe aliyewashinda kwa uzuri wa sura, pia kama hakupatikana basi awaswalishe msafi wa nguo kuliko wote, na kama watalingana katika hilo, sasa watapiga kura baina yao wote."

Maliki wamesema: "Atatangulia mbele kuwaswalisha Sultani (kiongozi wao) au naibu wake, kama hayupo mtu kama huyo, basi ataswalisha Imamu wa msikiti huo au mwenye nyumba, kisha anayezijua zaidi hukmu za Swala, kisha anayezijua vyema Hadith



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 189 2/1/2017 3:51:49 PM

kuliko wote, kisha aliyetangulia kuingia katika uislamu, kisha mwenye nasaba bora zaidi, kisha mwenye tabia njema zaidi, kisha mwenye nguo nzuri zaidi, na kama watalingana, basi watapiga kura kati yao wote."

Mahanbali wamesema: "Atatangulia aliye fakihi zaidi ambaye ni msomaji mzuri zaidi wa Qur'ani, kisha anayeisoma vyema Qur'ani tu, kisha anayezihifadhi vyema hukmu za Swala, kisha msomaji wa Qur'ani ambaye hazielewi hukmu za Swala yake, kisha mkubwa wa miaka, kisha mwenye nasabu tukufu, kisha wa kale wao katika kuhama, kisha mchaji Mungu zaidi, kisha aliyejihifadhi zaidi na maasia, kama watalingana basi watapiga kura."

Mashafi wamesema: "Atatangulia kiongozi (wao), kisha Imamu wa msikiti (huo), kisha aliye fakihi zaidi, kisha asomaye vyema zaidi Qur'ani, kisha mwenye kujinyima zaidi dunia, kisha aliyejiepusha zaidi na maasi, kisha wa kale wao katika kugura, kisha aliye mkubwa zaidi wa umri, kisha aliye na nasaba bora, kisha mwenye tabia na mwenendo mzuri zaidi, kisha mwenye nguo nadhifu zaidi, msafi wa mwili na vitendo, kisha mwenye sauti nzuri zaidi, kisha mwenye sura nzuri zaidi, kisha mwenye mke, kisha kama watalingana watapiga kura."

Maimamiyya wamesema: "Watakaposhindana watu kila mmoja akawa anataka kuswalisha yeye kwa ajili ya kutaka kupata thawabu za uimamu, si kwa sababu ya lengo la kidunia, basi atatangulia katika kuswalisha yule ambaye maamuma watamchagua kwa kuzingatia vigezo vya kisharia na malengo ya dini, si kwa malengo ya kidunia. Na kama watakhitilafiana basi ubora ni kumtanguliza aliye fakihi zaidi, kisha anayesoma vyema zaidi Qur'ani, kisha aliye mfasaha wa matamshi, mwisho ni yule mwenye kigezo cha kisharia."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 190 2/1/2017 3:51:49 PM

# SWALA YA MSAFIRI

Mafakihi wameafikiana kuwa kukusuru Swala kunazihusu Swala za rakaa nne nne tu za faradhi, hivyo Adhuhuri, Alasiri na Isha ataziswali rakaa mbili mbili kama Swala ya Asubuhi. Kisha wamehitilafiana kuhusu je, kukusuru mtu awapo safarini ni jambo la wajibu ambalo si ruhusa kuliacha, au ipo ruhusa ya kujiamulia kati ya kukusuru na kutimiza?

Mahanafi na Maimamiyya wamesema: "Ni jambo la wajibu, kwani kukusuru Swala safarini ni jambo lililoamuliwa (na sharia)."

Madhehebu yaliyobakia yamesema: "Kukusuru Swala mtu anapokuwa safarini si wajibu bali ni hiyari ya mtu, akipenda atakusuru na akipenda atakamilisha."

## MASHARTI YA KUKUSURU:

Kukusuru kuna masharti yake:

**1.** Kutimiza masafa, hii ni kwa itifaki ya madhehebu yote, na masafa hayo kwa Mahanafi ni farsakhi (24) kwenda tu peke yake, wala mtu haruhusiwi kukusuru Swala chini ya masafa hayo.

Maimamiyya wamesema: "Ni farasakhi (8) kwenda tu, au kwa kuunganisha kwenda na kurudi."[19]

Mahanbali, Maliki na Mashafi wamesema: "Ili kukusuru Swala kufanyike ni sharti safari iwe inafikia umbali wa farasakhi (16) kwenda peke yake, lakini haidhuru kama umbali huu utapungua kwa kiasi cha maili mbili." Kisha Maliki wameongezea: "Hapana ubaya kupungua maili nane."

[19] Kwa sharti aende na kurudi mchana na usiku wake, kwani kwa kufanya hivyo atakuwa safari yake imemshughulisha kwa siku nzima kamili, baadhi yao wamesema atakusuru anapokusudia kurudi kabla ya siku kumi.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 191 2/1/2017 3:51:49 PM

Na farasakhi moja ni sawa na kilomita 5 na mita arobaini (*Al-Fikhu alal Madhahibul Arbaa*, Juzuu ya 4 mlango unaotafiti masharti ya kukusuru Swala).

Kwa hivyo kufuatana na hesabu hiyo masafa ambayo mtu anaweza kukusuru Swala kwa Mahanafi ni kilomita 107 na nusu, na mita ishirini. Na kwa madhehebu matatu ni kilomita 80 na nusu na mita 140. Na kwa Maimamiyya ni kilomita 40 na mita 320.

**2.** Ni kuyakusudia masafa hayo kwa ukamilifu kabla hajaanza safari yake, kuanzia mwanzo wa safari yake, hii ni kwa itifaki ya mafakihi wote. Na nia ya mtu anayefuata kama vile mke, mtumishi, mateka na askari hufuata nia ya mwamrishaji wake na kiongozi wake, na kama hataijua nia yake basi yeye ataswali kamili.

**3.** Haijuzu kukusuru Swala isipokuwa baada ya kuyatoka majengo ya mji (wake), hii ni kwa madhehebu manne. Maimamiyya wamesema: "Hiyo haitoshi, bali ni sharti yatoweke (machoni mwake) asizione kuta za mji au afike umbali ambao hasikiki mwadhini wa mji wake." Na mpaka ambao waliuzingatia kuwa ndio mahali pa kuanzia safari ndio huo huo ambao wameuzingatia kuwa mahala pa kumalizia. Kwa maana ya kuwa arudipo mjini kwao basi bado ataendelea kukusuru hadi yamdhihirikie majengo yake au amsikie mwadhini wa mji wake.

**4.** Ni sharti safari yenyewe iwe ni ya halali, kama itakuwa safari yake ni ya haramu, kama vile ya kwenda kuiba na mfano huo, basi haruhusiwi kukusuru Swala, hii ni kwa itifaki ya madhehebu yote isipokuwa kwa Mahanafi tu, wao wamesema: "Mtu huruhusiwa kukusuru awapo katika safari ya aina yoyote ile iwayo, hata kama ni safari ya haramu, na mwisho wa yote ni

kuwa mtu huyo hupata dhambi ya kutenda kitendo cha haramu."

**5.** Ni msafiri kutomfuata mkaazi wa mji, au kumfuata msafiri anayetimiza Swala kamili, na kama atafanya hivyo, basi itampasa naye aswali Swala kamili, hii ni kwa mujibu wa madhehebu manne. Ama kwa Maimamiyya sharti hili halina uzito wowote, kwani wao wamejuzisha kwa mtu anayetimiza Swala yake kumfuata anayekusuru, na kinyume chake, kwa sharti tu kila mmoja wao atekeleze anavyopaswa kufanya. Msafiri kwa mfano anaposwali Swala ya Adhuhuri, Alasiri au Isha nyuma ya mtu anayeswali kamili, basi ataswali naye rakaa mbili kisha atakaa tashahhud pamoja naye, Imamu naye aendelee na Swala yake hadi mwisho, na ikitokea mkaazi wa mji anaswali nyuma ya msafiri, ataswali rakaa mbili naye, kisha atatimiza rakaa zilizobaki katika Swala peke yake.

**6.** Anuie kukusuru katika Swala anayotaka kuiswali, kama ataswali bila ya kutia nia ya kukusuru basi Swala hiyo ataiswali kamili, hii ni kwa Mahanbali na Mashafi. Maliki wamesema: "Nia ya kukusuru hutosha tangu ile ya mara ya kwanza aliyotia alipoanza safari, wala haina lazima ya kunuia upya katika kila Swala." Maimamiyya na Mahanafi wamesema: 'Nia ya kukusuru si sharti la wajibu wa kukusuru, hivyo kama hakunuia kukusuru itakuwa ni wajibu kwake kukamilisha, kwani hukmu haigeuzwi na nia, na kwa kuwa alinuia kusafiri tangu mwanzo", ila Maimamiyya wamesema: "Msafiri anaponuia kukaa sehemu kisha akafuta nia yake, basi atakusuru maadamu hakuwa ameswali kwa kukamilisha japo Swala moja, na kama ameshaswali Swala moja kwa kukamilisha kisha akaghairi nia yake (akaamua kusafiri), basi ataendelea kuswali kwa kukamilisha.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 193 2/1/2017 3:51:50 PM

**7.** Ni kutotia nia ya kukaa zaidi ya siku kumi na tano mfululizo, hii ni kwa madhehebu ya Hanafi, au siku kumi kwa Maimamiyya, au siku nne kwa madhehebu ya Maliki na Mashafi, au muda ambao ndani yake atawajibika kuswali rakaa ishirini kwa Mahanbali. Na Maimamiyya wameongeza kwa kusema, kama atakuwa hakukusudia kukaa wala kutokaa, na akawa amechanganyikiwa hajui ni muda gani atamaliza haja yake, basi ataendelea kukusuru hadi atakapopitisha siku thelathini, na baada ya hapo itakuwa ni wajibu kwake kukusuru hata kama ni Swala moja.

**8.** Kazi ya msafiri huyo isiwe ni yenye kumlazimu kuwa ni mwenye kuendelea na safari, kama vile madereva au wafanyabiashara ambao huwalazimu safari ya kudumu, na kukosa kutulia majumbani kwao pindi wanaporudi. Sharti hili ni kwa mujibu wa Mahanbali na Maimamiyya tu, na si kwa mujibu wa madhehebu mengine.

**9.** Asiwe ni yule ambaye nyumba yake iko pamoja naye kila aendapo, kama ilivyo kwa watu wa majangwani ambao hawana makazi ya kudumu, ambao huhamahama majangwani na mahali penye nyasi na malisho (maporini). Na sharti hili limetamkwa na Maimamiyya tu.

**10.** Mahanbali, Mahanafi na Maliki wamesema: "Msafiri anaporudi kutoka safarini, na akatia azima ya kurudi kwenda mahali ambapo alianzia safari yake hiyo, basi ataangalia, kama kughairi huko kumemjia kabla hajakwenda mwendo wa umbali unaofikia kiasi kinachomfanya mtu akusuru Swala basi safari yake itakuwa imebatilika, na papo hapo itampasa aswali Swala kamili, na kama atakuwa amekwenda masafa ya mpaka ulio-



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 194 2/1/2017 3:51:50 PM

wekwa na sharia kwa ajili ya kukusuru, basi ataendelea kukusuru hadi atakaporudi mjini."

Mashafi wamesema: "Popote pale anapoingiwa na fikra za kutoendelea na safari yake basi itambidi atimize Swala." (*Al-Wajiz* kitabu cha Imam Ghazali, Mlango wa Swala ya msafiri). Na maana ya maneno haya ni kuwa mtu huwajibika kuswali Swala ya kukamilika katika hali yoyote ile iwayo hata kama amekwisha kwenda umbali wa kutosha, kwa kuwa kule kuacha kulielezea jambo kirefu huwa kuna maana ya kuenea na kuyahusisha yote yaliyomo.

Maimamiyya wamesema: "Anapoghairi kusafiri au anaposita (aende au asiende) kabla hajakata masafa, ni wajibu kwake kukamilisha Swala. Na kama ameshakata masafa ni wajibu kwake kukusuru, hivyo kule kuendelea na nia ya safari ndilo sharti la kukusuru maadamu hajakata masafa. Ama baada ya kwenda kadiri ya masafa fulani basi hapo hupatikana ulazima wa kukusuru na hapo huwa hapana tena ulazima wa kutia nia ya kukusuru."

Kisha wanavyuoni wa madhehebu yote wameafikiana kuwa kila sharti linalozingatiwa kuwa ni sharti la kukusuru Swala, basi vilevile ndilo sharti la kula (kutofunga) awapo safarini (kuhusiana na funga ya mwezi wa Ramadhani). Na baadhi ya madhehebu mengine yamezidisha masharti mengine ya kumruhusu mtu kufungua saumu awapo safarini, mambo hayo tutayataja kwenye mlango wa Swaumu. Ama Maimamiyya wao hawakuzidisha chochote, bali wamesema; "Anayefungua Swaumu akala kwa safari, basi atakusuru Swala, na anayekusuru basi na afungue funga yake."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 195 2/1/2017 3:51:50 PM

## KUKUSANYA SWALA MBILI

Kutokana na udhuru wa safari, ipo ruhusa ya kuswali kwa pamoja Swala mbili Adhuhuri na Alasiri, na pia Swala ya Magharibi na Isha, kwa kutanguliza au kwa kucheleweşha, hii ni kwa mujibu wa madhehebu ya Imamu Malik, Shafi na Ahmad bin Hanbal. Ama Abu Hanifa, yeye amesema:

"Haijuzu kukusanya Swala mbili pamoja kwa udhuru wa safari katika hali yoyote ile."

Maana ya kuzikusanya kwa kutanguliza, ni kuziswali Swala mbili za Adhuhuri na Alasiri katika wakati wa Adhuhuri, na maana ya kuzikusanya kwa kuchelewesha, ni kuziswali Swala hizo katika wakati wa Alasiri.

## ASIYEJUA HUKMU ZA KUKUSURU SWALA, NA HUKMU YA ALIYESAHAU

Maimamiyya wamesema: "Mtu anayeswali Swala kamili hali ya kuwa yuko safarini kwa makusudi Swala yake itabatilika, na itamlazimu arudie kuiswali tena ndani ya wakati kama bado wakati wake ungalipo, na aiswali kwa kulipa kama wakati wake umepita. Na anayeswali hivyo kwa sababu ya kutojua wajibu wa kukusuru, basi hatairudia kamwe iwe ndani ya wakati au nje ya wakati. Na anaposwali kamili kwa sababu ya kusahau kisha akakumbuka hali ya kuwa bado wakati wa Swala hiyo ungalipo atairudia tena, na anapokumbuka baada ya wakati wake kwisha basi hatairudia."

Maimamiyya wamesema tena: "Anayeingiliwa na wakati wa Swala (fulani) hali yuko mjini kwake akiwa na makini ya kuweza



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 196 2/1/2017 3:51:50 PM

kuswali Swala hiyo, lakini asiswali, kisha akasafiri, basi itamlazimu aiswali Swala hiyo kwa kukusuru. Na kama ataingiliwa na wakati hali ya kuwa ni msafiri na asiswali Swala hiyo hadi akafika mjini kwake, au mahali atakapokaa muda wa siku kumi, basi ni juu yake aiswali kamili, hapa kigezo ni hali ya kutekeleza si hali ya kuwajibika."

## MAMBO YANAYOBATILISHA SWALA

Swala hubatilika kwa mambo yafuatayo:

**1.** Maneno (kusema), na uchache wake ni maneno ambayo yameunganishwa kwa herufi mbili hata kama ni yale yasiyoelezea maana yoyote, na vilevile kutamka herufi moja tu inapokuwa ni yenye kufahamisha maana, kama kusema *Qi* ambayo inajulisha kitendo cha kuamrisha (katika lugha ya Kiarabu) kutokana na neno *Waqaa,* lakini Swala haibatiliki kwa kutamka herufi moja isiyo na maana yoyote, na haibatiliki pia kwa kutoa sauti ambayo ina mchanganyiko wa herufi ambazo hazikukusudiwa.

Ama Mahanbali na Mahanafi, wao katika kubatilisha Swala hawakutofautisha baina ya maneno yanayotoka kwa kusahau au kwa makusudi.

Maimamiyya, Mashafi na Maliki wamesema: "Swala huwa haibatiliki kwa kutamka maneno kwa kusahau, maneno yenyewe yanapokuwa machache kwa namna ambayo hayafuti sura ya Swala."

Wala haibatiliki Swala kwa kukohoa iwe ni kwa haja fulani au bila ya haja, kwa madhehebu ya Maimamiyya na Maliki. Na hubatilisha Swala kwa madhehebu yaliyobakia ikiwa bila ya haja, lakini si vibaya kama pana haja, kama vile kuitengeneza sauti kusudi herufi zipate kutokea vyema kila moja kutoka kwenye matokeo yake, au kumuongoza Imamu alipokosea.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 197 2/1/2017 3:51:50 PM

Na mafakihi wameafikiana kuwa hujuzu kuomba dua ndani ya Swala kwa ajili ya kuomba kheri na msamaha kutoka kwa Mwenyezi Mungu, isipokuwa Mahanafi na Mahanbali walitilia mkazo kuwa dua hiyo iwe imepokewa kutoka ndani ya Qur'ani au kutoka kwenye Sunna ya Mtume ﷺ au iwe ni miongoni mwa maombi yanayaombwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu tu peke yake kama vile riziki na baraka.

Wala si katika maneno yanayobatilisha Swala kutamka tasbihi (kusema *Subhanallah*) ambayo itakuwa ni ya kumjulisha mtu kwamba yumo ndani ya Swala au kumuongoza Imamu au kurekebisha kosa.

Maimamu wanne wamesema: "Miongni mwa maneno yanayobatilisha Swala ni kuitikia salaam, kama anayeswali atasalimiwa na mtu naye yu katika Swala, akaitikia kwa kujibu kupitia kinywa chake, Swala yake itabatilika, lakini hapana ubaya kujibu maamkuzi kwa kutumia ishara."

Maimamiyya wamesema: "Ni wajibu kuitikia salaam kwa mfano wake ule ule ikiwa ni maamkuzi yaliyotamkwa kwa maneno *Assalam alaykum,* si kwa tamko jinginelo kama *Swabahulkhayr* (habari ya asubuhi) na mfano wake." Na wameshurutisha maamkuzi hayo yawe ni kwa maneno Assalam kwa utimilifu bila ya kugeuza kitu, mfano kama mtu amemwamkia mwenzake anayeswali kwa kumwambia *Salamun alaykum* basi naye atajibu hivyo hivyo *Salamun Alaykum* bila ya kuingiza *Alifu* na *Lam*, na jawabu la *Assalam Alaykum* liwe vivyo hivyo kwa *Alifu* na *Lam*.

**1.** Kitendo chochote kinachoigeuza sura ya Swala huibatilisha Swala, kwa namna ambayo itamfanya mtu anayemtazama adhanie kwamba huyo anayekifanya kitendo hicho hayumo ndani ya Swala. Na hili ni sharti walilowafikiana mafakihi wa madhehebu yote.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 198 2/1/2017 3:51:50 PM

**2.** Kula na kunywa hubatilisha Swala kwa itifaki ya madhehebu yote. Lakini wamekhitilafiana kuhusu kiwango kinachobatilisha Swala katika huko kula na kunywa. Maimamiyya wamesema: "Kula na kunywa kokote hubatilisha Swala kunapoondoa sura ya Swala, au kusababisha sharti moja miongoni mwa masharti yake kutotimia, kama vile mfuatano na mfano wake."

Mahanafi wamesema: "Kila kula na kunywa hubatilisha Swala, sawa kuwe ni kwa wingi au kwa uchache, hata kama kilicholiwa ni punje ya ufuta, na kilichonywewa ni tone la maji, pasi na tofauti yoyote katika kufanya hivyo iwe alikula kwa makusudi au kwa kusahau."

Mashafi wamesema: "Chochote kinachoingia hadi tumboni mwa mtu anayeswali katika chakula au kinywaji basi hubatilisha Swala, kiwe kingi au kichache, lakini hukmu hii inamuhusu mwenye kuswali ambaye amekula au kunywa kwa makusudi huku akijua uharamu wake. Ama kama alikula kwa kutojua au kwa kusahau basi hapo haidhuru kitu kama alikula kidogo, bali hudhuru kama alikula kwa wingi."

Mahanbali wamesema: "Chakula kingi hubatilisha Swala kiliwapo kwa makusudi au kwa kusahau, na chakula kichache hubatilisha Swala kinapoliwa kwa makusudi, na hakibatilishi kinapoliwa kwa kusahau."

**3.** Linapozuka jambo linalotengua wudhu au jambo linalolazimisha kuoga, hadathi kubwa au ndogo, basi hubatilisha Swala kwa madhehebu yote isipokuwa kwa Mahanafi ambao wamesema: "Jambo linalotengua wudhu hubatilisha Swala kama litazuka kabla ya kukaa *tashahhud* (*Tahiyyatu*) ya mwisho kwa kiasi cha kuisoma *tashhhud,* ama kama litazuka baada ya hapo na kabla ya kutoa salam halibatilishi Swala."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 199 2/1/2017 3:51:50 PM

**4.** Kucheka kwa sauti hubatilisha Swala kwa itifaki ya madhehebu yote, isipokuwa Mahanafi, kwao hukmu yake ni sawa na hukmu ya *hadath* kwa maelezo yaliyotangulia huko nyuma.

Na kwa kuwa mambo yanayobatilisha Swala yana umuhimu mkubwa na ni mengi yaliyotawanyika kwa aina mbalimbali, na kwa kuwa kila madhehebu ina rai ambazo inaafikiana na madhehebu mengine au kutofautiana nayo, basi ni kheri tuzielezee kwa mpigo (kwa ujumla) kama zilivyo katika kila madhehebu kwa mfumo unaofuata:

Mashafi wamesema: "Mambo yanayobatilisha Swala ni: kuzukiwa na *hadath* inayolazimu wudhu au kuoga. Kuongea, kulia na kunung'unika katika baadhi ya hali zake. Kufanya vitendo kwa kuzidisha. Kuwa na shaka katika kutia nia. Kuzukiwa na hali ya kusita ya kutaka kuikata Swala na kuendelea nayo. Kuhama kutoka Swala moja kwenda Swala nyingine, isipokuwa Swala ya faradhi ambayo anaweza akaigeuza kuwa Swala ya Sunna kama atataka kuswali Swala ya jamaa. Kufunua uchi (utupu) akiwa na uwezo wa kujisitiri kwa haraka. Kukaa uchi ilihali amepata nguo ya kumsitiri. Kuzukiwa na najisi isiyosamehewa ikiwa hakuweza kuepukana nayo haraka. Kurudia takbira ya kuhirimia. Kuacha nguzo kwa makusudi. Mwenye kuswali kumfuata katika Swala mtu asiyefaa kufuatwa kwa ajili ya ukafiri au sababu nyingine. Kuongeza nguzo ya Swala kwa makusudi. Kufika tumboni kitu kinachofunguza. Kugeuka upande usiokuwa Kibla kwa kifua. Na kutanguliza nguzo ya kitendo kabla ya ile inayoitangulia."

Maliki wamesema: "Yanayobatilisha Swala ni kuacha nguzo moja kwa makusudi au kwa kusahau kama hakukumbuka hadi akatoa salaam, huku mwenyewe akiamini kuwa ametimiza na kukamilika Swala yake na ukarefuka muda wa kukumbuka kwake tangu kumaliza Swala. Kuzidisha nguzo kwa makusudi kama rukuu au sijda. Kusoma *tashahhud* mahali pasipokuwa pa kusoma *tashahhud*



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 200 2/1/2017 3:51:50 PM

katika vikao vya Swala. Kucheka kwa sauti iwe ni kwa makusudi au kwa kusahau. Kula na kunywa kwa makusudi. Kusema kwa makusudi maneno yasiyo na maslahi na Swala. Kupuliza kwa mdomo makusudi. Kujitapisha kwa makusudi. Kuzuka jambo linalotangua wudhu. Kujifunua utupu au sehemu tu ya utupu. Kudondoka najisi kwa anayeswali. Kutenda kitendo kwa wingi. Kuzidisha rakaa zaidi ya nne katika Swala ya rakaa nne kwa dhamira au kwa kusahau. Kusujudu kabla ya kutoa salaam. Na kuacha Sunna tatu miongoni mwa Sunna za Swala kwa kusahau kisha akakosa kusujudu sijida ya kusahau kwa tendo hilo."

Mahanbali wamesema: "Yanayobatilisha Swala ni kufanya kitendo kwa wingi. Mwenye kuswali kupatwa na najisi isiyosamehewa. Kukipa mgongo Kibla. Kuzuka jambo linalotengua wudhu. Kufunua utupu makusudi. Mwenye kuswali kuegemea kitu kwa nguvu pasipo udhuru wowote. Kurudia kwenye *tahiyyatu* ya kwanza baada ya kwishaanza kusoma kama alikuwa ni mwenye kuelewa mwenye kukumbuka. Kuongeza nguzo makusudi. Kutanguliza nguzo ya nyuma kwa makusudi. Kufanya kosa la kisomo linalogeuza maana halisi akiwa ana uwezo wa kurekebisha lakini asifanye hivyo. Kukusudia kuikata Swala au kurudia rudia fikra hiyo mara kwa mara. Kuingiwa na shaka ya kupiga takbira ya kuhirimia Swala. Kucheka na kusema kwa makusudi au kwa kusahau. Maamuma kutoa salaam kabla ya Imamu wake kwa makusudi. Kula na kunywa kwa aliyesahau au kwa asiyejua. Kujikohoza kohoza bila sababu yoyote. Kupuliza upepo iwapo kwa kufanya hivyo tamko la herufi mbili litajitokeza. Na kulia bila ya hofu ya kumcha Mungu."

Mahanafi wamesema: "Yanayobatilisha Swala ni kusema (maneno yaliyo nje ya Swala) kwa makusudi, kwa kusahau na kwa kutojua ingawa ni maneno ya kawaida ya watu. Kufanya kitendo



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 201 2/1/2017 3:51:50 PM

kwa wingi. Kugeuza kifua upande usiokuwa Kibla. Kula na kunywa. Kujikohoza kohoza bila ya sababu yoyote. Kuugulia, kunung'unika, kupiga miayo (kufunua kinywa kwa kusinzia, kuchoka au uvivu). Kulia kwa kupaza sauti. Kumrehemu aliyechemua (chafya). Kusema *Innalilahi w*akati atakaposikia habari mbaya. Kusema *Alhamdulilahi* kama amesikia habari yenye kufurahisha. Kusema: *Subhanallah* au *Lailahailallah* kwa kusikia jambo la kushangaza. Kumuonyesha maji mtu anayetayammamu (kwa kuyakosa). Kuchomoza jua wakati akiwa anaswali ya Swala ya Asubuhi. Kupindukia jua upande wa Magharibi akiwa ndani ya Swala ya Iddi. Kuanguka bendeji (au pamba) kwa kupona kidonda. Kupatwa na *hadath* kwa makusudi, lakini kama *hadath* hiyo itampata bila hiyari, basi haitabatilisha Swala yake, bali atatawadha na aunganishe Swala yake kuanzia pale alipozukiwa na *hadath* (bila ya kuanza upya)."[20]

Maimamiyya: "Swala hubatilika kwa kufanya riya. Kuwa na shaka katika nia. Kutia nia ya kukata Swala kama atatenda kitu miongoni mwa vitendo vya Swala katika hali kama hiyo. Kugeuza nia ya kuswali kutoka Swala ya mwanzo kwenda swala ya mwisho, kama atakapohama kutoka Swala ya Adhuhuri kuwa Swala ya Alasiri, ama akigeuza nia kwa kuhama kutoka Swala ya Alasiri kuwa Swala ya Adhuhuri hapana neno, kwa mfano kama alikuwa akiswali Swala ya Alasiri akidhani kuwa ameshaswali Swala ya Adhuhuri, kisha akakumbuka kumbe Adhuhuri hakuiswali, hapo anaruhusiwa kugeuza nia na kuifanya Swala hiyo kuwa Adhuhuri, na pia yajuzu kughairi Swala ya jamaa kwa kuifanya ya peke yake, lakini hairuhusiwi Swala ya peke yake kuifanya ya jamaa, lakini inaruhusiwa kwa anayeswali Swala ya faradhi peke yake kuigeuza kuwa ya Sunna ili apate kuitekeleza Swala ya faradhi kwa jamaa. Na vilevile Swala hubatilika kwa kuzidisha *takbira* ya kuhirimia Swala, kama mtu atapiga *takbira* ya kufunga Swala kisha akapiga ya pili

[20] Maelezo kutoka kitabu *Al-fiq-hu a'lal madhahibul abaa*'.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 202 2/1/2017 3:51:50 PM

basi Swala itabatilika, na atahitajika kupiga *takbira* ya tatu, na kama atapiga takbira ya nne basi Swala itabatilika na atahitajika apige ya tano, na huendelea hivyo hivyo kubatilika kila zinapokuwa katika idadi inayogawanyika, kwa sababu ya kuongeza nguzo, na husihi iwapo katika witiri.

Pia Swala hubatilika kwa kuzuka najisi isiyosamehewa ambayo hawezi kuiondoa isipokuwa kwa kufanya vitendo vingi ambavyo vitaondoa sura halisi ya Swala sahihi. Na akitayammamu kwa kukosa maji, akaingia kwenye Swala kisha akayapata hali ya kuwa yumo ndani ya Swala, hapo itabatilika tayammamu yake pamoja na Swala anayoiswali kwa sharti tu kama atakuwa ameyapata maji kabla hajarukuu rukuu ya rakaa ya kwanza, kama atayapata baada ya hapo basi ataendela na Swala yake na itakuwa imeswihi.

Pia Swala hubatilika kwa kukosa kutimiza baadhi ya masharti ya Swala kama vile nguo za kumsitiri uchi na uhalali wa mahali pa kuswalia, kuzukiwa na *hadath*, kugeuka kwa makusudi mwili wote hadi ukaelekea nyuma, au kulia au kushoto, au upande ulio kati ya sehemu hizo mbili kwa namna ambayo itamtoa katika kukielekea Kibla. Pia hubatilika kwa kusema maneno yaliyo nje ya Swala kwa makusudi, kwa kulia kwa ajili ya mambo ya dunia, kucheka, kufanya kitendo kinachoharibu sura ya Swala, kwa kula na kunywa, kuzidisha kitu kinachoharibu umbo la Swala, kula na kunywa, kwa kuzidisha kitu ndani ya Swala au kupunguza kitu kwa makusudi. Na pia hubatilika kwa kuacha nguzo tano za Swala kwa makusudi au kwa kusahau, na nguzo hizo tano ni kutia nia, takbira ya kuhirimia Swala, kusimama, kurukuu na kusujudu mara mbili katika kila rakaa moja, na ieleweke kwamba nia yawezekana kuipunguza lakini haiyumkini kuiongeza kwa hali yoyote iwayo."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 203 2/1/2017 3:51:50 PM

**KUPITA MBELE YA MTU ANAYESWALI:**

Mafakihi wameafikiana kuwa kupita mbele ya mtu anayeswali hakubatilishi Swala, kisha wamekhitilafiana kuhusu uharamu wake. Maimamiyya wamesema: "Si haramu kwa anayepita wala kwa anayeswali, bali yapendekezwa kwa anayeswali aweke mbele yake sitara kama itakuwa mbele yake hapana kizuizi kinachozuia watu kupita mbele yake, na sitara iwe ni kitu kama vile kijiti, kamba au fungu la mchanga na mfano wa hivyo, ambacho anayeswali atakiweka mbele yake kama ishara ya kuitukuza Swala, na pia kujiondolea hali ya kusongwa songwa na watu ili apate wasaa wa kumwelekea vyema Mola wake."

Maliki, Mahanafi na Mahanbali wamesema: "Ni haramu kupita mbele ya mtu anayeswali kwa vyovyote vile iwavyo, sawa awe ametengeza kizuizi au hakutengeza." Bali Mahanafi na Maliki wameongeza kwa kusema: "Ni haramu kwa mwenye kuswali kujiingiza mahali wanapopita watu kama alikuwa na uwezo wa kujitenga nao."

Mashafi wamesema: "Huwa ni haramu kupita mbele ya mtu anayeswali kama atakuwa hakuweka sitara, wala si haramu wala si makruhu kama mbele yake pana sitara."

## SWAUMU

Kufunga katika mwenzi wa Ramadhani ni nguzo miongoni mwa nguzo za dini, na kuwa kwake wajibu hakuhitaji dalili baada ya kuthibiti kuwa hutoka kwenye Uislamu mtu anayekanusha wajibu wa Swaumu, kwa sababu Swaumu ni kama Swala imethibiti kwa dharura katika dini, hivyo huwa sawa katika kujua wajibu huo, yule asiye na elimu, msomi, mkubwa na mdogo.

Na Swaumu ya mwezi wa Ramadhani ilifaradhiwa katika mwezi wa Shabani mwaka wa pili wa Hijra, nayo ni faradhi ya wajibu juu



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 204 2/1/2017 3:51:50 PM

ya kila mtu aliyebaleghe, mwenye akili timamu, wala si ruhusa mtu kuacha kufunga mwezi huo isipokuwa kwa mojawapo ya sababu zifuatazo:

**1.** Hedhi na nifasi (damu ya uzazi): Kama mwanamke atapatwa na damu ya hedhi au damu ya kuzaa huwa haiswihi Swaumu muda huo, kwa itifaki ya mafakihi wote.

**2.** Ugonjwa: Nao una maelezo yafuatayo katika y kila madhehebu:

Maimamiyya wamesema: "Haijuzu kufunga Swaumu kwa mgonjwa ikiwa kufunga huko kunamletea au kumzidishia dhiki au shida ya maumivu, au kunachelewesha kupona, kwani maradhi ni madhara, na kujidhuru ni jambo lililoharamishwa, na katazo la kufanya ibada hupelekea ibada kuharibika. Hivyo basi kama mtu atafunga ilihali yuko katika hali hiyo ya ugonjwa, Swaumu yake haitaswihi, na yatosha mtu kuwa na dhana yenye nguvu kwamba, kama atafunga atazukiwa na maradhi au maradhi aliyo nayo yatazidi. Ama udhaifu tu, hata kama ni mwingi, wenyewe si sababu ya kula katika mwezi wa Ramadhani maadamu anahimili Saumu kwa kawaida, kwani sababu ya pekee ya kula ni ugonjwa wala si udhaifu na kukonda mwili, wala si mashaka au tabu, kwani kila taklifu haikosi kuwa na ugumu na uzito wake."

Madhehebu manne yamesema: "Anapougua mtu aliyefunga na akahofia kuzidiwa na maradhi kutokana na maradhi hayo, au akahofia kuwa yatachelewa kupona, basi akipenda atafunga na akipenda atafungua wala halazimiki kula (kufungua), kwa sababu ni ruhusa tu iliyotolewa kwa mgonjwa, na si wajibu wa lazima kula katika hali kama hiyo. Ama kama dhana kubwa itamthibitishia kuwa ataangamia (kufa) au kumsababishia mojawapo ya viungo vyake kupooza, basi itakuwa ni wajibu kwake kufungua, wala haitaswihi Swaumu yake."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 205 2/1/2017 3:51:50 PM

**3.** Mwanamke mjamzito aliyekaribia kujifungua ambaye alihofia kudhurika mtoto wake wa tumboni, na mnyonyeshaji. Mafakihi wa madhehebu manne wamesema: "Anapohofia mwanamke anayenyonyesha au mwenye mimba kudhurika mtoto wake au kudhurika yeye mwenyewe, Swaumu yake huswihi kama atafunga, na anaruhusiwa kula, na kama atakula basi hulazimika kulipa baadaye kwa itifaki ya madhehebu yote. Lakini wamekhitilafiana kuhusu fidia, yaani kafara.

Mahanafi wamesema: "Si wajibu kwake kulipa fidia kabisa."

Maliki wamesema: "Ni wajibu kwa mnyonyeshaji tu, na si kwa mwenye mimba."

Mahanbali na Mashafi wamesema: "Fidia ni wajibu kulipwa na wote wawili, mwenye mimba na mnyonyeshaji, ikiwa atafungua kwa ajili ya kumhofia mwanawe tu. Ama kama atafungua kwa ajili ya kujihofia yeye mwenyewe au yeye mwenyewe na mwanawe, basi katika hali kama hiyo hulipa bila ya kulipa fidia, na fidia hiyo hutolewa kwa kila siku aliyokula, ambayo ni kibaba kimoja cha chakula, ampe chakula hicho masikini."[21]

Maimamiyya wamesema: "Mwanamke mjamzito ambaye muda wake wa kujifungua umekaribia anapojichelea nafsi yake, au akachelea mwanawe kudhurika, ni wajibu kwake kula, wala haijuzu kwake kufunga, kwa sababu ni haramu kwa mtu kujidhuru." Na wameafikiana (Maimamiyya) kuwa atalazimika kulipa na kutoa fidia ya kibaba cha chakula kama alihofia mtoto kudhurika, ama ikiwa alihofia kudhurika yeye mwenyewe, baadhi yao wamesema: "Hulipa Swaumu bila ya kutoa fidia." Na wengine wamesema: "Hulipa Swaumu na pia hulazimika kulipa fidia."

**4.** Kuwa safarini: Kwa masharti yanayozingatiwa katika sharia ya kukusuru Swala, kama tulivyotangulia kusema huko nyuma,

[21] Inakadiriwa kuwa ni Gramu 800 za ngano na mfano wake.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 206 2/1/2017 3:51:50 PM

kadiri kila madhehebu ilivyoeleza hukmu zake. Na madhehebu manne, pamoja na masharti hayo yameongeza sharti jingine, nalo ni kuanza safari yake kabla ya kuchomoza alfajiri, ambapo afike mahali pa kuanzia kukusuru Swala kabla alfajiri haijaingia. Ama kama ataanza safari yake baada ya kuingia alfajiri basi huwa ni haramu juu yake kula, lakini akila atawajibika kulipa bila ya kafara.

Mashafi wameongeza sharti jingine, nalo ni kutokuwa ni kawaida kwa msafiri huyo kusafiri, kama vile dereva, kwani kule kuwa na ada kwake ya kusafiri hakumpi haki ya kufungua kwenye safari yake hiyo, na kwao wao safari ni sababu inayomruhusu tu mtu kula na wala haimwajibishi, hivyo msafiri ambaye ametimiza masharti yote ana hiyari ya kujiamulia, akitaka atafunga au akitaka atakula. Hii ni pamoja na kujua kuwa Mahanafi wao wamesema: "Kupunguza Swala safarini ni wajibu si ruhusa."

Maimamiyya wamesema: "Yakitimia kwa msafiri masharti ya kukusuru Swala, basi haikubaliwi funga yake, na kama atafunga basi atalipa bila ya kafara, hii ni ikiwa ataanza safari kabla ya kukengeuka jua. Ama akianza baada ya kukengeuka jua au baadaye, basi atabaki na Swaumu yake, na kama atafungua itakuwa ni wajibu kwake kutoa fidia ya mtu aliyefungua makusudi. Msafiri akifika mjini kwake au mahali atapoishi siku kumi, kabla ya kukengeuka jua, na hakuwa amefanya chochote kinachotengua Swaumu, ni wajibu kwake kubaki katika funga yake, na akifungua atakuwa kama aliyefungua kwa makusudi."

**5.** Mafakihi wote wameafikiana kuwa mwenye maradhi ya kusikia kiu kali anaruhusiwa kutofunga, na kama ataweza kulipa baadaye, basi ni wajibu kwake alipe pasipokutoa fidia, kwa itifaki ya madhehebu manne. Na kwa madhehebu ya Maimami-



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 207 2/1/2017 3:51:50 PM

yya ni wajibu kwake kutoa fidia ya kibaba cha chakula. Kisha wamekhitilafiana kuhusu kusikia njaa kali, je ni katika mambo yanayomruhusu mtu kufungua kama ilivyo katika kiu?

Madhehebu manne yamesema: "Njaa kali na kiu kali vina hukmu sawa, kwani vyote hivyo humhalalishia mtu kufungua." Maimamiyya wamesema: "Haimhalalishii isipokuwa kama itamsababishia maradhi."

**6.** "Kikongwe na ajuza ambao wameishiwa nguvu, ambao wana tabu na mashaka kiasi kwamba hawawezi kufunga, hao ni ruhusa kwao kutofunga, lakini watalipa fidia katika kila siku kwa kuwalisha maskini, na hukmu hii inamhusu pia mgonjwa ambaye hatarajiwi kupona katika siku zote za mwaka mzima." Na hukmu hii wameafikiana mafakihi wa madhehebu yote isipokuwa Mahanbali, wao wamesema: "Ni Sunna kulipa fidia kwa watu hao, na wala si wajibu."

**7.** Maimamiyya wamesema: "Swaumu si wajibu kwa mtu aliyezimia kama mtu huyo atazimia katika sehemu ya mchana, isipokuwa kama amenuia kufunga kabla ya kuzimia, kisha akarudisha fahamu, hapo ni wajibu aendelee na funga yake."

## UNAPOTOWEKA UDHURU:

Unapotoweka udhuru unaohalalisha mtu kutofunga katika mchana wa mwezi wa Ramadhani, kama mgonjwa kupona, au mtoto kubaleghe, au msafiri kuwasili kwao, au mwenye damu ya hedhi kutwahirika, basi yasunniwa ajizuie kwa kuupa heshima mwezi huo wa Ramadhani, hii ni kwa Mashafi na Maimamiyya. Ama kwa Mahanafi na Mahanbali, ni wajibu kufunga. Ama Maliki wao wamesema: "Si wajibu wala si Sunna."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 208 2/1/2017 3:51:50 PM

# MASHARTI YA SWAUMU

Tumetangulia kusema kwamba Swaumu ya mwezi wa Ramadhani ni faradhi ya wajibu juu ya kila mtu baleghe mwenye akili timamu (*mukallaf*). Kwa hivyo funga hii si wajibu kwa mwenye wazimu wakati wazimu unapompanda, na lau atafunga haitoswihi. Ama mtoto mdogo ambaye hajabaleghe si wajibu kwake kufunga lakini Swaumu yake huswihi anapofunga hasa anapokuwa ni mmaizi (mtambuzi).

Na vilevile ili Swaumu iswihi, ni wajibu anayefunga awe Mwislamu, atie nia, kama ilivyo wajibu katika ibada zote. Haikubaliwi Swaumu ya asiyekuwa Mwislamu, wala hatakiwi kujizuwia na mambo yanayotengua Swaumu bila ya nia, hii ni kwa itifaki ya mafakihi wote. Na pia asiwe ni mwenye damu ya hedhi au nifasi, na asiwe mgonjwa na msafiri kulingana na maelezo yaliyotangulia.

Ama mlevi na mtu aliyepoteza fahamu, Mashafi wamesema: "Haiswihi Swaumu ya watu wawili hao kama hali ya kutojitambua itadumu katika mchana mzima. Ama wakitokewa na hiyo katika baadhi ya wakati tu, Swaumu ya wote wawili huswihi, lakini ni wajibu kwa aliyezimia kulipa, sawa kuzimia huko kumetokana na yeye mwenyewe au kumetokea bila hiyari yake. Na wala si wajibu kulipa Swaumu kwa mtu aliyelewa isipokuwa kama ulevi huo umetokana na yeye mwenyewe."

Maliki wamesema: "Haiswihi Swaumu ya watu wawili hao inapokuwa kulewa au kuzimia kumeendelea kwa muda wa kuanzia kuchomoza kwa alfajiri hadi kuzama kwa jua, kumechukua sehemu kubwa ya wakati. Ama kukichukua nusu ya mchana au chini yake, na walikuwa na fahamu zao wakati wa kutia nia, na walinuia kisha ndipo wakapotewa na fahamu au kulewa, hapo haitakuwa wajibu



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 209 2/1/2017 3:51:50 PM

kwao kulipa.” Na wakati wa kutia nia ya Swaumu kwao wao ni kuanzia Magharibi hadi Alfajiri.

Mahanafi wamesema: “Mtu aliyepotewa na fahamu yake ni sawa kabisa na mwendawazimu, hivyo kama mtu ataendelea na wazimu kwa muda wa mwezi mzima wa Ramadhani, si wajibu kwake kulipa. Na kama atashikwa na wazimu kwa muda wa nusu ya mwezi, kisha fahamu ikamrudia katika nusu iliyobaki, basi atafunga siku zilizobakia na atalipa siku zilizompita wakati wa wazimu wake.”

Mahanbali wamesema: “Kulipa Swaumu ni wajibu kwa wote, aliyezimia na aliyelewa, sawa hali hiyo iwe imetokana na wao wenyewe, au imetokana na sababu zilizo nje ya uwezo wao.”

Maimamiyya wamesema: “Mlevi pekee ndiye anayelazimika kulipa Swaumu, sawa kulewa huko kuwe kumetokana na kitendo chake mwenyewe au hakikutokana na yeye mwenyewe. Si wajibu kulipa Swaumu kwa aliyezimia hata kama kuzimia huko kulikuwa ni kwa muda mchache.”

## VYENYE KUTENGUA SWAUMU

Vyenye kutengua Swaumu ni vile vitu ambavyo ni wajibu kujizuia navyo, tangu inapoingia alfajiri mpaka magharibi, navyo ni:

**1.** Kula na kunywa kwa kukusudia, hivyo viwili hufunguza Swaumu, na vyote humlazimisha mtu kulipa, kwa itifaki ya mafakihi wa madhehebu yote. Na wamekhitalifiana kuhusu wajibu wa kutoa kafara, Maimamiyya na Mahanafi wamesema: “Ni wajibu kwake kutoa kafara.” Mashafi na Mahanbali wamesema: “Si wajibu.”



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 210 2/1/2017 3:51:51 PM

Na mtu anayekula au kunywa kwa kusahau hali ya kuwa amefunga hatalipa wala hatatoa kafara, isipokuwa kwa Maliki tu, wao wamewajibisha kulipa tu. (Ijulikane kwamba, uvutaji wa sigara huingia katika kunywa, jambo ambalo siku hizi limekuwa kawaida kwa watu).

**2.** Kujamiiana kwa makusudi, hilo huharibu Swaumu, na pia anayefanya hivyo katika mchana wa mwezi wa Ramadhani huwa ni wajibu kwake kulipa na kutoa fidia, hii ni kwa itifaki ya mafakihi wote.

Fidia ni kumwacha mtumwa huru, kama hakumpata, atafunga miezi miwili ya kufuatana, na kama hakuweza basi au atalisha masikini sitini. Utoaji wa fidia ni wa hiyari kwa Maimamiyya na Maliki, kwa maana ya kwamba mhusika atachagua yeye mwenyewe moja kati ya hayo, ima kumwacha huru mtumwa, au kufunga au kulisha chakula.

Mashafi wamesema: "Kafara hiyo ni wajibu ifuate mpangilio, kwa maana ya kuwa, kwanza atamwacha mtumwa huru, kama hana atafunga siku sitini, akishindwa ndiyo atalisha masikini sitini." Na pia hiyo ndiyo kauli ya Mahanbali na Mahanafi.

Maimamiyya wamesema: "Ni wajibu kutekeleza mambo yote hayo matatu kwa pamoja: Kumwacha mtumwa huru, kufunga siku sitini na kuwalisha masikini sitini, kama alifungua kwa njia ya haramu (iliyo haramu), kama pale anapokula chakula cha kunyang'anya au kunywa pombe, au kuzini."

Ama kujamiina kwa sababu ya kusahau hakubatilishi Swaumu kwa madhehebu ya Mahanafi, Mashafi na Maimamiyya. Na hubatilisha Swaumu kwa madhehebu ya Mahanbali na Maliki.

**3.** Kujitoa manii (kupiga punyeto, kujipuli), tendo hili huharibu Swaumu kwa itifaki ya mafakihi wa madhehebu yote, kama



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 211 2/1/2017 3:51:51 PM

litafanyika kwa hiari ya mtu mwenyewe, bali Mahanbali wamesema: "Hata anapotokwa na madhii kwa sababu ya kurudiarudia kutazama, au kwa kitu kinginecho, Swaumu yake hubatilika."

Mafakihi wa madhehebu manne wamesema: "Kujitoa manii huwajibisha kulipa Swaumu bila fidia." Maimamiyya wamesema: "Kujitoa manii huwajibisha kulipa Swaumu pamoja na kutoa fidia."

**4.** Kujitapisha kwa makusudi huharibu Swaumu na hulazimu kuilipa kwa Maimamiyya, Mashafi na Maliki. Mahanafi wamesema: "Anayejitapisha kwa makusudi hafungui, isipokuwa kama matapishi yatajaa kinywa tele." Na Imamu Ahmad bin Hanbal ana riwaya mbili, na wameafikiana kuwa kutapika kwa bila hiyari hakubatilishi Swaumu.

**5.** Kuumika, kwa madhehebu ya Mahanbali peke yao, wao wamesema: Kuumika hubatilisha Swaumu ya anayeumika na anayeumikwa.

**6.** Kupigwa bomba kwa kimiminika, hilo hubatilisha Swaumu, na huwajibisha kulipa kwa itifaki ya mafakihi. Na kundi katika madhehebu ya Imamiyya limesema: "Kupigwa bomba mbali na kuwa huwajibisha kulipa Swaumu pia huwajibisha kutoa fidia, kama hapakuwa na dharura ya kupigwa bomba."

**7.** Kumeza vumbi zito, hii ni kwa mujibu wa Maimamiyya peke yao, kwani wao wamesema: "Vumbi zito linapofika tumboni, kama unga au kinginecho, Swaumu huharibika, kwa kuwa hilo vumbi liko karibu katika kufunguza kuliko bomba, na hata kuliko (moshi) wa sigara zilizoenea siku hizi."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 212 2/1/2017 3:51:51 PM

**8.** Kupaka wanja, huharibu Swaumu kwa mujibu wa madhehebu ya Maliki peke yao, kwa sharti tu kama ataupaka mchana, na kuipata ladha ya wanja kooni mwake.

**9.** Kukata (kufuta) nia ya Swaumu. Kama mtu amenuia kufungua kisha, akaamua kujizuia asile, basi Swaumu yake itabatilika. Hii ni kwa mujibu wa Maimamiyya na Mahanbali. Lakini haibatiliki katika madhehebu yaliyobaki.

**10.** Wengi katika Maimamiyya wamesema: "Kwa hakika kuzamisha kichwa chote pamoja na mwili au kichwa peke yake ndani ya maji hubatilisha Swaumu, na humlazimu mtu mwenye kufanya hivyo kulipa na kutoa fidia." Ama madhehebu yaliyobaki yamesema: "Hilo halibatilishi Swaumu."

**11.** Maimamiyya wamesema: "Anayebaki na janaba kwa makusudi katika mwezi wa Ramadhani hadi ikaingia alfajiri Swaumu yake hubatilika, na humlazimu kulipa pamoja na kutoa fidia." Madhehebu yaliyobakia yamesema: "Swaumu huwa swahihi na halazimiki kwa chochote."

**12.** Maimamiyya wamesema: "Anayekusudia kusema uwongo kwa kumsingizia Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, akazungumza au kuandika kwamba Mwenyezi Mungu au Mtume ﷺ alisema kadhaa au aliamrisha kadhaa, na hali anajua kwamba huo ni uwongo, basi Swaumu yake hubatilika, na humlazimu kulipa na kutoa fidia." Na kundi jingine katika mafakihi wao waliongezea kwa kusema kuwa, msema uwongo huyo hulazimika kutoa fidia ya kuacha mtumwa huru, kufunga miezi miwili na kuwalisha masikini sitini.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 213 2/1/2017 3:51:51 PM

# VIGAWANYO VYA SWAUMU

Mafakihi wamezigawa Swaumu katika vigawanyo vinne: Swaumu ya wajibu, Swaumu ya Sunna, Swaumu ya haramu, na Swaumu iliyo makruhu.

## SWAUMU YA WAJIBU:

Huingia katika Swaumu ya wajibu: Swaumu ya mwezi wa Ramadhani, na Swaumu ya kulipa mwezi huo. Na Swaumu ya fidia, na Swaumu ya nadhiri, hizi ni kwa itifaki ya madhehebu yote. Na maimamu wawili walizidisha vigawanyo vingine viwili, kimoja katika mlango wa Hijja na kingine katika mlango wa Itikafu. Na bila shaka tumeeleza kwa mapana huko nyuma kuhusu funga ya mwezi wa Ramadhani, masharti yake na mambo ambayo huiharibu, na katika sehemu hii tutazungumzia Swaumu ya kulipa mwezi wa Ramadhani na fidia ya funga yake, fidia ambayo ni wajibu kulipwa na mtu aliyeacha kufunga ndani ya mwezi huo. Ama kuhusu vigawanyo vingine, hivyo tutavielezea mahali pake maalum panapohusika.

## KULIPA SWAUMU YA MWEZI WA RAMADHANI:

Ndani yake kuna masuala yafuatayo:

**1.** Wameafikiana mafakihi wote kuwa mtu anayewajibika kulipa Swaumu iliyompita katika mwezi wa Ramadhani ni wajibu ailipe katika mwaka huo huo ambao alipitwa na Swaumu hiyo, yaani siku zilizopo baina ya Ramadhani iliyompita na Ramadhani ijayo, na ana ruhusa ya kuchagua siku apendazo ili kuweza kulipa Ramadhan ndani ya siku hizo, isipokuwa siku ambazo zimeharamishwa ndani yake kufunga, nazo tutazitaja baadaye. Na ni wajibu kwake kufanya haraka kulipa zinapobakia siku



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 214 2/1/2017 3:51:51 PM

sawa na zile zilizopita kabla Ramadhani nyingine kuingia.

**2.** Mtu atakayepata uwezo wa kulipa Swaumu ya mwezi wa Ramadhani ndani ya mwaka husika, lakini yeye akapuuza kwa uzembe wake tu hadi mwezi wa Ramadhani mwingine ukaingia, ni wajibu kwake kufunga mwezi wa Ramadhani uliopo kisha alipe Swaumu za mwezi uliopita na kutoa kibaba cha chakula kwa kila siku aliyokosa kufunga, hii ni kwa itifaki ya madhehebu yote isipokuwa Mahanafi, wao wamesema: "Atalipa bila ya kutoa fidia."

Na anaposhindwa kulipa kwa sababu ya maradhi yaliyoendelea tangu Ramadhani ya mwanzo hadi ikaingia Ramadhani ya pili, hana wajibu wa kulipa wala wa kutoa fidia, hii ni kwa madhehebu manne. Ama Maimamiyya wao wamesema: "Wajibu wa kulipa humwondoka, na huwajibika kutoa kibaba kwa kila siku iliyompita, yaani alishe masikini."

**3.** Kama alikuwa anao uwezo wa kulipa baada ya Ramadhani kumalizika, lakini akachelewa kwa nia ya kuwa atazilipa siku zilizo karibu na mwezi wa Ramadhani inayofuata, kwa lengo la kuwa aziunganishe siku zake za kulipa na Swaumu ya mwezi huo, kisha ukamzukia udhuru wa kisheria ambao utamzuia kulipa mpaka Ramadhani nyingine ikaingia, kama hali ilikuwa hivyo basi itamlazimu kulipa tu wala hatolazimika kutoa fidia.

**4.** Mtu anayekula katika mwezi wa Ramadhani kwa udhuru, kisha akamakinika kulipa lakini asilipe mpaka akafariki, Maimamiyya weamesema: "Ni wajibu kwa mwanawe mkubwa kumlipia Swaumu hiyo."

Mahanafi, Mashafi na Mahanbali wamesema: "Humtolea sadaka kwa kila siku moja, ya kibaba cha chakula."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 215 2/1/2017 3:51:51 PM

Maliki wamesema: "Walii wake humtolea sadaka hiyo kama alimuusia amtolee, na kama hapana usia hana wajibu wa kufanya hivyo."

**5.** Mtu aliyefunga Swaumu ya kulipa mwezi wa Ramadhani na wakati ni mpana, ni ruhusa kwake kuivunja Swaumu yake, iwe ni kabla au baada ya jua kukengeuka. Na kwa mujibu wa madhehebu manne hatakiwi kulipa chochote.

Maimamiyya wamesema: "Hujuzu kwake kufungua kabla ya kukengeuka jua, wala haijuzu kufungua baada ya hapo, kwa kuwa wajibu wake huwa umethibiti juu yake kwa kule kupita sehemu kubwa ya mchana, na tayari mahali pa kutilia upya nia pamepita, lakini kama atakhalifu akafungua baada ya hapo ni wajibu kwake kutoa fidia kwa kuwalisha masikini kumi, kama atashindwa kulisha maskini basi ni wajibu kwake kufunga siku tatu."

## SWAUMU ZA FIDIA:

Swaumu za fidia ziko za aina nyingi, miongoni mwazo ni Swaumu za kuua bila kukusudia. Swaumu ya fidia ya yamini na nadhiri, na Swaumu ya fidia ya *dhihar* (kumwambia mkeo mgongo wako ni kama wa mama yangu). Na aina zote hizi za Swaumu zina hukmu zake ambazo tutazifafanua katika milango yake. Na hapa tutazungumzia yanayohusiana na hukmu ya mtu anayetoa fidia kutokana na kutokufunga kwake katika mwezi wa Ramadhani.

Mashafi, Maliki na Mahanafi wamesema: "Mtu ambaye ana Swaumu za miezi miwili ambazo ni fidia ya kufungua katika mwezi wa Ramadhani, si ruhusa kwake kuacha kufunga hata siku moja ndani ya miezi miwili hiyo, kwa maana akifanya hivyo ule mfululizo utakatika, na kama atafungua kwa sababu ya udhuru au bila ya udhuru, itakuwa ni wajibu kwake basi kuanza upya Swaumu za miezi miwili kamili."

Mahanbali wamesema: “Kufungua kwa udhuru wa kisheria hakukatizi mfululizo.”

Maimamiyya wamesema: “Hutosha katika kupatikana uhakika wa mfululizo, kule kufunga mwezi wa kwanza wote kwa ukamilifu wake, na siku moja katika mwezi wa pili, anapofanya hivyo basi hujuzu kwake kufungua, kisha akafunga ili kujengea (kuunganishia) pale palipotangulia. Na kama atafungua mwezi wa kwanza pasi na udhuru ni wajibu kwake kuanza upya. Ama kama atafungua kwa udhuru wa kisheria kama ugonjwa au hedhi basi mfululizo hautakatika, bali atangojea udhuru umalizike kisha akamilishe Swaumu.”

Maimamiyya wameendelea kusema: “Mtu anayeshindwa kufunga miezi miwili, kuacha mtumwa huru na kuwalisha maskini sitini, atachagua kati ya kufunga siku kumi na nane (18) au atoe sadaka kwa kiasi anachomudu, na kama ataelemewa na hayo yote, basi atafanya analoliweza, kama ni kutoa sadaka au kufunga. Na pia, kama atashindwa kutekeleza moja ya hayo mawili basi atamwomba msamaha Mwenyezi Mungu (s.w.t.).”

Mashafi, Maliki na Mahanafi wamesema: “Kama mtu atashindwa kutekeleza chochote kati ya hizo fidia, itabaki dhima juu yake hadi atakapopata uwezo ndipo atekeleze.” Na hivi ndivyo zinavyohukumu kanuni za kisharia.

Mahanbali wamesema: “Kama atashindwa wajibu wa kutoa fidia utaporomoka kutoka kwake, na hata kama atapata uwezo baadaye haitakuwa wajibu kwake.”

Wameafikiana kuwa hiyo fidia hujirudia kadiri zinavyojirudia sababu zinazowajibisha kutoa fidia husika, iwapo zimetendwa katika siku mbili au zaidi. Hivyo atakayekula au kunywa katika siku mbili, ni wajibu kwake kutoa fidia mbili. Ama akila, au kunywa au



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 217 2/1/2017 3:51:51 PM

kumwingilia mwanamke mara nyingi katika siku moja, Mahanafi, Maliki na Mashafi wamesema:: "Hapo si wajibu kwake kulipa fidia sawa na idadi ya mara alizotenda, kwa kosa lolote lile."

Mahanbali wamesema: "Zinapotokea ndani ya siku moja sababu kadhaa zinazowajibisha fidia, kama atakuwa ameshatoa fidia kwa kosa la kwanza, yaani ikawa alifanya kosa la pili baada ya kutoa fidia ya kosa la kwanza, hapo ni wajibu kwake kulipa fidia ya pili, lakini kama hadi anatenda kosa la pili alikuwa bado hajatoa fidia, hapo atawajibika kutoa fidia moja kwa ajili ya makosa yote."

Maimamiyya wamesema: "Kama mtu atarudia udia kujamiiana katika mchana mmoja, basi atatoa kafara sawa na mara alizofanya kitendo hicho, ama kurudiarudia kula au kunywa kwenyewe hakumlazimu isipokuwa kafara moja tu."

## SWAUMU ZILIZO HARAMU:

Mafakihi wote wameafikiana kuwa kufunga katika siku ya Idd ya al-Fitr na al-Udhuha ni haramu, isipokuwa Mahanafi, wao wamesema: "Kufunga katika siku mbili za Idd ya al-Fitri na al-Udhuha ni makruhu iliyokatazwa." Na makruhu iliyokatazwa katika istilahi ya madhehebu yao, ni kitendo kinachokaribia sana kuwa haramu.

Maimamiyya wamesema: "Haijuzu kufunga Swaumu katika siku za *Tashriq*, kwa mtu aliye Mina, nazo ni tarehe 11,12 na 13 katika mwezi wa Dhulhijja."

Mashafi wamesema: "Si halali kufunga Swaumu katika siku za *Tashriq,* kwa mtu aliye katika Hijja au aliye popote pale."

Mahanbali wamesema: "Ni haramu kufunga katika siku za *Tashriq*, kwa mtu asiyekuwa Hijja, lakini kwa aliye katika Hijja si haramu."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 218 2/1/2017 3:51:51 PM

Mahanafi wamesema: "Kufunga katika siku hizo ni makruhu iliyokatazwa."

Maliki wamesema: "Ni haramu kufunga katika siku ya mwezi 11 na 12 ya Dhulhijja kwa asiyekuwa Hijja, na si haramu kwa aliye katika Hijja."

Na wameafikiana kuwa, si ruhusa mwanamke kufunga Swaumu ya Sunna bila ya idhini ya mumewe, kama Swaumu yake hiyo itagongana na haki miongoni mwa haki za mume, isipokuwa Mahanafi, wao wamesema: "Swaumu ya mwanamke anayofunga bila idhini ya mumewe ni makruhu, na si haramu."

## SIKU YA SHAKA:

Wameafikiana mafakihi wote kuwa mtu anayefungua katika siku ya shaka kisha ikambainikia kuwa siku hiyo ni mwezi wa Ramadhani, ni wajibu kwake kujizuilia na kulipa baadaye. Kisha wamekhitilafiana kuhusu je, kama alifunga katika siku ya shaka na ikabainika kuwa siku hiyo ilikuwa ni mwezi wa Ramadhani, je Swaumu hiyo itatosheleza wala si wajibu kwake kulipa au la?

Mashafi wamesema: "Swaumu hiyo haitoshelezi, na ni wajibu kwake kulipa." Na hii pia ndiyo kauli ya Maliki na Mahanbali.

Mahanafi wamesema: "Hutosheleza na hapana haja ya kulipa."

Na wengi katika Maimamiyya wamesema: "Si wajibu kwake kulipa, isipokuwa kama alifunga kwa nia ya Ramadhani, hapo ndipo huwa wajibu kwake kulipa."

## SWAUMU ZA SUNNA:

Inapendekezwa kufunga katika siku za mwaka mzima, isipokuwa katika siku ambazo sharia imekataza watu wasifunge humo. Lakini



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 219 2/1/2017 3:51:51 PM

Swaumu hizo za Sunna zimekokotezwa katika siku zake maalum, miongoni mwake ni kufunga siku tatu katika kila mwezi, na ni bora ziwe ni zile siku nyeupe nazo ni tarehe 13,14 na 15 katika mwezi wa Kiarabu. Na miongoni mwake ni Swaumu ya siku ya Arafah, nayo ni tarehe tisa (9) ya mwezi wa Dhulhijja. Na miongoni mwake ni Swaumu ya mwezi wa Rajabu na Shaaban, na kufunga kila siku ya Jumatatu na Alhamisi ya kila mwezi. Na siku nyinginezo zilizotajwa katika vitabu vikubwa vya Fikihi. Na kusunniwa kwa Swaumu hizo kuna uwafikiano kwa mafakihi wote.

### SWAUMU ZILIZO MAKRUHU:

Imeandikwa katika kitabu *Al-fiqhu Alal Madhahibil Arbaa* kuwa, miongoni mwa Swaumu zilizo makruhu ni kuipwekesha siku ya Ijumaa kwa kufunga. Na pia kuipwekesha siku ya Jumamosi, na siku ya Nairuz kwa wasiokuwa Mashafi. Na kufunga kabla ya kuandama mwezi wa Ramadhani kwa siku moja au siku mbili, si zaidi ya hapo.

Na imeandikwa katika kitabu cha Fikihi ya Maimamiyya kwamba, Swaumu ya mgeni bila idhini ya mwenyeji wake ni makruhu, na pia Swaumu ya mtoto pasipo idhini ya mzazi wake, na Swaumu ya shaka katika mwezi wa Dhulhijja anapohofia mtu kuwa huenda ikawa siku hiyo ni Idd.

## KUTHIBITI MWANDAMO WA MWEZI

Waislamu wote wamekongamana kuwa yeyote anayeuona mwezi peke yake humlazimu kutenda kwa mujibu wa elimu na ujuzi wake bila ya kuwepo tofauti yoyote kati ya mwezi mwandamo wa Ramadhani na wa Shawwal (mfungo mosi). Kwa hivyo basi atakayeuona wa kwanza yeye peke yake, ni wajibu kwake kufunga hata kama watu wote watakuwa hawakufunga.[22] Na atakayeuona wa pili (mfun-

[22] Lakini Hanafiyya wamesema: "Lau mtu ataapa mbele ya kadhi, naye kadhi akapinga



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 220 2/1/2017 3:51:51 PM

go mosi) yeye peke yake ni wajibu kwake kufungua hata kama watu wote wa dunia nzima hawatafungua, bila ya kuwepo tofauti yoyote kati ya kuwa aliyeuona ni mwadilifu au si mwadilifu, alikuwa ni mwanamume au ni mwanamke. Kisha madhehebu yametofautiana katika masuala yanayofuata:

**1.** Mahanafi, Maliki na Mahanbali wamesema: "Ikithibiti kuonekana kwa mwezi katika mji wowote ule, ni wajibu kwa watu wa miji mingine kufunga, bila kujali kuwa mji huo uko karibu au mbali na mji ulioonekana mwezi, wala matlai ya mwezi hayazingatiwi.

Maimamiyya na Mashafi wamesema: "Watu wa mji fulani wanapouona mwezi na ikawa mji mwingine wa pili hawakuuona, kama miji hiyo itakaribiana (itakuwa ni jirani) katika matlai basi hukmu ya miji hiyo miwili huwa moja, na kama matlai (mawio) yanatofautiana basi kila mji au nchi itafuata hukmu yake."

**2.** Unapoonekana mwezi mchana kabla ya kukengeuka jua au baada yake katika siku ya thelathini ya mwezi wa Shaabani, je mchana huo utakuwa ni mwisho wa Shaaban ambapo huwa si wajibu kufunga siku hiyo, au utakuwa ni mwanzo wa Ramadhani ambapo ni wajibu kufunga? Na pia unapoonekana katika wakati wa mchana wa siku ya thelathini ya mwezi wa Ramadhani je siku hiyo itakuwa ni mwezi wa Ramadhani au Shawwal? Na kwa maneno mengine, je hiyo siku iliyoonekana mwezi itahesabiwa ni katika mwezi uliopita au unaofuata?

Maimamiyya, Mashafi, Maliki na Mahanafi wamesema: "Siku hiyo huwa ni katika mwezi uliopita si huo unaofuata,

---

ushuhuda wake basi itampasa mtu huyo kukidhi bila ya kafara." (*Al-fiqhu alal Madhahibil Arbaa*).



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 221 2/1/2017 3:51:51 PM

na ni wajibu kwake kufunga siku ya pili yake kama siku hiyo ilikuwa ni mwisho wa Shaaban, na ni wajibu kwake kufungua mnamo siku ya pili yake kama ilikuwa ni siku ya mwisho wa Ramadhani.

Wameafikiana kuwa kuandama kwa mwezi huthibiti kwa kuuona, kutokana na kauli ya Mtume ﷺ: "Fungeni kwa kuuona mwezi, na fungueni kwa kuona mwezi." Kisha wakatofautiana kuhusu kukosa kuuona mwezi:

Maimamiyya wamesema: "Huthibiti kuandama kwa miezi yote miwili wa Ramadhani na Shawwal kwa *tawatur* (kuenea habari) na pia kwa ushahidi wa waadilifu wawili, bila ya kuwepo na tofauti yoyote kati ya kuwa kulikuwa na mawingu au kulikuwa ni kusafi. Wala bila ya kuwepo na tofauti yoyote kati ya kuwa hao mashahidi wawili wanatoka mji mmoja au miji mbalimbali iliyo jirani, kwa sharti kwamba pasitokee kupingana katika ushahidi wao kuuelezea mwezi. Ushahidi wa wanawake haukubaliwi, pia wa watoto na wa mtu fasiki na wa mtu asiyejulikana hali yake.

Mahanafi wametofautisha kati ya mwezi mwandamo wa Ramadhani na wa Shawwal (mfungo mosi), wamesema: "Mwezi mwandamo wa Ramadhani huthibitishwa kuandama kwake kwa ushahidi wa mwanamume mmoja, na mwanamke mmoja, kwa sharti wawe ni Waislamu, wawe na akili timamu tena wawe ni waadilifu. Ama mwezi wa Shawwal huo hauthibiti isipokuwa kwa ushahidi wa wanaume wawili au mwanamume mmoja na wanawake wawili, na hii ni kama huko juu mbinguni kulikuwa na kizuizi chenye kuzuia kuonekana kwa mwezi waziwazi. Ama kama kutakuwa ni kusafi hakuna mawingu basi hauthibiti isipokuwa kwa ushahidi wa kundi kubwa la watu ambao kutokana na habari zao itapatikana yakini, bila ya kutofautisha kati ya mwezi mwandamo wa Ramadhani na Shawwal."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 222 2/1/2017 3:51:51 PM

Mashafi wamesema: "Huthibiti kuonekana kila mwezi mwandamo wa Ramadhani na Shawwal kwa ushuhuda wa mwadilifu mmoja, kwa sharti mtu huyo awe ni mwislamu, mwenye akili timamu na awe ni mwadilifu, na hakuna tofauti katika hili, sawa mbingu iwe ina mawingu au ni safi."

Maliki wamesema: "Haithibiti kuonekana mwezi isipokuwa kwa ushahidi wa watu wawili walio waadilifu, bila ya kutofautisha kati ya mwandamo wa Ramadhani au Shawwal, wala kati ya kuwa kuna mawingu au ni kusafi."

Mahanbali wamesema: "Mwezi wa Ramadhani huthibiti kuandama kwake kwa ushahidi wa mtu mwadilifu, sawa awe ni mwanamume au ni mwanamke, ama kuandama kwa mwezi wa Shawwal hakuthibiti isipokuwa kwa ushuhuda wa wanaume wawili waadilifu.

**1.** Kama hakuna mtu aliyedai kuonekana kwa mwezi wa Ramadhani basi mwezi wa Shaaban utakamilishwa siku thelathini na itakuwa ni wajibu watu kufunga katika siku inayofuata baada ya thelathini. Hii ni kwa itifaki ya wanazuoni wote, isipokuwa Mahanafi, kwani wao wamesema: "Ni wajibu kufunga baada ya mwezi ishirini na tisa (29) ya Shaaban, si baada ya siku thelathini." Na hii ni kwa mnasaba wa kuandama mwezi wa Ramadhani, ama kuhusu mwezi wa Shawwal, Mahanafi na Maliki wamesema: "Kama mbingu imetanda mawingu basi ni wajibu kufunga kwa kukamilisha siku thelathini, na ni wajibu baada yake kufungua, na kama mbingu ni safi basi ni wajibu kufunga siku inayofuatia baada ya thelathini, na hukanushwa ushahidi wa watu waliothibitisha kuandama kwa mwezi mwanzo wa Ramadhani hata kama idadi yao ni kubwa kiasi gani."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 223 2/1/2017 3:51:51 PM

Mashafi wamesema: "Ni wajibu kufunga baada ya kukamilika siku thelathini, hata kama kuandama kwa mwezi wa Ramadhani kumethibiti kwa ushahidi wa mtu mmoja, pasi na kutofautiana kati ya anga lenye mawingu au lililo safi."

Mahanbali wamesema: "Kama itathibiti kuandama kwa mwezi wa Ramadhani kupitia kwa waadilifu wawili basi ni wajibu kufungua baada ya kukamilika siku thelathini. Na kama ulikuwa umethibiti kuandama kwake kwa ushahidi wa mwadilifu mmoja basi itakuwa ni wajibu kufunga siku thelathini na moja."

Maimamiyya wamesema: "Huthibiti kuandama kwa miezi, wa Ramadhani na Shawwal, kwa kukamilika siku thelathini, sawa anga liwe safi au lina mawingu, maadamu kuanza kwake kulithibiti kwa njia ya kisharia iliyo sahihi.

## KUANDAMA KWA MWEZI KUPITIA WANAJIMU

Katika mwaka huu (1960) serikali za Pakistani na Tunisia zilipitisha kuwa mwandamo wa mwezi utegemee kauli za wanajimu ili kuondoa fujo na zogo linalojitokeza,[23] na ili kuondoa yale matatizo na usumbufu wanaoupata watu kwa ajili ya kutojua kwao ni lini siku ya Idd. Kwani wakati mwingine hufikwa na Iddi ghafla bila ya kujiandaa, na wakati mwingine huwa wamejiandaa lakini ikaja siku nyingine isiyokuwa ile walioitarajia.

Kwa kweli tendo la nchi mbili hizi (Pakistani na Tunisia) lilizusha zogo kubwa mabarazani na hata kwenye vilabu kwa majibizano makali kutokana na serikali hizo kupitisha uamuzi huo, wengine wakiunga mkono na wengine wakiupinga.

[23] Katika mwaka wa 1939 katika nchi ya Misri siku ya Idd ya al-Udhuha ilikuwa siku ya Jumatatu, Saudia ikawa siku ya Jumanne, na Bombay ikawa siku ya Jumatano.

Anayetetea azimio hilo lililopitishwa alisema: "Katika dini hakuna hoja inayokanusha watu kutegemea kauli za wataalamu wa elimu ya unajimu (*Astrologers*), bali katika Qur'ani tukufu imo Aya inayotufahamisha kwamba jambo hilo lafaa, nayo ni hii: "**Na ameziweka alama nyingine. Na kwa nyota (pia) wao wanafuata njia. (*An Nahl:16*).** Ikiwa inatilia mkazo na kuunga mkono jambo hilo."

Wanaopinga wakasema: "Azimio hilo lililopitishwa na serikali hizo linapingana na Hadith tukufu ya Mtume ﷺ inayosema: "Fungeni kwa kuuona mwezi, na fungueni kwa kuuona mwezi." Ambapo ilivyofahamika kutokana na Hadith hii ni kuwa tufunge kwa kuuona, na kuuona kwa macho ni tendeo lililozoeleka tangu zama za Mtume ﷺ. Ama kwa kutumia darubini (mangala) na kufuatia kuuona kwa kuhesabu nyota na manazili, huko kuko mbali sana na tamko la Hadith."

Kwa hakika kabisa pande zote mbili hazikutoa hoja yenye nguvu. Ama kuhusu kutumia nyota, makusudio yake ni kujua njia na mapitio ya miji, haina maana kujua siku ya kuandama kwa mwezi. Ama Hadith inayoelezea kuuona mwezi haikutengana na ujuzi uliosalimika usio na makosa, kwani kuona ni njia ya kupata elimu (yaani kuuona hupelekea kwenye elimu), lakini sio lengo hasa, kama hali ilivyo katika njia zote ambazo humfikisha mtu palipo na uhakika wa kitu. Lakini sisi tunasema: "Kwa hakika maneno ya wanajimu hayafaidishi kwa mkato wala kuondoa shaka ya mtu kama vile shaka inavyoondolewa kwa kuona, kwa sababu maneno yao (wanajimu) yako katika kukurubia uhakika lakini si uhakika wenyewe, na hili lathibitika kwa kutofautiana na kupingana kwa maneno yao kuhusu usiku ambao huandama ndani yake mwezi, na saa ya kuandama kwake na katika muda wa kuendelea kwake."

Lakini siku wanajimu watakapofikia katika hali ya ujuzi wa hali ya juu utakaofikia kutosheleza kielimu kwa kiasi cha kuwafikiana



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 225 2/1/2017 3:51:51 PM

maneno yao, na ukweli wa maneno yao utakapokaririka mara baada ya mara, hadi maneno yao yakawa ya kuaminika sawa sawa kama vile siku ya wiki, na kujulikana kwamba kesho ni juumamosi au ni jumapili, katika hali kama hiyo ndipo itakapowezekana kuyategemea maneno yao, bali hii itategemea na fikra na imani ya mtu atakayeyapata maneno yao, na papo hapo itampasa atupilie mbali kila linalowakhalifu.[24]

# ZAKA

Zaka ziko za aina mbili: Zaka za mali, na Zaka za mwili. Na mafakihi wameungana pamoja kuwa, Zaka haiswihi bila ya kutiliwa nia. Ama masharti ya kuwa kwake wajibu ni kama yafuatayo:

## MASHARTI YA ZAKA YA MALI:

Zaka ya mali ina masharti yake:

**1.** Mahanafi na Maimamiyya wamesema: "Kuwa na akili timamu na kubaleghe ni sharti katika wajibu wa kutoa Zaka, si wajibu kutoa Zaka kutoka katika mali ya mwendawazimu na mtoto mdogo."[25] Maliki, Mahanbali na Mashafi wamesema: "Akili na kubaleghe si sharti katika wajibu wa kutoa Zaka, kwa hivyo ni wajibu kutoa Zaka katika mali ya mwendawazimu na mtoto mdogo, na ni juu ya walii (anayemsimamia) kuitolea Zaka mali hiyo."

**2.** Mahanafi, Mashafi na Mahanbali wamesema: "Si wajibu kutoa Zaka katika mali ya mtu asiyekuwa mwislamu, (Taz. *Al-Fiqhu*

[24] Kwa maelezo zaidi yanayohusu utafiti kuhusu jambo hili rejea Juz. ya kwanza ya kitabu chetu *'Fiqhul Imam Jaafaris Sadiq'* katika kifungu cha kuthubutu kuandama mwezi, mwishoni mwa mlango wa Swaumu.

[25] Isipokuwa kwa dhehebu la Hanafiyya, kuwa na akili na kubaleghe hakuzingatiwi katika kupasa kutoa Zaka ya mimea na matunda.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 226 2/1/2017 3:51:51 PM

*alal madhahibil arbaa*). Maimamiyya na Maliki wamesema:

"Ni wajibu kutoa Zaka kutoka katika mali ya asiyekuwa mwislamu, kama ilivyo wajibu kutoa katika mali ya mwislamu bila ya tofauti yoyote."

**3.** Umiliki kamili ni sharti katika wajibu wa kutoa Zaka. Na kila madhehebu imerefusha maneno yake kuhusiana na suala hili la umiliki kamili, na kuelezea kiasi cha umiliki huo. Na makutano ya kauli za madhehebu ni kuwa, mwenye kumiliki mali inayofikia kiwango cha kutolewa Zaka ni sharti awe ana uwezo kamili juu ya mali hiyo, kwa namna ambayo mali hiyo iwe iko chini ya uwezo wake, ambapo anaweza kuitumia vyovyote atakavyo. Wala si wajibu kutoa Zaka katika mali iliyopotea, au katika mali ya kupora, hata kama imebaki kwenye miliki yake. Ama kuhusu deni, kama ni yeye ndiye anayedai basi si wajibu kwake kutoa Zaka ya deni hilo isipokuwa baada ya kulipwa, kama vile mahari ya mke ambayo bado yako kwenye dhima ya mume, kwani deni halimilikiwi isipokuwa kwa kukabidhiwa mdai, na kama ni yeye ndiye mdaiwa, basi hukmu yake iko katika masharti yafuatayo:

**4.** Kupitiwa na hauli mbili (miaka mwili) ya mwezi wa kuandama, hii ni kwa mali isiyokuwa ya punje, matunda na madini, maelezo yake yatafuata.

**5.** Kufikia kiwango (kinachopasa kutolewa Zaka ndani yake). Na kiasi chake kinatofautiana kwa kutofautiana aina ya mali inayopasa kutolewea Zaka. Na maelezo yake yatafuata.

**6.** Mtu mwenye deni, na akawa na mali inayofikia kiwango cha kutolewa Zaka ndani yake, je ni wajibu kwake kutoa Zaka au si wajibu, na kwa neno jingine, je deni huzuia kutoa Zaka?

Maimamiyya na Mashafi wamesema: "Si sharti kwamba mali isiwe na deni ndio iwe wajibu kuitolea Zaka, hata mwenye kudaiwa ni wajibu kwake kutoa Zaka, hata kama deni hilo litajumuisha kiwango chote cha Zaka." Bali Maimamiyya wameongeza kuwa: "Kama mtu atakopa kiwango cha mali kinachopasa kutolewa Zaka, na mali hiyo ikabaki kwa mkopaji mwaka mzima, ni wajibu kwa mkopaji kutoa Zaka."

Mahanbali wamesema: "Deni huzuia wajibu wa kutoa Zaka, mtu kama ana deni na akawa ana mali basi itamlazimu alipe deni lake kwanza, kisha kama katika mali yake itabaki kiasi cha kiwango kinachotolewa Zaka ndipo ataitolea Zaka, na kama haifiki basi si wajibu kwake kutoa."

Maliki wamesema: "Deni huzuia wajibu wa kutoa Zaka ya dhahabu na fedha, lakini halizuii wajibu wa kutoa Zaka ya nafaka, wanyama na madini. Hivyo yule mwenye deni ikiwa ana dhahabu na fedha zilizotimia kiwango cha kutolewa Zaka, ni wajibu kwake kulipa deni lake, na si wajibu kwake kutoa Zaka. Ama kama ana deni, na ana kiwango cha mali nyingine isiyo dhahabu na fedha, ambayo inatakiwa kutolewa Zaka, ni wajibu kwake kutoa Zaka."

Mahanafi wamesema: "Kama deni ni haki ya Mwenyezi Mungu iliyo kwenye dhima yake, wala hakuna anayeidai katika waja wa Mungu, kama vile Hijja na fidia, basi deni hili halitazuia wajibu wa kutoa Zaka, na kama deni hilo ni la waja, au ni la Mungu lakini bado anadaiwa na watu deni hili la Mungu, kama pale atakapokuwa anadaiwa na Imamu Zaka iliyopita ambayo hakuitoa, basi deni hilo litazuia wajibu wa kutoa Zaka katika aina za mali inayopasa kutolewa Zaka, isipokuwa Zaka ya chakula (mimea) na matunda."

Kisha wote wameafikiana kuwa si wajibu kutoa Zaka katika mapambo na johari, wala katika vyombo vya nyumbani na mnyama

anayemtumia kwa kumpanda, na silaha, na vinginevyo miongoni mwa vitu anavyovihitajia katika matumizi ikiwemo vitabu na ala nyinginezo.

Maimamiyya wamesema tena: "Si wajibu kutoa Zaka katika vinoo vya dhahabu na fedha." Maelezo kamili juu ya vifaa hivyo yatakuja baadaye.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 229 2/1/2017 3:51:52 PM

# MALI AMBAZO NI WAJIBU KUZITOLEA ZAKA

Qur'ani tukufu kwa hakika kabisa imeyazingatia makundi mawili ya watu, mafukara na maskini; kuwa ni washirika halisi wa matajiri katika mali zao. Bila ya shaka Aya ya 19 katika *Suratu Dhariyat* imetamka hilo:

وَفِيٓ أَمۡوَٰلِهِمۡ حَقّٞ لِّلسَّآئِلِ وَٱلۡمَحۡرُومِ ١٩

**"Na katika mali zao mna haki ya kupewa masikini aombaye na ajizuiaye kuomba." (51:19).**

Aya hii ukweli ni kwamba haikutofautisha kati ya mali ya ukulima, ya uzalishaji wala ya biashara, na kwa ajili hiyo ndipo mafakihi wa madhehebu yote wakaipasisha Zaka katika wanyama, nafaka na matunda, kadhalika katika pesa na madini. Kisha wamekhitilafiana katika kuainisha baadhi ya aina za vitu hivyo, na kiwango cha baadhi ya aina, na katika kuainisha viwango vya mafungu ya mafukara katika aina ya tatu.

Maimamiyya pia wamewajibisha Khumsi (fungu la tano) ambayo ni 20 kwa mia katika faida iliyozalishwa na biashara. Na mafakihi wa madhehebu manne wamesema: "Kiwango kinachotolewa kutoka katika mali ya biashara ni robo ya kumi – yaani mbili na nusu katika mia."

Aidha katika madini, Mahanafi, Maimamiyya na Mahanbali wamewajibisha ndani yake kutolewa Khums, na wasiokuwa wao wamewajibisha robo ya kumi, na yafuatayo ni maelezo ya yale waliyoafikiana na waliyohitilafiana ndani yake:

## ZAKA YA WANYAMA:

Mafakihi wote wameafikiana kuwa Zaka ni wajibu kutolewa kutoka katika aina tatu za wanyama: Ngamia, ng'ombe, na katika ng'ombe pia wanahusika nyati; na mbuzi wakiwemo kondoo. Na pia wameafikiana katika wajibu wa kutoa Zaka kutoka katika mnyama kama vile farasi, nyumbu na punda isipokuwa kama ni katika mali ya biashara. Nao Mahanafi wamewajibisha Zaka kwa farasi peke yake (kati ya wanyama hao) kama watakuwa katika jumuiko la wake na waume.

## MASHARTI YA ZAKA KATIKA WANYAMA:

Katika Zaka ya wanyama kuna masharti manne:

1. **Niswab:** Ni kufikia kiwango, nacho ni kama ifuatavyo katika ngamia: Wanapofikia watano (5), ndani yake hutolewa mbuzi mmoja. Wakifikia kumi (10), mbuzi wawili. Wakifikia kumi na tano (15), mbuzi watatu. Wakifikia ishirini (20), mbuzi wanne. Hii ni kwa itifaki ya madhehebu yote. Ama wanapofikia ishirini na tano (25), Maimamiyya wamesema: "Hutolewa mbuzi watano." Na mafakihi wa madhehebu manne wamesema: "Hutolewa *Binti Makhadh*, naye ni ngamia aliyefikia umri wa miaka miwili." Maimamiyya wamewajibisha kutolewa *Binti Makhadh* iwapo ngamia watafikia ishirini na sita (26). Kama ngamia watafikia kiwango hicho, basi wote watakuwa *nisab* yake ni moja tu.

Na wanapofikia thelathini na sita (36) hutolewa *Bint Labun*, kwa itifaki ya wote, na *Bint Labun* ni ngamia aliyeingia katika mwaka wa tatu. Na wanapofikia arobaini na sita (46) hutolewa *Huqah* kwa itifaki yao wote. Na *Huqah* ni ngamia aliyeingia katika mwaka wa nne. Na wanapofikia sitini na moja (61) hutolewa *Jadiah* kwa itifaki



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 231 2/1/2017 3:51:52 PM

ya wote. Na *Jadiah* ni ngamia aliyeingia katika mwaka wa tano. Na wanapofikia sabini na sita (76) hutolewa *Bint Labun* wawili kwa itifaki ya wote. Wakifikia tisini na mmoja (91) hutolewa *Huqqah* wawili kwa  itifaki ya wote.

Wameafikiana pia kuwa kiwango kinachozidi 190 hakina kitu cha kutolewa mpaka ngamia wafikie mia na ishirini na mmoja (121), lakini kila madhehebu ina maelezo yake na kauli yake wanapofikia idadi hiyo, nazo hupatikana katika vitabu vya Fikihi.

Aidha wameafikiana kuwa chini ya ngamia watano hakuna Zaka, wala kati ya kiwango kilichotangulia na kinachofuatia, hivyo "Kila ngamia watano, ni mbuzi mmoja, na ngamia tisa ni mbuzi mmoja pia. Ngamia kumi ni mbuzi wawili, na ngamia kumi na nne ni mbuzi wawili pia, na ni hivyo hivyo mpaka mwisho.

## KIWANGO CHA NG'OMBE:

Katika kila ng'ombe thelatini, hutolewa *Tabii*, na katika kila ng'ombe arobaini hutolewa *Musinnah*, na katika kila ng'ombe sitini, hutolewa *Tabii* wawiwili. Na katika kila ng'ombe sabini hutolewa *Musinnah* mmoja na *Tabii* mmoja. Na katika kila ng'ombe themanini hutolewa *Musinnah* wawili, na katika kila ng'ombe tisini hutolewa *Tabii* watatu. Na katika kila ng'ombe mia na ishirini hutolewa *Musinnah* watatu au *Tabii* wanne na kuendelea kama hivyo.

Na kati ya faradhi mbili hakuna kitolewacho, na kiwango cha Zaka ya ng'ombe kwa mfumo huo tulioutaja umekubaliwa na mafakihi wa madhehebu yote.

Ng'ombe anayeitwa *Tabii* ni yule ambaye amekamilisha mwaka na anaingia katika mwaka wa pili. Na *Musannah* ni ng'ombe anayeingia katika mwaka wa tatu. Na Maliki wamesema: "*Tabii*; ni ng'ombe aliyekamilisha miaka miwili na anaingia katika mwaka wa

tatu. Na *Musinnah*, ni ng'ombe ambaye amekamilisha miaka mitatu na anaingia katika mwaka wa nne.

**KIWANGO CHA MBUZI:**

Katika kila mbuzi arobaini hutolewa mmoja, na katika kila mbuzi 121, hutolewa mbuzi wawili. Na katika kila mbuzi 201 hutolewa mbuzi watatu kwa itifaki ya madhehebu yote.

Na Maimamiyya wamesema: "Mbuzi wanapofikia idadi ya 301 ndani yake hutolewa mbuzi wane; na huendelea hivyo hivyo hadi wanapofikia mia nne (400) na zaidi yake, hapo huwa kila mia (100) mbuzi mmoja.

Mafakihi wa madhehebu manne wamesema mbuzi mia tatu na moja (301) ni sawa na mia mbili na moja (201), hutolewa mbuzi watatu tu, hadi wanapofikia idadi ya mia nne (400), na wanapozidi hapo, basi kwa kila mia hutolewa mbuzi mmoja.

Kisha mafakihi wote wameafikiana kuwa kati ya faradhi mbili pana msamaha, hakuna Zaka itolewayo kwa kilichoongezeka kati yake.

**2.** *Assaum:* Ni mnyama wa kuchungwa ambaye hula nyasi za kujiotea katika muda mrefu wa siku za mwaka, asiyemlazimu mwenye mnyama huyo kumgharamia chakula isipokuwa kwa nadra. Na sharti hili limekubaliwa na mafakihi wote, isipokuwa Maliki tu, wao wamesema: "Ni wajibu kutoa Zaka ya wanyama wanaochungwa na hata wanaofugwa."

**3.** *Hauli*, hupitiwa na mwaka kamili kwa wanyama walio katika fungu la kutolewa Zaka, yaani wanyama hao wabaki kwa mwenye kuwamiliki muda wa mwaka kamili, hii ni kwa kila mny-



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 233 2/1/2017 3:51:52 PM

ama anayeunda idadi inayopasa kutolewa Zaka katika fungu husika. Kwa mfano mtu alikuwa na mbuzi arobaini mnamo mwanzo wa mwaka na baada ya kupita miezi fulani akapungua mmoja kwa kufa, kumpa mtu hiba au kumuuza, kisha wakakamilika arobaini, basi katika hali kama hiyo haitakuwa wajibu kuwatolea Zaka unapofika mwisho wa mwaka, bali utaanza mwaka kwa hesabu mpya. Maimamiyya, Mashafi na Mahanbali wakubaliana katika sharti hili.

Ama Mahanafi, wao wamesema: "Inapopungua kiwango cha wanyama katika mwaka, kisha wakatimia idadi inayolazimu kutolewa Zaka ifikapo mwisho wa mwaka, ni wajibu kutolewa Zaka kama ambavyo ingepaswa kama kiwango hicho kingedumu tangu mwanzo wa mwaka hadi mwisho.

Na *hauli* (mwaka) inayozingatiwa na mafakihi katika sharia ni *hauli* ya mwandamo wa mwezi. Yaani ni miezi kumi na miwili ya kuandama.

**4.** Ni kutokuwa wanyama hao wamefugwa maalum kwa ajili ya kufanya kazi, kama kulima kwa ng'ombe, na kusafirishia mizigo kwa ngamia, huwa hakuna Zaka inayotolewa kwa wanyama wanaofanya kazi hata kama watafikia kiwango chochote kile, isipokuwa Maliki wao wamesema: "Ni wajibu Zaka kutolewa katika wanyama wafanyao kazi na wasiofanya kazi bila ya tofauti yoyote."

Aidha wameafikiana kuwa kama mtu anao wanyama wa aina mbalimbali, wasiofikia idadi inayopasa kutolewa Zaka katika kila aina ya wanyama, basi haitamlazimu kuwachanganya, mfano lau mtu ana ng'ombe wasiofikia thelathini, na mbuzi wasiofikia arobaini basi haitampasa kutimiza *niswab,* kiwango kinachotolewea Zaka, kwa kuwachanganya ng'ombe na mbuzi, wala mbuzi na ng'ombe.

Kisha wamekhitilafiana kuhusu itakuwaje kama wanashirikiana watu wawili katika kiwango kimoja cha kutoa Zaka.

Maimamiyya, Mahanafi, na Maliki wamesema: "Si wajibu kwao wote wawili wala kwa mmoja wao kutoa Zaka, maadamu sehemu ya kila mmoja wao haifikii kiwango chake kinachopasa kutolewa Zaka (lau wangegawana)."

Mashafi na Mahanbali wamesema: "Ni wajibu kutolewa Zaka katika mali ya shirika inapofikia kiwango kinachopasa kutolewa Zaka, hata kama sehemu ya kila mmoja wao lau watawagawanya, haitafikia kiwango cha kupasa kutoa Zaka."

## ZAKA YA DHAHABU NA FEDHA

Mafakihi wamesema mengi kuhusiana na dhahabu na fedha, na wakapasisha katika vitu hivyo viwili kutolewa Zaka na wakasema: "Kiwango kinachopasa kutolewa Zaka katika dhahabu ni *mithqal* ishirini, (na kila *mithqal* ni 4.68gms, hivyo ni sawa na 9.60gms ). Na kiwango cha fedha ni dirhamu mia mbili.

Na wamekubaliana kwamba ni sharti madini hayo yapitiwe na mwaka ilihali yakiwa mikononi mwa mwenye kuyamiliki, tena yakiwa katika kiwango kinachopasa kutolewa Zaka. Kiasi kinachopasa kutolewa Zaka ya vitu viwili hivyo ni robo ya kumi katika kila mia."

Maimamiyya wamesema: "Ni wajibu kutolewa Zaka katika dhahabu na fedha zinapokuwa zimetengenezwa katika sarafu ya pesa, ama kama haziko hivyo kama vile vinoo vya dhahabu na mapambo haipasi Zaka ndani yake."

Na mafakihi wa madhehebu manne wameafikiana kuwa ni wajibu kutolewa Zaka vipande vya dhahabu kama ilivyo wajibu

katika sarafu (mfano wa shilingi), kisha wao wamekhitilafiana katika mapambo. Baadhi yao wakasema ni wajibu kutolewa Zaka, na wengine wakasema si wajibu.

Nasi natutosheke na ishara hii kwa sababu ya kutokuwepo umuhimu wowote wa kusema mengi kuhusu vitu viwili hivyo, kwani katika wakati wetu huu wa leo havionekani, au si kweli kama kuna watu waliorundika vipande vya dhahabu na fedha.

Ama noti za kimali (pesa), Maimamiyya wamewajibisha litolewe fungu la tano, yaani litolewe moja kati ya mafungu matano, katika ile sehemu ya faida iliyopatikana ndani ya mwaka mzima. Maelezo zaidi yatafuata.

Maliki, Mashafi na Mahanafi wamesema: "Katika pesa si wajibu ndani yake kutolewa Zaka isipokuwa zinapokamilika sharti zote kwa pamoja; kufikia kiwango na kiwango hicho kupitiwa na mwaka."

Mahanbali wamesema: "Si wajibu Zaka katika noti isipokuwa zinaposarifiwa kwa dhahabu au fedha."

## ZAKA YA MIMEA NA MATUNDA:

Wameafikiana katika kiwango kinachopasa ndani yake kutolewa Zaka katika vyakula na matunda, kuwa ni '*ushru'* yaani fungu la kumi katika kila mafungu mia, kama itakuwa imekuzwa kwa maji ya mvua au maji ya mto unaopita (karibu na shamba). Na ni wajibu kutolewa nusu ya kumi inapokuzwa kwa maji ya kisima kilichogharimiwa katika uchimbaji wake na mfano wa maji kama hayo.

Na wamekubaliana tena isipokuwa Mahanafi kwamba kufikia *nisabu* ni jambo linalozingatiwa katika nafaka na matunda.

Mahanafi wamesema: "Ni wajibu kutolewa Zaka katika kila kinachochipua ardhini kama vile matunda na mimea mingineyo



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 236 2/1/2017 3:51:52 PM

isipokuwa kuni, nyasi na mianzi." Maliki na Mashafi wamesema: "Ni wajibu kutolewa Zaka kila ambacho huwekeka akiba ya kutumika baadaye kama vile ngano, shairi, mchele, tende na zabibu." Mahanbali wamesema: "Zaka ni wajibu katika kila ambacho hupimwa na kuwekwa akiba katika matunda na mimea." Maimamiyya wamesema: "Zaka si wajibu isipokuwa katika ngano, shairi na  nafaka, aidha ni wajibu pia katika tende na zabibu, na si wajibu katika vingine visivyokuwa hivyo, bali hupendekezwa tu kuvitolea Zaka."

## ZAKA YA MALI YA BIASHARA

Mali ya biashara ni ile inayomilikiwa kwa lengo la mapatano ya kubadilishana mali kwa fedha, kwa shabaha ya kupata faida na chumo, nayo hapana budi iwe mtu ameimiliki kwa njia hiyo ya biashara, lakini lau mtu atamiliki mali kwa njia ya urithi haitakuwa ni mali ya biashara kwa itifaki ya mafahiki wote.

Na Zaka ya mali ya biashara ni wajibu kwa mafakihi wa madhehebu manne, na ni Sunna kwa Maimamiyya. Nayo hutolewa Zaka yake kulingana na kima cha bidhaa ambazo hufanyiwa biashara. Na kiwango chake ni kumi ya robo, yaani hutolewa moja katika kila arobaini.

Na mafakihi wote wameungana kuwa ni sharti mali hiyo ipitiwe na mwaka tangu alipotia nia ya kufanya biashara. Unapotimia mwaka katika biashara na akawa amepata faida hapo hufungamana na hukmu ya Zaka.

Maimamiyya wamesema: "Ni sharti kwamba mtaji uwepo kuanzia mwanzoni mwa mwaka hadi mwisho wake, hivyo kama mtaji utapungua mnamo katikati ya mwaka hatalazimika kulipa Zaka



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 237 2/1/2017 3:51:52 PM

mwaka huo, na kima kilichopungua kinaporudi tena basi hesabu ya mwanzo itavunjika na itaanza hesabu mpya kuanzia pale iliporudi ile sehemu iliyokuwa imepungua."

Mashafi na Mahanbali wamesema: "Kinachozingatiwa katika sharti la kupita mwaka si kuwepo mali yote, bali kama mtu hatamiliki kiwango kinachopasa kutolewea Zaka mwanzoni mwa mwaka, na akawa pia hakumiliki kiwango kinachopasa kutolewea Zaka katikati ya mwaka, lakini kisha akakimiliki kiwango hicho mnamo mwisho wa mwaka, ni wajibu kwake kutoa Zaka."

Mahanafi wamesema: "Kinachozingatiwa katika wajibu wa kutolewa Zaka ni kupitia pande mbili za mwaka, mwanzoni na mwishoni, si katikati yake, kwa maana ya kuwa; kama mtu anamiliki kiwango kinachopasa kutolewa Zaka mwanzoni mwa mwaka, kisha kikapungua katikati ya mwaka, baadaye kikakamilika mwishoni mwa mwaka, hapo ni wajibu kwake kutoa Zaka, ama kama kiwango kitapungua katika mwanzo wa mwaka, au mwisho wa mwaka, haitakuwa wajibu kwake kutoa Zaka."

Vilevile ni sharti chombo kinachofanyiwa biashara kiwe kina thamani inayofikia kiwango cha Zaka, ili kipate kusimama mahali pa kiwango cha mali inayopasa kutolewa Zaka. Na thamani yake ilingane sawa na kiwango kinachopasa kutolewa Zaka katika dhahabu na fedha. Hivyo kitalinganishwa na kimojawapo, kitakapolingana nacho au kuzidi hapo ndipo huwa wajibu kutolewa Zaka. Na kama thamani yake itapungua kwa kuwa chini kuliko thamani ya kile chenye thamani ndogo, ambacho ni fedha, basi haitapasa Zaka ndani yake. Na mwandishi wa kitabu cha *Al-Fiqhu Alal Madhahibil Arbaa* kilichochapishwa mwaka 1922 amekisia thamani yake kuwa ni *kirshi* mia tano na ishirini na tisa na thuluthi mbili za ki -Misri.

### ZAKA HUTOLEWA KUTOKA KATIKA DHIMA AU KUTOKA KATIKA KITU CHENYEWE?

Wametofautiana mafakihi kuhusu je, ni wajibu kutoa Zaka kutoka katika mali yenyewe husika, ambapo mwenye kustahiki kupewa Zaka huwa ni mshirika wa mwenye kuitoa, katika mali ya Zaka, kama ilivyo kwa washiriki wengineo? Au Zaka ni wajibu uliyopo katika dhima ya mmiliki kama ilivyo katika madeni, lakini Zaka inafungamana na mali kama vile linavyofungamana deni na mali alizoziacha mtu aliyekufa?

Mashafi, Maimamiyya na Maliki wamesema: "Kwa hakika Zaka ni wajibu itolewe kutoka katika mali yenyewe husika, na fukara ni mshirika halisi wa mwenye kumiliki mali, hiyo ni kwa dalili ya kauli yake Mwenyezi Mungu mtukufu aliposema: *'*Na katika mali zao mna haki ya kupewa maskini aombaye na ajizuiaye asiyeomba." (*Adh-Dhariyat:19*). Vilevile zimeenea Hadith zinazoelezea kuwa Mwenyezi Mungu amewashirikisha matajiri na maskini katika mali walizo nazo matajiri. Hata hivyo sheria imeruhusu tajiri aitekeleze haki hii kwa kumhurumia, aitoe katika mali nyingine ambayo ndani yake hamna Zaka."

Mahanafi wamesema: "Zaka hufungamana na mali yenyewe husika kama ilivyofungamana haki ya rehani katika mali iliyowekwa rehani, na haki hiyo huwa haiondoki ila kwa kuirudisha mali hiyo kwa mwenye kustahiki kupewa." Na kutoka kwa Imam Ahmad kuna riwaya mbili moja yawafikiana na Mahanafi.

## WATU WANAOSTAHIKI KUPEWA ZAKA

Wameafikiana mafakihi wa madhehebu yote kwamba watu wanaostahiki kupewa Zaka ni aina nane, nao ni wale waliotajwa ndani ya Qur'ani katika Aya ya 60 ya *Surat Tawbah* isemayo:



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 239 2/1/2017 3:51:52 PM

"إِنَّمَا ٱلصَّدَقَٰتُ لِلْفُقَرَآءِ وَٱلْمَسَٰكِينِ وَٱلْعَٰمِلِينَ عَلَيْهَا وَٱلْمُؤَلَّفَةِ قُلُوبُهُمْ وَفِى ٱلرِّقَابِ وَٱلْغَٰرِمِينَ وَفِى
سَبِيلِ ٱللَّهِ وَٱبْنِ ٱلسَّبِيلِ ....."

**"Hakika sadaka ni ya (watu hawa tu) mafukara, na maskini, na wanaozitumikia na wanaotiwa nguvu nyoyo zao (juu ya uislamu), na kuwakomboa watumwa, na wenye madeni, na katika njia ya Mwenyezi Mungu na mwana njia.…"**

Ama kauli za madhehebu katika kuwapanga hao wanaostahiki zitajulikana katika maelezo yafuatayo:

## FUKARA:

**1.** Mahanafi wamesema: "Fukara ni mtu anayemiliki chini ya kiwango kinachopasa kutolewa Zaka, hata kama ni mwenye afya njema mwenye pato. Ama mtu anayemiliki mali ya aina yoyote ambayo thamani yake inafikia kiwango cha kutolewa Zaka, na ikawa mali hiyo ni yenye kubaki baada ya mahitaji yake ya kimsingi kama vile makazi, vyombo na nguo na vinginevyo vilivyo katika mfano wa hivyo, basi haijuzu kwa mtu huyo kupewa Zaka." Na hoja yao ya kusema hivyo ni kuwa, kila mwenye kumiliki kiwango kinachopasa kutolewa Zaka ndani yake humlazimu atoe Zaka, na anayelazimika kutoa Zaka haipasi kupewa Zaka.

Madhehebu yaliyobakia yamesema: "Linalozingatiwa kwa mtu ni jinsi alivyo muhitaji, wala haiangaliwi anamiliki nini katika mali, hivyo yeyote asiyekuwa muhitaji ni haramu kwake kupewa Zaka hata kama hana anachomiliki katika mali, na aliyemuhitaji ni halali kupewa Zaka hata kama atakuwa ni mwenye kumiliki mali inayofikia kiwango cha kutolewa Zaka au nyingi zaidi, kwani ufukara maana yake ni uhitaji, kama alivyosema Mwenyezi Mungu (s.w.t.).



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 240 2/1/2017 3:51:52 PM

﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ أَنتُمُ ٱلْفُقَرَآءُ إِلَى ٱللَّهِ ۖ ..... "

**"Enyi watu, nyinyi ndio wenye haja kwa Mwenyezi Mungu….." (Fatir; 35:15).** Yaani nyinyi ndio wahitaji kwake."

Mashafi na Mahanbali wamesema: "Mtu mwenye kumiliki nusu ya mahitaji yake hahesabiwi kuwa ni fukara, na pia huwa ni halali kwake kupewa Zaka."

Maimamiyya na Malikiy wamesema: "Fakiri kisheria ni mtu asiyemiliki kitu cha kutosheleza mahitaji yake na familia yake kwa mwaka mzima, kwa hivyo mtu ambaye ana kiwanda au kipande cha ardhi au wanyama ambao hawatoshelezi mahitaji ya familia yake kwa kipindi cha mwaka mzima, mtu huyo ni halali kupewa Zaka."

Maimamiyya, Mashafi na Mahanbali wamesema: "Mwenye uwezo wa kuchuma mali si halali kwake kupewa Zaka." Mahanafi na Maliki wamesema: "Bali ni halali kwake kupewa Zaka."

Maimamiyya wamesema: "Anayedai kuwa ni fukara husadikiwa bila ya kuchunguzwa wala kuapishwa kama hana mali inayoonekana waziwazi, na iwapo hajajulikana kwa uongo wake (hana sifa ya uwongo), kwani kuna watu wawili walimwendea Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa akigawa sadaka, wakamwomba awape nao kidogo, Mtume (s.a.w.w.) akawaangalia kwa makini kisha akawaambia: 'Mkitaka nitawapa lakini (mjue) hapana fungu la tajiri wala la mtu mwenye nguvu za kuchuma.' Akachukua sehemu akawapa bila ya kutaka kithibitisho cha kiapo."

## MASIKINI:

**2.** Maimamiyya, Mahanafi na Maliki wamesema: "Masikini ni mtu mwenye hali mbaya zaidi kuliko fukara." Mahanbali na



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 241 2/1/2017 3:51:52 PM

> Mashafi wamesema: "Si hivyo, bali fukara ndiye mwenye hali mbaya zaidi kuliko masikini, kwa kuwa fukara ni asiyekuwa na kitu chochote anachokimiliki, au asiyeweza kupata nusu ya mahitaji yake. Na masikini ni mtu anayemiliki nusu ya mahitaji yake, kwa hiyo hupewa nusu nyingine katika Zaka."

Na kwa vyovyote iwavyo, hakuna hitilafu ya kimsingi kati ya madhehebu katika suala la kuainisha fukara na masikini. Na linalozingatiwa ni kuwa Zaka ni kizibo cha kuziba dhidi ya mwenye shida ya kuzidi kama vile kukosa makazi, chakula, nguo, matibabu, elimu au mengineyo katika mambo ambayo humlazimu mwanaadamu kuwa nayo.

Kisha mafakihi wa madhehebu yote isipokuwa Maliki wameafikiana kuwa inayempasa kutoa Zaka haijuzu kwake kuwapa wazazi wake, babu zake, watoto wake, watoto wa watoto wake wala mkewe."

Ama Maliki wamejuzisha kumpa Zaka babu na bibi (nyanya) na watoto wa watoto (wajukuu), kwa kuwa matumizi yao hayamlazimu yeye kulingana na ilivyo katika madhehebu yao.

Pia wameafikiana kuwa inajuzu kuwapa Zaka ndugu (kaka), ammi na wajomba. Bali uhakika ni kuwa haijuzu kumpa baba na watoto kutoka katika fungu la mafukara na masikini, lakini inajuzu kuwapa kama ni kutoka katika mafungu mengine yasiyokuwa hayo wawili (la masikini na mafukara), kama pale anapokuwa baba au mtoto walipigana katika njia ya Mwenyezi Mungu, au ni katika wale wanaotiwa nguvu Uislamu wao, au walioingia deni katika kutengeneza mambo aliyoamrisha Mwenyezi Mungu kama kupatanisha ndugu, au alifanya kazi ya kuikusanya Zaka. Kwani watu hao hupokea Zaka kwa vyovyote ilivyo hali yao wawe ni matajiri au mafukara. (Kitabu, *Tadhkiratul Allamah*, Juz. ya kwanza mlango wa Zaka).



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 242 2/1/2017 3:51:52 PM

Na vyovyote hali inavyokuwa ni kwamba ndugu wa karibu ambaye matumizi yake hayamlazimu mwenye kutoa Zaka ni aula, yaani kumpa Zaka ni bora zaidi.

Kisha wamekhitilafiana katika suala la kuisafirisha Zaka kutoka mji mmoja hadi mwingine. Mahanafi na Maimamiyya wamesema: “Kuwapa Zaka watu wa mjini kwake ni bora zaidi isipokuwa linapotokea jambo lisilo budi ambalo litadhihirisha ubora wa kuisafirisha Zaka.”

Mashafi na Maliki wamesema: “Haijuzu kuihamisha Zaka kutoka mji mmoja hadi mwingine.” Mahanbali wamesema: “Si kosa kuisafirisha Zaka katika mji ambao umbali wake haulazimu kukusuru Swala, bali ni haramu iwapo mji unaosafirishiwa Zaka utakuwa mbali kwa umbali unaolazimu kukusuru Swala.”

**WANAOITUMIKIA:**

**3.** Wanaoitumikia Zaka ni wale wanaozunguka kuzikusanya Zaka, kwa itifaki ya mafakihi wa madhehebu yote.

**WANAOTIWA NGUVU NYOYO ZAO:**

**4.** Wanaotiwa nguvu nyoyo zao, ni wale watu ambao hupewa sehemu katika Zaka kwa ajili ya maslahi ya Uislamu. Kisha mafakihi wa madhehebu wamekhitilafiana kuhusu je, hukmu yao bado ipo hadi leo hii au imefutwa? Kama tutakadiria kuwa haikufutwa, je inamhusu asiyekuwa Mwislamu tu? Au hata walio Waislamu lakini imani zao ni dhaifu?

Mahanafi wamesema: “Sharia hii iliwekwa zama za mwanzo za Uislamu kutokana na udhaifu wa Waislamu, ama kwa hivi sasa ambapo Uislamu umekuwa na nguvu tosha hukmu hiyo imeondoka pamoja na kuondoka sababu yake.”

Ama madhehebu yaliyobaki yamerefusha sana maelezo yanayohusu hao wanaotiwa nguvu nyoyo zao pamoja na kugawa viwango vya watu hao. Lakini hata hivyo, maelezo hayo yote tunaweza kuyarejesha kwenye maana moja, nayo ni kuwa hukmu hiyo haikufutwa bali bado ipo na inaendelea, na kwamba sehemu ya wanaotiwa nguvu nyoyo zao hupewa Mwislamu na asiyekuwa Mwislamu, kwa sharti la kuwa, ni lazima katika kufanya hivyo kuwe na maslahi yanayorudi kwa Uislamu pamoja na Waislamu kwa ujumla.

Bila shaka Mtume (s.a.w.w.) alimpa Swafwan bin Umayya sehemu ya fungu hilo hali alikuwa ni mushrik (kafiri), pia alimpa Abu Sufyani na wengineo kama yeye, baada ya kudhihirisha Uislamu wao kwa ajili ya kuchelea uovu wao na vitimbi vyao viovu dhidi ya dini na Uislamu.

## KUACHA MTUMWA HURU:

**5.** Kuacha mtumwa huru, kuna maana ya kumnunua mtumwa kwa mali ya Zaka na kumwacha huru. Katika kufanya hivyo ndani yake mna dalili iliyo wazi kuwa Uislamu umeweka njia mbalimbali za kuweza kuwakomboa walio watumwa na kuiondoa fikra ya utumwa katika jamii ya wanaadamu. Hata hivyo, katika wakati wetu huu wa sasa hukmu hii ya watumwa haina mahali pake tena pa kulijadili Swala hili, maana hakuna tena utumwa.

## WALIOZIDIWA NA MADENI WASIYOWEZA KUYALIPA:

**6.** Wenye madeni (wanaokusudiwa hapa) ni watu ambao wana madeni ambayo hayatokani na sababu za maasi, nao hupewa Zaka ili wapate kulipa madeni yao, hii ni kwa itifaki ya mafakihi wote.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 244 2/1/2017 3:51:52 PM

## KATIKA NJIA YA MWENYEZI MUNGU:

**7.** Njia ya Mwenyezi Mungu; mafakihi wa madhehebu manne wamesema: "Wanaokusudiwa walio katika njia ya Mwenyezi Mungu ni wapiganao jihadi ambao wamejitoa mhanga kuupigania Uislamu."

Maimamiyya wamesema: "Njia ya Mwenyezi Mungu inawajumuisha wapiganaji jihadi, wenye kujenga misikiti, mahospitali, madrasa na mambo mengineyo yenye maslahi kwa Waislamu wote."

## WASAFIRI WALIOHARIBIKIWA:

**8.** Mwana njia, ni msafiri mgeni aliyeishiwa na mali akiwa mbali na kwao, hujuzu kwa mtu huyu kupewa kiasi cha Zaka ambacho kinaweza kumrudisha hadi kwao.

**Tanzuo**: Kwanza, mafakihi wameafikiana kuwa ni haramu kupewa Zaka Banu Hashim kwa aina zake zote, inapokuwa Zaka hiyo inatoka kwa wengineo wasiokuwa wao, bali huwa halali kupeana wao kwa wao.

Pili: Je inafaa Zaka yote kupewa masikini mmoja? Maimamiyya wamesema: "Ndiyo, yafaa hata kama Zaka hiyo anayopewa itamtoa kutoka kwenye umasikini hadi kwenye kutajirika, kwa sharti apewe kwa mpigo (mara moja) na si kidogo kidogo." Mahanafi wamesema: "Hujuzu kupewa Zaka mtu mmoja iwapo haitamtajirisha." Na hii ndio kauli ya Mahanbali. Maliki wamesema: "Yafaa kutoa Zaka kumpa mtu mmoja, isipokuwa mwenye kuitumikia, yeye haifai kuchukua zaidi ya ujira wake wa kazi aliyofanya." Mashafi wamesema: "Ni wajibu kuieneza Zaka kwa watu aina zote nane kama watapatikana, kama baadhi yao watakosekana basi watapewa watakaopatikana,



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 245 2/1/2017 3:51:52 PM

na uchache wa kiasi kinachofaa ni kupewa watu watatu katika kila kundi.

Tatu: Mali zinazopasa kutolewa Zaka ni aina mbli: Inayolazimu kupitiwa na mwaka, nayo ni wanyama na kima cha biashara, hii si wajibu kutolewa Zaka kabla ya kupita mwaka. Na kwa Maimamiyya mwaka ni kupitiwa na miezi kumi na mmoja hali mali hiyo ikiwa imo mikononi mwa mwenye kupaswa kuitolea Zaka, na uwe umeandama mwezi wa kumi na mbili.

Na aina ya pili ya mali ni ile ambayo si wajibu kupitiwa na mwaka, kama vile matunda na nafaka, kwani aina hiyo ni wajibu kutolewa Zaka mara tu baada ya kukamilika, kukomaa na kuwa tayari kwa kuliwa. Ama wakati wa kutoa Zaka ya matunda ni tangu pale yanapoiva na kuchumwa, kuanikwa hadi kukauka, na kwa upande wa nafaka ni tangu pale zinapovunwa, kusafishwa majani makavu na maganda yake. Hii ni kwa itifaki ya mafakihi wa madhehebu yote.

Kama mtu atachelewesha kutoa Zaka wakati wake wa kutoa unapofika, ilihali uwezo wa kutoa Zaka anao, atapata dhambi, na atalazimika atoe Zaka vilevile. Kwa sababu amechelewesha jambo la wajibu na kulidhikisha hadi kulitoa nje ya wakati wake, na amefanya uzembe kwa kuchelewesha kutoa (ilivyompasa).

## ZAKA YA FITRI

Zaka ya Fitri, pia huitwa Zaka ya mwili, na kuna maneno mengi kuhusu mtu anayewajibika kutoa, mtu anayetolewa, kiwango chake, wakati wa kuitoa, na ni nani anayestahiki kupewa.

### ANAYEWAJIBIKA KUTOA:

Mafakihi wa madhehebu manne wamesema: “Zaka ya Fitri ni wajibu kwa kila Mwislamu mwenye uwezo, awe ni mtu mkubwa au mtoto,



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 246 2/1/2017 3:51:52 PM

ni wajibu kwa walii (msimamizi) kutoa Zaka ya Fitri kuwapa mafukara, kutoka katika mali ya mtoto na ya mwendawazimu." Na aliye na uwezo kwa mujibu wa madhehebu ya Hanafi ni mtu anayemiliki kiwango cha kutolewa Zaka au kima chake kilichozidi baada ya matumizi yake ya lazima."

Mashafi, Maliki na Mahanbali wamesema: "Mtu mwenye uwezo, ni yule aliye na kitu kilichozidi (kilichobaki) baada ya kutimiza chakula chake na chakula cha watu wake katika siku ya Idd na usiku wake, bila kujumuisha mahitaji ya muhimu kama vile makazi, nguo na vifaa vya lazima (katika vyombo vya nyumbani)." Na Maliki wameongeza kuwa: "Mwenye uwezo wa kukopa huhesabiwa kuwa ni mwenye uwezo, iwapo tu ana matarajio ya kulipa."

Maimamiyya wamesema: "Ni sharti katika kutoa Zaka ya Fitri, kubaleghe, kuwa na akili timamu na kuwa na uwezo. Zaka ya Fitri si wajibu kutolewa kutoka katika mali ya mtoto mdogo wala mwendawazimu kutokana na Hadith inayosema: 'Imeinuliwa kalamu kwa watu watatu, kwa mtoto hadi anapobaleghe, kwa mwendawazimu hadi anaporudisha fahamu zake, na kwa aliyelala hadi anapoamka.' Ama mtu aliye na uwezo kwao wao ni yule ambaye anayamiliki matumizi yake ya lazima ya mwaka mzima pamoja na matumizi ya kutosheleza familia yake, sawa iwe anayapata kwa sahali au kwa nguvu (na jasho), sawa awe na njia ya kuvuna mahitaji yake au kitega uchumi."

Mahanafi wamesema: "Ni wajibu kwa mtu Mukallaf kutoa Zaka ya Fitri kwa kujitolea yeye mwenyewe, watoto wake wadogo na watumishi (watumwa) wake, na hata mtoto wake mkubwa kama ni mwendawazimu, lakini kama ni mwenye akili timamu si wajibu kwa baba yake kumtolea Zaka ya Fitri, kama ambavyo si wajibu kwa mume kumtolea mke wake."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 247 2/1/2017 3:51:53 PM

Mahanbali na Mashafi wamesema: "Ni wajibu kujitolea Zaka ya Fitri yeye mwenyewe na anayemsimamia kwa chakula chake, nao ni (kama vile) wazazi wawili walio mafukara, na watoto wa kiume wasiokuwa na mali, hadi wanapobaleghe na wakawa wana uwezo wa kuchuma, na wanawe wa kike hadi wanapoolewa, na mke."

Maimamiyya wamesema: "Ni wajibu kujitolea yeye mwenyewe na kila ambaye pindi usiku wa kuamkia Idd ya Fitri ulipoingia, alikuwa ni katika walio chini ya uangalizi wake, pasi na kuwepo na tofauti kati ya mtu anayemlazimu matumizi yake na mwinginewe, wala kati ya mkubwa na mdogo, wala kati ya Mwislamu na asiyekuwa Mwislamu, wala kati ya ndugu wa karibu na ndugu wa mbali aliye mgeni, hata kama kawasili kwake kama mgeni wake kabla ya kuandama kwa mwezi wa Shawwal kwa muda mfupi, kwa hivyo naye akawa miongoni mwa familia yake katika usiku huo, naye pia itampasa amtolee Zaka ya Fitri. Na hukmu ni hiyo hiyo kama atazaliwa mtoto au ataoa mke kabla ya kutua jua la usiku wa kuamikia Siku ya Idd. Lakini anapozaliwa mtoto au kuoa mke au mgeni kuwasili baada ya jua kutua, hapo si wajibu kumtolea Fitri. Na kila ambaye Fitri yake ni wajibu ulio juu ya mwingine, si wajibu kwake kujitolea yeye mwenyewe hata kama mtu huyo ni tajiri."

## KIWANGO CHAKE:

Mafakihi wa madhehebu wameafikiana kuwa kiwango ambacho ni wajibu kukitoa katika Zaka ya Fitri kwa kila mtu ni pishi moja, sawa ziwe za ngano, shairi, tende, zabibu, mchele au mahindi na vyenginevyo katika nafaka zinazoliwa kwa wingi katika mji anaoishi. Isipokuwa Mahanafi wao wamesema: "Hutosha kutoa nusu ya pishi ya ngano kwa kila mtu mmoja, pishi yakaribia kuwa sawa na kilo tatu."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 248 2/1/2017 3:51:53 PM

## WAKATI WA KUTOA:

Mahanafi wamesema: "Wakati wake wa wajibu, ambao ni wajibu kutoa Zaka ya Fitri ni tangu kuingia alfajiri ya siku ya Idd hadi mwisho wa umri wa mtu, kwa sababu Zaka ya Fitri ni miongoni mwa faradhi zilizo pana, kwa hivyo huswihi kuitekeleza kwa kuitanguliza na kuichelewesha."

Mahanbali wamesema: "Ni haramu kuchelewesha kuitoa hadi baada ya siku ya Idd, lakini hufaa kuitoa siku mbili kabla ya Idd, na haijuzu kuitoa kabla ya muda huo."

Mashafi wamesema: "Wakati wake wa wajibu ni kuanzia sehemu ya mwisho ya mwezi wa Ramadhani hadi sehemu ya mwanzo wa mwezi wa Shawwal, kwa maana ya kuwa ni mara tu baada ya kutua jua na kabla yake kwa muda mchache katika siku ya mwisho ya mwezi wa Ramadhani. Na husunniwa kuitoa mnamo mwanzo wa siku ya Idd, na ni haramu kuitoa Fitri baada ya kutua jua la siku ya kwanza ya Idd, isipokuwa kwa udhuru."

Imepokewa kutoka kwa Imam Malik mapokezi mawili: Mojawapo ni kuwa ni wajibu itolewe magharibi ya siku ya mwisho ya Ramadhani.

Maimamiyya wamesema: "Wajibu wa Zaka ya Fitri unatokana na kuingia Usiku wa Iddi, na ni wajibu kutolewa tangu jua linapotua hadi wakati wa kukengeuka jua. Na bora ni kuitekeleza kabla ya Swala Idd, na kama katika wakati huu hatampata mwenye kustahiki kupewa, itamlazimu mukallaf aizuie kwa muda kwa kuitenganisha na mali yake ilihali akinuia kuitoa na kuikabidhi baada tu ya fursa kupatikana, na kama ataichelewesha bila kuitoa katika wakati huu ilihali yupo anayestahiki kupewa, itakuwa ni wajibu kwake kuitoa baadaye, na kamwe wajibu huo haumtoki kwa hali yoyote iwayo."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 249 2/1/2017 3:51:53 PM

**ANAYESTAHIKI KUPEWA:**

Mafakihi wa madhehebu yote wameafikaina kuwa wanaostahiki kupewa Zaka ya Fitri ndio wale wale wanaostahiki kupewa Zaka nyinginezo, nao ni wale waliotajwa katika Aya ya 60 ya Surat Tawba inayosema; **"**Sadaka hupewa (watu hawa) - mafukara na maskini …"

Aidha wameafikiana kuwa hufaa kutoa iliyo thamani ya nafaka badala ya nafaka yenyewe, pia hufaa zaidi kupewa walio ndugu wa karibu (wenye shida) ambao wanahitajia Zaka hiyo, kisha majirani, kwani imepokewa katika Hadith tukufu kuwa: "Jirani (anayehitajia) sadaka ni mwenye haki zaidi ya kupewa."

# KHUMSI (FUNGU LA TANO)

Maimamiyya katika vitabu vya Fikihi wametenga mlango maalum wa Khumsi ambao huutaja baada ya mlango wa Zaka. Na asili ya wao kuipa umuhimu kama huo ni kutokana na Aya ya Qur'ani tukufu ambayo Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amesema ndani yake:

۞ وَٱعْلَمُوٓا۟ أَنَّمَا غَنِمْتُم مِّن شَىْءٍ فَأَنَّ لِلَّهِ خُمُسَهُۥ وَلِلرَّسُولِ وَلِذِى ٱلْقُرْبَىٰ وَٱلْيَتَٰمَىٰ وَٱلْمَسَٰكِينِ وَٱبْنِ ٱلسَّبِيلِ إِن كُنتُمْ ءَامَنتُم بِٱللَّهِ وَمَآ أَنزَلْنَا عَلَىٰ عَبْدِنَا ....."

**"Na jueni ya kwamba chochote mnachopata ngawira, basi khums (sehemu ya tano) yake ni ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake na jamaa na mayatima na masikini na msafiri (aliyeharibikiwa), ikiwa nyinyi mmemwamini Mwenyezi Mungu na tuliyoteremsha kwa mja Wetu …" (Surat Anfal: 8:41).**

Nao Maimamiyya hawakuhusisha ghanima kuwa ni lile pato linalopatikana au linaloingia mikononi mwa Waislamu kutoka



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 250 2/1/2017 3:51:53 PM

katika mali isiyokuwa ya Waislamu, iliyopatikana kwa njia ya kuwamwaga jasho farasi na wapandaji wake (yaani kwa kupigana vita), bali wao wameihusisha katika aina saba miongoni mwa mali ambazo tutazitaja hivi punde pamoja na kueleza fikra za madhehebu mengine na hukmu yao ilivyo katika kila sampuli ya mali hiyo.

1. **Ngawira:** Mali iliyotekwa kwenye vita. Katika aina hii ya mali hutolewa Khumsi kwa itifaki ya mafakihi wa madhehebu yote.

2. **Madini:** Nayo ni kila kitu kinachotoka ardhini na kikawa si katika jinsi ya ardhi miongoni mwa vitu ambavyo vina thamani kama vile dhahabu, fedha, risasi, shaba, zebaki, mafuta (petroli), kiberiti na vilivyo katika mfano wa vitu tulivyovitaja.

Maimamiyya wamesema: "Ni wajibu kutoa Khumsi ya madini iwapo thamani yake itakuwa inafikia *Niswab* ya dhahabu, nayo ni Dinari ishirini au iwe inafikia *Niswabu* ya fedha ambayo ni Dirhamu mia mbili, lakini inapokuwa chini ya hapo huwa hapatolewi Khumsi."

Mahanafi wamesema: "Katika madini haizingatiwi *Niswab*, bali wajibu ni kutolewa Khumsi katika wingi na uchache wake."

Maliki, Mashafi na Mahanbali wamesema: "Kama madini yatakuwa hayafikii *Niswab* basi haitatolewa kitu chochote, lakini kama yatafikia *Niswab* ya Zaka itatolewa robo ya kumi (2 ½) katika kila mia."

3. **Hazina:** Nayo ni mali iliyozikwa ardhini kwa kipindi kirefu, na wenye mali hiyo wamekufa wote na athari yao imetoweka na kusahaulika hata ikawa hawajulikani tena.

Mafakihi wa madhehebu manne wamesema: "Katika mali iliyofukuliwa kutoka ardhini ni wajibu kutolewa Khumsi wala haizingatiwi kiwango (niswab), kwani wingi wake na uchache wake ni sawa katika wajibu wa kutolewa Khumsi."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 251 2/1/2017 3:51:53 PM

Maimamiyya wamesema: "Mali iliyofukuliwa kutoka ardhini hukmu yake ni kama ya madini katika wajibu wa kutolewa Khumsi, ambapo huzingatiwa kufikia *Niswab* (kiwango chake kilichowekwa na sheria).

**4.** Maimamiyya wamesema: "Chochote ambacho hutolewa baharini kwa kupigiwa mbizi, kama vile lulu na marijani ni wajibu kutolewa sehemu ya tano (Khumsi), iwapo itakuwa kima chake kinafikia uzito wa dinari na kuzidi baada ya kuondolewa mashaza yake." Ama katika madhehebu mengine, si wajibu kwao kutolewa chochote hata kama vitu hivyo vitafikia uzito wa namna gani.

**5.** Maimamiyya wamesema: "Ni wajibu kutoa Khumsi (sehemu ya tano) katika kila mali iliyozidi katika matumizi ya mwaka mzima ya mtu na familia yake, kutoka popote itakapopatikana faida yake, sawa pato lake hilo awe amelipata katika biashara, sanaa, ukulima, wadhifa (kazi ya mwezi) au kibarua. Aidha hukmu ni kama hiyo hata kama ziada hiyo alipata kutokana na milki au kwa kupewa hiba na kwa njia yoyote nyingine ya kisharia. Hivyo basi kama itazidi baada ya matumizi yake hata senti moja au kitu chenye kulingana na senti, basi atawajibika kuitolea Khumsi yake."

**6.** Maimamiyya wamesema: "Kama mtu atapata mali iliyopatikana kwa njia ya haramu, kisha mali hiyo ikachanganyika na mali ya halali, akawa haelewi kiasi cha mali ya haramu ni kipi, na pia akawa hamuelewi mtu mwenye mali ile ya haramu. Hapo atawajibika kuitolea Khumsi mali yake yote katika njia ya Mwenyezi Mungu, akifanya hivyo basi mali yake yote iliyobakia itakuwa ni halali, sawa iwe iliyokuwa haramu ni chache



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 252 2/1/2017 3:51:53 PM

katika Khumsi (iliyotolewa) au ni nyingi. Ama kama anaijua ni ipi hasa iliyo mali ya haramu, ni wajibu kwake kuirudisha mali yote ile iliyo ya haramu. Na kama haijui ni ipi hasa iliyo mali ya haramu lakini anajua thamani na kiwango chake, basi ni wajibu kwake kutoa kiwango chake bila ya kupungua kitu, hata kama itajumuisha mali yote. Na kama anawajua wenye mali lakini hajui haki yao katika mali hiyo ni kiasi gani, basi ni wajibu kwake kuwaridhisha kwa njia ya kusameheana na kuelewana. Kwa neno jingine; ni kuwa kutoa Khumsi ya mali yote ni pale mtu anapokuwa hajui kiasi cha mali ya haramu, na hamjui mwenye mali hiyo ya haramu.

**7.** Maimamiyya wamesema: "Kama *Dhimiy* atanunua ardhi kutoka kwa Mwislamu, ni wajibu kwa *Dhimiy* huyo kuilipia Khumsi yake."

## MAENEO YA KUTUMIA KHUMSI:

Mashafi na Mahanbali wamesema: "Ngawira, nayo ni hiyo Khumsi, hugawanywa mafungu matano, moja ni fungu la Mtume, nalo hutumika kwa maslahi ya Uislamu. Jingine hupewa ndugu wa karibu na Mtume ﷺ nao ni wale ambao wanaungana kinasaba kwa Hashim kwa upande wa baba, bila ya kuwepo tofauti kati ya tajiri miongoni mwao wala masikini. Na mafungu matatu yaliyobaki hutolewa kwa mayatima, masikini na walioharibikiwa wakiwa ugenini, sawa wawe wanatokana na ukoo wa Hashim (Bani Hashim) au wengineo."

Mashafi wamesema: "Fungu alilokuwa akipewa Mtume ﷺ limefutika baada ya kufa kwake. Ama hao karaba wa Mtume ﷺ hupewa kama wengineo katika mafukara, watapewa kutokana na huo ufukara lakini si kwa sababu ya ukaribu wao kwa Mtume."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 253 2/1/2017 3:51:53 PM

Maliki wamesema: "Mambo yanayohusu ugavi wa Khumsi huachwa mikononi mwa Imam, naye ataitumia mahali popote pale anapoona kuwa pana maslahi (kwa Uislamu)."

Imamyya wamesema: "Kwa yakini kabisa, fungu la Mwenyezi Mungu, fungu la Mtume ﷺ na fungu la akraba zake, ugavi na matumizi yake hutegemezwa kwa Imamu au naibu wake, naye atazitumia katika mambo ya maslahi kwa Waislamu. Na mafungu matatu yaliyobaki watapewa mayatima wa kibani Hashim na masikini wao, pamoja na waliokatikiwa njiani (ugenini) katika hao hao Bani Hashim. Kamwe hawashirikiani katika mafungu hayo na yeyote mwingine asiyekuwa Bani Hashim.

Tunamalizia kifungu hiki cha ugavi wa mali ya Khumsi kwa maneno aliyoyasema As-Sha'arani katika kitabu *"Al Mizan'* kwenye mlango wa Zaka ya madini: "Imam ana jukumu la kuweka kwa wenye madini kiwango maalum anachoona kuwa kitafaa kwa kuendeshea Baitul mal (Hazina Kuu ya Waislamu). Kwa ajili ya kuhofia kuwa mali ya wenye madini isilimbikizane hatimaye wakaja kudai ufalme. Wakazitumia kwa askari na kwa kufanyika hilo ikawa sababu ya kutokea ufisadi katika nchi."

Na haya ni maelezo ya pili ya nadharia mambo leo, kwani rasilimali huwafanya wenye nayo kutaka utawala (kama inavyodhihiri leo hii). Na tangu bwana huyo aliyekufa alipotoa fikra hiyo hadi leo hii ni miaka mia nne na sita imepita.

# HIJJA

## MASHARTI YAKE:

Ni wajibu mtu kuhiji linapopatikana sharti la kubaleghe, kuwa na akili timamu na kuwa na uwezo.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 254 2/1/2017 3:51:53 PM

**KUBALEGHE:**

Hijja si wajibu kwa mtoto, awe ni mtambuzi au asiyekuwa mtambuzi, lakini kama mtoto mtambuzi atakwenda kuhiji basi Hijja yake itaswihi. Hata hivyo Hijja yake hiyo itakuwa ni Sunna, ambapo atalazimika kuhiji tena Hijja ya faradhi atakapobaleghe na akawa na uwezo. Hii ni kwa itifaki, iwapo hakubaleghe kabla ya kusimama Arafah.

Na inajuzu kwa mlezi wa mtoto asiyekuwa mtambuzi kuhiji naye, amvalishe nguo ya kuhirimia Hijja, amfundishe Talbiya (neno *Labbaikallahuma Labbaika*). Kama ataweza kuitamka vyema, la hawezi atamtimizia yeye. Amwepushe na mambo yaliyo haramishwa (kutendwa katika Hijja) kwa mtu anayehiji. Aidha amwamrishe kufanya kila kitendo ambacho atamudu kukitenda yeye mwenyewe moja kwa moja, kisha afanye kwa niaba yake katika matendo ambayo hawezi kuyatenda.

Kisha mafakihi wamekhitilafiana katika mambo mawili yanayofungamana na Hijja ya mtoto mtambuzi. La kwanza, je huswihi Hijja ya mtoto huyo katika hali zote mbili, yaani anapohiji kwa idhini ya walii wake na hata asipoidhinishwa? Pili, lau atabaleghe muda mfupi tu kabla hajafikia kusimama Arafah, je itajuzu kwake kutekeleza Hijja ikiwa ni faradhi au hapana?

Maimamiyya, Mahanbali na Imam Shafi katika moja ya kauli zake mbili wamesema: "Idhini ya walii ni sharti la kuswihi ihram."

Abu Hanifa amesema: "Haisifiki Hijja ya mtoto kuwa ni sahihi, hata anapokuwa ni mtambuzi, sawa awe kapata idhini ya walii au hakupata idhini. Kwa sababu kusudio la Hijja hiyo ni kufanya mazoezi na si jingine." (*Fathul-Bariy*, *Al-Mughniy* na *at-Tadhkirah*).



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 255 2/1/2017 3:51:53 PM

Maimamiyya, Mahanbali na Mashafi wamesema: "Kama mtoto huyo anayehiji atabaleghe kabla hajasimama Arafah itatosha Hijja yake kuwa sahihi ya Uislamu."

Na Mahanafi na Maliki wamesema: "Kama atahirimia Hijja upya itatosheleza, la hakuhirimia tena basi haitatosheleza…" Na maana yake ni kuwa, itambidi kuanza Hijja upya. Angalia *At-Tadhkirah*.

**WAZIMU:**

Mwendawazimu si mahali pa kuwajibishwa, hivyo kama mwendawazimu atahiji na akaweza kuyatekeleza mambo yote yanayotakikana kutendwa na mwenye akili timamu awapo kwenye Hijja, Hijja hiyo haitatosha kuwa Hijja ya faradhi kama baadaye akili itamrudia. Lakini kama wazimu wake ni wa muda, ni wa kwenda na kurudi, na akawa amepata fahamu kwa kiasi cha muda unaotosha kutimiza Hijja yote kwa ukamilifu, kwa sehemu zake zote na masharti yake yote, hapo Hijja itakuwa ni wajibu juu yake. Na kama kiasi cha muda aliopata fahamu na akili hautoshi kutekeleza matendo yote kwa ukamilifu, hapo Hijja haitakuwa wajibu juu yake.

**KUWA NA UWEZO:**

Kuwa na uwezo ni sharti la wajibu wa Hijja kwa itifaki ya mafakihi wote, kufuatana na kauli ya Mwenyezi Mungu (s.w.t.) aliposema; "Kwa anayeweza kuenda njia hiyo. (*Al-Imran*: 97)

Kisha wamekhitilafiana kuhusu neno 'kuwa na uwezo' – *Istitwa'a* – na bila shaka ufumbuzi wake umepokewa kama ilivyokuja katika Hadith tukufu kwa maana ya kuwa na *Zadi* na *Rahilah*. Na neno *Rahilah* ni kinaya cha ujira wa safari na kwenda kutoka huko kwao hadi Makka, kisha kurudi kutoka Makka hadi kwao. Na neno *Zadi* ni neno lenye maana ya kuwa na kumiliki



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 256 2/1/2017 3:51:53 PM

mahitaji yake katika mali za kusafiria, kununulia chakula, kinywaji (maji) na kulipia nyumba kwa muda wote anaokuwa huko na gharama za kutayarisha nyenzo za usafiri, pasipoti na kadhalika. Na mengineyo yasiyokuwa hayo katika mambo yanayofungamana na hali yake na mweko wake wa kiafya, kwa sharti kwamba gharama zote hizo zitokane na mali iliyozidi baada ya kulipa madeni yake na kutimiza matumizi ya familia yake, pamoja na kukamilisha mambo yanayomlazimu katika kuendesha maisha yake kama kuwa na ardhi kwa ajili ya kilimo, kuwa na zana kwa mtu anayefanya kazi ya mkono. Na kuwa na rasilimali kwa mfanyabiashara. Yote haya iwe ni pamoja na kuwepo usalama wa nafsi, mali yake na heshima yake.

Katika haya yote hakuna aliyekhalifu wenzake isipokuwa Maliki, wao wamesema: "Yeyote anayeweza kwenda basi Hijja ni wajibu wake." Kama ambavyo pia wao hawakuhusisha matumizi ya watu wake wanaomtegemea na familia yake, bali waliwajibisha juu yake aviuze vyombo vyake vya mahitaji yake ya lazima katika maisha kama ardhi, wanyama na nyenzo zake za kufanyia kazi, si tu hata vitabu vyake vya elimu na nguo zake za kuvaa ili aende kuhiji. Angalia *Fiqh Alal Madhahabil Arbaa.*

Na kama mtu si wajibu juu yake kuhiji kutokana na kukosekana uwezo, lakini yeye akajipinda na kujikalifisha kwenda kuhiji, kisha baadaye akapata uwezo, je, itampasa arudie kuhiji au ile ya mwanzo itatosheleza faradhi?

Maliki na Mahanafi wamesema: "Itamtoshelezea wala haitamlazimu kuhiji tena apatapo uwezo." *(Fiqh Alal Madhahibil Arbaa)*.

Mahanbali wamesema: "Mtu anayeacha haki inayomlazimu kuitenda, kama vile kulipa deni, kisha akaenda kuhiji (kabla



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 257 2/1/2017 3:51:53 PM

ya hajalipa deni) Hijja hiyo itatosha kuwa Hijja ya faradhi." (*Manarussabil*, pia *Fathul Qadir* na *Fiqh Alal Madhahibil Arbaa)*.

Maimamiyya wamesema: "Kama mtu atajikalifisha kuhiji hali hana uwezo, Hijja hiyo haitatosha kuwa Hijja ya faradhi pindi atakapopata uwezo, kwani aliyewekewa sharti hana budi kufuata sharti alilowekewa katika hali zote mbili; katika hali ya kupata na kukosa, na alipokuwa hana uwezo hakuwa amewajibika. Hivyo ile Hijja yake ya kwanza itakuwa ni Sunna, na baadaye kwa kuwa uwezo kwake umethibiti ni wajibu kwake kwenda Hijja tena."

Kuharakisha:

Maimamiyya, Maliki na Mahanbali wamesema: "Kwa hakika wajibu wa Hijja ni jambo linalopasa kutekelezwa kwa haraka (maadamu uwezo umepatikana). Kamwe haijuzu kuchelewesha wajibu huo baada tu ya uwezo kupatikana, na kama mtu atachelewesha basi atakuwa bila shaka yoyote ameasi, lakini hata hivyo, Hijja yake huswihi, na itakuwa ni ya kutekeleza faradhi (si ya kukidhi) atakapojihi baadaye.

Mwenye kitabu kiitwacho *al-Jawahir* amesema: "Mradi wa neno kuharakisha, ni wajibu kufanya haraka kwenda Hijja katika mwanzo kabisa wa mwaka aliopata uwezo, na kama hatokwenda basi atakwenda mwaka unaofuatia huo… na kuendelea, lakini hapana shaka (kwa kitendo chake hicho) atakuwa ameasi kwa sababu ya kuichelewesha Hijja, ambapo alikuwa ana uwezo wa kwenda mnamo muda huo wa mwanzo wa uwezo wake, bila ya kuwa na uhakika wa kwenda Hijja baadaye (maana kifo hakina hodi)."

Mashafi wamesema: "Wajibu wa Hijja ni wa polepole si wa kujiharakisha, kwa maana ya kuwa inajuzu kuichelewesha Hijja hadi wakati mtu atakapo.[26]

---

[26] Kauli hii ingawa inasaidiwa na fani, kwani Hadith zinazosisitiza kuharakishwa Hijja zinahitaji kujadiliwa vyema, lakini ieleweke kuwa tendo hilo linapelekea kupuuza jambo



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 258 2/1/2017 3:51:53 PM

# TANZUO ZA KUWA NA UWEZO

## HIJJA YA MWANAMKE:

Je, katika Hijja ya mwanamke lipo sharti la ziada zaidi ya masharti ya Hijja ya wanaume?

Wameafikiana kuwa hapana sharti la kupatikana idhini ya mume kwa mke katika Hijja ya wajibu, na huyo mume naye si ruhusa kwake kumkataza mke kwenda Hijja. Kisha wamekhitilafiana kuhusu mwanamke ambaye hana mume na wala hana maharimu wake anayeweza kufuatana naye; je, ni wajibu kwa mwanamke huyo kwenda kuhiji au hapana?

Maimamiyya, Maliki na Mashafi wamesema: "Kuwa na maharimu au mume si sharti la wajibu wa Hijja kwa mwanamke. Katika hali yoyote iwayo, ni wajibu kwake kuhiji, sawa mwanamke huyo awe ni msichana au ni mzee, awe ameolewa au hajaolewa. Kwa kuwa huyo maharimu yake ni wasila tu wa kumuamanisha, si lengo halisi, hivyo ima atakuwa na usalama katika safari yake au si mwenye usalama; ama katika hali ya kwanza Hijja ni wajibu juu yake, wala hapana haja ya kupatikana maharimu. Na katika hali ya pili mwanamke huyo huzingatiwa kuwa hana uwezo wa kwenda Hijja (haitompasa kwenda hiji) hata kama anaye maharimu. Hivyo basi hapana tofauti yoyote kati ya mume na mke katika upande huu. Na kwa vyovyote iwavyo; uchambuzi kama huu na mingine mfano wake ulikuwa na uzito katika siku zilizopita ambapo safari ilikuwa ndefu na njiani kumejaa mambo ya kuhofisha usalama, ambapo ilibidi suala kama hili lijadiliwe, lakini sasa hivi suala kama hilo halina mfungamano wowote unaoweza kuleta mazao yenye maana,

lililo wajibu. Na si tu kupuuza, pia linahatarisha kutotekelezwa ibada hiyo, basi huko kufanya haraka katika kuhiji ni tendo linalofanya ihifadhiwe zaidi na pia ni kujitoa shakani katika kutekeleza dini.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 259 2/1/2017 3:51:53 PM

kwa sababu siku hizi za leo watu wote wana amani na usalama wa nafsi zao na mali zao popote pale wanapokwenda.

Mahanbali na Mahanafi wamesema: "Bila shaka kuwepo mume au maharimu (wa mwanamke) ni sharti la kuswihi Hijja kwa mwanamke, hata kama ni kikongwe, kamwe haijuzu kwake kuhiji bila ya kutimiza sharti hilo." Lakini Mahanafi wameweka sharti kwamba baina ya mahali anapoishi mwanamke na Makka kuwe na umbali wa siku tatu. Na sharti hili linatokea kwa nadra sana katika wakati wetu huu wa leo, hasa baada ya kuwepo usahali katika vyombo vya mawasiliano. Hili kama tulivyokwisha sema, tunaongeza kusema kuwa hapana haja ya kutela mjadala mrefu katika suala hili katika wakati wetu wa leo, kwani kuweka sharti la kuwepo maharim (wa mwanamke) hakuna maana yoyote ya kimsingi.

## HIJJA YA KUFADHILIWA:

Katika kitabu *Al-Mughni* cha madhehebu ya Mahanbali imeandikwa maneno haya: "Mtu anapotoa mali kumpa mtu mwingine ili kuendea Hijja si wajibu mtu huyo kukubali hiba hiyo, na wala hawi ni mwenye uwezo kwa fedha hizo alizopewa, sawa mtu aliyempa pesa hizo ni mtu wa kando au ni ndugu wa karibu, na sawa awe amemgharamia usafiri na matumizi yake au la."

Na imepokewa kutoka kwa Shafii kwamba mtu anapopewa pesa na mwanawe ambazo zinaweza kumpeleka Hijja basi itamlazimu aende, kwa kuwa amemudu kuweza kwenda Hijja pasi na masimango yatakayomlazimu wala aibu itakayompata.

Maimamiyya wamesema: "Anapopewa mali kwa njia ya zawadi bila ya kumpa sharti la kuwa aende Hijja, haitakuwa ni wajibu kwake kwenda Hijja kwa mali hiyo vyovyote atakavyokuwa huyo aliyempa, (sawa awe ni ndugu yake, mwanawe au mtu wa kando).



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 260 2/1/2017 3:51:53 PM

Na kama alimpa kwa sharti kwamba aende Hijja basi itamlazimu akubali kupokea na aende akahiji, hata kama huyo aliyempa alikuwa mtu wa kando, kwani huyo aliyepewa pesa huwa amekuwa na uwezo."

## KUOA:

Lau mtu atakuwa na mali inayomtosha kuolea mke tu au kuendea Hijja tu, je atangulize nini kati ya hayo mawili?

Katika kitabu *Fathul Qadir* Juzuu ya pili cha madhehebu ya Mahanafi mmeandikwa kuwa, kwa yakini Abu Hanifa aliulizwa kuhusu jambo hilo, akajibu kwa kusema, atangulize Hijja. Lakini kutoa jibu la kutanguliza Hijja pamoja na kuwa huko kuoa huwa ni wajibu (ni lazima) katika baadhi ya hali, kunatoa dalili ya kuonyesha kuwa haifai kuichelewesha Hijja.

Mashafi, Mahanbali na walio wahakiki katika Maimamiyya wamesema: "Atatanguliza kuoa kama itakuwa kuacha kuoa kutamsababishia kupata mashaka, kwa hiyo hatatanguliza kuhiji.' (*Kifayatul Akyar, Al Mughni na Urwatul Wuthqa)*.

## KHUMSI NA ZAKA:

Khumsi na Zaka vinaitangulia Hijja, wala hahesabiwi mtu kuwa ni mwenye uwezo wa kwenda Hijja isipokuwa baada ya kutekeleza utoaji wa haki hizo mbili, kikamilifu kama ilivyo madeni mengineyo.

## UWEZO WA GHAFLA:

Mtu anayekwenda kwenye mji ulio karibu na mji mtukufu wa Makka kwa lengo la biashara au jambo jinginelo, akakaa hapo hadi msimu wa Hijja ukaingia, na akawa ana uwezo wa kuifikia Baitul



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 261 2/1/2017 3:51:53 PM

Haram, basi muda huo huwa ni mwenye uwezo, na kama atarudi kwao alikotoka bila ya kutekeleza Hijja basi dhima itabaki kama ilivyo juu yake. Na mafakihi wote wamekubaliana katika hukmu hii.

# KUWEKA NAIBU

## VIGAWANYO VYA IBADA:

Ibada kwa kuzingatia mwili na mali zinagawanyika sehemu tatu:

**1.** Ibada za kimwili tu, ambazo ndani yake hazina athari yoyote ya mali, kama vile Swala na Swaumu. Maimamu wa madhehebu manne wamesema: "Aina hii ya ibada haikubali kutendwa kwa unaibu kwa hali yoyote iwayo, si kwa ajili ya maiti wala mtu aliye hai." Maimamiyya wamesema: "Hakubaliwa kwa ajili ya waliokufa tu, ama kwa mtu aliye hai haijuzu kwake kumweka naibu (badala) wa kumswalia Swala zake au kumfungia Swaumu kwa vyovyote vile."

**2.** Ibada za kimali tu, ambazo hazifungamani na mwili hata chembe, kama vile Khumsi na Zaka, aina hii ya ibada iko ruhusa ya kuweka naibu kwa itifaki ya wanavyuoni. Kwa hiyo inajuzu kwa mtu mwenye pesa kuweka mtu atakayemwakilisha kumtolea Zaka ya mali yake na sadaka nyinginezo.

**3.** Ibada zilizofungamana na mwili na mali pamoja, kama vile Hijja ambayo inahitaji vitendo kama vile kutufu, kwenda Saayi na kurusha vijiwe. Vilevile inahitaji pesa kwa ajili ya kulipia usafiri na mambo yote yanayomlazimu katika safari.

Na wanavyuoni wameafikiana kwa kauli moja kuwa, mtu aliye na uwezo wa kuhiji yeye mwenyewe na akawa ametimiza



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 262 2/1/2017 3:51:53 PM

masharti yote yanayohitajika, ni wajibu kuitekeleza Hijja hiyo yeye mwenyewe, kamwe haijuzu kuweka naibu muda huo, na kama atamweka mtu wa kumtekelezea basi haitaswihi, kwa hivyo itampasa kuhiji yeye binafsi, na kama hatofanya hivyo Mashafi, Mahanbali na Maimamiyya wamesema: "Haitamporomoka faradhi hiyo afapo, haswa kwa upande wa kimali, na hapo itakuwa ni wajibu aajiriwe mtu kwa ujira unaofaa kama hakuusia kutekelezewa Hijja, ujira huo utolewe kutoka katika mali halisi iliyoachwa na hayati."[27]

Mahanafi na Maliki wamesema: "Humporomoka wajibu wa Hijja kwa upande wa kimwili, lakini aliyekufa kama atakuwa aliusia akahijiwe basi itatolewa katika theluthi moja ya mali yake kama ilivyo katika sadaka nyinginezo, na kama hakuusia, si wajibu kuweka (kumwajiri) mtu wa kumhijia."

## MWENYE UWEZO KIMALI, ASIYEJIWEZA KIAFYA:

Mtu aliyekamilisha masharti ya Hijja kwa upande wa mali lakini hawezi kutekeleza Hijja yeye mwenyewe kwa sababu ya ukongwe au maradhi ambayo hayatazamiwi kupona, wajibu wa kwenda Hijja yeye mwenyewe binafsi humporomoka kwa itifaki (ya mafakihi), hiyo ni kutokana na kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema; "…wala hakuweka juu yenu mambo mazito katika dini…" ( Hajj:78).

Lakini je, ni wajibu kwake kumwajiri mtu wa kujihi kwa niaba yake, na kama hakufanya hivyo je, Hijja itabaki kuwa ni dhima juu yake kwa kuwa ameacha kutekeleza wajibu?

Mafakihi wote, isipokuwa Maliki, wameafikiana kuwa: "Ni wajibu kwake kuajiri mtu atakayemuhijia." Maliki wamesema: "Hijja si wajibu ila kwa mtu anayeweza kwenda yeye mwenyewe binafsi." (*Al-Mughni* na *at-Tadhikrah*).

---

[27] Imamiyya, Maliki na Shafii wamejuzisha kuajiri kwa ajili ya Hijja, lakini Hanafi na Hambali wamekataza.

Na kama atapona huyu, na baada ya kwishakumuajiri atakayemwakilisha katika Hijja, udhuru wake ukamuondokea, je ni wajibu kwake kuhiji tena yeye mwenyewe? Mahanbali wamesema: "Si wajibu juu yake Hijja nyingine." Maimamiyya, Mashafi na Mahanafi wamesema: "Ni wajibu, kwa sabau aliyofanya mwanzo ilikuwa ni kutekeleza wajibu wa upande wa mali yake, na hii ya sasa ni wajibu wa upande wa mwili wake."[28]

## KUWEKA NAIBU KATIKA HIJJA YA SUNNA:

Mahanafi na Maimamiyya wamesema: "Anayetekeleza wajibu uliomlazimu wa Hijja ya Uislamu, kisha akapenda kumpa unaibu mtu wa kwenda kuhiji Hijja ya Sunna badala yake, anayo ruhusa ya kufanya hivyo hata kama anao uwezo wa kwenda yeye mwenyewe binafsi."

Mashafi wamesema: "Haijuzu."

Imam Ahmad bin Hanbali ana mapokezi mawili ya kukataza na kujuzisha.

Maliki wamesema: "Hujuzu kwa mgonjwa ambaye maradhi yake hayatarajiwi kupona, na kwa mtu aliyekwishahiji Hijja ya faradhi ya Uislamu, kumwajiri mtu mwingine kwenda Hijja, na Hijja hiyo itakuwa ni yake (mwajiri), lakini kufanya hivyo ni makruhu. Wala haiandikwi kuwa ni Hijja ya aliyeajiriwa bali huwa ni Hijja ya Sunna ya mwajiri, na mwajiriwa hupata thawabu za kumsaidia (mwajiri) katika kuhiji, aidha hupata baraka za dua (alizoomba huko). Na mtu atakwenda kumhijia marehemu aliyeusia au hata ambaye hakuusia, basi mwajiriwa haandikiwi thawabu yoyote si katika Hijja ya faradhi wala ya Sunna. Wala kamwe faradhi ya Hijja ya Uislamu haimwondoki." (*Fiqh Alal Madhahibil Arbaa).*

---

[28] Kauli hii inawafikiana na ya Sayid Al-Khui katika kitabu chake kiitwacho *Al-Mansak.*



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 264 2/1/2017 3:51:53 PM

## MASHARTI YA NAIBU:

Ni sharti naibu awe ni mtu aliye baleghe, awe ni mwislamu, awe ni mwenye akili timamu, tena awe amekwishatekeleza Hijja yake ya wajibu, pia anayeaminika kuwa ataitekeleza. Na inajuzu mwanamume kuwa naibu wa mwanamke, na mwanamke kuwa naibu wa mwanamume hata ijapokuwa wote wawili aliyewekwa naibu na mweka naibu hawajawahi kuhiji. (*Swarura*).[29]

Je naibu huyo ataanzia safari yake ya kwenda Hijja katika mji wake au ataanzia mji wa maiti, na au ataanzia katika mojawapo ya vituo vya kuhirimia Hijja? Mahanafi na Maliki wamesema: "Ataanzia safari yake ya Hijja kuanzia mji wa maiti kama aliyemuweka naibu hakumchagulia mahali maalum, la kama alimtaka aanzie mahali maalum basi atafuata kauli yake."

Mashafi wamesema: "Kipimo ni *Miqat,* kama mwajiri atamwainishia *Miqat* maalumu basi mwajiriwa atalazimika kutenda kufuatana na kauli yake (muajiri), la kama hakumwainishia *Miqat* maalum basi aliyeajiriwa atajichagulia popote atakapo."

Mahanbali wamesema: "Ni wajibu ahiji kwa kuanzia safari mahali ulipompatia marehemu wajibu wa kwenda Hijja, si kuanzia katika mji aliofia, hivyo kama uwezo aliupata akiwa alikohamia, kisha baadaye alirudi katika mji wake na akafia katika mji wake, basi atawekewa naibu ambaye ataanzia safari kutoka kule alikohamia, na si kuanzia katika mji wake, ila tu kama kati ya mji wake na alikohamia kuna umbali usioruhusu kukusuru Swala."

Maimamiyya wamesema: "Hijja ina sehemu mbili za kuikusudia, miongoni mwake ni inayoitwa *Baladiya,* ambayo huanzia kwenye mji wa marehemu. Na nyingine inaitwa *Miqatiya* ambayo huanzia

[29] Swarura ni mtu ambaye bado hajaenda kuhiji, na Shafi na Hanbali wamesema: "Huyo Swarura anapokwenda kuhiji kwa niaba ya mtu mwingine, basi Hijja hiyo huwa yake." Maliki, Hanafi na Imamiyya wamesema: "Hapa Hijja hufuata alivyonuia."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 265 2/1/2017 3:51:53 PM

kwenye *Miqat*. Basi iwapo mtu atachagua mojawapo kati ya njia hizo mbili itafaa, na kama atasema ianziwe kwenye *Miqa*t bila kubainisha ni *Miqat* gani, basi kama upo uwezekano wa kufuata mojawapo kuurahisi atafuata, na kama haiwezekani basi Hijja hiyo itakuwa ya *Miqat*, naye atamuhijia kulingana na *Miqat* iliyo karibu zaidi na Makka kama litawezekana hilo. La kama ni zito kwake basi atahirimia kuanzia *Miqat* iliyo karibu na mji wa maiti. Na ujira wa kwenda *Miqat* katika Hijja ya wajibu utachukuliwa katika mali halisi iliyoachwa na marehemu, na ujira wa baada ya Miqat utachukuliwa kutoka katika theluthi." (*Al-Jawahir*).

## NAIBU KUCHELEWA:

Mtu anapoajiriwa (katika Hijja) basi anawajibika kutekeleza haraka, wala haijuzu kwake kuichelewesha Hijja hadi akaitoa nje ya mwaka huo (alioajiriwa), wala haruhusiwi mwajiriwa kuweka naibu katika kutekeleza Hijja aliyoajiriwa yeye, kwa sababu kitendo hicho (cha Hijja) huwa amekabidhiwa yeye. Na iwapo hatutajua kuwa mwajiriwa amekwenda kuhiji na akawa anafanya kazi zake za kawaida (nyumbani) basi tutachukulia kuwa hakuenda Hijja, (tutaamini hivyo) hadi itakapothibiti kinyume chake. Na tunapojua kuwa alikwenda Hijja na akatekeleza matendo yote kwa ujumla, lakini tukaingiwa na shaka ya kuwa, je ameyatekeleza matendo yake kwa usahihi kama inavyotakikana au amebadilisha kitu katika matendo ya wajibu; tutachukulia kuwa ametenda yote kwa usahihi, hadi itakapodhihiri kinyume cha hivyo.

## KUGHAIRI:

Mahanafi na Maimamiyya wamesema: "Mtu anapomchagua mtu wa kuwa naibu wake katika Hijja, kama vile Hijja ya Tamattui au ya Ifrad au ya Qiran, basi si ruhusa kwa mwajiriwa kubadili aina ya Hijja.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 266 2/1/2017 3:51:54 PM

Ama atakapoainishiwa kuwa aanzie Hijja kutoka mji fulani maalum, lakini yeye akaanzia mji mwingine, ikiwa hakufanya hivyo kwa malengo yake, Hijja hiyo itatosheleza, kwa maana kufuata njia maalum kwa hakika halikuwa ndilo lengo hasa, lakini lengo lake lilikuwa ni kutekelezwa Hijja, na ukweli ni kuwa imeshatekelezwa." (Tazama *Fiqh Alal Madhahibil Arbaa)*.

# UMRA

**Maana yake:** Maana ya Umra kilugha ni kufanya ziyara yoyote kwa jumla. Ama kisheria ni kuizuru nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu kwa namna maalum.

## VIGAWANYO VYAKE:

Umra hugawanyika katika sehemu mbili: Ya kwanza ni ile isiyoambatana na Hijja, hii wakati wake ni siku yoyote katika mwaka mzima, hii ni kwa itifaki ya mafakihi wote, na wakati bora wa kufanya Umra hiyo kwa madhehebu ya Imamiyya ni mwezi wa Rajab. Ama kwa wasiokuwa wao ni mwezi wa Ramadhani.

Ama ya pili ni ile inayoambatana na Hijja, ambapo mwenye kufanya ibada ya Hijja, katika safari yake hiyo hiyo moja, ataanza kwanza kufanya Umra ndipo afanye ibada ya Hijja, kama wanavyofanya mahujaji wanaoishi nchi za mbali na mji wa Makka tukufu. Na wakati wake ni ndani ya miezi ya Hijja, nayo ni mwezi wa Shawwal (mfungo mosi), Dhulqaada (mfungo pili) na Dhulhijja (mfungo tatu), hii ni kwa itifaki ya mafakihi pamoja na kuwepo tofauti kati yao kuhusu mwezi wa Dhulhijja, je wote kamili ni miongoni mwa miezi ya Hijja au ni kumi la mwanzo pekee?

Na kama mtu atafanya Umra inayoambatana na Hijja basi utakuwa umemwondoka wajibu wa kufanya Umra isiyoambatana na Hijja, hii ni kwa yule anayeona kuwa ni wajibu kufanya Umra.

**TAFAUTI ILIYOPO KATI YA UMRA MBILI:**

Sayyid al-Khui amezitenganisha Umra *Mufrada* (isiyoambatana na Hijja) na Umra *Tamattui* (inayoambatana na Hijja) kwa mambo kadhaa yanayofuata:

**1.** Kwa yakini Twawafu ya kuhalalisha tendo la ndoa (Twawafu Nisaa) ni wajibu katika Umra isiyoambatana na Hijja (Mufrada), lakini si wajibu katika Umra inayoambatana na Hijja (*Tamattui)*, wengine wamesema: "Hakuna kabisa sharia ya kuifanya."

**2.** Kwa hakika Umra inayoambatana na Hijja (*Tamattui)* wakati wake huanzia mwanzo wa mwezi wa Shawwal, mpaka tarehe tisa ya mwezi wa Dhulhijja. Ama Umra isiyoambatana na Hijja (*Mufrada*) wakati wake ni katika mwaka mzima (siku yoyote ile).

**3.** Mtu aliyefanya Umra *Tamattui* hulazimika kupunguza tu nywele ili kujihalalishia yote yale aliyojiharamishia kwa ihram. Ama aliyefanya Umra *Mufrada* ana hiyari kati ya kupunguza nywele na kunyoa. Maelezo yake yatakuja.

**4.** Kwa uhakika Umra *Tamattui* na Hijja hutakiwa vyote viwili vifanyike katika mwaka mmoja, lakini haiwi hivyo katika Umra ya *Mufrada*.

Katika kitabu kiitwacho *Ad-Dini Walhajj* kilichokusanya madhehebu manne imeandikwa: Kuna uhakika wa kuwa Maliki



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 268 2/1/2017 3:51:54 PM

na Mashafi wamesema: “Kwa yakini mwenye Umra *Mufrada* ni halali kwake kila kitu, hata kujamiiana, atakaponyoa au kupunguza nywele, kama tu hakumswaga mnyama wa sadaka ya Hijja, kinyume na hivyo ataendelea kuwa katika masharti ya ihram mpaka atakapojitoa katika Hijja na Umra pamoja, katika siku ya kuchinja.

## MASHARTI YAKE

Huko nyuma tumetangulia kutaja masharti ya Hijja. Na yote tuliyoyataja katika masharti ya Hijja ndiyo pia masharti ya Umra.

## HUKUMU YAKE:

Mahanafi na Maliki wamesema: “Umra ni Sunna iliyotiliwa mkazo, si faradhi.”

Mashafi, Mahanbali na mafakihi wengi wa madhehebu ya Imamiyya wamesema: “Umra ni faradhi kwa mtu mwenye uwezo wa kwenda, hiyo ni kwa mujibu wa kauli yake Mwenyezi Mungu (s.w.t.) aliposema; “Na timizeni Hijja ya Umra kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, (Suratul Baqarah: 196).

Lakini huwa Sunna kwa asiyekuwa na uwezo, Tazama kitabu *Fiqhus-Sunna* Juzuu ya 5, na kitabu *Fiqh Alal Madhehebil Arbaa*, na *Jawahir* na *Al-Mughni*).[30]

Katika kitabu *Fiqh Alal Madhahibil Arbaa* imeandikwa: “Ni wajibu katika Umra yaleyale ambayo ni wajibu katika Hijja, aidha yaliyosuniwa katika Hijja ndiyo yaliyosunniwa katika Umra. Lakini Umra inatofautiana na Hijja katika mambo kadhaa, na miongoni

[30] Katika kitabu *Al-Mughni* imepokewa kuwa Ahmad bin Hanbal amesema kuwa, wakazi wa Makka hawalazimiki kwenda Umra, kwa sababu lililo kubwa katika matendo ya Umra ni kutufu Al-Kaaba, nao hufanya hivyo, kwa hivyo kutufu kwao huko hutosheleza badala ya Umra.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 269 2/1/2017 3:51:54 PM

mwake ni kuwa, hiyo Umra haina wakati wake maalumu, na wala haupiti. Pia anayefanya Umra halazimiki kwenda kusimama Arafah, hashuki Muzdalifa na wala hatupi vijiwe.[31]

Katika kitabu cha madhehebu ya Imamiyya kiitwacho *Al-Jawahir* mmeandikwa hivi: "Yaliyo wajibu katika matendo ya Hijja ni mambo kumi na mawili: Ihram, kusimama Arafah, kusimama Muzdalifa, kushuka Mina, kutupa vijiwe, kuchinja, kunyoa, kupunguza nywele, kutufu pamoja na kuswali rakaa mbili za kutufu, kusai na kutufu Twawafu Nisaa pamoja na rakaa zake mbili.........Na matendo ya wajibu ya Umra isiyoambatana na Hijja (*Mufrada*) ni manane: Kutia nia, kuhirimia[32] Umra, kutufu pamoja na rakaa zake mbili, kusai, kupunguza nywele na Twawafu Nisaa pamoja na rakaa zake mbli."

Kutokana na maelezo haya inatudhihirikia kuwa mafakihi wameafikiana wote kwa jumla kuwa matendo ya Hijja ni mengi zaidi kuliko ya Umra, yakiongezeka kuanzia kwenye kusimama Arafah na matendo yanayoandamana na kisimamo hicho. Isipokuwa Maimamiyya wamewajibisha kwa mwenye kwenda Umra Mufrada kutufu tena Twawafu Nisaa, kama ambavyo Imam Malik amewakhalifu wenzake wote kwa kusema kuwa si wajibu kunyoa wala kupunguza nywele katika Umra Mufrada.

---

31 Kitabu *Fiqh Alal Madhahibil Arbaa* kimetungwa katika jumuiko mbili: Asili ya kitabu, na *Taaliq* (maelezo ya ziyada) na ni kawaida ya mtunzi wa kitabu hicho kueleza hukmu waliyowafikiana maimamu wanne, na katika maelezo yaliyo chini ya msitari (kama haya unayoyasoma ) hueleza hukmu waliyotofautiana ndani yake, kwa kuelezea kiini cha madai ya kila madhehebu miongoni mwa madhehebu hayo manne kadiri wanavyoona mafakihi wao. Na haya tuliyoyanukuu hapo juu yanatoka katika asili ya kitabu hayakutoka kwenye *Taaliq*.

32 Imekuja katika kitabu A*ddini Walhajj Alal Madhahibul Arbaa,* kwamba tofauti ya Umra na Hijja ni kuwa sehemu ya kuhirimia na mwanzo wa eneo huru, hiyo ni kwa mkaazi wa Makka na wingine, si katika Miqat za Hijja. Na hakuna tofauti kwa Imamiyya baina ya Miqat ya mwenye kufanya Umra na ya mwenye kuhijji kulingana na Ihram.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 270 2/1/2017 3:51:54 PM

**TANZUO MBILI:**

Ya kwanza: Kwa hakika wajibu wa kufanya Umra Mufrada haufungamani na kuwa na uwezo wa kwenda kuhiji, kama atakuwa na uwezo wa Umra tu, kwa mfano lau itathibiti kwa mtu fulani alipata uwezo wa kwenda hadi Makka katika siku zisizokuwa za Hijja, na wala hana uwezo wa kwenda Makka katika msimu wa Hijja, itakuwa ni wajibu kwake kwenda Umra na si Hijja, na kama atakufa kabla ya kuitekeleza Umra basi gharama ya kumweka mtu wa kumtekelezea itatolewa kutoka katika mali aliyoiacha."[33]

Vilevile kama itathibitika kwa mtu fulani kuwa anaweza kwenda Hijja isiyoambatana na Umra (Mufrada) ni wajibu kwake kwenda kuhiji, kwa sababu kila moja kati ya hizo mbili ni ibada kamili isiyotegemea nyingine, na hii ni sawa na Umra isiyoambatana na Hijja (Mufrada). Ama Umra Tamattui (inayoambatana na Hijja) wajibu wake unategemea wajibu wa Hijja, kwa sababu Umra Tamattui imo ndani ya Hijja.

Tanzo la pili: Maimamiyya wamesema: "Haijuzu kwa mtu anayetaka kuingia Makka kuvuka *Miqat* wala kuingia kwenye haram yake tukufu ila awe amehirimia (Hijja au Umra) hata kama alikuwa hapo mbeleni alikwishahiji au kufanya Umra mara nyingi kiasi gani, isipokuwa tu kama atakuwa mwenye kurudiarudia kuingia na kutoka katika mwezi huo huo, kwa maana kama ataingia katika mji wa Makka baada ya kuhirimia kisha akatoka, halafu akaingia tena kabla

[33] Kwenye kitabu *Al-Madarik* katika madhehebu ya Imamiyya amesema: "Hii ndiyo kauli iliyo mashuhuri zaidi miongoni mwa kauli zao na iliyo nzuri zaidi, yaani kutosheleza kupasa Umra badala ya Hijja. Na mwenye kitabu *Al-Jawahiri* amesema: "Kwa hakika maneno ya mafakihi hayatoki nje ya kuwa ni yenye tashwish (wasiwasi)… kisha akaendelea kusema: "Jambo ambalo linaweza kupewa mtazamo wenye nguvu ni kupomoka wajibu wa Umra kwa mtu anayeishi mbali na Makka, na kwamba iliyo wajibu kwake ni Umra ya *Tamattui* ambayo kupasa kwake kunafungamana na kupasa kwa Hijja.' Na Sayyid al-Hakim amesema: Kauli iliyo karibu zaidi ni kutopasa Umra m*ufrada*. Na Sayyid Khui amesema: "Haiko mbali na kuwa haipasi."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 271 2/1/2017 3:51:54 PM

ya kupita siku thelathini, basi haitakuwa wajibu kwake kuhirimia tena akitaka kuingia tena, kinyume na hivyo itakuwa ni wajibu kwake kuhirimia. Hivyo kuhirimia kwa mtu anayeingia Makka kuna uzito sawa na wudhu kwa mtu anayetaka kugusa msahafu."

Kwa maelezo hayo unabainika uzushi wa wale wanaosema kuwa Shia hawaitukuzi Baitul Haram (Al-Ka'aba), na kwamba kuhiji kwao ni kwa lengo la kuvichafua vituo vitakatifu …" Ametakasika Mwenyezi Mungu na wametakasika na madai watu hawa wanaoitukuza misingi ya ibada iliyowekwa na Mwenyezi Mungu mwenyewe, wafuasi wanaomfuata Mtume ﷺ na Ahlulbayti wake, kwa hakika huo ni uzushi mkubwa.

Abu Hanifa amesema: "Haijuzu kwa mtu aliye nyuma ya *Miqat* kuingia ndani ya Haram takatifu ila baada ya kuhirimia. Ama kwa walio kinyume na mtu kama huyo, basi hujuzu kwao kuingia bila ya kuhirimia."

Imam Malik yeye hakuona kama hivyo (yaani, hakuchangia kitu hapo). Na Imam Shafi yeye ana kauli mbili.

Na tutosheke na kiasi hiki cha maneno tuliyoelezea kuhusu ibada ya Umra, kwani lengo letu hasa lilikuwa ni kuwaangazia tu juu ya ibada hiyo ya Hijja ijapokuwa ni katika baadhi ya sehemu zake tu. Na bila shaka zitazidi kueleweka habari na tofauti zake katika maelezo yatakayofuatia.

## AINA ZA HIJJA

Mafakihi wa madhehebu yote wameafikiana kuwa Hijja ziko za aina tatu: *Tamattui*, [34]*Qiran* na *Ifrad*. Aidha wameafikiana kuwa maana

[34] Lakini Umar bin al-Khattab alikataza Hijja ya *Tamattui*, akatilia mkazo katika Hijja mbili tu ya *Qiran* na *Ifrad*, akasema; "Muta mbili zilikuwepo wakati wa uhai wa Mtume ﷺ na mimi naziharamisha Muta zote mbili, na nitamuadhibu



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 272 2/1/2017 3:51:54 PM

ya *Tamattui* ni kuanza kufanya matendo ya Umra ndani ya miezi ya Hijja na baada ya kumaliza matendo ya Umra ndipo afanye matendo ya Hijja.

Vilevile wameafikiana kuwa Hijja ya *Ifrad,* ni kwanza mtu ahijji, baada ya kumaliza vitendo vya Hijja ndio ahirimie Umra na afanye matendo yake.

Na maimamu wa madhehebu manne wameafikiana kuwa maana ya *Qiran* ni kuhirimia Hijja pamoja na Umra kwa wakati mmoja kwa kusema anayehijji "*Labbaika Allahumaa Bil hajji wa Umra."*

Maimamiyya wamesema: "Kwa yakini *Qiran* na *Ifrad* zote ni kitu kimoja, havitengani isipokuwa katika jambo moja, nalo ni kuwa anayehiji *Qiran* hupeleka mnyama wakati wa kuhirimia kwake, ambapo hulazimika amchinje mnyama aliyempeleka, ama anayekwenda kuhiji Hijja ya *Ifrad* hatalazimika kuchinja mnyama." Na kwa neno jingine, Maimamiyya kwa hakika hawajuzishi kuingiliana kati ya Ihram mbili[35] wala haijuzu kuleta Hijja na Umra kwa nia moja kwa hali yoyote ile iwayo. Na hilo limejuzishwa na wasiokuwa wao katika Hijja ya Qiran wakasema: "Kwa hakika Hijja hiyo imeitwa hivyo hivyo kwa sababu mna kukusanya Hijja na Umra kwa wakati mmoja."

Maimamiyya wamesema: "Hapana si kwa maana hiyo, bali kwa sababu imeongezeka kumswaga mnyama baada ya kuhirimia."[36]

---

atakayezifanya …" Alikusudia Muta ya wanawake (ambayo ni ndoa ya muda) na Muta ya Hijja yaani Hijja ya *Tamattui*. Wakamtolea kisingizio baadhi ya wanavyuoni wa kisunni cha yeye kufanya hivyo, kuwa alitaka nyumba takatifu 'Baitul Haram' isiwe tupu kwa kukosa wenye kuzuru katika miezi isiyokuwa ya Hijja. Angalia kitabu *Ahkamul Qur'ani* cha Jassas Juzuu ya kwanza mlango unaoelezea *Tamattui Bil Umra Ilalhajj*.

[35] Imepokewa katika kitabu al-Jawahir na al-Madarik na al-Hadaiq kwamba, haijuzu kwa mtu aliye katika ihramu kuanzisha ihramu nyingine, mpaka pale atakapomaliza matendo ya ihramu ya kwanza aliyohirimia.

[36] Ibn aqil wa Shia amejitenga na kuafikiana na wanavyuoni wa Sunni kwamba Qiran ni kukusanya baina ya Umra na Hajj katika Ihram moja.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 273 2/1/2017 3:51:54 PM

Mafakihi wa madhehebu manne wamesema: "Hujuzu kwa mtu yeyote awaye, awe wa Makka au asiyekuwa wa Makka, kujichagulia namna yoyote ya Hijja anayoitaka kati ya aina tatu za Hijja. *Tamattui*, *Qiran* na *Ifrad* pasi na kuwepo karaha yoyote. Isipokuwa Abu Hanifa amesema: "Ni makruhu kwa mkaazi wa Makka kufanya Hijja *Tamattui* na *Qiran*."

Kisha hao mafakihi wa madhehebu manne wametofautiana kuhusu ni ipi iliyo bora kati ya Hijja tatu hizi. Mashafi wamesema: "*Ifrad* na *Tamattui* ni bora zaidi kuliko *Qiran."* Mahanafi wamesema: "*Qiran* ni bora zaidi kuliko hizo mbili." Mahanbali na Maimamiyya wamesema: "*Tamattui* ndiyo iliyo bora zaidi." (Tazama Kitabu *Fiqh Alal Madhahibil Arbaa, al-Mughni, Mizan sha'arani na Fiqhs Sunnah,* Juzuu ya tano).

Maimamiyya wamesema: "Kwa hakika Hijja *Tamattui* huwa ni faradhi kwa mtu aliye mbali na Makka kwa kadiri ya maili arobaini na nane,[37] haijuzu kwake kuhiji aina nyingine isipokuwa kama ana dharura. Ama *Qiran* na *Ifrad* hizo mbili ni faradhi kwa wakazi wa Makka na kwa ambaye anaishi kati yake na Makka kwa kiasi cha umbali ulio chini ya maili arobaini na nane, na kwao nao haijuzu kwao aina nyingine zaidi ya aina hizi mbili. Wanaodai hivyo walitoa dalili ya kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu aliposema***:***

"..... فَإِذَآ أَمِنتُمۡ فَمَن تَمَتَّعَ بِٱلۡعُمۡرَةِ إِلَى ٱلۡحَجِّ فَمَا ٱسۡتَيۡسَرَ مِنَ ٱلۡهَدۡيِۚ فَمَن لَّمۡ يَجِدۡ فَصِيَامُ ثَلَٰثَةِ أَيَّامٖ فِي ٱلۡحَجِّ وَسَبۡعَةٍ إِذَا رَجَعۡتُمۡۗ تِلۡكَ عَشَرَةٞ كَامِلَةٞۗ ذَٰلِكَ لِمَن لَّمۡ يَكُنۡ أَهۡلُهُۥ حَاضِرِي ٱلۡمَسۡجِدِ ٱلۡحَرَامِ ....."

**"Basi mwenye kujistarehesha kwa kufanya Umra kisha ndio akahiji, basi achinje mnyama aliye sahali kumpata (naye ni mbuzi). Na**

[37] Sayyid Al-Hakim pia alifuata kauli hiyo. Sayyid Khui amesema: "Ni kiasi cha Farasakhi kumi na sita." Baadhi yao wakasema: "Ni maili kumi na mbili."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 274 2/1/2017 3:51:54 PM

**asiyepata afunge siku tatu katika Hijja na siku saba mtakaporudi (kwenu); hizi ni (siku) kumi kamili. Hayo ni kwa ajili ya yule ambaye watu wake hawako karibu na msikiti mtakatifu wa Makka." (al-Baqarah 2:196).**

Maimamiyya wamesema tena kuwa haifai kwa mtu anayelazimika kuhiji Hijja *Tamattui* kubadilisha aina nyingine ya Hijja, isipokuwa kama atazongwa na wakati au anapozukiwa na damu ya hedhi (kama ni mwanamke), hapo ndio anaweza akabadilisha kwenda kwenye *Qiran* au *Ifrad*, baada ya kuhiji ndio afanye Umra. Na upeo wa kuzongwa na wakati ni kutomakinika kwenda Arafah baada ya kupinduka jua.

Na hukumu ni kama hiyo hiyo haijuzu kuhiji kinyume chake kwa mtu ambaye anawajibika kufanya Hijja ya *Qiran* au *Ifrad* kama ilivyo kwa watu wa Makka na vipembe vyake, haijuzu kwake kuhiji kwa njia ya *Tamattui* isipokuwa anapolazimika kufanya hivyo, kama anapohofia kuzukiwa na damu ya hedhi (kama ni mwanamke). Mwenye kitabu *Al-Jawahir* baada ya kwisha kunukuu maneno hayo alisema: "Haya nimeyakuta bila ya kuwepo ikhtilafu."

Na wote waliafikiana kuwa mtu anayehiji Hijja ya *Ifrad* halazimiki kuchinja mnyama, lakini kama mwenyewe atachinja kwa kupenda kwake basi kufanya hivyo ni kheri kwake.

# VITUO VYA KUHIRIMIA (MIQAT)

## MIQAT (VITUO):

Hapana budi kwa Umra na Hijja kwa aina zake zote, kuanza kwa kuhirimia, nako ni nguzo miongoni mwa nguzo zake kwa mujibu wa madhehebu ya Imamiyya, na kwa wengineo ni wajibu. Na wameafikiana kwa kauli moja kuwa kituo cha kuhirimia Hijja (Miqat) kwa



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 275 2/1/2017 3:51:54 PM

watu wa Madina, ambacho wanatakiwa kuanzia Hijja (kuhirimia) ni Masjidus Shajarah, ambapo pia huitwa Dhulhalifa. Na kituo cha kuhirimia Hijja (Miqat) cha watu wa Sham, Misri na Moroco ni Juhfa.[38] Na kituo cha kuhirimia Hijja (Miqat) cha wakazi wa Iraq ni Aqiq. Na wakazi wa Yemen kituo chao pamoja na watu wanaopita njia yao ni Yalamlam.

Maimamiyya wamesema: "Qarn ni kituo cha kuhirimia Hijja (Miqat) cha wakazi wa Twaif. Na kila apitaye njia hiyo ya Twaif wakati akienda Makka." Mafakihi wa madhehebu manne wamesema: "Hata, hapo Qarn ni kituo cha wakazi wa Najd." Maimamiyya wamesema: "Kituo cha wakazi wa Najd, na kituo cha wakazi wa Iraq ni Aqiq."

Kama ambavyo wameafikiana kuwa vituo hivyo ni kwa wakazi wa nchi na miji iliyotajwa hapo nyuma, ndivyo wameafikiana kuwa hivyo pia ndio vituo vya kila anayepita humo miongoni mwa wale wanaokwenda Hijja, hata kama mtu huyo si katika wakazi wa sehemu hizo. Hivyo kama mtu wa Sham atataka kwenda kuhiji kutokea mji wa Madina, akapitia Dhulhalifa basi atahirimia kutokea hapo. Na kama atapitia Yemen basi kituo chake kitakuwa Yalamlam, na kama ni kutokea Iraq itakuwa Aqiq, na kuendelea kama hivyo. Na ambaye hatapita kwenye vituo hivyo basi kituo chake kitakuwa mahali ambapo patakuwa pameelekeana na chochote kati ya vituo hivyo.

Na mtu ambaye nyumba yake iko karibu sana na Makka kuliko vituo hivyo (Miqat) basi kituo chake ni nyumba yake, hapo ndipo atakapohirimia. Na ambaye nyumba yake iko ndani ya Makka

[38] Waliokusudiwa hapo ni wakazi wa Syria, Lebanon, Palestina na Jordan. Hata hivyo kwa sasa hivi njia zimebadilika. Sayyid Al-Hakim amesema: "Bila shaka msafiri anayesafiri kwa ndege haimpasi kuhirimia muda ndege ipitapo juu ya Miqat na inaposhuka Jiddah atahirimia kuanzia Hudaibiyya. Pia anaweza akahirimia kuanzia Jiddah kama atalazimika."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 276 2/1/2017 3:51:54 PM

basi kituo chake (Miqat) ni hiyo Makka yenyewe hasa. Na kwa madhehebu ya Imamiyya vituo vya mwenye kwenda Umra *Mufrad* ni hivyo hivyo vya anayekwenda Hijja.

## KUHIRIMIA KABLA YA KUFIKA KWENYE KITUO (MIQAT):

Maimamu wa madhehebu manne wameafikiana kuwa hujuzu kuhirimia kabla ya kufikia kwenye kituo (Miqat), kisha wakatofautiana rai kuhusu ni njia gani iliyo bora zaidi. Malik na Ibn Hanbal wamesema: 'Iliyo bora ni kuhirimia kwenye kituo (Miqat)." Abu Hanifa amesema: "Njia iliyo bora ni kuhirimia kutoka mjini kwake." Shafii ana kauli mbili.

Maimamiyya wamesema: "Haijuzu kuhirimia kabla ya kufikia kwenye kituo (Miqat) isipokuwa kwa mtu aliyekusudia kwenda kufanya Umra ndani ya mwezi wa Rajab, akawa anahofia kumalizika muda kama atangojea hadi afike kwenye kituo (Miqat) ndio ahirimie, na pia kwa aliyeweka nadhiri ya kuhirimia kabla ya kufika kwenye kituo (Miqat)".[39] (Tazama kitabu *At-tadhkirah* na *Fiqhus-Sunna*).

## KUHIRIMIA BAADA YA KUVUKA KITUO (MIQAT):

Mafakihi wa madhehebu yote wameafikiana kuwa; haijuzu kuvuka kituo (Miqat) bila ya kuhirimia, na kama atavuka bila ya kuhirimia itampasa arejee hadi kwenye Miqat akahirimie hapo.

Maimamu wanne wamesema: "Kama hatarejea kituoni hapo kuhirimia, Hijja yake itaswihi, lakini atalazimika kuchinja mnyama. Hata hivyo hupata dhambi kama hakuwa na sababu yoyote ya kumzuia kurudia kwenye kituo (Miqat), lakini kama itapatikana

---

39 Sayyid Al-Hakim na Sayyid Khui wamejuzisha kuweka nadhiri ya kuhirimia kabla ya kufikia Miqat.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 277 2/1/2017 3:51:54 PM

sababu ya kumzuia kurudi kama kuhofia hatari njiani au wakati kubana, hatakuwa na dhambi, na hakuna tafauti katika hukmu hiyo kati ya kuwa mbele yake kuna vituo vingine vya kuhirimia katika njia anayopita au hakuna."

Maimamiyya wamesema: "Mtu anayeacha kuhirimia kwenye kituo (Miqat) kwa makusudi hali ya kuwa amedhamiria kuhiji au kufanya Umra, kisha asirudi kwenye kituo hicho, na mbele yake hakuna kituo kingine kisichokuwa hicho alichokiacha, basi kuhirimia kwake na Hijja yake vitabatilika, na hukmu inabaki hivyo sawa awe alikuwa na udhuru au la."

Na kama aliacha kwa kusahau au kwa kutojua na uwezekano wa kurejea anao atatakiwa kurejea. Na kama haiwezekani kurejea basi atahirimia kwenye kituo (Miqat) kilicho mbele yake, na kama hakuna kituo (Miqat) kingine mbele yake basi atahirimia katika umbali unaowezekana nje ya Haram takatifu au ndani yake, akitanguliza uwezekano wa kwanza kabla ya wa pili, (kitabu *At-Tadhikirah,* na *Fiqh Alal Madhahabil Arbaa*).

**Kuhirimia kabla ya kuingia miezi ya Hijja:**

Maimamiyya na Mashafi wamesema: "Lau mtu atahirimia Hijja kabla ya kuingia miezi ya Hijja basi Ihram yake haitaswihi, lakini Umra huswihi kutokana na kauli yake Mwenyezi Mungu aliyetukuka aliposema; 'Hijja ni miezi maalum' (Baqarah:197)."

Mahanafi, Maliki na Mahanbali wamesema: "Hijja yake huswihi lakini ni makruhu, (kitabul *At-Tadhikrah*, na *Fiqhus-Sunna*).



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 278 2/1/2017 3:51:54 PM

# KUHIRIMIA

## WAJIBU WAKE NA SUNNA YAKE:

### Kuhirimia na Sunna zake:

Hakuna tofauti kuwa kuhirimia ni nguzo miongoni mwa nguzo za Umra, na pia ni nguzo miongoni mwa nguzo za Hijja *Tamattui*, *Ifrad* na *Qiran*. Aidha hakuna ikhtilafu kuwa Ihram ndilo tendo la kwanza linalopasa kuanzia ibada ya anayekwenda Hijja au Umra. Hukmu ni hiyo hiyo awe amekwenda Umra *Mufrada* au alikwenda Hijja *Tamattui* au *Qiran* au *Ifrad*. Nayo Ihram ina Sunna na Wajibu.

Wameafikiana kuwa yasunniwa kwa mtu anayetaka kuhirimia (kwanza) ausafishe mwili wake, akate kucha zake, apunguze masharubu yake na aoge hata kama ni mwanamke mwenye damu ya hedhi au ya nifasi, kwani lengo linalotakikana ni unadhifu. Nna afuge nywele zake za kichwani tangu mwanzo wa mwezi wa Dhulqaadah pindi atakapo kwenda kuhiji Hijja *Tamattui*. Pia ni Sunna kuondoa nywele kutoka juu ya mwili na makwapani. Na ahirimie baada ya Swala ya Adhuhuri au Swala yoyote nyingine ya faradhi mbali na hiyo. Aidha inapendekezwa kwa ajili ya kuhirimia aswali rakaa sita au rakaa nne au kwa uchache rakaa mbili.

Ama kujitwahirisha kutokana na hadath si sharti katika kuswihi kwa Ihram.

Mahanafi na Maliki wamesema: "Mtu anapokosa maji, sharti la kuoga huporomoka. Na hakuna cha kutayammamu badala yake." Mahanbali na Mashafi wamesema: "Atatayammamu badala ya kuoga." Maimamiyya wamekhitalifiana wao kwa wao, wako waliokataza kutayammamu na wako waliojuzisha.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 279 2/1/2017 3:51:54 PM

Na haki ni kuzuia, kama walivyosema Mahanafi na Maliki, kwa sababu huku kutayammamu ni miongoni mwa ibada ambayo haiwezi kufanywa (kisheria) hadi pawepo na dalili, na hapa hapana dalili … katika kitabu *Mustamsikil Urwa* cha Sayyid Al-Hakim Juz. 7, amesema maneno haya: "Kwa hakika mchanga kuwa kwa ujumla ni mbadala wa maji, na kwamba unatosha hata kwa muda wa miaka kumi, na kwamba mchanga ni kimojawapo kati ya vitu viwili vinavyotwahirishia, na kwamba Mola wa maji na mchanga ni Mmoja, hayo yote yanatosha kuthibitisha kuwa mchanga ni mbadala wa maji katika hali hii na mfano wake."

Inajibiwa kuwa, dalili hizi ambazo bila shaka zimefahamisha kuwa mchanga ni mbadala wa maji zinahusika pale maji yanapofungamana na suala la kutwaharisha hadathi, na si maji kama maji, kwani kinyume na hivyo ingelipasa tuupe mchanga hukmu zote za maji pindi yanapokosekana, hata katika kuondolea najisi, isipokuwa pale dalili ilipoonesha kinyume. Na kamwe hakuna aliyesema hilo hata mwenye kitabu *Mustamsik* ninavyodhani hakusema hivyo, bali katika uk. 26 wa kitabu chake cha Hijja, chapa ya nne amesema waziwazi kuwa kuoga josho hilo ni Sunna wakati wa kutaka kuhirimia, (hata) kwa mwenye hedhi na mwanamke mwenye damu ya kuzaa. Na maana ya kauli hiyo ni kuwa kwa hakika josho hili haliondoi hadath na halikusudiwi jingine isipokuwa unadhifu tu. Hili, na kuongezea ni kuwa kwa hakika sisi tunajua kuwa mchanga huwa mbadala wa maji katika utwahirishaji wa hadathi, na wala hauwi mbadala wake katika utwaharishaji wa najisi kama vile damu na mkojo. Kufikia hapa tunakuwa na shaka ya kuwa je, huo mchanga unaweza kuwa mbadala wa maji katika josho hili, na haiwezekani kushikilia ujumla katika kuondoa shaka na kuthibitisha ubadala wake kisheria, kwani kufanya hivyo ni sawa na kushikamana na jambo la ujumla katika jambo la utata au mfano wa nje.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 280 2/1/2017 3:51:54 PM

Sayyid alitumiwa maelezo haya akayatolea jibu kwa kauli yake hii: "Kwa yakini huku kuwekwa na sheria kuoga josho la Sunna ni kwa ajili ya kujitwahirisha, na kujitwahirisha huko si kwa jinginelo zaidi ya kuondoa hadath tu. Kwa hiyo basi, josho la Sunna ni lenye kutwahirisha vilivyo katika daraja ya hadath. Na ubadala wa mchanga unajumuisha maeneo ya kuoga josho la Sunna. Na kujumuisha kwake hilo hakulazimu kujumuisha utwaharishaji wa najisi, kwa sababu ya kutofautiana aina kati ya hadathi na khabath, na pia kutofautiana mahali pake. Kwani bila ya shaka mahali pa utwaharishaji wa kwanza ni nafsi na mfano wake, na mahali pa utwaharishaji wa pili ni mwili, pamoja na kuwepo asili moja baina ya utwaharishaji wa kuoga josho la wajibu na la Sunna. Na dalili ya ubadala inajumuisha mambo yote mawili.

Kwa ujumla, josho la Sunna hutwaharisha kutokana na hadath kama zilivyo hata kama ni katika baadhi ya daraja zake, na kwa hali hiyo dalili ya mchanga kuwa mbadala wa maji inajumuisha josho hilo. Na pia josho la kuondoa damu ya Hedhi ni lenye kutwahirisha Hadath, kama ambavyo mwanamke mwenye damu ya hedhi anapooga josho la kuondoa Janaba basi hutwahirika, hata kama bado atabaki na hadath ya Hedhi. Na Mwenyezi Mungu ndiye aliye Mjuzi, Mwenye kuhifadhi."

Maimamiyya wamesema: "Husuniwa kufuga nywele za kichwa." Mashafi, Mahanafi na Mahanbali wamesema: "Bali yasunniwa kuzinyoa." (*Fiqh Alal Madhahibil Arbaa).*

Mahanafi wamesema: "Yasunniwa kwa mtu anayetaka kuhirimia ajipake manukato mwilini na nguoni kwa uturi ambao hautabakia kiini chake baada ya kuhirimia, hata japo itabakia harufu yake."

Mashafi wamesema: "Husuniwa kujipaka manukato mwilini baada ya kuoga isipokuwa kwa mwenye Swaumu, wala haidhuru kupaka nguo uturi."

Mahanbali wamesema: "Atapaka uturi mwili tu, ama kupaka nguoni ni makruhu." (*Al Fiqh Alal Madhahibil Arbaa)*.

Mahanafi, Maliki na Mashafi wamesema: "Yasuniwa kwa mwenye kuhirimia aswali rakaa mbili kwanza kabla hajahirimia." (Tazama kitabu hicho tulichokitaja hapo juu).

Maimamiyya wamesema: "Ni bora zaidi kuhirimia kufanywe baada ya Swala ya Adhuhuri au Swala nyingineyo yoyote ambayo ni ya faradhi. Na kama hana Swala ya faradhi ya kuiswali wakati wa kuhirimia kwake basi ataswali rakaa sita, au nne na kwa uchache wake rakaa mbili." (Tazama kitabu *Al-Jawahir)*.

**KUWEKA SHARTI:**

Mwenye kitabu *at-Tadhkirah* amesema: "Imependekezwa kwa mtu anayetaka kuhirimia ajiwekee sharti juu ya Mola Wake wakati wa kufunga Ihram, kama kusema: "Ee Mola Wangu! Mimi ninataka kutekeleza jambo ulilonamrisha nilitende, basi likitokea jambo lolote litakalonizuia nisiweze kulifanya, basi nijaalie nitoke kwenye Ihram." na kwa kulipendekeza hilo Imam Shafi, Abu Hanifa na Ahmad wamesema: "Isipokuwa kuweka sharti huko hakuna maana ya kuwa kunaporomosha faradhi ya Hijja kama litapatikana jambo litakalomzuia kutimiza kuhirimia kwake."

**WAJIBU WA KUHIRIMIA:**

Wajibu wa kuhirimia ni mambo matatu: Kutia nia, kuleta talbiya na kuvaa nguo za Ihram, mkiwemo tafauti baina ya madhehebu katika baadhi ya mambo.

**KUTIA NIA:**

Hapana haja ya kusema mengi katika nia maana hakuna amali yoyote inayotaka kufanywa bila ya kukusudiwa, kwa maana nia ndilo



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 282 2/1/2017 3:51:55 PM

jambo linalotia msukumo wa kufanya jambo, tena hiyo nia kwa hakika kabisa ni jambo lililo lazima kutendeka (wakati wa kukusudia kufanya jambo). Na ni kwa ajili hiyo ndio maana baadhi ya wanavyuoni wakasema: "Lau tungelazimishwa kufanya kitendo (amali) chochote kile bila ya nia basi ingelikuwa tumekalifishwa kufanya jambo lisilowezekana."

Kwa hivyo basi inafaa tusarifu maneno yetu kwa mtu anayekwenda kufanya ibada hiyo kwa kuuliza swali hili, je mtu huwa ni mwenye kuhirimia kwa kiasi tu cha kunuia Ihram, au hapana budi aongeze kitu kingine pamoja nayo? Pamoja na hivyo ifahamike kuwa lau mtu atahirimia kimakosa au kimchezo bila ya kukusudia basi kuhirimia kwake kutakuwa batili.

Mahanafi wamesema: "Ihram haiwi ni yenye kutimia katika sheria kwa kutia tu nia bila ya kuleta Talbiya." (*Fathul Qadir*).

Mashafi, Maimamiyya na Mahanbali wamesema: "Ihram hutimia kwa kutia tu nia." (*Al-Jawahir* na *Fiqhus-Sunna*).

Maimamiyya wakaongeza kusema: "Ni lazima nia iwe ni yenye kukutanishwa na kuanza kwa Ihram. Kamwe haitoshi kutiwa nia katikati yake wakati Ihram ikiwa inaendelea. Aidha ni wajibu aainishe ihramu yake kwa kutaja kama ni Hijja au Umra, na kutaja kwamba Hijja hiyo ni *Tamattui*, *Qiran* au *Ifrad*, na kuwa anajihijia yeye mwenyewe binafsi au anahiji kwa niaba ya mtu mwingine, na kwamba ni Hijja ya Uislamu au nyingineyo. Na lau atanuia bila ya kuitaja aina ya Hijja aliyoikusudia, na akataka kufanya hivyo baadaye, basi Ihram yake itabatilika (*Al-Urwatul Wuthqa*)."

Na katika kitabu *Al-Mughni* cha Mahanbali mmekuja maelezo ambayo kwa ufupi wake ni:



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 283 2/1/2017 3:51:55 PM

"Inapendekezwa kwa mtu kutaja aina ya kuhirimia anakokusudia." Na kwa maana hii hii amesema Malik na Imam Shafi katika moja ya kauli zake mbili, amesema: "Kuitamka ni bora zaidi … basi lau mtu ataitamka Ihram, akanuia Ihram ya ibada tu wala asitaje Hijja wala Umra, itaswihi naye atakuwa ni mwenye kuhirimia… Hata hivyo baadaye itamlazimu aielekeze upande wa ibada yoyote anayoitaka."

Na wameafikiana kuwa lau mtu atanuia katika kuhirimia kwake akasema nanuia kama vile alivyohirimia fulani itaswihi iwapo hiyo nia iliyotajwa ilikuwa imetaja aina fulani ya Hijja au Umra. (*Al-Jawahir* na *Mughni).*

## TALBIYA:

Wameafikiana kuwa talbiya huanza kuletwa katika Ihram, kisha wakakhitilafiana katika hukmu yake kwa upande wa wajibu na Sunna, na katika wakati wake.

Mashafi na Mahanbali wamesema: "Hiyo talbiya ni Sunna na husuniwa kuiwasilisha pamoja na Ihram, lakini lau mtu atanuia Ihram pasi na kuleta talbiya huswihi."

Maimamiyya, Mahanafi[40] na vilevile Maliki wamesema: "Kuleta talbiya ni wajibu." Kisha wamekhitilafiana katika maelezo yao. Mahanafi wamesema: "Kwa hakika talbiya au kinachosimama makamu yake kama vile tasbihi na kutoa mnyama ni sharti miongoni mwa masharti ya kuhirimia."

Maliki wamesema: "Ihram haibatiliki kwa kitenganisho kirefu baina ya tabliya na Ihram, na wala kwa kuiacha kabisa lakini aliyeiacha hulazimika kumwaga damu, kwa maana ya kuchinja mnyama."

[40] Kwa Mahanafi kumswaga mnyama husimama makamu ya Talbiya kama ilivyokuja katika kitabu cha Ibn Abidini na *Fathul-Qadir*.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 284 2/1/2017 3:51:55 PM

Maimamiyya wamesema: "Haiwezi kukamilika Ihram ya Hijja *Tamattui* wala Hijja *Ifrad*, wala Umra ya Hijja mbili hizo, na hata Umra *Mufrada* isipokuwa kwa kuleta tabliya, tena hapana budi kuikariri mara nne. Ama kwa mtu anayetaka kuhiji Hijja *Qiran* atahiari kati ya kuleta tabliya, kufanya *Ish'ar* au kufanya *Taqlid."*[41] Na kwao *Ish'ar* inahusika kwa ngamia, na *Taqlid* anashirikiana ngamia na wengineo katika aina za wanyama wanaopelekwa kuchinjwa huko."

## TAMKO LA TALBIYA:

Na tamko la Tabliya ni kusema; *"Labbaikallahuma Labbaika, Lasharikalaka Labbaika. Innalhamdu Waniimata Laka Walmulku lasharikalaka."* Kwa Ijmai ya kauli ya wanavyuoni, ni kuwa haishartiwi kuwa na tohara wakati wa kutamka Talbiya. (*At-Tadhkira*).

Ama wakati wake, ataanza pale pale wakati wa kuhirimia, na ni mustahabbu kuendelea nayo mpaka atakapokwenda kurusha vijiwe. Na ni mustahabu kuisoma kwa sauti kwa asiyekuwa mwanamke isipokuwa katika misikiti ya jamaa, hasa msikiti wa Arafah.

Maimamiyya wamesema: "Ni Sunna kukatiza Talbiya anapoyashuhudia majumba ya Makka, ama mwanamke atapaza sauti kidogo kiasi cha kujisikia yeye mwenyewe na anayemfuatia tu. Vilevile husuninwa amswalie Mtume na jamaa zake. (*At-Tadhikirah* na *Fiqhus-Sunna*).

## VAZI LA MWENYE KUHIRIMIA:

Wameafikiana kuwa mwanamume anayehirimia haijuzu kwake kuvaa nguo zilizoshonwa, wala nguo iliyoshonwa katika muundo wa kikoi,

[41] Maana ya *ish'ar* ni kupasua sehemu ya kulia ya nundu ya ngamia. Na maana ya *Taqlid* ni kutungika sandali (au mfano wake) kwenye shingo ya mnyama, ili iwe alama inayomtambulisha kuwa ni mnyama wa sadaka ya Hijja.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 285 2/1/2017 3:51:55 PM

wala kanzu au suruali, na wala si ruhusa kwake kujifunika kichwa na uso wake. Lakini Shafii na Ahmad wamesema: "Inajuzu kwake kujifunika uso wake. Na wala haijuzu kwake kuvaa (viatu vya) khoffu mbili isipokuwa tu kama hakupata sandali, hapo anaweza akavaa khoffu lakini baada ya kuzikata sehemu ya chini ya vifundo viwili."[42]

Ama mwanamke atafunika kichwa chake, na uso wake atauacha wazi, isipokuwa atapohofia kutazamwa na wanaume kwa njia ya kuleta shaka, lakini haijuzu kwake kuvaa glovu na anaweza akavaa nguo za hariri na khoffu mbili.

Abu Hanifa amesema: "Inajuzu kwa mwanamke kuvaa nguo iliyopindwa." (*At-Tadhkirah* na *Bidayatu Wanihayah* cha Ibn Rushd). Na katika kitabu *Fiqhu Alal Madhhabil Arbaa,* chini ya kichwa cha maneno 'Mambo yanayotakiwa kwa mwenye kuhirimia kabla hajahirimia bado,' imeandikwa maneno haya yafuatayo:

Mahanafi wamesema: "Miongoni mwa mambo hayo ni kuvaa msuli na shuka (nguo ya kujitanda), na msuli ni nguo inayositiri kuanzia kitovu hadi magotini. Na shuka ni nguo ambayo hufunika mgongo, kifua na mabega, nayo ni Sunna."

Maliki wamesema: "Husunniwa kuvaa (shuka mbili) ya kujifunga kiunoni hadi magotini na moja ya kujitanda, na kandambili. Na kama atavaa nguo aina nyingine zisizoshonwa, ambazo si shuka (nyeupe) ya kujitanda na si msuli, lakini zikawa zimefunika mwili, hakuna neno. Na nguo zinazoufunika mwili ni zile zinazofunika viungo."

Mahanbali wamesema: "Inasunniwa kwake kabla ya kuhirimia kuvaa msuli na shuka, ziwe nyeupe, nadhifu na ziwe ni mpya, avae na kandambili."

---

[42] *Na'al* ni viatu vyenye sehemu ya chini tu, wala havina sehemu ya kufunika vifundo, wala hazina sehemu za ubavu, wala sehemu ya kuziba juu ya nyayo. Na khoffu ni viatu ninavyoziba sehemu zote za miguu kuanzia vifundo, na ubavu na juu ya nyayo kama ilivyo kwa viatu maarufu vya kileo tulivyovizoea.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 286 2/1/2017 3:51:55 PM

Mashafi wamesema: “Na miongoni mwazo ni kuvaa msuli na shuka, zote mbili ziwe nyeupe tena zilizo mpya, la hakuweza kupata mpya basi naavae za mfuo.”

Maimamiyya wamesema: “Msuli na nguo ya kujitanda kwenye kuhirimia, zote mbili ni wajibu. Tena inapendekezwa ziwe zimetokana na uzi wa pamba nyeupe. Pia hujuzu kwa mwenye kuhirimia kuvaa nguo zaidi ya mbili kwa sharti ya kuwa zisiwe zimeshonwa. Aidha inajuzu kwake kubadili nguo za kuhirimia, lakini ilivyo bora (kwao Maimamiyya) ni kutufu akiwa na nguo mbili zile zile alizokuwa amezivaa wakati wa kuhirimia. Na masharti ya nguo hizo ni yale yale ya nguo za anayetaka kuswali kuhusiana na utohara, na kwamba isiwe ni ya hariri kama anayehirimia ni mwanamume, wala isiwe ngozi ya mnyama katika wanyama wasioliwa nyama yao.” Bali kundi katika madhehebu yao limesema: “Haijuzu kabisa kuwa ni aina ya ngozi.”

Kwa vyovyote itakavyokuwa tofauti iliyopo katika madhehebu kuhusu nguo anazofaa kuvaa mwenye kuhirimia ni ndogo sana, na inatosha kutoa dalili juu ya hilo kwa kusema kuwa, kila ambalo linajuzu kwa Maimamiyya vilevile linajuzu kwa madhehebu manne.

## YALIYO HARAMU KWA ALIYE NDANI YA IHRAMU

Sharia imemkataza mambo kadhaa, mengi yake tutayataja katika maelezo yafuatayo, yule aliye ndani ya ihramu:

### KUOA:

Maimamiyya, Mahanbali, Maliki na Mashafi wamesema: “Haijuzu kwa aliye ndani ya ihramu kufunga ndoa yeye mwenyewe binafsi,



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 287 2/1/2017 3:51:55 PM

wala kumuoza mwenzake, wala kumwakilisha mtu wa kumuolea, na kama atafanya hivyo basi ndoa haitaswihi."

Maimamiyya wameongeza kusema: "Vilevile haijuzu kwake kuwa shahidi katika ndoa." Abu Hanifa amesema: "Yajuzu kwake kufunga ndoa, na huwa ni sahihi kabisa." Mahanafi, Maliki, Mashafi na Maimamiyya wamesema: "Hujuzu kwa aliye ndani ya ihramu kumrejea mkewe aliyemtaliki akiwa bado yumo ndani ya eda yake." Mahanbali wamesema: "Hijuzu."

Maimamiyya wamesema: "Aliye ndani ya ihramu anapofunga ndoa hali ya kuwa anafahamu kuwa ni haramu, basi mwanamke huyo huwa ni haramu kwake milele kwa kitendo tu cha kufunga ndoa, hata kama hakumwingilia. Ama kama alifanya kwa kutojua uharamu huo basi hatakuwa haramu kwake hata kama alimwingilia." (*Al-Jawahir, Fiqh Sunna* na *Fiqh Alal Madhahibil Arbaa*).

## KUJAMIIANA:

Mafakihi wameafikiana kuwa haijuzu kwa aliye ndani ya ihramu kumwingilia mkewe, au kustarehe naye kwa aina yoyote ya starehe za kimapenzi. Na kama atajamiiana kabla ya kujitoa katika ihramu[43] basi Hijja yake itaharibika, lakini ni juu yake kuendelea na Hijja yake hadi aikamilishe, kisha mwaka unaofuatia aje kulipa, kwa sharti la kutenganishwa baina ya mtu na mkewe katika Hijja hiyo ya kulipa.[44]

[43] Amalizapo kutupa vijiwe na kunyoa mwenye kuhirimia huwa halali kwake mambo kadhaa ambayo yalikuwa ni haramu juu yake, kama vile kuvaa nguo zilizoshonwa na mfano wake. Na hii ndiyo halali ya kwanza ambayo haihalalishi kumuingilia mwanamke na kujitia uturi. Na aishapo kutufu Twawafu ya mwisho huwa halali juu yake kila kitu hata kumuingilia mkewe. Na hii ndiyo halali ya pili, maelezo yake yatafuata.

[44] Mwenye kitabu *Tadhikira* amesema: "Hufaa iwe kuwatenganisha mke na mume katika Hijja yao ya kukidhi kuwa kando na mahali walipofanya kitendo walichofanya katika Hijja yao ya kwanza. Na maana ya kuwatenganisha ni kutobakia peke yao, na kila wanapokutana awe mtu wa tatu muhrim. Kwani kupatikana kwake kutazuia kutokea tendo la kujamiana.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 288 2/1/2017 3:51:55 PM

Hilo ni wajibu katika madhehebu ya Imamiyya, Maliki na Hanbali. Na kwa madhehebu ya Shafi na Hanafi ni Sunna (kitabu *al-Hadaiq* na *Fiqh Sunnah)*. Maimamiyya, Mashafi, Maliki na Mahanbali wamesema: "Humlazimu kuchinja ngamia kufuatia kosa lililoharibu Hijja yake." Mahanafi wamesema: "Hapana. Si ngamia, bali ni mbuzi."

Na wameafikiana kuwa, kama alimwingilia mkewe baada ya kujitoa katika ihramu ya kwanza basi Hijja yake haitaharibika, na wala hatalipa, lakini itamlazimu achinje ngamia kwa mujibu wa Maimamiyya, Mahanafi na Shafii katika moja ya kauli zake mbili. Ama Malik yeye amesema: "Hulazimika kuchinja mbuzi." (*Al-Hadaiq* na *Fiqh Sunna*).

Kama mwanamke aliingiliwa kwa kupenda kwake, Hijja yake inaharibika na itamlazimu atoe fidia ya ngamia kisha aje kuilipa Hijja hiyo mwaka unaofuata… Na kama alifanya kwa kutenzwa nguvu hatalazimika chochote, bali itakuwa juu ya mumewe kutoa kafara ngamia wawili, mmoja kwa ajili yake na mwengine kwa ajili ya mkewe. Na kama mwanamke huyo alikuwa ameshatoka kwenye Ihram hatalazimika chochote juu yake, wala haitampasa kutoa kafara, na mume pia hatalazimika chochote kwa sababu ya mkewe. (*At-Tadhkirah*).

Na anapombusu mkewe lakini bila kushusha manii Hijja yake haiharibiki. Kwa itifaki ya mafakihi. Mafakihi wa madhehebu manne wamesema: "Itamlazimu kumwaga damu, kwa maana ya kutoa fidia, ijapokuwa mbuzi." Na mwenye kitabu *at-Tadhikrah* miongoni mwa Maimamiyya amesema: "Kama atambusu kwa matamanio basi atachinja ngamia, na kama si hivyo basi ni mbuzi."

Kama atambusu na kushusha manii, Maliki wamesema: "Hijja yake itabatilika." Na Mafakihi waliobaki wameungana katika kuwa



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 289 2/1/2017 3:51:55 PM

Hijja yake ni sahihi, lakini atalazimika kutoa kafara. Nayo ni ngamia kwa mujibu wa madhehebu ya Hanbali na kundi katika madhehebu ya Imamiyya. Na hulazimika kuchinja mbuzi kwa Mashafi na Mahanafi. (*Al-Hadaiq* na *al-Mughni*).

Na kama atamtazama mwanamke wa kando hadi akatokwa na manii, Hijja yake haitabatilika, bali kwa madhehebu ya Imamiyya atalazimika kuchinja ngamia. Hiyo pia ndiyo kauli ya Imam Shafi, Abu Hanifa na Ahmad bin Hanbali, kwani kushusha huko kulitendeka bila ya kufanyika kitendo. Lakini Maimamiyya wamesema: "Atalazimika kuchinja ngamia kama ni tajiri, na kama ni mtu wa maisha ya katikati atachunja ng'ombe, akiwa masikini basi atachinja mbuzi."

Malik amesema; "Akirudia kutazama tena hadi akapatwa na janaba basi Hijja yake itabatilika na itamlazimu kulipa." Na mwenye kitabu *At-Tadhikrah* amesema: "Atalazimika pia kutoa fidia ya ngamia."

## MANUKATO:

Wameafikina kuwa aliye katika ihramu ya Hijja yeyote ile awayo, awe ni mwanamume au mwanamke, huwa ni haramu juu yake manukato, kuyanusa, kujipamba kwayo na hata kuyala … Na kwamba aliyehirimia Hijja anapokufa haijuzu kumuosha wala kumpaka kafuri wala chenginecho katika aina za manukato. Na kama mtu aliyehirimia Hijja atajipamba manukato kwa kusahau au kwa kutojua uharamu wake, Maimamiyya na Mashafi wamesema: "Halazimiki kutoa fidia." Mahanafi na Maliki wamesema: "Hulazimika kutoa fidia." Ahmad ana mapokezi mawili. Na kama atalazimika kutumia manukato kwa sababu ya maradhi anaruhusiwa kujipaka na wala hatatoa fidia.

Maimamiyya wamesema: "Kama mtu aliye ndani ya ihramu atajipaka manukato kwa makusudi itamlazimu kuchinja mbuzi, hukmu hiyo inabaki kuwa hivyo hata kama alitumia manukato hayo kama pambo au chakula. Na wala hapana ubaya wa kujipaka uturi wa al-Kaaba hata kama ndani yake mna zafarani, matunda na mrihani." (*Al -Jawahir*).

## KUJIPAKA WANJA:

Imeandikwa katika kitabu *At-Tadhkirah* kwamba wamekongamana wanavyuoni wetu, yaani wa Ki-Imamiyya, kwamba, kwa yakini haijuzu kujipaka wanja mweusi wala wanja ambao una manukato, sawa aliye katika ihramu awe ni mwanamume au mwanamke, na hujuzu kujipaka chenginecho kisichokuwa viwili hivyo.

Katika kitabu *Al-Mughni* mmeandikwa kuwa, kujipaka wanja wa Ithmud (aina ya jiwe linalotumiwa kama wanja) ni makruhu, na wala hatoi fidia mwenye kutumia wanja huo. Sitambui kama kuna hitilafu yoyote juu ya hukmu hiyo baina ya wanavyuoni. Ama kujipaka wanja kwa kifaa kisichokuwa hilo jiwe (Ithmud), si makruh maadamu wanja huo hautakuwa na manukato.

## KUCHA, NYWELE NA MITI:

Wameafikiana kuwa hairuhusiwi kukata kucha, kupunguza nywele na kunyoa, sawa iwe ni nywele za kichwani au za mwilini. Na akifanya kinyume chake basi atalazimika kutoa fidia.[45]

Ama kukata miti na mimea iliyo katika Haram takatifu, wameafikiana kuwa haijuzu kuikata au kuing'oa ile mimea

[45] Imamiyya wamesema: "Akikata kucha za mikono na miguu yake atalipa mbuzi mmoja kama ni katika kikao kimoja. Na kama ni katika vikao zaidi ya kimoja basi atalipa mbuzi wawili. Na fidia ya kukata ukucha ni pishi la chakula, na pishi moja ni karibu gramu 800.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 291 2/1/2017 3:51:55 PM

aliyoiotesha Mwenyezi Mungu bila ya wasita wa mwanadamu, hata mwiba isipokuwa nyasi zinazonukia vizuri ziitwazo Adhkhar.

Kisha wamekhitilafiana kuhusu miti iliyomea kwa wasita wa mwanaadamu. Imam Shafi amesema: "Hapana tofauti kati ya aina hizo mbili, zote haijuzu kuzikata au kuzing'oa, bali katika mimea yote hiyo ni wajibu kutolewa fidia. Na katika mti mkubwa atatoa ng'ombe, na kwa mti mdogo atatoa mbuzi."

Maliki wamesema: "Mtu hupata dhambi kwa kukata mti na wala halazimiki kutoa chochote, sawa mti uliokatwa ni miongoni mwa miti aliyoiotesha Mwenyezi Mungu au iliyoota kwa wasita wa mwanadamu."

Maimamiyya, Mahanafi na Mahanbali wamesema: "Yajuzu kukata kilichooteshwa na mwanaadamu na hakuna lolote. Ama kilichooteshwa na Mwenyezi Mungu, kuna fidia." Nayo kwa Maimamiyya ni ng'ombe kwa kukata mti mkubwa, na mti mdogo ni mbuzi. Mahanafi wamesema: "Hutolewa mnyama kulingana na kima chake." (*Fiqh Sunna na Al-Lummuah,* cha Maimamiyya). Na wameafikiana kuwa hakutolewi fidia yoyote kwa kukata kilicho kikavu iwe ni mti au nyasi.

## KUTAZAMA KIOO:

Haijuzu kwa mtu aliye katika ihramu kutazama kioo, na akifanya hivyo halazimiki kutoa fidia. Hii ni kwa itifaki ya mafakihi. Na wala hakuna kinachomkataza kutazama ndani ya maji.

## HINA:

Mahanbali wamesema: "Hujuzu mwanamume au mwanamke kujipaka sehemu yoyote ya mwili isipokuwa kichwani." Mashafi

wamesema: "Yajuzu hivyo isipokuwa mikono na miguu miwili." Mahanafi wamesema: "Haijuzu kujipaka hina kwa mtu aliye katika ihramu, kwa hali yoyote iwayo, iwe mwanamume au mwanamke." (*Fiqh Sunnah*).

Na kauli iliyo mashuhuri, kwa Maimamiyya ni kuwa kwa yakini kujipaka hina ni makruhu si haramu. (*Al-Lummuah*).

**KUJIWEKA CHINI YA KIVULI NA KUFUNIKA KICHWA:**

Wameafikiana kuwa mtu aliye katika ihramu haijuzu kwake kujifunika kichwa chake kwa kupenda kwake. Maliki na Maimamiyya wamesema: "Vilevile haijuzu kwake kuzama ndani ya maji kiasi ambacho maji yatakuwa juu kupita kichwa chake." Lakini inajuzu kuosha kichwa chake na kujieneza maji juu yake kwa itifaki ya mafakihi isipokuwa Maliki, kwani wao wanasema: "Haijuzu kwa aliye katika ihramu kujiosha uchafu isipokuwa mikononi tu."

Na kama mtu atajifunika kichwa kutokana na kusahau, Maimamiyya wamesema: "Hatoi chochote." Na hiyo ndiyo kauli ya Mashafi. Mahanafi wamesema: "Atatoa fidia."

Wameafikiana isipokuwa Mashafi, kuwa mwanamume aliye katika Ihramu huwa haramu juu yake kujiweka chini ya kivuli katika hali ya kwenda, hivyo haijuzu kwake kupanda gari, ndege na chochote kingine kama hivyo ambacho ikiwa kina paa. Ama anapokuwa anakwenda kwa miguu inajuzu kwake kupita chini ya kivuli katika hali ya kuvuka.[46]

Na kama mtu atalazimika kujiweka chini ya kivuli hali ya kuwa ni msafiri kutokana na maradhi, joto au baridi, itajuzu. Lakini

[46] Mwenye kitabu *At-Tadhkirah* amemnukuu Abu Hanifa kuwa amesema: "Hapana ruhusa ya kujiweka chini ya kivuli wakati wa kwenda." Na mwenye *Rahmatul Umma* amemnukuu akisema inajuzu.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 293 2/1/2017 3:51:55 PM

atalazimika kutoa fidia kwa mujibu wa madhehebu ya Imamiyya. Maimamiyya wamesema: "Hujuzu kwa mwanamke kujiweka chini ya kivuli, hali ya kuwa anakwenda." (*At-Tadhkirah*).

## KUVAA NGUO ZILIZOSHONWA, NA KUVAA PETE:

Wameafikiana kuwa mwanamume aliye katika ihramu haruhusiwi kuvaa nguo zilizoshonwa, na hata za kuzonga kama vile kilemba na Tarbush na mfano wake. Lakini hilo linaruhusiwa kwa mwanamke isipokuwa glovu (visoksi vyenye vidole vitano, huvaliwa mikononi hasa na wanawake) na nguo iliyopata manukato (uturi).

Maimamiyya wamesema: "Kama mtu atavaa nguo iliyoshonwa kwa kusahau au kwa kutojua, halazimiki kutoa chochote, lakini akivaa kwa kudhamiria kusudi ajikinge joto au baridi basi itamlazimu kuchinja mbuzi."

Vilevile wamesema: "Haijuzu kuvaa pete ikiwa ni pambo, lakini hujuzu kuivaa kwa lengo jingine. Aidha haijuzu kwa mwanamke kuvaa vitu vya urembo."

## KUSEMA MANENO MACHAFU NA MJADALA:

Mwenyezi Mungu aliyetukuka amesema katika Aya ya 197 katika Suratul Baqarah:

"..... فَمَن فَرَضَ فِيهِنَّ ٱلْحَجَّ فَلَا رَفَثَ وَلَا فُسُوقَ وَلَا جِدَالَ فِي ٱلْحَجِّ ....."

**"….basi hakuna kuingiliana na wanawake wala kutoka katika mipaka wala mabishano katika Hijja …" (Baqarah; 2:197)**

Maana ya neno *Ar-rafath,* ni kujamiiana, na imetangulia kuelezwa huko nyuma kuhusu hukmu za kujamiiana. Na maana ya *Fusqu,*ni



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 294 2/1/2017 3:51:55 PM

kusema uongo, ikasemwa, ni kutukana (kusema maneno ya matusi), na ilisemwa, ni kufanya maasi. Na vyovyote itakavyokuwa, vitendo hivyo vyote ni haramu kwa aliye katika Hijja na mwingine, lakini imesisitizwa zaidi kwa aliye katika Hijja kuliko mtu mwingine. Na maana ya *Jidal* ni kubishana. Maimamiyya wamepokea Hadith kutoka kwa Imam as-Sadiq عليه السلام kuwa amesema: "Huko (kubishana) ni kauli ya mtu anapomwambia mwenzake: "Sivyo hivyo wallahi. Na wallahi ndivyo.'" Na kadhalika. Na huu ndio uchache wa mabishano.

Maimamiyya wamesema: "Anaposema uongo mara moja itamlazimu mbuzi. Akisema uongo mara mbili itamlazimu ng'ombe, mara ya tatu ngamia, na akiapa ilihali ni mkweli, hatalazimika chochote isipokuwa atakaporudia kuapa mara tatu, hapo atalazimika kutoa mbuzi."

## KUUMIKA:

Wameafikiana kuwa inaruhusiwa kuumika kwa dharura. Mafakihi wa madhehebu manne wamejuzisha kuumika hata bila ya dharura mradi tu hakutasababisha kung'oa nywele. Ama mafakihi wa Kiimamiyya wamekhitilafiana wao kwa wao, wako waliojuzisha na waliokataza. (*At-Tadhkirah* na *Fiqh Alal Madhahibil Arbaa)*.

## KUUA CHAWA:

Imekuja katika kitabu *Al-Lumuah* cha Maimamiyya kuwa, haijuzu kwa aliye katika ihramu kuua vijidudu vya mwilini kama vile chawa na papasi, bali inajuzu kumuondoa. Sayid Al-Hakim katika kitabu *Mansik* amesema: "Inajuzu kuua kunguni na viroboto kusudi kwa kujikinga nafsi yake." Ama sisi hatuna shaka yoyote kuhusu kujuzu kukiondoa kile kinachoudhi, na kama kukiondoa huko kutahitaji kukiua, inajuzu pia.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 295 2/1/2017 3:51:55 PM

Jambo la kushangaza ni habari hii iliyonukuliwa kutoka kwa Ibn Abbas kwamba aliulizwa kuhusu mtu aliye katika Hijja, akamuona chawa juu ya mwili wake akamuondoa akamuangusha ardhini, kisha akajiwa na hofu ya kuwa haijuzu kufanya hivyo, akawa anamtafuta ili amrejeshe mahali pake alipokuwa, lakini asimpate, nini hukmu yake? Ibn Abbas akasema; “Hicho ni kitu kilichopotea hakitafutiki.”

Na katika kitabu *Al-Mughni* mmeandikwa maneno yafuatayo: “Aliye katika Hijja haruhusiwi kujiondolea chawa, kwani kufanya hivyo kuna maana ya kuondoa chawa kutoka mwilini mwake, ambapo ni jambo lililokatazwa… Na kama mtu atakwenda kinyume na amri hiyo akajidondolea chawa au kuua chawa hatatoa fidia kwa tendo hilo, yaani kwa mujibu wa madhehebu ya Hanbali.

Mahanafi wamesema: “Atalisha kitu chochote (kama sadaka).”Maliki wamesema: “Atatoa fumba la chakula.”

**Kuwinda:**

Wameafikiana kwa kauli moja juu ya uharamu wa kujiingiza katika kuwasumbua wanyama mwitu kwa kuwaua au kuwachinja, au kumwelekeza mtu mwenye nia hiyo upande walioko wanyama hao, au kumwashiria. Na kutokana na hukmu hiyo ndio ikawa ni haramu pia kuyatatiza mayai na vifaranga vya ndege. Ama wanyama wa baharini inajuzu kuwavua na kamwe hapana kutoa fidia katika kufanya hivyo. Hii ni kwa mujibu wa kauli yake Mwenyezi Mungu (s.w.t.) aliposema:

أُحِلَّ لَكُمْ صَيْدُ ٱلْبَحْرِ وَطَعَامُهُۥ مَتَٰعًا لَّكُمْ وَلِلسَّيَّارَةِ ۖ وَحُرِّمَ عَلَيْكُمْ صَيْدُ ٱلْبَرِّ مَا دُمْتُمْ حُرُمًا....."

**“Mmehalalishiwa kuvua baharini na chakula chake, kwa manufaa yenu (nyinyi wakazi wa mji huo) na kwa wasafiri. Na mmeharamishiwa kuwinda bara maadamu mko katika ihram…..” (Al-Maidah; 5: 96).**

Na huko kuharamishwa mawindo ya bara yaliyo ndani ya Haram takatifu kunamhusu mkaazi na aliye katika ihramu. Ama yaliyo nje ya Haram ni halali kwa mkaazi na si kwa aliye katika ihramu. Hivyo kama mtu aliye ndani ya ihramu atamchinja mnyama mwitu, basi mnyama huyo atakuwa nyamafu, na atakuwa ni haramu kuliwa na watu wote. Aidha wameafikiana kuwa yajuzu kwa mtu aliye ndani ya Hijja kuua kipanga, kunguru (*ghurabu*), panya na nge, na baadhi yao wakaongezea mbwa mkali anayeuma watu ovyo na kila mnyama mwenye madhara.

Mashafi na Maimamiyya wamesema: "Mnyama mwitu aliyeuawa kama ni katika wanyama wenye mfano miongoni mwa wanyama wa kufugwa, katika sura na umbo, kama vile nyati, basi muuaji atahiyari kati ya kutoa mnyama wa mfano wake katika wanyama wafugwao majumbani, amchinje amtoe sadaka, na kati ya kutoa thamani ya mnyama huyo wa mjini, kwa pesa taslimu azinunulie chakula akigawe kwa masikini, ambapo kila masikini mmoja apate vibaba viwili, navyo ni sawa na gramu 1,600 takriban. Aidha atahiari pia kufunga badala ya kutoa chakula, badala ya kila vibaba viwili atafunga siku moja. Na hii pia ndio kauli ya Maliki, isipokuwa wao wamesema: "Mhusika atalinganisha thamani ya mnyama mwitu aliyemuua, si mfano wake."

Mahanafi wamesema: "Atakuwa wa dhamana ya kutoa kima cha mnyama aliyemuwinda, awe ana mfano wake katika wanyama wafugwao au hana, na akishamfanyia makisio ya thamani yake hapo atahiari kati ya kununua kwa thamani hiyo, mfano wa mnyama aliyemuua, na amtoe, na baina ya kununua chakula na akitoe sadaka, na baina ya kufunga kwa kila kibaba siku moja." (*At-Tadhkirah* na *Fiqh Sunna*).

Na mafakihi hao wote wameitegemea Aya ya 95 katika Suratul Maidah inayosema:



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 297 2/1/2017 3:51:55 PM

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَقۡتُلُواْ ٱلصَّيۡدَ وَأَنتُمۡ حُرُمٞۚ وَمَن قَتَلَهُۥ مِنكُم مُّتَعَمِّدٗا فَجَزَآءٞ مِّثۡلُ مَا قَتَلَ مِنَ ٱلنَّعَمِ يَحۡكُمُ بِهِۦ ذَوَا عَدۡلٖ مِّنكُمۡ هَدۡيَۢا بَٰلِغَ ٱلۡكَعۡبَةِ أَوۡ كَفَّٰرَةٞ طَعَامُ مَسَٰكِينَ أَوۡ عَدۡلُ ذَٰلِكَ صِيَامٗا لِّيَذُوقَ وَبَالَ أَمۡرِهِۦ .....“

**“Enyi mlioamini! Msiue windo na hali (ya kuwa) mko katika Ihram. Na miongoni mwenu atakayemuua kwa kusudi, basi malipo yake yatakuwa ni mfano wa aliyemuua katika wanyama wa kufugwa, kama watakavyo hukmu waadilifu wawili miongoni mwenu. Mnyama huyo apelekwe al-Kaaba (kama sadaka); au kutoa kafara kwa kuwalisha masikini; au badala ya hayo ni kufunga, ili aonje ubaya wa jambo lake.….” (Suratul Maidah; 5:95).**

Na maana ya *Yahkum bihi dhawaadlin* ni kupatikana watu wawili walio waadilifu watoe uamuzi wao kwa kusema kuwa; mnyama huyu wa kufugwa ni sawa na mnyama wa pori aliyeuawa.

Na maana ya kauli yake Mwenyezi Mungu *Hadyan Balighal Kaabata,* ni kuwa anapofika Makka atamchinja mfano wa aliyemuua katika wanyama wa kufugwa, kisha amtoe sadaka.

Na katika kitabu *As-Sharaiu* cha Maimamiyya mmeandikwa maneno haya: “Kwa hakika aliyehirimia Hijja yeyote anapovaa au kula kitu kilichoharamishwa kukila au kukivaa, basi itamlazimu kutoa mbuzi.” Lakini ni kama tu kafanya hivyo kwa makusudi, si kwa kusahau au kutojua.”

Aidha wameafikiana Maimamiyya na Mashafi kuwa fidia hufutika juu ya mtu aliyetenda kosa kwa kutojua au kwa kusahau, isipokuwa katika windo tu, kwani katika tendo hilo itampasa kutoa fidia kwa vyovyote iwavyo hata kama alitenda katika hali ya kusahau. (kitabu *Al-Jawahir* na *Fiqh Sunnah)*.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 298 2/1/2017 3:51:56 PM

## MPAKA WA HARAM MBILI:

Hakuna tofauti katika uharamu wa kuwinda au kukata mti baina ya Haram ya Makka na ya Madina. Katika kitabu *Fiqh Sunna* yamo maelezo yanayosema: "Kwa yakini mpaka wa Haram ya Makka imesimamishwa juu yake alama katika pembe zake tano (zinazojuulikana), nazo ni mawe yaliyoinuka juu kiasi cha mita moja kwa urefu wake, yaliyosimamishwa katika pande mbili za kila njia.

Kwa upande wa Kaskazini mpaka upo mahali paitwapo *At-Taniim,* na kati ya mpaka huo na Makka pana umbali wa kilomita sita. Kwa upande wa Kusini upo *Idhwah,* na kati yake na Makka pana umbali wa kilomita kumi na mbili. Na upande wa Mashariki mpaka upo *Al-Juuranah,* na kati yake na Makka pana umbali wa kilomita kumi na sita. Na upande wa Magharibi mpaka upo *As-Shamisi,* na kati yake na Makka pana umbali wa kilomita kumi na tano.

Ama mpaka wa Haram ya Madina (Haram ya Mtume ﷺ, kiasi chake ni umbali wa maili kumi na mbili kuanzia *Iyri* hadi *Thaur*. Na *Iyri* ni jabali lililoko *Miqat*, na *Thaur* ni jabali lililoko *Uhud*. Mwanachuoni mkubwa wa Kiimamiyya Allamah Al-Hiliy katika kitabu chake *At-Tadhkirah* amesema: "Kwa hakika mpaka wa Haram ya Makka ni *Barid* katika *Barid –Barid* ni maili kumi na mbili. - Na mpaka wa Haram ya Madina ni kuanzia *Airi* Hadi *Iyri*."[47]

Mafakihi wa madhehebu wamerefusha maneno mno katika suala la mawindo na fidia yake, wakaanzia kwa mnyama mbuni ambaye anafanana mno na ngamia, wakaendelea hadi katika kuwinda panzi. Waliwachimbua matawi na kuweka hukmu nyingine mbalimbali … Ama sisi natutosheke na hayo tuliyoyataja kwa sababu ya kukosekana maana ya kurefusha na kutoa mifano mingi kati ya wanyama na

[47] Katika kitabu *Al-Mughni* mna maelezo haya; Kwa hakika wajuzi wa mji wa Madina kamwe huwa hawautambulishi kwa Thaur na Iyri." Hata hivyo si mbali sana kusema kuwa, huenda kwa sababu ya kupita muda mrefu majina yalibadilika.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 299 2/1/2017 3:51:56 PM

wanyama, kwani bila ya shaka mtu anayekwenda kuzuru Haram hizo mbili huenda akiwa na lengo la ibada tu, aliyeyapa nyongo hayo yote, wala haendi huko kwa lengo la kutembea au kuwinda.. Aidha, tumeacha baadhi ya mambo ambayo ni wajibu kuyaacha mtu anapokwenda Hijja, kama vile kubeba silaha kwa ajili ya kujikinga, na kukusanya nyasi kwa ajili ya chakula cha ngamia, na mengine mengi kama hayo ambayo hapana tena wasaa wa kuyazungumzia (tusipoteze bure muda), kwa kuwa maudhui yake yameishakupita au hutokea kwa nadra sana kama bado yanatokea.

# KUTUFU

Kutufu (al- Kaaba) ni nguzo miongoni mwa nguzo za Umra, na vilevile Twawafu *Ifadhwa* nayo ni nguzo ya *Tamattui*, *Ifrad* na *Qiran*. Huko nyuma tumetangulia kusema kuwa kuhirimia ndio kitendo cha mwanzo kabisa kinachopasa kuanziwa ibada, sawa awe amekwenda kufanya Umra ya *Mufrada* (isiyoambatana na Hijja) au awe amekwenda kuhiji Hijja ya *Tamattui*, *Ifrad* au *Qiran*.

## KATI YA ANAYEHIJI NA ALIYE KWENYE UMRA:

Sasa imebaki tujue; ni tendo gani la pili linalofuatia moja kwa moja baada ya kuhirimia, je ni kutufu au kusimama Arafah, au ni tendo gani?

Jibu: Ipo tofauti katika jambo hilo kulingana na mtekelezaji wa ibada hiyo na kusudio lake alilodhamiria wakati wa kuhirimia kwake. Kama alihirimia Umra basi itamlazimu afuatishe Twawafu na si amali nyingine, sawa awe alitaka kufanya Umra *Mufrada* au Umra *Tamattui*. Kwani Twawafu kwa mtu mwenye kufanya Umra ndilo tendo la pili kwake baada ya kuhirimia, kwa itifaki ya mafakihi.

Ama katika kuhirimia kwake iwapo alikusudia Hijja tu, kama pale anapokusudia Hijja *Ifrad* au Hijja *Tamattui* baada ya kumaliza amali zake za Umra, basi yeye baada ya kwisha kuhirimia tendo la pili kwake ni kusimama Arafah, maelezo kamili yatafuata.

Na kwa maelezo mengine ni kuwa, anayeingia Makka kwa ajili ya Umra tu, au kwa ajili ya Hijja *Tamattui,* basi kwanza kabisa kabla hajafanya amali nyingine yoyote, ataanza kwa kutufu, kisha atasai (kati ya Swafa na Marwa), kisha atapunguza nywele. Na baada ya hayo yote ndio atahirimia upya kama yuko katika Hijja *Tamattui,* ama kama yuko katika nyingineyo, si wajibu kwake kwenda moja kwa moja kutufu baada ya kuhirimia, bali ataichelewesha Twawafu hadi baada ya kusimama Arafah na baada ya kushuka Mina. Maelezo yake yatafuata kwa kirefu.

## VIGAWANYO VYA TWAWAFU KWA SUNNI:

Maimamu wa madhehebu manne wameigawa Twawafu katika vigawanyo vifuatavyo:

**1.** *Tawaful Qudum*: Ambayo hufanywa na mahujaji wanaotoka nchi za nje, na wasiokuwa wakazi wa Makka na vitongoji vyake. Hutufu Tawafu hiyo mara tu wanapoingia Makka, nayo inafanana sana kwao na rakaa mbili za *Tahiyyatul* Masjid. Na ni kwa ajili hiyo ndiyo ikaitwa; *Twawafut-Tahiyyah* (Twawafu ya kuamkia al-Kaba). Wameafikiana kuwa, kutufu huko kumependekezwa tu, kwa hivyo atakayeacha halazimiki kutoa chochote, isipokuwa Maliki wamesema: "Anayeacha kutufu Tawawafu hiyo hulazimika kuchinja."

**2.** *Twawafuz-Ziyara*: Ambayo pia huitwa T*wawaful Ifadhw*a, na Twawafu hii hufanywa na mwenye kuhiji baada ya



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 301 2/1/2017 3:51:56 PM

kwisha kutekeleza amali zake za Mina, kutupa vijiwe hapo Jamaratul Aqaba, kuchinja, kunyoa au kupunguza nywele, basi atarejea tena Makka na kutufu. Na Twawafu hii iliitwa Twawafu ya *Ziyara* kwa sababu aliyehiji huwa ameiacha Mina na kuizuru al-Kaaba kwa ajili yake. Na iliitwa *Twawafu Ifadhwa* kwa kuwa haji huwa amerejea Makka kutokea Mina. Vilevile huitwa Twawafu ya Hijja kwa kuwa Tawafu hiyo ni nguzo katika nguzo za Hijja kwa itifaki ya mafakihi. Na kwa kutimiza Tawafu hii huwa halali kwake kila kitu kilichokuwa haramu kwa aliye Hijja, hata kuwaingilia wake zao kwa mujibu wa madhehebu yasiyokuwa ya Imamiyya. Ama Maimamiyya wao wamesema: "Haiwi halali kwake kujamiiana na mwanamke hadi akasai kati ya Swafa na Marwa, kisha atufu Twawafu ya pili. Na ni kwa ajili hiyo ndio Twawafu hii ikaitwa Twawafu *Nisaa* (Twawaf ya kuhalalisha kujamiiana). Hivi punde itatufunukia baada ya maelezo yake yatakayofuata.

**3.** *Twawaful Wadaa*: Nayo ndio amali ya mwisho inayofanywa na Alhaji anapojitayarisha kutoka Makka kwa safari ya kurudi kwao. Mahanafi na Mahanbali wamesema kwamba Twawafu hiyo ni wajibu lakini anayehiji anapoiacha hulazimika kuchinja tu. Maliki wamesema: "Ni Sunna, na kamwe hakuna chochote anacholazimika kutoa anayeiacha." Imam Shafii ana kauli mbili. (*Al-Mughni, Fiqh Alal Madhahibil Arbaa* na *Fiqh Sunnah*)

## VIGAWANYO VYA TWAWAFU KWA SHIA:

Shia wameafikiana na Ahlul Sunna kuwa Twawafu hizi tatu ni wajibu, na kuwa hiyo ya pili ambayo ni *Twawafuz-Ziyara* ni nguzo mion-



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 302 2/1/2017 3:51:56 PM

goni mwa nguzo za Hijja, na Hijja hubatilika kwa kuiacha Twawafu hiyo.[48]

Na kwamba hiyo Twawafu ya kwanza nayo ni T*wawaful Qudum* ni Sunna tu, inajuzu kuiacha. Ama Twawafu ya tatu nayo ni hiyo *Twawafu Wadaa,* Shia wanaafikiana na Maliki kuwa ni Sunna ambayo hawajibiki aliyeiacha kutoa chochote.

Lakini Shia wameongezea Twawafu nyingine baada ya hizo tatu, nayo ni *Twawafun Nisaa,* wakasema: Twawafu hiyo ni wajibu na kwamba haifai kuiacha katika Umra *Mufrada* na hata katika Hijja, katika aina zake zote, iwe ni *Tamattui*, *Qiran* au *Ifrad*. Hawakujuzisha kuiacha isipokuwa katika Umra *Tamattui*, kwa kutosheka na Twawafu *Nisaa* ambayo ni sehemu ya Hijja *Tamattui*.

Na kwa kauli nyingine ni kuwa Sunni wamesema: "Baada ya Twawafu ya Hijja hakuna Twawafu nyingine iliyo wajibu, na kwamba baada ya hiyo ya Hijja huwa halali kujamiiana."

Shia wamesema: "Sivyo hivyo, bali anayehiji baada ya kwishakutufu Twawafu ya Hijja, aende akasai kisha atufu kwa mara ya pili. Na Twawafu hii ya pili ndiyo hasa Twawafu inayohalalisha kujamiiana." Wakasema tena: "Anayehiji anapoacha kutufu Twawafu hii huwa haramu juu yake wanawake, na hata kufunga ndoa, kama alikuwa ni mwanamume, na kama ni mwanamke huwa ni haramu kwake wanaume, hadi mtu huyo atakapofanya Twawafu hiyo yeye mwenyewe au kwa kumwajiri mtu wa kuitufu badala yake. Na kama kijana mdogo aliye mtambuzi atahiji kisha asitufu Twawafu ya Nisaa, hata kama ni kwa kusahau au kwa sababu ya kutojua ulazima wake, anapobaleghe wanawake watakuwa haramu kwake na hana ruhusa ya kuoa hadi akaitekeleze Twawafu hiyo yeye mwenyewe au amuweke naibu atakayekwenda kutufu badala yake."

[48] Mwenye kitabu *Al-Hadaiq* amesema: "Mtu anapoiacha kwa makusudi Hijja yake hubatilika. Na ni wajibu kuilipa aiachapo kwa kusahau."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 303 2/1/2017 3:51:56 PM

Kwa ujumla Shia wanawajibisha kwa mtu anayehiji Hijja *Tamattui* kutufu Twawaf tatu: Ya kwanza, ni ya Umra, nayo ni nguzo katika hiyo Umra, ya pili, ni Twawafu ya Hijja, nayo vilevile ni nguzo katika Hijja. Ya tatu, ya wanawake, nayo ni sehemu ya wajibu, si nguzo, inafanana na Sura Al-Fatiha kwenye Swala. Ama Sunni, wao wanakubaliana na Shia katika hayo yote isipokuwa katika Twawafu Nisaa, kwani wao wanaikana. Ama *Mufrad* na *Qiran* kila moja kati ya hizo ina Twawafu mbili kwa mujibu wa madhehebu ya Shia.[49]

## WAKATI WA KUINGIA MAKKA:

Wameafikiana kuwa inapendekezwa kwa anayeingia Makka aoge kwanza na aingine kwa upande wa nyanda za juu, tena iwe ni kupitia mlango wa Bani Shaiba, na anyanyue mikono yake miwili anapoiona Nyumba tukufu. Apige Takbira na alete Tahlil kisha aombe dua zilizopokewa au aombe dua yoyote anayoiweza. Isipokuwa Malik yeye amesema: "Asinyanyue mikono yake kuomba dua, bali aende hadi kwenye jiwe jeusi (Hajarul Aswad) akalibusu au aliguse kama akiweza kufanya hivyo, la hakuweza; basi atalinyooshea mkono wake kisha ndio aombe dua."

Maimamiyya wamesema: "Inasuniwa aingine Makka bila viatu miguuni na atafune Adhkhar - mmea unaonukisha kinywa kwa harufu njema), kama hakuweza basi atasafisha kinywa chake (kama kwa kupiga mswaki) na ajibidiishe kuondoa harufu mbaya ya kinywa chake."

---

[49] Ibn Rushd katika kitabu chake *Al-Bidaya* amesema: "Mafakihi wote wamekongamana kuwa mwenye kuhiji *Tamattui* kwa kuanzia Umra hadi Hijja, ni wajib kwake Twawaf mbili. Ama Mufrad Twawafu ni moja, wakakhitilafiana mwenye kuhiji Qiran, Shafi akasema: "Analazimika Twawafu moja." Amesema hivyo pia Ahmad na Malik. Abu Hanifa akasema: "Ni Twawafu mbili."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 304 2/1/2017 3:51:56 PM

## MASHARTI:

Mashafi., Maliki na Mahanbali wamesema: "Husharitiwa katika kutufu kuwa tohara kutokana na hadath na najisi, pia haiswihi kwa mwenye janaba, mwenye damu ya hedhi na mwenye damu ya nifasi. Na vilevile hushartiwa kujisitiri tupu kikamilifu kama ilivyo katika Swala."

Katika Juzuu ya tano ya kitabu *Fiqh Sunnah* uk. 154 chapa ya mwaka 1955 mtunzi wake As-Sayyid Sabiq amesema: "Mahanafi wanaona kwamba kujitoharisha hadath si sharti katika kutufu, bali ni wajibu unaomlazimisha mtu kumwaga damu (ya mnyama) pindi anapokiuka wajibu huo. Hivyo kama mtu atakuwa ni mwenye hadath ndogo (kukosa wudhu), akatufu akiwa katika hali hiyo, Twawafu yake itaswihi lakini atalazimika kuchinja mbuzi. Na kama atatufu hali ya kuwa ni mwenye janaba au hedhi,[50] pia Twawafu itaswihi lakini atalazimika kuchinja ngamia na arudie kutufu maadamu bado yuko Makka."

Na katika kitabu *Fiqh Alal Madhahibil Arbaa* Juzuu ya kwanza, uk. 535 kilichochapishwa mwaka 1939. Mna maneno haya: "Ama utohara wa nguo na mwili na mahali pa kutufu ni Sunna iliyosisitizwa kwa mujibu wa madhehebu ya Kihanafi, na kama atatufu hali ya kuwa nguo zake zote ni zenye najisi, halazimiki malipo yoyote (kama fidia)."

---

[50] Katika kitabu *Al-Jawahir,* kitabu *Al-Hadaiq,* A*l-Masalik*, *Urwatul Wuthqa* na vinginevyo katika vitabu vya Fiqh ya Kiimamiyya, mmeandikwa maneno haya: "Kwa hakika mwenye janaba na mwenye hedhi haijuzu kwao kupita na kufanya njia (mkato) katika msikiti mtukufu (haram Makka) au ndani ya msikiti wa Mtume ﷺ wachilia mbali kukaa, lakini hujuzu kwa watu wenye hadath hizo kupita kama njia bila ya kukaa ndani ya misikiti mingineyo. Na kwa maelezo haya utaeleweka uzushi na upachikaji uwongo waliobandikizwa Imamiyya, walipozuliwa kwamba wao huenda kwenye Masjidul Haram (msikiti wa Makka) kwa uchafuzi.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 305 2/1/2017 3:51:56 PM

Maimamiyya wamesema: "Utohara kutokana na hadath na najisi ni sharti katika Twawafu ya wajibu, aidha husharitiwa kujisitiri tupu kwa nguo tohara zisizokuwa za kupora. Tena isiwe zimetokana na hariri wala dhahabu, sawa na ilivyo katika Swala." Bali wengi katika wao wamelitilia mkazo jambo la Twawafu hata kuliko Swala, maana katika Swala wamesema kuwa husamehewa damu chache iliyo na uduara unaolingana na uduara wa dirham, lakini hawajaisamehe katika Twawafu, na kwamba wanawake hawaruhusiwi kuvaa nguo za hariri na kujipamba kwa dhahabu."

Hao Maimamiyya wamesema tena: "Mtu anayetufu anasharitiwa awe ametahiriwa, kamwe haitoswihi kwa mtu mwenye govi (zunga), awe ni mtu mkubwa au mtoto." (*Al-Jawahir* na kitabu *Al-Hadaiq)*.

## NAMNA YA KUTUFU

Hapana budi uitaje Twawafu kwa dhati yake katika nia. Kwa mujibu wa Maimamiyya na Mahanbali.

Maliki, Mashafi na Mahanafi wamesema: "Hutosha kutia nia ya Hijja kwa ujumla, kamwe haisharitiwi kutia nia maalum ya kutufu." (*Al-Jawahir*).

Na tumetangulia kusema huko nyuma kuwa, nia ni dhamira ya kutaka kutenda jambo, na vilevile nia ni sababu au msukumo fulani anaokuwa nao mtu wakati anapotaka kufanya jambo, kwa hiyo jambo hilo halina haja ya kugombania au kujadiliana bure kupoteza wakati, kwa sababu nia ni jambo linalotendeka moyoni mwa mtu kwa lazima kila anapokusudia kufanya jambo apende au asipende.

Na katika kitabu *Bidayatul Mujtahid* cha Ibn Rushd mmeandikwa maneno yafuatayo: "Na kwa mujibu wa kongamano la mafakihi wa



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 306 2/1/2017 3:51:56 PM

Kisuni wamesema kwa kauli moja kwamba, namna yoyote ile ya Twawafu iwe ni ya wajibu au isiyokuwa ya wajibu, hapana budi ianziwe palipo na jiwe jeusi (*Hajarul Aswad)*. Na katika kitabu *Fiqh Sunnah* imeelezwa kuwa: 'Na amalizie hapo hapo.' Na kama ataweza kulibusu basi alibusu au aliguse, na alibusu tena baada ya kuligusa kama itawezekana. Aiweke al-Kaaba upande wake wa kushoto wakati wa kutufu, aende kufuatia upande wake wa kulia wakati akiizunguka, na aizunguke mizunguko saba, aizunguke kwa mwendo wa haraka[51] katika mara zake tatu za kwanza, kisha katika mizunguko minne iliyobaki atakwenda mwendo wa kawaida. Hali hiyo ya mwendo wa haraka ifanyike katika kutufu Twawafu *Qudum*, mara tu baada ya kuingia Makka kwa kusudio la Hijja au Umra, lakini si kwa mwenye Hijja *Tamattui*, wala mwanamke. Na atagusa nguzo ya Yamani."

Maimamiyya wamesema: Kutufu kuna wajibu zake, nazo ni:

**1.** Kutia nia, maelezo yake yametangulia.

Atufu kwa mwendo wa miguu kama anaweza, akishindwa atufu hali ya kuwa amepanda (mnyama). Sharti hili wengi katika wanavyuoni wa Kiimamiyya hawakulipa uzito, hata hivyo kundi katika wao wametoa rai kuwa inaruhusiwa kutufu juu ya mnyama kwa kuhiari, kama ilivyokuja katika kitabu *Al-Kafi* na kitabu *Manla Yahdhuruhul Faqih,* kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alitufu juu ya ngamia wake.

**2.** Aanzie Twawafu kwenye jiwe jeusi, kwa namna ambayo sehemu ya mwili wake itakuwa imeelekeana na sehemu ya mwanzo ya jiwe hilo wakati wa kuanza kutufu, kisha aanze

[51] Kuchapuka mwendo maana yake ni kuenda mwendo wa haraka huku hatua zake zikikaribiana bila ya kuruka au kupiga misamba, katika kitabu *Al-Lumma'ah* cha kiimamiya mnaelezwa kuwa kuchapuka husunniwa katika mizunguko mitatu ya kwanza katika Twawaf Qudum sawa sawa kwama walivyo kongamanana mafakihi wote.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 307 2/1/2017 3:51:56 PM

> mwendo kwa upande wa kushoto, na amalizie hapo hapo, kwa namna ambayo ataelekeana nalo kama alivyoanza, kwa kukamilisha mizunguko saba bila ya kupungua au kuzidisha hatua. Na kwa sababu ya kuchelea kuzidisha au kupunguza hatua ndio maana imekuwa ni wajibu kuanzia mwanzo wa jiwe, kwani kama ataanzia katikati yake hatakuwa na usalama wa kutozidisha au kupunguza. Na kama ataanzia upande wa mwisho wa jiwe atakuwa hakuanzia palipo na jiwe … Na maelezo mengine kadha yalisemwa kuhusiana na sharti hili.

Maelezo haya na mengine mengi mfano wake yameelezwa katika vitabu vya Fikihi. Mwenye kitabu *Al-Jawahir* ameyatundika maelezo marefu yanayotoa dalili ya usawa wa kimaumbile na usalama wa kitabia. Na mimi nitadondoa sehemu chache tu ya maelezo yake marefu kama ifuatavyo: "Haifichiki hali ya kuwepo uwezekano wa kupatikana mashaka, shida na dhiki, wakati wa kuzingatia nukta hiyo, hasa katika wakati wetu huu wa leo kutokana na msongamano mkubwa wa Mahujaji. Na hakika kuizingatia nukta hiyo huenda kukazusha wasiwasi kama ambavyo huo wasiwasi ni katika hali ambazo zinafanana sana na wendawazimu.[52] Bila shaka imepokewa kuwa Mtume ﷺ alifutu akiwa juu ya mnyama wake, katika hali kama hiyo nukta hiyo haiwezi kutimia wala kutekelezwa na mtu aliye juu ya mnyama."

Tunalolifahamu kutokana na jumla ya maneno yake ni kuwa yeyote anayechagua kauli ya mwenye kitabu *Sharaiu* ambacho ni matini ya kitabu *Al-Jawahir*, ambapo ndani yake Sheikh hakuongeza chochote zaidi ya ibara hii: "Wajibu ni kuanzia palipo na jiwe na kumalizia hapo hapo," na maana yake ni kama ilivyo dhahiri katika ibara ya *Al-Jawahir,* unatosha ulingano wa kijamii.

[52] Ibara hii ameitaja mwenye *Al-Jawahir* muda alipotoa mshabaha unaowahusu baadhi ya watu walio na wasiwasi mwingi wakati wa kutia nia ya Swala, akawafananisha na hao walioweka masharti chungu nzima ya Twawafu.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 308 2/1/2017 3:51:56 PM

Na kauli ya Sayyid Al-Hakim katika *Mansak* inaeleza na kuhisisha dhana hiyo, anasema: "Ni juu ya anayetaka kutufu, aanzie nje kidogo kabla ya jiwe jeusi akiwa amekusudia kutekeleza linalopasa juu yake katika huko kutufu kwake, (nako ni kuanzia palipo na jiwe na kumalizia hapo). Kama atatufu kama hivyo basi itaeleweka kwamba kaanzia palipo na jiwe na kumalizia hapo."

**3.** Ni kuiweka al-Kaaba upande wake wa kushoto, Sayyid al-Hakim amesema: "Hutosha katika kupata uhakika wa kuiweka kushotoni kupatikana uhakika wa kijamii, kamwe haidhuru kugeuka kidogo maadamu uhakika wa kuwa ipo kushotoni mwake upo." Sayyid Khui amesema: "Dhahiri ni kuwa linalozingatiwa ni kuwepo uhakika wa kuelekea kunakofahamika."

**4.** *Hajar Ismail* iwe ndani wakati wa kutufu. Kwa maana ya kuwa atufu kando yake pasina kuingia ndani yake.[53] Nayo iwe upande wake wa kushoto, na kama atatufu kupitia kati-kati yake baina ya al-Kaaba na *Hajar Ismail* kwa kuiweka upande wake wa kulia, basi Twawafu yake itakabilika.

**5.** Awe mwili wake wote uko nje ya al-Kaaba. Kwa kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amesema: "Na waizunguke (kwa kando yake) nyumba ya kale." (Al-Hajj:29). Kwa maana waitufu kando yake kwa kuizunguka, si kuingia ndani yake. Katika lugha ya Kiarabu wewe husema; '*Marartu Bizaid*; Nimepishana na Zaid', husemi 'Marartu Fizaid; Nimepishana ndani ya Zaid.' Basi kama atapita juu ya ukuta wake au katika kiasi kilichobaki nje katika msingi wa ukuta wake

[53] Hijri Ismail bin Ibrahim عليه السلام ilikuwa nyumba yake, na humo mna kaburi la mama yake. Katika *Al-Jawahir* amesema kuwa Imam Ali aliulizwa kuhusu Hijri Ismail akasema: "Nyie mnaliita Hatim, ambalo lilikuwa ni zizi la mbuzi wa Ismail. Mama yake alizikwa hapo, naye kwa kuchelea lisije kukanyagwa akaliweka jiwe juu yake."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 309 2/1/2017 3:51:56 PM

baada ya jengo lake, Twawafu itabatilika. Na lililokusudiwa katika neno *Baitul Atiq* (nyumba ya kale) ni al-Kaaba aliyoitukuza Mwenyezi Mungu.

**6.** Twawafu yake itendeke kati ya al-Kaaba na Maqam Ibrahim, jiwe ambalo Ibrahim عليه السلام alisimama juu yake alipokuwa akiijenga al-Kaaba.

**7.** Ni kukamilisha mizunguko saba kamili bila kuzidi wala kupungua. Njia bora zaidi ili kufanya usawa katika kufanya kama inavyotakikana, ni kuwa na mtu anayejua vyema maeneo hayo ili amwelekeze na kumweleweshа.

**8.** Na anapomaliza Twawafu yake ni wajibu juu yake kuswali rakaa mbili kando ya Maqam Ibrahim, hata panapokuwepo msongamano wa watu. Na kama haiwezekani basi aswali popote pale anapoweza humo msikitini kuziswali. Hulazimika kufanya hivi inapokuwa Twawafu aliyotufu ni ya wajibu, na kama ni ya Sunna ataziswali atakapo. (kitabu At-*Tadhikira*, *Al-Jawahir* na *Hadaiq*).

Na kwa maelezo haya inabainika wazi kuwa mafakihi wa madhehebu yote wameafikiana kuwa Twawafu huanzia panapo jiwe jeusi na kumaliza hapo hapo. Na kuiweka al-Kaaba ubavu wa kushoto kwa anayetufu. Katika hali ya kuwa nje ya a-Kaaba, na kuwa Twawafu ni mizunguko saba, na kwamba kuligusa jiwe na nguzo ni Sunna.

Kisha wamekhitilafiana kuhusu kufuatanisha na kutoacha mwanya kati ya mizunguko hiyo saba. Maliki, Maimamiyya na Mahanbali wamewajibisha. Mashafi na Mahanafi wamesema: "Ni Sunna, kama mtu atatenganisha kwa kipindi kirefu pasi na udhuru wowote, Twawafu haibatiliki, bali ataunganisha Twawafu yake mahali alipokomea." (*Fiqh Sunna*).



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 310 2/1/2017 3:51:56 PM

Akasema tena Abu Hanifa: "Anapotufu mizunguko minne kisha akaacha, kama bado atakuwa angalipo Makka itamlazimu kukamilisha Twawafu yake. Na kama itakuwa ameshaitoka Makka atalazimika kuchinja." (*At-Tadhikrah)*.

Wamehitilafiana tena kuhusu wajibu wa kutufu kwa miguu, Mahanafi, Mahanbali na Maliki wamewajibisha. Mashafi na kundi katika Maimamiyya wamesema: "Si wajibu na inajuzu kutufu kwa miguu au kutufu juu ya mnyama akipenda."

Aidha wamekhitalifiana kuhusu rakaa mbili zinazoswaliwa baada ya kutufu. Maliki, Mahanafi na Maimamiyya wamesema: "Ni wajibu, nazo ni kama Swala ya asubuhi hasa." Mashafi na Mahanbali wamesema kuwa ni Sunna tu.

**SUNNA ZA TWAWAFU:**

Imeandikwa katika kitabu *Fiqh Sunnah* chini ya kichwa cha maneno 'Sunna za Twawafu' maelezo yafuatayo: "Twawafu ina Sunna nyingi miongoni mwazo ni kulibusu jiwe jeusi wakati wa kuanza kutufu, pamoja na kuleta Tahlil na Takbir, kuinua mikono miwili kama inavyofanywa katika Swala, kuligusa jiwe jeusi kwa mikono miwili hiyo kwa kuigusisha juu yake. Na kulibusu kwa mdomo bila ya kutoa sauti (ya busu), kuweka shavu juu yake kama itawezekana, la haiwezekani basi ataligusa tu. Na katika Sunna zake ni kuvaa rubega,[54] na miongoni mwake ni kuharakisha mwendo na kugusa Nguzo ya Yamani."

Katika kitabu *Allumuatud – Dimishqiyya* cha Maimamiyya mmeelezwa hivi: "Miongoini mwa Sunna za Twawafu ni kusimama

[54] Kuvaa rubega ni kupitisha katikati ya shuka chini ya kwapa la kulia na pembe zake mbili zije juu ya bega la kushoto. Na katika kitabu *Fiqh alal madhahibil arba* kusunniwa kuvaa rubega kumenasibishwa kwa Shafiiyya na Hanbaliyya lakini hakukunasibishwa kwa Malikiyya.

mkabala na jiwe jeusi na kuomba dua hali ya kuinua mikono yake miwili, kusoma Suratul Qadr, na kumtaja Mwenyezi Mungu (s.w.t.). Na kuwa na utulivu wakati wa kwenda (twawaf) na kuligusa jiwe jeusi na kulibusu palipo na uwezekanao, na kuliashiria kwa mkono. Na kuzigusa nguzo zote kila apitapo kwenye nguzo hizo, na kuzibusu. Na kuigusa nguzo Mustajar katika mzunguko wa saba, nayo imeelekea mlango wa al-Kaaba, mbali na Nguzo ya Yaman. Na kuikurubia al-Kaaba, na ni makruh kusema sema maneno yasiyokuwa dhikri au Qur'ani."

Aidha Maimamiyya wamesema: "Inapendekezwa anayetufu, atufu twawafu 360, na kama hakumudu basi angalau mizunguko 36, na ziyada hiyo iunganishwe na mzunguko wa mwisho. Na kwa mazingatio haya inaelekea kufutika kwa karaha ya kuzidisha mara."

**HUKMU YA TWAWAFU:**

Maimamiyya wamesema: "Pindi mwanamke anapozukiwa na damu ya hedhi wakati akiwa katika Twawafu, kama itamzukia baada ya mzunguko wa nne atakatiza Twawafu yake kisha aende akasai, na amalizapo kusai atakamilisha Twawafu akishatoharika, na wala haitamlazimu tena kusai. Na kama itatokea kabla ya kutimiza mzunguko wa nne, atangojea Arafah; na kama ametwahirika na amepata uwezo wa kufanya amali nyingine atafanya, la hakuweza basi Hijja yake itakuwa Hijja *Mufrada*."

Tumetangulia kusema kuwa Mahanafi wanajuzisha kwa mwanamke mwenye damu ya hedhi kufanya Twawafu, kamwe katika kutufu hawakushurutishwa utohara.

Katika kitabu *Fathul Qadir* cha Mahanafi imeandikwa: "Katika Twawafu Ziyara, mtu anapoiacha mizunguko mitatu na chini ya hapo hulazimika kuchinja mbuzi. Na anayeacha mizunguko minne



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 312 2/1/2017 3:51:56 PM

huendelea milele kuwa ni aliye katika ihramu (sawa na kuwa bado hajafanya Twawafu), hadi atufu, kwa kuwa sehemu aliyoiacha huwa ni nyingi zaidi kuliko aliyotufu, kwa hivyo huwa kana kwamba hajatufu."

Maimamiyya wamesema: "Anapomaliza mizunguko ya Twawafu kisha akazukiwa na shaka, ya kuwa je amezileta kwa usahihi kama inavyotakikana kisharia, na kuwa hakuzidisha au kupunguza, au imezidi na au amepunguza? Hapo Twawafu yake haiathiriki kwa shaka kama hiyo, bali atajipa moyo wa kuwa ameleta kwa usawa kama inavyotakikana na pia imetimia, na ataendelea na amali zake nyingine bila ya kufanya chochote.

Na kama shaka yake ni kabla ya kumaliza, basi atachunguza iwapo ametimiza mizunguko saba katika hali yoyote ile, kama lau atatia shaka kati ya amezunguka mizunguko saba au nane, atapitisha kuwa ametufu kwa usahihi na ishie hapo.

Na kama hatakuwa na uhakika thabiti wa kukamilisha mizunguko saba, kama pale atakapokuwa na shaka ya kuzunguka kati ya mizunguko sita au saba, mitano au sita, na kuendelea chini ya hapo, basi Twawafu yake yote itabatilika tangu shinani, naye itamlazimu aianze upya. Na ilivyo bora ni kuikamilisha hiyo iliyozukiwa na shaka hatimaye aanze nyingine mpya.

Na hukmu hiyo inahusu Twawafu iliyo ya wajibu, ama ya Sunna basi anayetufu atajengea daima kwenye uchache na kisha atatimiza iwapo moja kati ya sehemu mbili za shaka yake itakuwa haifikii mara saba (katika mizunguko aliyozunguka), pasina kuweka tofauti kati ya kuwa shaka yake imemzukia katikati ya Twawafu au imemzukia mwishoni mwa mzunguko wa mwisho.

Ama wasiokuwa Maimamiyya kaida kwao ni kujengea kwenye uchache zaidi katika kuchukua yakini, kama ilivyo katika shaka kwenye idadi ya rakaa.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 313 2/1/2017 3:51:56 PM

Hii ndiyo Twawafu kwa mambo yake ya wajibu, Sunna na hukmu zake. Nayo kikamilifu ni namna moja tu kama ilivyo rukuu na sijda katika Swala, huwa ni kwa namna moja katika Swala ya faradhi na ya Sunna, na Twawafu ni vivyo hivyo, ni namna moja sawa iwe ni sehemu ya Umra *Mufrada*, au Umra *Tamattui*, au Hijja *Qiran* na *Ifrad*, iwe ni Twawafu Ziyara, Twawafu *Nisaa*, Twawafu *Qudum* au Twawafu *Widaa*.

Huko nyuma tumetangulia kuonyesha kuwa Twawafu hufanywa mara moja tu baada ya kuhirimia katika amali za Umra, iwe ni *Mufrada* au Umra *Tamattui*. Ama katika amali za Hijja Twawafu huja baada ya anayehiji kumaliza ibada yake huko Mina siku ya Idd, na maelezo kamili yatafuata baadaye chini ya kichwa cha maneno: Mina na kuendelea.

## KUSAI NA KUPUNGUZA NYWELE

Wameafikiana kuwa kusai hufuata baada ya Twawafu, na pia baada ya kuswali rakaa mbili za Twawafu, kwa wale waliowajibisha rakaa mbili za Twawafu. Na kwamba atakayesai kabla ya kutufu basi itamlazimu arejee akatufu, kisha ndio akasai. Na mimi sikumpata yeyote kati ya mafakihi aliyewajibisha kufuatanisha baina ya Twawafu na kusai, kwa hali ya kuanza kusai mara moja baada tu ya kumaliza kutufu.[55]

[55] Amesema Sayyid al-Hakim: "Si wajibu kufanya haraka kwenda sai baada ya kumaliza kutufu na Swala yake, lakini haijuzu kuichelewesha hadi kesho yake kwa hiyari." Sayyid Khui amesema: "Ni juu yake asicheleweshe kusai baada ya kutufu na Swala yake, kwa muda usio wa kawaida, wala haijuzu kuahirisha mpaka kesho yake pamoja na hiyari." **Nasema:** Walivyoonelea mabwana hawa wawili ni haki ambayo imejulishwa na Hadith sahih, kinyume na dhahiri iliyomo katyika kitabu Sharaiu. Na imekuja katika kitabu *Mansak* cha Sayyid al-Hakim: "Haizingatiwi kufuatanisha katika mizunguko ya Sai, inajuzu kutenganisha, kuikata kisha kuunganisha na ya mwanzo, hata kama ni baada ya mzunguko wa kwanza."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 314 2/1/2017 3:51:56 PM

## YALIYO SUNNA WAKATI WA KUSAI:

Ndani ya kitabu *Fiqh Sunna* imeandikwa: "Inasunniwa kupanda juu ya jabali Swafa na Marwa, na kuomba dua juu yake kuhusu chochote anachotaka kuomba katika mambo ya dini na dunia, huku akiwa ameelekea Kibla."

Linalojulikana katika tendo la Mtume ﷺ ni kuwa alitokea mlango wa Swafa… kisha akapanda juu yake hadi akawa anaiona Nyumba tukufu, akaelekea Kibla, akampwekesha Mwenyezi Mungu, akamtukuza kwa takbira tatu, akamhimidi na akasema:

*Lailaha Ilallahu Wahdahu Lashariikalahu, Lahulmulki Walahulhamdi, Yuhyi Wayumit Wahuwa alakulishayin Qadir. Lailaha Ilallahu Wahdahu. Anjaza Waadahu, Wanaswara Abdahu, Wahazamal Ahzaba Wahdahu.*

Maana yake: "Hakuna Mola wa haki isipokuwa Allah peke yake, hana mshirika, ufalme ni Wake, na shukrani ni Zake, huhuisha na kufisha, naye ni Muweza juu ya kila kitu. Hakuna Mola isipokuwa Allah peke yake, ametimiza waadi Wake, akamnusuru mja Wake na akayashinda makundi (ya maadui) peke Yake."

Katika kitabu cha Maimamiyya *Al-Jawahir* imeandikwa: "Yasunniwa kuligusa jiwe, kunywa maji ya Zamzam na kujimwagia mwilini, na kutokea kutoka kwenye mlango unaokabiliana na jiwe jeusi na apande jabali Swafa, ailekee nguzo ya Iraq, amshukuru Mwenyezi Mungu na kumsifu kwa sifa Zake njema. Arefushe muda wa kusimama Swafa na amtukuze Mwenyezi Mungu kwa Takbira na aseme: *Lailaha Ilallahu Wahdahu Lasharikalahu, Lahulmulki Walahulhamdi, Yuhyi Wayumit Wahuwa Hayyun Layamut Biyadihilkhair Wahuwa Alakullishayin Qadir.* Aikariri mara tatu na kisha aombe dua iliyopokewa."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 315 2/1/2017 3:51:56 PM

Hapa kama unavyoona hakuna tofauti baina ya Maimamiyya na Sunni isipokuwa kitu kidogo katika maelezo, na sikuoana yeyote kati ya mafakihi ambaye amewajibisha utohara wa hadath na najis katika kusai, bali mengi katika madhehebu yameeleza waziwazi kuwa imependekezwa, kama ambavyo wote isipokuwa Mashafi wamekubaliana kuwa mtu anatakiwa kwanza aliguse jiwe ndio aende akasai.

Vilevile wamekongamana kuwa husunniwa kwa anayesai aende kwa mwendo wa haraka afikapo *Maylayni* kwa mujibu wa maelezo ya Mahanafi na Maliki. Na afikiapo katikati ya masafa, kwa mujibu wa maelezo ya Mashafi. Na afikapo kati ya mnara na *Zaqaq At-Tarain* kwa mujibu wa maelezo ya Maimamiyya. Hapana shaka yoyote kwamba kuvijua vituo hivyo vilivyotajwa na kila madhehebu itabidi apatikane kiongozi anayevijua.

## JINSI YA KUSAI:

Wameafikiana juu ya ulazima wa kusai kati ya Swafa na Marwa,[56] lakini wamekhitilafiana kuhusu je kusai ni nguzo au hapana. Maimamiyya, Mashafi na Maliki wamesema: “Ni nguzo.” Abu Hanifa amesema: “Ni wajibu si nguzo.” Ahmad ana riwaya mbili (Taz. *At-Tadhikira* na *Fiqh Sunna)*.

Wameafikiana kuwa idadi ya mizunguko ya kusai ni saba, na kwamba anayesai aanzie mlima Swafa na amalize Marwa,[57] na arejee kutoka hapo Marwa hadi Swafa, vivyo hivyo hadi zitimie mara saba, na atahesabu kwenda ni duru kamili, na kurejea ni duru kamili. Kwa namna hii basi zitapatikana mara nne za kwenda kutoka Swafa hadi Marwa, na tatu za kurudi kutoka Marwa hadi Swafa. Hivyo Sai

[56] Swafaa na Marwaa ni mahali pawili penye majabali mawili yaliyo juu kiasi.

[57] Mwenye *Al-Mizan* amemnukuu Abu Hanifa akisema kuwa hapana ubaya wa kuanzia kinyume chake. Anayesai anaweza akaanzia Marwa akamalizia Swafaa.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 316 2/1/2017 3:51:57 PM

itakuwa imeanzia Swafa na kumalizikia mara ya saba upande wa Marwa.

Kisha mafakihi hao wamekhitilafiana kuhusu kujuzu kusai juu ya mnyama kwa anayemudu kwenda kwa miguu, wote isipokuwa Mahanbali wamesema: "Hujuzu kusai juu ya mnyama kwa awezaye kwenda kwa miguu na asiyeweza." Mahanbali wamesema: "Haijuzu isipokuwa kwa asiyejiweza tu."

Na mimi simwoni kati yao aliyewajibisha kutenganisha kati ya hizo duru za kusai[58] isipokuwa Mahanbali tu, imenukuliwa kutoka kwao na mwenye kitabu *Fiqh Alal Madhahabil Arbaa* kwamba kutenganisha ni wajibu kwao. Na kama hivyo imenukuliwa kutoka kwa Maliki kwamba anayetenganisha kwa muda mrefu basi itamlazimu aivunje na aanze upya, lakini husamehewa iwapo katenganisha kwa muda mchache. Kama pale kunapotokea haja ya kutaka kuuza bidhaa au kununua kwa muda usiokuwa mrefu sana.

**TANBIHI:**

Sayyid al-Hakim katika kitabu chake cha Ibada ya Hijja amesema: "Anayesai ni wajibu aelekee kwa uso wake kule anakokwenda, wakati wa kwenda na wakati wa kurudi kwake, hivyo kama anayesai hatoelekea aendako kwa uso wake, au akaenda kinyumenyume, au kiubavuubavu haitatosheleza … lakini hapana ubaya wa kugeuza uso kwa uchache hali ya kuwa sehemu ya mbele ya mwili wake imeelekea mbele anakokwenda."

Na maana ya kauli yake hii ni kuwa ni juu yako unayesai kuelekea Marwa kwa mwili wako wote wakati ukiwa katika mwendo wa kwenda Marwa, na kuelekea Swafa wakati wa kurudi, haijuzu

[58] Na imekuja katika kitabu *Mansak* cha Sayyid Al-Hakim: "Haizingatiwi kufuatanisha katika mwendo wa sai. Yaruhusiwa kutenganisha, kuzikata kisha kuunganisha na ya mwanzo, hata kama ni baada ya Sai ya kwanza."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 317 2/1/2017 3:51:57 PM

kwenda kiubavuubavu hali ya kuwa bega lako moja likiwa mbele, kama unavyofanya kwenye msongamano. Kwa hiyo unaruhusiwa kugeuza uso wako tu (ikiwa kuna ulazima wa kufanya hivyo) wakati wa kutembea bila ya kugeuza mwili wako wote.

Sayyid al-Khui katika kitabu chake cha Ibada ya Hijja amesema maneno yanayokaribiana na haya, na maelezo yake ndiyo haya: "Ni wajibu kuelekea Marwa wakati wa kwenda, kama ambavyo ni wajibu kuelekea Swafa wakati wa kurudi. Hivyo kama anayesai ataipa Marwa mgongo wakati wa kwenda, au akaipa mgongo Swafa wakati wa kurudi, haitatosheleza. Aidha haijuzu kugeukia kulia wala kushoto, wala kugeuza mgongo wakati wa kwenda na kurudi."

## HUKUMU ZA KUSAI:

Ambaye hakuweza kusai hata kwa kutumia mnyama basi atamweka naibu atakayesai kwa niaba yake, na Hijja yake itaswihi. Na wala hapana ubaya wa kugeukageuka kuliani wala kushotoni, na hata kugeuka nyuma wakati wa kwenda na kurudi.

Na anayezidisha zaidi ya mara saba kwa kukusudia, sai yake hubatilika, lakini anayezidisha kwa kusahau haibatiliki. Mtu anayesai anapotia shaka katika idadi ya mara alizokwenda na kurudi, au katika kuswihi kwake baada ya kumaliza kusai, atajipa uhakika wa kuwa iko swahihi na hatakuwa na chochote cha kufanya.

Na mwenye kitabu *Al-Jawahir* alitoa kithibitisho cha kuwa shaka hiyo ilimjia baada ya kumaliza, kutokana na misukosuko na kufuata habari za watu.

Na kama shaka ya idadi ya mara itakuwa imemzukia kabla ya kukamilisha idadi ya mizunguko, mwenye kitabu *al-Jawahir* amesema: "Hapana ikhitilafu, na hapana mushkil kuwa kusai huko kumebatilika kutokana na shaka hiyo, kwa sababu ya kuwepo



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 318 2/1/2017 3:51:57 PM

uwezekano wa kupungua au kuzidi, na yote hayo mawili kila moja linabatilisha.

Na anapotia shaka ya kuwa ameanzia Swafa, ili iwe swahihi, au kaanzia mahali pengine, ili iwe imebatilika? Hapo atachunguza kwa makini, kama atakuta shaka yake inahusu pia idadi ya mizunguko, kwa kiasi cha kuwa haelewi amezunguka mizunguko mingapi, kusai kwake kutakuwa batili.

Na kama aliidhibiti idadi ya mara alizokwenda na kurudi, lakini shaka yake ikawa ni katika upande alioanzia tu, iwapo mizunguko aliyokwishazunguka ni shufa, kama vile miwili, minne au sita naye akawa yuko upande wa Swafa au anaiendea Swafa, basi kusai kwake kutakuwa sahihi, kwa kuwa atakuwa anafahamu hali ilivyo, kwani katika hali hii ni kuwa alianzia Swafa. Na hukmu ni hiyo hiyo kama mizunguko aliyokwishazunguka ni witiri, kama vile mitatu, au mitano au saba, naye akawa yuko upande wa Marwa au anakwenda upande wa Marwa. Lakini kama jambo litakuwa kinyume, kama pale mzunguko utakapokuwa ni wa witiri, na yeye yuko Swafa, au mzunguko ni wa shufa, na yeye yuko Marwa, hapo kusai kwake kutakuwa batili, na ni wajibu kuanza upya. (kitabu *Al-Jawahir*).

Na kwa madhehebu yaliyobaki ni kwamba, anayezukiwa na shaka ya idadi ya mara alizokwenda atachukulia kuwa kaenda chache, kama ilivyo katika Swala. (*Kifayatul Akhyar*). Abu Hanifa amesema: "Lau mtu anayehiji ataacha kusai kabisa. Hijja yake haibatiliki kwa sababu sio nguzo bali atalazimika kuchinja."

## KUPUNGUZA NYWELE

Ahmad bin Hanbal na Malik bin Anas wamesema: "Katika kunyoa au kupunguza nywele, ni wajibu iwe kichwa chote." Abu Hanifa amese-



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 319 2/1/2017 3:51:57 PM

ma: "Hutosha robo yake tu." Shafi amesema: "Hutosha nywele tatu." (*Kararah*) Maimamiyya wamesema: "Mwenye kupunguza ana hiyari ya kupunguza nywele za kichwa au shArafah au ndevu au akate kucha."

Na wameafikiana kuwa kupunguza ni ibada ya wajibu, na si nguzo.

Sayyid al-Hakim amesema: "Uwajibu wake ni kama kutoa salam katika Swala. Kwa sababu kwa kupunguza huko, hujitoa ndani ya ihramu yule aliyekuwa ndani ya ihramu, kama ambavyo kwa salam hujitoa ndani ya Swala yule aliyekuwa ndani ya Swala."

Na ni wajibu kupunguza au kunyoa mara moja katika Umra *Mufrada,* na mara mbili katika Hijja *Tamattui*, na hapa tunakuletea maelezo yake kwa kirefu.

## KUPUNGUZA NYWELE KATIKA UMRA:

Maimamiyya wamesema: "Aliye katika Umra *Tamattui,* baada ya kusai ni wajibu kwake kupunguza nywele, kamwe haijuzu kwake kunyoa, na anapomaliza kupunguza nywele humhalalikia yote yaliyokuwa haramu juu yake wakati alipokuwa katika ihram. Na kama atanyoa basi itamlazimu atoe fidia ya mbuzi. Ama kama alikuwa akifanya Umra *Mufrada* bado atakuwa na hiari ya kujiamulia baina ya kunyoa na kupunguza nywele, hukmu hii ni sawa awe anaye mnyama wa kuchinja au hana.

Na iwapo ataacha kupunguza nywele kwa makusudi hali alikuwa amekusudia kuhiji Hijja *Tamattui*, na akahirimia Hijja kabla ya kupunguza nywele, Umra yake itabatilika, na hapo itakuwa ni wajibu kwake kuhiji Hijja ya *Ifrad*, kwa maana ya kuwa atafanya matendo ya Hijja kisha baada yake afanye matendo



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 320 2/1/2017 3:51:57 PM

ya Umra *Mufrada*. Na ilivyo bora ni kurudia Hijja hiyo mwaka utakaofuatia."[59]

Wasiokuwa Maimamiyya wamesema: "Mtu amalizapo kusai huwa na haki ya kujichagulia kati ya kunyoa nywele na kupunguza. Ama kuhalalikiwa na yale yaliyokuwa haramu juu yake; ataangalia kama alikuwa akifanya Umra isiyokuwa *Tamattui* basi yatamuhalalikia mara tu baada ya kupunguza nywele au kunyoa, sawa awe ana mnyama wa kuchinja au hana. Na kama alikuwa ni mwenye Umra *Tamattui* huwa ni halali kwake mambo hayo iwapo hakuwa na mnyama, na kama anaye mnyama atabaki kuwa ni aliye katika ihram. (A*l-Mughni*).

## KUPUNGUZA NYWELE KATIKA HIJJA:

Kupunguza nywele kwa mara ya pili ni miongoni mwa ibada za Hijja katika aina zake zote, iwe ni *Tamattui*, *Ifrad* au *Qiran*. Na atafanya kitendo hicho baada ya kumaliza huko Mina.

Wameafikiana kuwa atahiyari kati ya kupunguza nywele au kunyoa, na kunyoa ni bora zaidi, kisha wamekhitilafiana kuhusu mtu mwenye nywele ndogo; je mtu huyo hulazimika kunyoa au naye pia anahiari ya kujichagulia kama wengine? Mashafi, Mahanbali na Maliki wamesema: "Ni wajibu kunyoa." Mahanafi na Maimamiyya wamesema: "Atajiamulia kwa hali yoyote ile." Wameafikiana kuwa, wanawake hawanyoi bali ni wajibu kwao kupunguza tu.

---

[59] Hili linawafikiana na fatwa ya Sayyid al-Hakim na Sayyid Khui, lakini Sayyid al-Hakim ametenganisha kati ya aliyefanya kwa kusahau na mjinga asiyeelewa. Akampa udhuru yule aliyesahau na akamnyima mjinga asiyeelewa, bali huyu mjinga amemuunganisha na aliyefanya kwa kukusudia, na ndio haki. Kwa sababu mjinga ni mwenye kukusudia, tofauti kabisa na aliyesahau, kwani huyu amefanya bila kukusudia. Tumetanabahisha hili ili mtu asije kuchanganya kati ya mjinga, mjuzi na anayefanya kusudi. Isijedhaniwa kuwa Sayyid amemuunganisha mjinga na mjuzi, hali maarufu ni kumuunganisha aliyesahau na mjuzi, na si na mjinga.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 321 2/1/2017 3:51:57 PM

Abu Hanafi amesema: “Mtu ambaye kichwani mwake hana nywele kama vile mwenye kipara na mfano wake, ni wajibu kwake kupitisha wembe juu yake (juu ya upara).” Na hiyo ndio kauli ya baadhi ya Maimamiyya. Waliobakia wamesema: “Ni Sunna kupitisha wembe juu ya upara.” (*Al-Hadaiq* na *Fiqh Sunna*).

Maimamiyya wamesema: “Kunyoa nywele au kupunguza ni wajibu kufanyike Mina. Na kama ataondoka Mina kabla ya kunyoa au kupunguza nywele itamlazimu arejee akanyoe au kupunguza nywele zake mahali hapo, sawa awe ni mjuzi au mjinga, kafanya kwa makusudi au kwa kusahau. Na ikiwa kuna uzito kurejea tena hadi Mina, basi atanyoa au kupunguza mahali penginepo.” Madhehebu yaliyobaki yamesema: “Kunyoa au kupunguza nywele ni wajibu kufanyike Haram.” (Fiqh Sunna).

Wameafikiana kuwa, anapopunguza au kunyoa nywele haimuwii halali kwake wanawake. Maliki wakaongezea manukato kwa wanawake. Ukiachana na hayo mawili, Maimamiyya wameongeza pia kuwinda, na kwao wao uharamu wa kuwinda unatokana na heshima ya Haram tukufu. Na huwa halali mambo mengine yasiyokuwa haya matatu kwa itifaki ya madhehebu yote. Kwa mujibu wa madhehebu manne huhalalika kila kitu hata wanawake baada ya kutufu *Twawafu Ziyara.*

Kwa Maimamiyya haihalalikiwi wanawake wala mapambo isipokuwa baada ya kutufu Twawafu Nisaa. Tunamaliza kwa kusema maneno yaliyoandikwa katika kitabu *At-Takdhkirah*, amesema Allamah al-Hiliy: “Kama mwenye kuhiji ataondoka Mina kabla ya kunyoa atarejea mahali hapo kama anaweza, apunguze nywele hapo au anyoe. Kama hakuna uwezekano wa kurejea atanyoa mahali alipo, kisha azipeleke nywele zake Mina ili akazizike huko. Lakini iwapo atashindwa kuzipeleka hatalazimika chochote… Na kwa ujumla



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 322 2/1/2017 3:51:57 PM

wakati wa kunyoa ni siku ya Idd kwa itifaki ya mafakihi, kufuatana na kauli yake Mwenyezi Mungu (s.w.t.) aliposema:

"..... وَلَا تَحْلِقُوا رُءُوسَكُمْ حَتَّىٰ يَبْلُغَ الْهَدْيُ مَحِلَّهُ ....."

**"Wala msinyoe vichwa vyenu mpaka wanyama hao wafikie machinjoni mwao." (Sura Al-Baqara 2:196).**

Na mahali pa kuchinjia wanyama ni Mina katika siku ya Idd. Imethibiti kutoka kwa Mtume ﷺ kwamba alitupa vijiwe, akachinja kisha akanyoa nywele hapo Mina katika siku ya Idd."

Maelezo ya hukmu ya kutangulia kunyoa kabla ya kuchinja yatakujia wakati wa kuzungumzia amali za Mina chini ya kichwa cha maneno 'Mina'.

## KUSIMAMA ARAFAH

Ni juu ya aliye katika Umra *Mufrada* au katika Hijja *Tamattui* ahirimie, atufu, aswali rakaa mbili, asai na kupunguza nywele. Na mpangilio huu ni wajibu. Atangulize kuhirimia kwanza kabla ya vyote, na twawafu itangulie Swala, na Swala itangulie kusai, na amalize kwa kupunguza nywele.[60]

### TENDO LA PILI KATIKA HIJJA:

Amali za Hijja huanza kwa kuhirimia, sawa kabisa kama ilivyo katika Umra. Ama amali ya pili katika matendo ya Hijja ambayo hufua-

60 Sheikh Abdul Muta'al As-Swaidi amesema: "Mpangilio huu ni wajibu katika matendo ya Umra, ama katika Hijja hakuna mpangilio wowote baina ya kutufu na kunyoa, wala baina ya kusai na kusimama Arafah, (*Al-Fiqhul Muswawar* ya madhehebu ya kishafi)



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 323 2/1/2017 3:51:57 PM

tia Ihram, na ambayo huhesabiwa kuwa ni katika jumla ya nguzo za Hijja kwa itifaki ya mafakihi, ni kusimama Arafah, bila ya kuwepo tofauti kati ya kuwa Hijja hiyo ni *Tamattui* au *Mufrad*. Lakini hujuzu kwa wenye kuhiji Hijja *Ifrad* na *Qiran* waliokuja toka nje ya Makka, kutufu *Twawaful Qudum* ambayo ni sawa kabisa na rakaa mbili za *Tahiyyatul Masjid,* mara tu baada ya kuhirimia na kabla ya kutoka kwenda Arafah.

Sayyid al-Hakim amesema katika kitabu chake *Al-Mansak* maneno haya yafuatayo: "Mtu anayehiji Hijja *Qiran* na *Mufrada,* anapoingia Makka, hujuzu kwake kutufu Twawafu ya Sunna kabla ya kwenda kusimama Arafah."

Katika kitabu *Fat'hul-, Sharhu* ya Bukhari, Ibn Hajar amesema: "Wote wameafikiana kwamba mtu aliyehirimia Hijja *Mufrad* haidhuru kitu kwake kutufu al-Kaaba, yaani kabla ya kwenda Arafah. Ama mwenye kuhiji Hijja *Tamattui* hutosha kwake kutufu Twawafu ya Umra badala ya *Twawaful Qudum*.

**KABLA YA KUSIMAMA ARAFAH:**

Wameafikiana kuwa anayehiji ni sunna kwake kuitoka Makka akiwa katika Ihram siku ya Tarwiya, nayo ni siku ya nane ya mwezi wa Dhulhijja, aelekee Arafah kupitia Mina.

Katika kitabu A*t-Tadhikrah* na kitabu *Al-Jawahir* cha Maimamiyya mna maneno yasemayo kuwa husunniwa kwa mtu anayetaka kutoka kwenda Arafah, asiitoke Makka kabla ya kuswali Dhuhrain (Adhuhuri na Alasiri) kwanza. Mafakihi wa madhehebu manne wamesema: "Inasunniwa kuswali Dhuhrain (Adhuhuri na Alasiri) huko Mina." (Kitabu *Al-Mughni*).

Vyovyote iwavyo, ieleweke kuwa hujuzu kuharakisha kwenda Arafah kabla ya kuingia siku ya Tarwiya kwa siku moja au mbili

kabla yake, hasa kwa mgonjwa, mzee na mwanamke na anayehofia msongamano. Kama ambavyo hujuzu kuicheleweshा hadi asubuhi ya siku ya tisa, kwa sharti la kuwa jua linapokengeuka awe ameshafika Arafah.

Na mimi, sijamuona yeyote miongoni mwa mafakihi wa madhehebu ya kiislamu, ambaye amesema kuwa, ni wajibu kulala Mina usiku wa Arafah, au kuna wajibu wa kutenda amali yoyote nyingine katika usiku huo. Bali mwanachoni al-Hilliy amesema katika kitabu *at-Takdhikrah:* "Kulala Mina usiku wa kuamkia Arafah kumesunniwa kwa ajili ya kujipumzisha, la si kwa kuwa ni ibada (ya Hijja), wala mtu huwa halazimiki chochote anapoacha." Na katika Kitabu *Fat'hul-Bari* na *Fat'hul-Qadir* mmeandikwa kama hivyo.

Na maelezo hayo ya Allamah al-Hilliy yameeleweka vyema hata hayana haja ya kushereheshwa wala kuelezwa kwa kirefu. Kwani bila ya shaka yoyote, hapo mbeleni siku zilizopita usafiri ulikuwa kama kipande cha Jahanamu (kulingana na dharubu yake), kwa hiyo ikapendekezwa kwa mwenye kuhiji aende akakeshe Mina ili apumzike, na kesho yake ndio aende Arafah akiwa mkakamavu na aliyechangamka. Ama leo hii safari ni starehe tupu, kwa hiyo akikesha usiku wa Arafah hapo Makka, kisha kesho asubuhi, au baada ya Swala ya Adhuhuri - kama inavyofanywa na mahujaji siku hizi - akiondoka kuelekea Arafah kupitia Mina, huwa imetosha na kutosheleza. Na kamwe hakuna fidia inayotolewa kwa mtu anayefanya hilo. Ndiyo, ni wajibu kutupa vijiwe hapo Mina, lakini hiyo ni baada ya kusimama Arafah. Na ubainifu wake utafuata.

## WAKATI WA KUSIMAMA ARAFAH:

Wameafikiana kuwa wakati wa kusimama Arafah ni siku ya mwezi tisa wa Dhulhijja. Kisha wamekhitilafiana kuhusu muda wa kuanzia



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 325 2/1/2017 3:51:57 PM

kuwepo na kusimama Arafah, na muda wa kumaliza kisimamo cha siku hiyo.

Mahanafi, Mashafi na Maliki wamesema: "Huanza tangu jua linapokengeuka katika siku hiyo ya mwezi tisa hadi alfajiri ya mwezi kumi." Mahanbali wamesema: "Bali ni tangu alfajiri ya siku ya tisa hadi alfajiri ya siku ya kumi." Maimamiyya wamesema: "Ni tangu kukengeuka kwa jua katika siku hiyo ya mwezi tisa hata machweo ya jua la siku hiyo kwa anayetaka kufanya hivyo, ama kwa aliyezongwa basi ni hadi kuchomoza kwa alfajiri."

Na husunniwa kuoga mwili kwa ajili ya kusimama Arafah, nalo ni sawa na josho la siku ya Ijumaa, wala hapo hapana amali yoyote inayofanywa zaidi ya kuhudhuria kwa maana ya kuwepo tu na kupatikana mahali hapo katika hali yoyote ile, na sehemu yoyote ya eneo hilo, sawa awe amelala, ameamka (yuko macho), awe juu ya mnyama, amekaa au anatembea tembea.

## MIPAKA YA ARAFAH:

Mipaka ya Arafah ni Batnu Urna na Thawba, Namira hadi Dhil Majaz, haya ni majina ya maeneo. Basi haijuzu kusimama katika mipaka hii, wala chini ya Araki, kwa kuwa sehemu hizi si katika Arafah, na kama mtu atasimama hapo basi Hijja yake kwa mujibu wa madhehebu yote -isipokuwa Malik - itabatilika. Huyu Malik amesema: "Lau mtu atasimama Batnu Urna itajuzu lakini itamlazimu achinje mnyama."

Na Arafah pote ni sehemu ya kusimama, mahali popote anaposimama ndani yake hutosha kuwa kasimama Arafah, na hujuzu kwa itifaki ya wanavyuoni.

Imam Ja'far as-Sadiq عليه السلام amesema: "Mtume صلى الله عليه وآله alisimama kwenye uwanja wa Arafah watu wakasongana kando yake wakawa



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 326 2/1/2017 3:51:57 PM

wanakimbilia kusimama kandoni mwa ngamia wake wakimzingira. Akamtenga ngamia wake kando nao, nao wakafanya kama hivyo (yaani wakamsogelea tena). Mtume akasema: 'Enyi watu! Sehemu ya kusimama si hapa tu kando ya ngamia wangu, lakini uwanja huu wote (alikuwa akiasharia Arafah), ni sehemu ya kusimama, na kama sehemu ya kusimama isingelikuwa isipokuwa kando kando tu ya ngamia wangu, basi watu wasingelipata nafasi.'" (*At-Tadhkirah*)

## MASHARTI YA KUSIMAMA ARAFAH:

Hapana sharti la kuwa tohara kwa mtu anayesimama Arafah kwa itifaki ya wanavyuoni. Maimamiyya na Maliki wamesema: "Ni wajibu kutia nia na kukusudia kuwepo Arafah. Na kukusudia kunahitaji kuijua Arafah yenyewe, hivyo kama atapitia hapo Arafah hali ya kuwa hajui, au anajua lakini hakuwa amekusudia kusimama kisimamo alichoamrishwa, kusimama kwake huko hakutazingatiwa ni kusimama Arafah."

Mashafi na Mahanbali wamesema: "Hapashurutiwi kukusudia wala kuwa na elimu ya kupajua, bali sharti lililozingatiwa ni kutokuwa mwendawazimu, mlevi au mwenye kughumiwa (aliyepotewa na fahamu)."

Mahanafi wamesema: "Hapashuritiwi kutia nia, wala kuwa na elimu (kujua) wala kuwa na akili, kwani anayehudhuria Arafah katika wakati wake uliowekwa, Hijja yake husiwhi, awe amenuia au hakunuia, awe alipajua mahali hapo au hakupajua (awe ni mjinga), awe ni mwenye akili au ni mwendawazimu." (*Fiqh Sunna n*a *at-Tadhikrah*).

Je, ni wajibu kusimama Arafah katika wakati wote uliowekwa kisharia kuwepo hapo? Au hutosha kuwepo kwa kiasi kinachotosha kuitwa kisimamo, hata kama ni kwa muda mfupi sana?

Maimamiyya wamesema: "Kusimama Arafah kuna nyakati mbili: Wakati wa kujiamulia na wakati wa kulazimika, na wa mwanzo ni tangu kukengeuka kwa jua la siku ya mwezi tisa mpaka machweo ya siku hiyo. Na wa pili ni mpaka alfajiri ya mwezi kumi. Hivyo mwenye uwezo wa kusimama tangu kukengeuka kwa jua la siku ya tisa, hadi machweo ya jua lake, akaukamilisha wakati huu kikamilifu, ni wajibu kwake kufanya hivyo, lakini nguzo katika kisimamo hicho ni kile kiasi kinachotosha kuitwa kisimamo. Na wakati uliobaki ni wajibu usiokuwa nguzo.

Na linalolazimu kauli hiyo ni kuwa, anayeacha kabisa kusimama Arafah Hijja yake hubatilika, kwa sababu huwa ameacha nguzo. Ama iwapo atasimama kiasi kichache, basi atakuwa ameacha wajibu usiokuwa nguzo, kwa hivyo Hijja yake itaswihi. Na kama hakuweza kusimama kikamilifu katika ule wakati wa hiyari kutokana na udhuru miongoni mwa nyudhuru za kisheria, basi huo wakati mchache atakaosimama katika usiku wa kuamkia Idd utatosha."

Mashafi, Maliki na Mahanbali wamesema: "Inatosha kuhudhuria tu, hata kama ni kwa kipindi kifupi tu." *(Fiqh Alal Madhahibil Arbaa,* na *Manarus Sabil*).

Maimamiyya wamesema: "Mtu akitoka Arafah kwa makusudi kabla jua halijakengeuka itamlazimu arudi Arafah (mara moja), na akirudi hatolazimika kitu chochote. Kinyume na hivyo, atatoa fidia kwa kuchinja ngamia, akishindwa naafunge siku kumi na nane mfululizo. Na kama ametoka kwa kusahau, na hakukumbuka hadi wakati ukapita, hatalazimika kutoa kitu chochote, kwa sharti tu awahi kusimama Muzdalifa ndani ya wakati wake. Na kama atakumbuka kabla ya kupita wakati, kama anaweza kurejea ni wajibu arejee, na kama hatarejea na hali ni hiyo, atalazimika kuchinja ngamia."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 328 2/1/2017 3:51:57 PM

Maliki wamesema: “Anayesimama Arafah baada ya kukengeuka jua kisha akatoka kabla ya jua kuchwa, itamlazimu arudi tena kuhiji mwaka utakaofuata, isipokuwa tu kama atarejea Arafah kabla ya alfajiri.”

Na katika kitabu *Al-Fiqhul Muswawwar* cha madhehebu ya Shafi mna maelezo yafuatayo: “Anayehiji anapoacha kusimama Arafah kwa kusahau, ni wajibu kwake aigeuze Hijja yake iwe Umra, kisha atatekeleza amali zilizobaki miongoni mwa amali za Hijja hadi amalize, kisha itampasa arudie Hijja yake haraka sana katika mwaka unaofuata.”

Na husunniwa kwa mwenye kusimma Arafah awe na utohara kamili, na aelekee Kibla na aombe istighfari kwa wingi, pia kuomba dua akiwa mwenye unyenyekevu wa hali ya juu na moyo hadhiri.

## KUSIMAMA MUZDALIFA

Kusimama Muzdalifa ni kitendo ambacho hufuata baada ya kusimama Arafah, kwa Ijmai ya wanavyuoni. Na mafakihi wote wameafikiana kuwa anayehiji huondoka Arafah na huenda moja kwa moja Muzdalifa, na mahali hapo ndipo penye *Mash'arul Haram* zilizokusudiwa na Aya tukufu ya Mwenyezi Mungu:

”..... فَإِذَآ أَفَضۡتُم مِّنۡ عَرَفَٰتٖ فَٱذۡكُرُواْ ٱللَّهَ عِندَ ٱلۡمَشۡعَرِ ٱلۡحَرَامِۖ وَٱذۡكُرُوهُ كَمَا هَدَىٰكُمۡ .....“

**“…..Na mtakaporudi kutoka Arafah mtajeni Mwenyezi Mungu penye Mash'aril Haram. Na mkumbukeni kama alivyo kuongozeni…..” (Suratul Baqarah 2:198).**



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 329 2/1/2017 3:51:57 PM

Aidha wameafikiana kuwa husunniwa kuicheleweshа Swala ya Magharibi ya usiku huo wa mkesha wa Idd hadi akaiswalie hapo Muzdalifa. Mwenye kitabu *at-Tadhkirah* amesema: "Lichwapo jua wakiwa Arafah, wamiminike kuondoka hapo kabla ya kuswali Swala ya Magharibi, hadi wakaiswalie huko Mash'ar, na mtu aombe dua iliyonakiliwa kutoka kwa Mtume ﷺ."

Mwenye kitabu *Al-Mughni* naye amesema: "Ilivyo Sunna kwa anayetoka Arafah ni kutoswali Swala ya Magharibi mpaka afike Muzdalifa, na akusanye Magharibi na Isha, katika hili hapana hitilafu baina ya madhehebu yote."

Ibn Mundhir amesema: "Wanavyuoni wote wameafikiana bila ya kuwepo tofauti yoyote kuwa, Sunna ni anayehiji akusanye pamoja Swala ya Magharibi na Isha, na asili yake ni kuwa Mtume ﷺ alizikusanya Swala hizo mbili (akaziswali pamoja)."

Na wameafikiana isipokuwa Mahanafi kuwa, anayeswali Magharibi kabla ya kufika Muzdalifa, bila kuzikusanya pamoja Swala mbili hizo, Swala yake imeswihi hata kama atakuwa amekhalifu Sunna. Abu Hanifa amesema: "Swala yake hiyo haitoshelezi."

## MPAKA WA MUZDALIFA:

Katika kitabu *At-Tadhkirah* na kitabu *Al-Mughni* mmeelezwa hivi: "Kwa yakini Muzdalifa ina majina matatu: Muzdalifa, Jam'u na Mash'aril Haram. Na mpaka wake ni kuanzia Maazma hadi Hayadh, na hadi bonde la Muhsir. Na Muzdalifa yote ni sehemu ya kusimama kama ilivyo Arafah, kwa hiyo popote asimamapo mwenye kuhiji hutosha."

Na katika kitabu *Al-Madarik* mmekuja maneno haya: "Kwa hakika maneno mkato ya mafakihi wa Kiimamiyya ni kuwa, unapozidi msongamano wa watu hujuzu kupanda hadi juu ya



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 330 2/1/2017 3:51:57 PM

jabali. Napo ni mojawapo ya mahali ambapo huishia mipaka ya Muzdalifa."

**KULALA NA KUSIMAMA:**

Je, ni wajibu kulala Muzdalifa katika usiku wa mkesha wa Idd au hutosha kusimama katika Mash'aril Haram hata kwa muda mchache baada ya kuingia alfajiri?

Yapasa ieleweke kwa yakini kabisa linalokusudiwa katika neno 'Kusimama' ni kuwepo mahali hapo katika hali yoyote na namna yoyote, iwe ni kwa kutembeatembea, kukaa au kuwa juu ya mnyama, kama hali ilivyo katika Arafah.

Mahanafi, Mashafi na Mahanbali wamesema: "Ni wajibu kulala Muzdalifa, na anayeacha kufanya hivyo basi ni wajibu kwake kuchinja." (*Al-Mughni*). Maimamiyya na Maliki wamesema: "Si wajibu, lakini kulala ni bora zaidi, kama alivyoeleza Shihabbudin Al-Baghdadi al-Makki katika kitabu *Irshadus-Salik*. Na ni njia ya kujitoa shaka, kama alivyoeleza Sayyid al-Hakim na Sayyid Khui." Na vyovyote iwavyo, hakuna mwanachuoni yeyote aliyesema kuwa huko kulala ni nguzo."

Ama kusimama Mash'aril Haram baada ya kuingia alfajiri, Ibn Rushd katika kitabu *Al-Bidayatu Wan-Nihayah* amenukuu kutoka kwa idadi kubwa ya wanavyuoni wa kisunni kuwa, ni miongoni mwa Sunna za Hijja, wala si faradhi miongoni mwa faradhi zake.

Na katika kitabu *At-Tadhikrah* mna maelezo haya: "Ni wajibu kusimama Masha'ril Haram baada ya kuingia alfajiri, hivyo kama mtu ataondoka kabla ya kuingia alfajiri kwa hiari yake, tena kwa makusudi kabisa, baada ya kuwa amesimama hapo wakati wa usiku, atalazimika kuchinja mbuzi."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 331 2/1/2017 3:51:57 PM

Abu Hanifa amesema: "Ni wajibu kusimama baada ya kuingia alfajiri." Kama isemavyo kauli yetu, na waliobakia wamesema kuwa yajuzu kuondoka baada ya kupita nusu ya usiku. Kwa maelezo haya imeeleweka kuwa inajuzu kuondoka Muzdalifa kabla ya kuingia alfajiri kwa wasiokuwa Maimamiyya na Mahanafi.

Maimamiyya wamesema: "Kwa hakika kusimama Mash'ari kuna nyakati mbili: Wakati wa kwanza ni kwa asiyekuwa na udhuru wa kuchelewa, nao ni kati ya mawio mawili katika siku ya Idd, yaani ni kati ya kuchomoza alfajiri na kuchomoza jua, kwa maana ya kuwa, asimame hapo kipindi chote hiki kwa ukamilifu wake. Na anayeondoka Mash'ari kabla ya kuingia alfajiri, kwa makusudi na kwa kutambua, hata kama ni kwa muda mchache, baada ya kuwa amekesha hapo, Hijja yake haibatiliki iwapo amekwishasimama Arafah, lakini atalazimika kuchinja mbuzi. Na kama ataacha kwa kutojua hatolazimika chochote, kama inavyoeleza waziwazi riwaya iliyotangulia.

Na wakati wa pili ni wa wanawake na mwenye udhuru unaomzuia kusimama kati ya mawio mawili, wakati huu unaendelea hadi linapokengeuka jua la siku ya Idd." Mwenye kitabu *Al-Jawahir* amesema: "Ijmai imesimamia hapo, ukiachilia mbali nususi zilizopo."

Na hili linawafikiana na fatwa ya Sayyid al-Hakim na Sayyid al-Khui, lakini Sayyid huyu hakufanya kukengeuka jua kuwa ndio mpaka wa mwisho kwa aliyezongwa, bali alisema: "Inamtosha kusimama kwa kiasi cha wakati wowote baada ya kuchomoza jua."

Maimamiyya wamesema: "Kwa hakika kusimama sehemu tu ya nyakati hizi mbili zilizowekwa, ndio nguzo miongoni mwa nguzo za Hijja, kwa hiyo anayekosa kusimama kabisa pasi na udhuru wowote katika wakati wa kujiamulia, na pia katika wakati wa dharura, na akawa hakusimama wakati wa usiku, Hijja yake



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 332 2/1/2017 3:51:58 PM

ni batili. Lakini kama ataacha kwa udhuru wa kisheria, Hijja yake haitabatilika, kwa sharti tu awe ameshasimama Arafah. Na anayepitwa na kisimamo cha Arafah na Mash'ari, akakosa kusimama katika viwanja hivyo vyote viwili katika wakati wa hiyari na wa udhuru, Hijja yake itabatilika, hata kama aliacha kwa udhuru uliowekwa kisheria, naye itawajibika arudie kuhiji tena mwakani Hijja ya wajibu, kama Hijja hiyo aliyokuwa anahiji ni ya wajibu. Na yasunniwa airudie mwakani kama Hijja hiyo aliyokuwa anahiji ni ya Sunna." (*Al-Jawahir*).

Na kusimama Mash'aril Haram kuna daraja kubwa zaidi kwa Maimamiyya kuliko kusimama Arafah. Na kutokea hapa ndipo waliposema kuwa anayepitwa na kisimamo cha Arafah, akawahi kusimma Mash'aril Haram kabla ya kuchomoza jua, Hijja yake huwa imetimu. (*at-Tadhkirah*).

**MAMBO YALIYO SUNNA:**

Maimamiyya wamesema: "Husunniwa kwa mtu mwenye kuhiji Hijja yake ya kwanza, ambaye hajawahi kuhiji siku za nyuma; mguu wake uguse Mash'aril Haram." (*Al-Jawahir*). Na Maimamiyya, Mashafi na Maliki wamesema: 'Husuniwa achukue kutoka hapo Muzdalifa vijiwe vyake, aende navyo hadi Mina, na idadi yake ni vijiwe sabini."

Na mwenye kitabu *at-Tadhkirah* amesema: "Kwa hakika siri katika kufanya hivyo ni kumtaka anayehiji, anapofika Mina asishughulikie jambo lolote jingine zaidi ya kutupa vijiwe." Na imenukuiwa kutoka kwa Ahmad bin Hanbal kuwa amesema: "Chukua vijiwe popote pale upatakapo."

Na wala hapana khitilafu kuwa kuokota vijiwe mahali popote atakapo mtu ni jambo  linalojuzu. Na yasunniwa awe yuko kwenye



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 333 2/1/2017 3:51:58 PM

tohara na alete tahlili na takbira na kuomba dua zilizopokewa na zisizopokewa.

## MINA

Wameafikiana kwa kauli moja kwamba matendo ya ibada ya Hijja ambayo hufuatia baada ya kisimamo cha Mash'aril Haram ni amali zifanywazo Mina. Na Mahujaji huondoka Muzdalifa baada ya kuchomoza jua, na kama mtu atatoka Muzdalifa kabla ya kuchomoza jua na akaupita mpaka wake, humlazimu kutoa fidia ya mbuzi kwa mujibu wa kauli ya al-Khui.

Na hapo Mina pana amali mbalimbali ambazo huendelea kuanzia siku ya kuchinja ambayo ni siku ya Idd hadi asubuhi ya mwezi kumi na tatu au usiku wa mwezi kumi na mbili. Hapo Mina aidha ndipo panapoishia matendo yaliyo wajibu katika Hijja. Na siku tatu ambazo hufuata baada ya Idd huitwa, *Ayyaamut-Tashrik* nazo ni mwezi kumi na moja, kumi na mbili na kumi na tatu.[61]

Na katika Mina mnamo siku ya Idd ni wajibu kutendwa aina tatu ya matendo ya ibada za Hijja:

**1.** Kutupa vijiwe vya Aqaba.

**2.** Kuchinja.

**3.** Kunyoa au kupunguza nywele.

Na baada ya kuwa wameafikiana kuwa Mtume ﷺ kwanza alitupa vijiwe kisha ndio akachinja kisha akanyoa, wametofautiana kuhusu je, mpangilio huo kuufuata ni wajibu kwa namna ambayo

[61] Wametofautiana kuhusu siku za Tashrik ni tatu au ni mbili? Ama sababu ya kuitwa kwa jina hilo, ni kwa sababu watu walikuwa wakizianika nyama za udhhiya na kuzikausha na jua.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 334 2/1/2017 3:51:58 PM

haijuzu kulitanguliza alilolicheleweshs Mtume, wala kulichelewesha alilolitanguliza Mtume, au kufuata mpangilio huo ni Sunna tu ambayo inajuzu kuiacha?

Mashafi na Ahmad wamesema: "Hakuna chochote juu ya mtu aliyetanguliza au kuchelewesha." Maliki amesema: "Anayenyoa kabla hajatupa vijiwe basi itamlazimu alipe fidia, na anayenyoa kabla ya kuchinja au anayechinja kabla ya kutupa vijiwe, hapana makosa juu yake."

Na Abu Hanifa amesema: "Kwa hakika akinyoa kabla ya kuchinja au kutupa vijiwe, itamlazimu achinje fidia. Na kama alikuwa anahiji Hijja *Qiran* basi itamlazimu achinje wanyama wawili." (Kitabu *Al-Bidayah* cha Ibn Rushd).

Maimamiyya wamesema: "Kama anayehiji atatanguliza baadhi juu ya baadhi nyingine huku akijua, tena kwa makusudi, basi Hijja yake itakuwa imetimu, wala hatalazimika kuirudia." Mwenye kitabu *al-Jawahir* amesema: "Kwa hakika kabisa nimekuta hivyo bila ya tofauti yoyote." Na katika kitabu *al-Madarik*: "Kwa yakini mafakihi wa Kiimamiya wamepitisha hivyo."

Katika sehemu inayofuata tumeitengea kila ibada ya Hijja inayofanyika Mina kifungu chake maalum.

## JAMARATUL-AQABAH

### IDADI YA JAMARAT:

Ni wajibu kutupa vijiwe kwenye Jamarat hapo Mina kwa kila mtu aliyekwenda Hijja, awe amekwenda Hijja *Tamattui*, *Qiran* au *Mufrada*, na idadi ya Jamarat ni kumi, ambazo zimegawanywa katika siku nne:



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 335 2/1/2017 3:51:58 PM

**Ya kwanza:** Ni katika siku ya Idd, ambapo ni Jamarat moja ndio hupigwa vijiwe, nayo huitwa '*Jamaratul-Aqaba*', nasi tumeitengea faslu hii ili kuieleza kwa ubainifu.

**Ya pili:** Ni siku ya kumi na moja katika mwezi wa Dhulhijja, na siku hiyo ni Jamarat tatu ndizo hupigwa vijiwe.

**Ya tatu:** Ni siku ya kumi na mbili katika mwezi wa Dhulhijja, na siku hiyo ni Jamarat tatu ndizo hupigwa vijiwe.

**Ya nne:** Ni siku ya kumi na tatu katika mwezi wa Dhulhijja, na siku hiyo ni Jamarat tatu ndizo hupigwa vijiwe. Hii ni kwa aliyelala Mina katika usiku wa mwezi kumi na tatu; la haikuwa hivyo basi katika siku hii hapatakuwa na ulazima juu yake wa kutupa vijiwe.

## JAMARAT INAYOPIGWA VIJIWE SIKU YA KUMI:

Wameafikiana kuwa atakayeipiga vijiwe *Jamaratul-Aqaba* katika wakati uliopo baina ya kuchomoza kwa jua na kuzama kwake, katika siku ya mwezi kumi, kupiga huko kutatosheleza na kutosha. Kisha wamekhitilafiana kuhusu kuipiga *Jamaratul-Aqaba* kabla ya wakati huo au baada yake. Maliki, Mahanafi, Mahanbali na Maimamiyya wamesema: "Haijuzu kuipiga *Jamaratul-Aqaba* kabla ya alfajiri, na kama atatupa vijiwe kabla ya wakati huo bila ya udhuru ni wajibu kwake kurudia." Nao wamejuzisha kutanguliza kabla ya wakati huo kwa mwenye udhuru, kama kuzidiwa kwa ajili ya utu uzima, ugonjwa na hofu.

Mashafi wamesema: "Hapana ubaya wowote wa kutanguliza, kwani huo wakati uliotajwa ni wa kusunniwa tu, na si wa wajibu.' (kitabu *At-Tadhikrah* na *Bidayah* cha Ibn Rushd).

Ama anapocheleweshа kuipiga Jamarat hadi jua likatoweka katika siku hiyo ya kuchinja, Imam Malik amesema: "Iwapo atapiga



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 336 2/1/2017 3:51:58 PM

usiku au kesho yake basi itamlazimu kuchinja." Mashafi wamesema: "Halazimiki chochote anapoipiga usiku au kesho yake." (kitabul a*l-Bidayah* cha Ibn Rushd).

Maimamiyya wamesema: "Wakati wa kuipiga Jamarat hii (*Jamaratul-Aqaba)* huanzia tangu kuchomoza jua hadi kuzama kwake, na akisahau atalipa kesho. Akisahahu tena atalipa siku ya mwezi kumi na mbili, na kama hakukumbuka siku hiyo basi atalipa siku ya kumi tatu. Na kusahau kunapoendelea hadi akaondoka Makka, basi atalipa mwaka unaofuata, yeye mwenyewe au atamweka naibu wa kwenda kumlipia."[62]

## MASHARTI YA KUTUPA VIJIWE:

Kutupa vijiwe vya kuipiga Jamarat kuna masharti yake;

Kutia nia, hilo limeelezwa wazi na Maimamiyya.

i. Kupiga kwa vijiwe saba, kwa itifaki ya mafakihi.

**ii.** Iwe kinachotupwa ni kijiwe kimoja, kisha kingine. Kimoja kimoja, haifai viwili au vingi zaidi kwa mkupuo mmoja. Mafakihi wote wameafikiana katika sharti hili.

**iii.** Hicho kijiwe kifike kwenye Jamarat, yaani panapolengwa hasa. Hili pia wameafikiana.

**iv.** Kufikia kwenye Jamarat iwe ni kutokana na kurusha, haku-tatosha kukibwaga kiholela kwa mujibu wa Maimamiyya na Mashafi. Na kwa Mahanbali na Mahanafi hujuzu. (kitabu *Al-Mughni*).

**v.** Hicho kinachotupwa kiwe ni kijiwe, haifai kutupa kibo-nge cha chumvi, chuma au shaba, kibao, kidongo na mfano

[62] Hii inawafikiana na fatwa ya Sayyid al-Hakim na al-Khui.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 337 2/1/2017 3:51:58 PM

wa vitu hivyo. Kwa mujibu wa mafakihi wote, isipokuwa Abu Hanifa, yeye amesema: "Chochote kiwacho ambacho kimetokana na jinsi ya ardhi hujuzu, iwe kidongo, mchanga ulioganda au jiwe." (*Al-Mughni*).

**vi.** Kijiwe chenyewe kiwe ni kipya, hakijatumiwa mbeleni katika kupiga, hilo limeelezwa na Mahanbali.

Hapashartiwi utohara wakati wa kutupa vijiwe, na kama anayetupa atakuwa tohara basi ni bora zaidi.

Maimamiyya wamesema: "Kijiwe hicho inasunniwa kiwe na ukubwa wa kiasi cha kichwa cha kidole (ncha), na kiwe kimango, si cheusi, cheupe wala chekundu." Wengine wamesema: "Yasunniwa kiwe na ukubwa wa haragwe."

Maimamiyya wamesema: "Yasunniwa kwa anayehiji atekeleze vitendo vyake vyote katika hali ya kuelekea Kibla, isipokuwa wakati wa kuipiga *Jamaratul-Aqaba* mnamo siku ya Idd, husunniwa awe amekipa mgongo, kwa kuwa Mtume ﷺ alitupa vijiwe katika hali hiyo." Wasiokuwa wao wamesema: "Bali yasunniwa kuelekea Kibla, hata katika hali hiyo.

Na yasunniwa kwa mtu anayetupa awe anakwenda kwa miguu. Na hujuzu awapo amepanda mnyama. Na anapotupa kijiwe asiwe mbali na Jamarat kiasi cha zaidi ya dhiraa kumi. Na kutupa kufanywe kwa mkono wa kulia, na aombe dua iliyopokewa au nyingineyo. Na katika dua zilizopokewa ni hii:

"*Allahumma Ijialhu Hajjan Mabrur, Wadhammban Maghfur. Allahumma Inna Hadhihi Haswayati, Faahswihunnali Waarfaahunna Fiamali, Allahu Akbar, Allahumma Id'hari Shaitwana Ani.*"

"Ee Mola! Ijaalie Hijja yangu hii iwe Hijja iliyotakabaliwa, na dhambi zangu ziwe zimeghufuriwa. Ee Mola! Hakika hivi vijiwe

vyangu ninavyovitupa, vihesabu kwa ajili yangu, na uvinyanyue katika amali yangu, Allah ni mkuu kabisa. Ee Mola! Msukume shetani mbali nami."

**KUINGIWA NA SHAKA:**

Anapoingiwa na shaka ya je ameswibu lengo au la? Atajengea kuwa hakusibu. Na anapojiwa na shaka ya idadi, atajengea kuwa katupa vichache, kwani asili ni kutopatikana ziyada.

Hivyo basi, kwa yakini kuipiga *Jamaratul-Aqaba* ndiyo amali ya awali anayoitekeleza mwenye kuhiji miongoni mwa ibada zinazotekelezwa Mina katika siku ya Idd, kisha ndipo achinje au anyoe au apunguze nywele baadaye, baada ya hapo ndio aondoke kurejea Makka kwa ajili ya kwenda kutufu katika siku hii hasa. Na hapana Jamarat inayopigwa vijiwe katika siku ya Idd isipokuwa hii tu (*Jamaratul-Aqaba)*.

Maneno yanayohusu wanyama wanaochinjwa huko Mina yanafuata katika kifungu kinachofuata.

## WANYAMA WA KUCHINJWA

Wajibu wa pili katika matendo ya Mina katika siku ya Idd ni kuchinja wanyama, na maneno yanayohusu wanyama hao kwanza yako katika vigawanyo: Walio wajibu na wasiokuwa wajibu. Kisha walio wajibu nao wanagawanyika kwenye vigawanyo kadhaa.

Pili: Mtu anayepaswa kuchinja mnyama.

Tatu: Sifa za mnyama anayefaa kuchinjwa.

Nne: Wakati na mahali anapochinjiwa.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 339 2/1/2017 3:51:58 PM

Tano: Hukmu ya nyama yake.

Sita: Mbadala wake kwa ambaye hakupata mnyama wa kuchinja wala thamani yake. Tunakuletea maelezo kamili.

**VIGAWANYO VYA WANYAMA:**

Wanyama wanaochinjwa Mina wamegawanyika, wapo wale wa wajibu na wa Sunna. Na walio Sunna ni *Udhuhiya*. Katika tafsiri ya neno lake Mwenyezi Mungu (s.w.t.): "Na swali kwa ajili ya Mola wako na uchinje." (Kauthar: 2). Kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t.) alimuamuru Mtume wake Muhammad ﷺ achinje baada ya kuswali Swala ya Idd. Imepokewa riwaya inayosema kuwa Mtume ﷺ aliwachinja kondoo wawili *Aqran* (mwenye pembe), na *Amlah* (ambaye weupe wake umezidi weusi wake).

Maliki na Mahanafi wamesema: "Kuchinja *Udhuhiya* ni wajibu kwa kila jamii (familia) katika kila mwaka, kama ilivyo kutoa Zaka ya Fitri."

Maimamiyya na Mashafi wamesema: "Kwa hakika siku za Udhuhiya ambayo ni Sunna, kwa aliye Mina ni siku nne; Siku ya Idd, na siku tatu zinazofuatia siku ya Idd, nazo ni *Ayyamut-Tashriq*." Ama kwa asiyekuwepo Mina, siku za Udhuhiya kwake ni tatu tu: Siku ya Idd, mwenzi kumi na moja na mwezi kumi na mbili." Maliki, Mahanbali na Mahanafi wamesema: "Siku za Udhuhiya ni tatu tu, kwa aliyeko na asiyekuwepo Mina."

Na vyovyote iwavyo, bora ya wakati wake ni siku ya Udhuhiya, mara tu baada ya kuchomoza jua, na kuendelea hadi wakati unaotosha kuswali Swala ya Idd na kusoma khutba mbili. (*At-Tadhkirah*).

Na dhabihu ya wajibu kwa nassi ya Qur'ani tukufu ni kwa ajili ya mambo manne:

**1.** Dhabihu kwa ajili ya *Tamattui*, amesema Mwenyezi Mungu (s.w.t.):

"..... فَمَن تَمَتَّعَ بِٱلْعُمْرَةِ إِلَى ٱلْحَجِّ فَمَا ٱسْتَيْسَرَ مِنَ ٱلْهَدْيِ ....."

**"Basi mwenye kujistarehesha kwa kufanya Umra kisha ndipo akahiji basi achinje mnyama aliyesahilika." (Al-Baqara 2:196).**

**2.** Dhabihu kwa ajili ya kunyoa, nayo ni ya kujiamulia. Amesema Mwenyezi Mungu:

"..... فَمَن كَانَ مِنكُم مَّرِيضًا أَوْ بِهِۦٓ أَذًى مِّن رَّأْسِهِۦ فَفِدْيَةٌ مِّن صِيَامٍ أَوْ صَدَقَةٍ أَوْ نُسُكٍ ....."

**"Na atakayekuwa mgonjwa katika nyinyi au ana vya kumuudhi kichwani mwake, basi na atoe fidia kwa kufunga au (kwa kutoa) sadaka au kuchinja wanyama." (Al-Baqarah; 2:196).**

**3.** Dhabihu wa malipo, amesema (s.w.t.):

"..... فَمَن كَانَ مِنكُم مَّرِيضًا أَوْ بِهِۦٓ أَذًى مِّن رَّأْسِهِۦ فَفِدْيَةٌ مِّن صِيَامٍ أَوْ صَدَقَةٍ أَوْ نُسُكٍ ....."

**"Miongoni mwenu atakayemuua kwa makusudi, basi (chinjeni) wanyama kilicho sawa na alichokiua, katika wanyama wanaofugwa, kama watakavyohukumu waadilifu wawili miongoni mwenu, mnyama huyu apelekwe iliko al-Kaaba."**

**4.** Dhabihu wa kuzuiwa: Amesema (s.w.t.):

وَمَن قَتَلَهُۥ مِنكُم مُّتَعَمِّدًا فَجَزَآءٌ مِّثْلُ مَا قَتَلَ مِنَ ٱلنَّعَمِ يَحْكُمُ بِهِۦ ذَوَا عَدْلٍ مِّنكُمْ هَدْيًۢا
بَٰلِغَ ٱلْكَعْبَةِ ....."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 341 2/1/2017 3:51:58 PM

**"Na kama mkizuiwa, basi chinjeni wanyama walio wepesi kupatikana." (Al-Baqarah 2:196). Nao ni mbuzi. (*At-Tadhkira*).**

Na ukiachana na wanyama hawa wanne, huongezewa wanyama wengine ambao nao huwa ni wajibu kuwachinja, ambao wajibu wake unatokana na ahadi, nadhiri na yamini. Katika vifungu vya maelezo vinavyofuata tutazungumzia wanyama ambao ni sehemu muhimu miongoni mwa matendo ya Hijja, na ni ibada miongoni mwa ibada zake.

## NI NANI ANAYEWAJIBIKA KUCHINJA DHABIHU?

Si wajibu kuchinja mnyama wa dhabihu kwa aliyekwenda kufanya Umra *Mufrada*, wala kwa aliyekwenda kuhiji Hijja *Mufrada*. Hii ni kwa itifaki ya mafakihi. Aidha wameafikiana kwa kauli moja kuwa ni wajibu kuchinja mnyama wa dhabihu kwa mtu aliyekwenda kufanya *Tamattui* kwa mtu asiyekuwa mkaazi wa Makka.

Mafakihi wa madhehebu manne wamesema: "Ni wajibu kwa mwenye kufanya *Qiran* pia." Maimamiyya wamesema: "Si wajibu kutoa dhabihu kwa mwenye kufanya *Qiran* isipokuwa kama aliweka nadhiri, au anapokuwa kaambatana pamoja na mnyama huyo tangu alipoingia katika ihram."

Kisha wamekhitilafiana kuhusu mtu wa Makka anapofanya *Tamattui*, je naye ni wajibu kuchinja ama la? Mafakihi wa madhehebu manne wamesema: "Si wajibu juu yake kuchinja dhabihu." Kwani imeandikwa katika kitabu *Al-Mughni:* "Hapana ikhtilafu baina ya wanavyuoni kuwa kuchinja kwa ajili ya *Tamattui* si wajibu kwa aliyopo Masjidul Haram."

Maimamiyya wamesema: "Kama mkaazi wa Makka atahiji Hijja *Tamattui*[63] ni wajibu juu yake dhabihu." Ndani ya kitabu *Al-Jawahir*

[63] Tumetangulia kueleza huko nyuma kuwa faradhi ya mkaazi wa Makka kwa Imamiyya ni *Qiran* au *Ifrad*, na kwa wasiokuwa wao ana hiari kujiamulia kati ya aina tatu za Hijja.

mmeandikwa kuwa, kama mkaazi wa Makka atafanya *Tamattui*, atawajibika kuchinja dhabihu kwa kauli iliyo mashuhuri sana."

Kisha wameafikiana kuwa mnyama wa dhabihu aliye wajibu si nguzo miongoni mwa nguzo za Hijja.

**SIFA ZA MNYAMA WA DHABIHU:**

Mnyama wa dhabihu ana masharti yafuatayo:

**1.** Awe ni katika wanyama wa kufugwa kama vile ngamia, ng'ombe, mbuzi na kondoo kwa itifaki. Katika kitabu *Al-Mughni* mmeandikwa kuwa, Mahanafi, Maliki, Mashafi na Mahanbali wamesema: "Katika mbuzi haifai ila awe ana umri wa miezi sita. Kondoo awe ana umri wa mwaka. Na ng'ombe awe ana umri wa miaka miwili, na ngamia awe ana umri wa miaka mitano." Na hili linawafikiana na maelezo yaliyomo katika kitabu *Al-Jawahir* cha Maimamiyya, isipokuwa mwenye kitabu hiki alilifasiri neno *thania* kwa maana ya ngamia anayeingia katika mwaka wa sita. Na *Maaz* kuwa ni aliyeingia katika mwaka wa pili.

Sayyid al-Hakim na Sayyid al-Khui wamesema: "Katika ngamia hujuzu yule aliyeingia katika mwaka wa sita, na katika ng'ombe na kondoo awe ameingia katika mwaka wa tatu." Kisha wote wawili wakasema: "Ilivyo bora zaidi ni mbuzi awe ameingia katika mwaka wa pili."

**2.** Mnyama huyo awe ni kamili asiyekuwa na kasoro yoyote. Kwa hivyo aliyekonda hafai, wala kiguru na mwenye maradhi, wala mkubwa asiye na bongo. Kisha wamekhitilafiana kuhusu mnyama aliyehasiwa na asiyekuwa na pembe, asiye na sikio moja au analo lakini ni dogo na aliyekatwa mkia.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 343 2/1/2017 3:51:58 PM

Sayyid al-Hakim na Sayyid al-Khui wamesema: Mnyama mwenye mojawapo ya ila zilizotajwa haijuzu kuchinjwa." Mwenye kitabu *Al-Mughni* amesema: "Hujuzu aina yoyote kati ya wanyama hao."

Mwanachuoni al-Hilliy katika kitabu *at-Tadhkirah* amesema: "Wanyama wa kike katika ngamia na ng'ombe ni bora zaidi. Na wa kiume katika kondoo na mbuzi ni bora zaidi. Na hapana tofauti kati ya mafakihi katika kujuzu kinyume chake." Mwenye kitabu *Al-Mughni* amesema: "Dume na jike katika dhabihu ni sawa."

## WAKATI NA MAHALI PA KUCHINJIA:

Ama wakati wa kuchinja dhabihu, Maliki, Mahanafi na Mahanbali wamesema: "Ni siku ya Idd na siku mbili zinazofuata, mwezi kumi na moja na mwezi kumi na mbili." Isipokuwa Mahanafi wamesema: "Wakati huu kwa hakika ni wa kuchinja dhabihu ya *Qiran* na *Tamattui*, ama nyinginezo hazifungamani na wakati maalum." Na kamwe Maliki hawakutofautisha baina ya aina za dhabihu kama ilivyokuja katika kitabu *Al-Fiqh Alal Madhahibil Arbaa*.

Mahanbali wamesema: "Akitanguliza kuchinja kabla ya wakati wake itakuwa ni wajibu kwake kuchinja badala yake. Na kama atachelewesha kuchinja hadi baada ya wakati wake, kama alikuwa ni dhabihu wa Sunna huporomoka kwa kutoweka wakati wake, na kama ni wa wajibu atalipa." Mahanafi wamesema: "Kama atachinja dhabihu wa *Tamattui* na *Qiran* kabla ya kuingia siku tatu za Idd, hatatosheleza. Lakini akichelewesha atatosheleza, isipokuwa atalazimika kutoa kafara ya kuchelewa kuchinja."

Mashafi wamesema: "Wakati wa kuchinja wanyama wa dhabihu ya wajibu kwa aliyehiji Hijja ya *Tamattui* ni baada ya kuhirimia kwake Hijja, na hujuzu kutanguliza kabla ya hapo wala hakuna



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 344 2/1/2017 3:51:58 PM

kikomo cha mwisho wake, lakini bora ni amchinje siku ya kuchinja (Siku ya Iddi)." (Kitabu a*l-Fiqh Alal Madhahibil Arbaa*).

Maimamiyya baada ya kuwajibisha kutia nia wakati wa kuchinja dhabihu wamesema: "Kwa hakika wakati wa kuchinja ni siku ya Idd, lakini anapoichelewesha kuchinja hadi siku ya pili, ya tatu au ya nne hujuzu, lakini hupata dhambi kwa kuchelewesha huko. Na hukmu ni hiyo hiyo lau atachinja katika baki ya siku za mwezi wa Dhulhijja."

Na mwenye kitabu *Al-Jawahir* amenukuu kutokuwepo tofauti baina ya mafikihi katika jambo hilo, hata kama kuchelewa huko kumetokea bila udhuru. Na wala kamwe haijuzu kutanguliza kuchinja kabla ya kuingia siku ya kumi (ya Dhul-Hijja) katika madhehebu ya Kiimamiya.

Ama mahali pa kuchinjia ni katika Haram kwa mujibu wa madhehebu ya Hanafi, Shafi na Hanbali. Na Mina imo ndani ya Haram[64] na vituo vingine. Tumeshabainisha mpaka wake katika kifungu kilichotangulia chini ya anwani 'Yaliyo haramu kwa aliye katika ihram.' Chini ya 'Mpaka wa Haram mbili.'

Maliki wamesema: "Kuchinja dhabihu huko Mina kuna masharti matatu:

**La kwanza:** Awe amepelekwa kwa ajili ya ihramu ya Hijja, si kwa ajili ya Umra.

**La pili:** Asimame na mnyama huyo Arafah, sehemu ya usiku wa kuamkia Idd.

**La tatu:** Atake kumchinja mnyama huyo katika siku ya Idd au siku inayofuata baada ya Idd."

Maimamiyya wamesema: "Mwenye kuhiji Hijja *Tamattui* asichinje mahali pengine ghairi ya Mina, hata kama *Tamattui* yake

[64] Kutoka Mina hadi Makka pana umbali wa farsakhi moja.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 345 2/1/2017 3:51:58 PM

ni ya Sunna, si ya wajibu. Ama mnyama anayepelekwa kwa ihramu ya Umra yeye atachinjiwa Makka." (*At-Tadhkirah*).

Na kwa hali yoyote ile iwayo, kuchinja mnyama wa dhabihu huko Mina inajuzu kwa mafakihi wa madhehebu yote, na ndio bora zaidi. Ibn Rushd amesema: "Kwa ujumla kuchinja Mina wamekongamana juu yake wanavyuoni wote." Na kwa kuongezea ni kuwa, kwa hakika ikhtilafu iliyopo baina ya Maimamiyya na wasiokuwa wao, ni kwamba Maimamiyya wamesema: "Pana ulazima wa kuchinja Mina", na wenzao wanasema kuchinja Mina ni jambo la hiari si lazima, anaweza akachinja mahali popote pale katika eneo la Haram.

**NYAMA YA DHABIHU:**

Mahanbali na Mashafi wamesema: "Mnyama ambaye ni wajibu kuchinjiwa Haram, nyama yake ni wajibu kuwagawia masikini hapo hapo." Mahanafi na Maliki wamesema: "Hujuzu kuigawa nyama yake katika Haram na penginepo." Mashafi wamesema: "Wanyama wa dhabihu ya wajibu haifai kula katika nyama yake, na wa Sunna hujuzu kula."

Maliki wamesema: "Nyama ya dhabihu yoyote ni ruhusa kuila isipokuwa dhabihu wa fidia ya kuwa na vya kumuudhi kichwani, dhabihu wa malipo ya kuwinda (mnyama pori), dhabihu wa nadhiri iliyowekwa kwa ajili ya masikini, na dhabihu wa Sunna anapokuwa ameharibika kabla ya kufika mahali pake." (Kitabu *Al-Mughni*, *Fiqh Alal Madhahibil Arbaa* na *Fiqh Sunna*).

Maimamiyya wamesema: "Atatoa sadaka theluthi moja ya nyama ya dhabihu, kumpa fukara aliye muumini, na theluthi moja atawazawadia waumini hata kama ni matajiri, na theluthi iliyobaki atakula yeye mwenyewe." Kitabu *Al-Jawahir,* na *Mansak c*ha Sayyid al-Hakim na *Mansak* cha Sayyid al-Khui).



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 346 2/1/2017 3:51:58 PM

## BADALI:

Wameafikiana kuwa, anayehiji akosapo kupata mnyama wa kuchinja, na akakosa pia thamani ya mnyama, atafunga Swaumu siku kumi kamili, siku tatu miongoni mwa hizo azifunge katika siku za Hijja, na saba baada ya yeye kurudi kwa watu wake (kwao). Kwa mujibu wa kauli yake Mwenyezi Mungu (s.w.t.) aliposema:

”..... فَمَن لَّمْ يَجِدْ فَصِيَامُ ثَلَٰثَةِ أَيَّامٍ فِي ٱلْحَجِّ وَسَبْعَةٍ إِذَا رَجَعْتُمْ تِلْكَ عَشَرَةٌ كَامِلَةٌ .....“

**“Na asiyepata (mnyama afunge siku tatu katika Hijja na siku saba mtakaporudi (kwenu); hizo ni siku kumi kamili.” (2:196)**[65]

Na kipimo cha uwezo wa kuchinja dhabihu hutizamwa pale awapo eneo la kuchinjia, hivyo ukikosekana mahali pake pa kuchinjia, moja kwa moja atageukia katika kufunga, hata kama anao uwezo wa kuchinja awapo katika mji wake, kwa sababu wajibu wake una wakati maalumu, hivyo hali inapokuwa hivyo uwezo wake hutizamwa ndani ya wakati wake, ni sawa kabisa na ulivyo ulazima wa maji katika tohara. (*At-Tadhikrah)*.

## KUMWEKA MTU WA KUKUCHINJIA:

Ilivyo bora kwa anayehiji atekeleze kuchinja yeye mwenyewe binafsi, na pia hujuzu kumweka mtu mwingine amchinjie kwa kuwa

[65] Inaeleweka wazi kwamba kila hukmu ambayo ina *nassi* kutoka katika Qur’ani huwa ni yenye kuwafikiana kati ya madhehebu yote ya kiislamu, huwa hapana tofauti ya kuswihi kwake baina ya Sunni na Shia. Bali hitilafu iliyoko kati yao hutokea katika hukmu isiyokuwa na *nassi* ya Qur’ani, au katika ujumla wake, udhaifu wake au kupingana kwake na hukmu nyingine, au katika tafsiri yake na mafungamano yake, na hii ni dalili mkato inayofahamisha kwamba Waislamu wa madhehebu yote wanachimbua sharia na hukmu zao kutoka kwenye chombo kimoja.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 347 2/1/2017 3:51:59 PM

ni miongoni mwa matendo ambayo hukubalika kuweka naibu, kwa sharti anayewakilisha unaibu atie nia hiyo wakati wa kuchinja tangu awali, na bora zaidi ni kunuia wote pamoja.

Maimamiyya wamesema: “Husunniwa kwa anayehiji (ambaye ameweka mtu wa kumchinjia, aweke mkono wake juu ya mkono wa mchinjaji, au awepo wakati wa kuchinja (huyo mnyama).”

Katika kitabu *Manahijul-Yaqin* cha Sheikh Abdullah Al-Muqamqani wa madhehebu ya Imamiyya mmeandikwa hivi: “Anapokosea aliyewakilisha katika jina la mwakilishwa; au anapolisahau jina lake, haidhuru kitu, kwani linalotegemewa ni kukusudia.” Na hii ni kauli ya sawa kabisa, maana imepokewa kutoka kwa Imam عليه السلام wakati mwakilishi mmoja katika ndoa alipokosea jina la mwanamke, akataja jina jingine, Imam akasema: “Hapana ubaya.”

**Aliyekinai na mwombaji:**

Katika Qur’ani Tukufu Aya 36 katika Suratul Hajj, Mwenyezi Mungu (s.w.t.) anasema:

“..... فَكُلُوا۟ مِنْهَا وَأَطْعِمُوا۟ ٱلْقَانِعَ وَٱلْمُعْتَرَّ ۚ كَذَٰلِكَ سَخَّرْنَـٰهَا لَكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٣٦﴾

**“Basi kuleni na mlisheni aliyekinai na aombaye. Kama hivyo tumewafanya hawa wawe dhalili kwenu ili mpate kushukuru.”**

Imam as-Sadiq amesema: “Aliyekinai ni yule ambaye huridhika kwa unachompa wala hakasiriki au kununa kwa hasira. Na aombaye ni yule apitaye kwako ili umpe, kwa maana ya kuwa hukupa usumbufu wa kukuomba.”



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 348 2/1/2017 3:51:59 PM

**AKOSAPO NGAMIA:**

Aliyelazimika kuchinja ngamia wa kafara au nadhiri lakini hakumpata, hulazimika kuchinja mbuzi saba, azichinje kwa taratibu, na kama hakumakinika kupata atafunga siku kumi na nane. (Kitabu *At-Tadhkirah*).

***Taqlid* na *Ishiari*:**

*Taqlid* ni kuweka katika shingo ya mnyama wa dhahibu sandali na mfano wake. Na *Ishiari* ni kupasua upande wa kulia wa nundu ya ngamia na ng'ombe hadi atoe damu, na amtapakaze kwa damu hiyo.

Na kwa hakika tendo hili la kufanya *Taqlid* na *Ishiari* limesunnishwa kwa mujibu wa mafakihi wa madhehebu yote isipokuwa Abu Hanifa, yeye amesema: "Husunniwa kumfunga sandali mbuzi na ngamia, ama kumpasua nundu ngamia na ng'ombe haijuzu hata chembe kwa hali yoyote iwayo. Kwa sababu huko ni kumwadhibu mnyama na kumuumiza." (Kitabu *Al-Mughni*).

Na sisi sote ni miongoni mwa watetezi wanaotetea kuwafanyia upole wanyama, na hasa sote ni Waislamu. Bila shaka Uislamu umehalalisha kuchinja wanyama (katika Udhuhiya na dhabihu), bali Uislamu huo huo umewajibisha kuchinja mnyama wa dhabihu kwa mujibu wa Abu Hanifa na fatwa yake na tendo lake, basi huko kumfanyia *Ishiari* ni njia iliyo bora zaidi.

**KUMPA SADAKA ASIYEKUWA MWISLAMU:**

Sayyid al-Khui katika kitabu chake *Manasikul-Hajj* amesema: "Anayehiji anapotoa sadaka au akamtoa hidaya dhabihu wake kumpa mtu, hujuzu kwa huyu wa mwisho kumpa yeyote amtakaye hata asiyekuwa Mwislamu." Kwa ujumla, Maimamiyya wameha-

lalisha kumpa wakfu na sadaka isiyokuwa ya wajibu Mwislamu na asiyekuwa Miislamu.

Sayyid Abul Hassan Al-Asfahani katika kitabu *Wasilatuni Najat* amesema: "Haizingatiwi kwa mtu anayepewa sadaka iliyo ya Sunna ufukara, imani bali wala Uislamu, kwani hujuzu kupewa tajiri, na asiyekuwa mfuasi wa madhehebu ya Imamiyya, na dhimmiy (kafiri aliye kwenye dhima) hata kama wote wawili ni wa kando (si katika akraba wa anayetoa sadaka)." Bali Sayyid Kadhim katika maelezo ya ziyada ya kitabu *Al-Urwa* amesema: "Hujuzu kutoa sadaka kumpa asiyekuwa Mwislamu hata kafiri anayepigana vita na Waislamu."

## KUZIKA NYAMA YA DHABIHU NA KUICHOMA MOTO:

Siku hizi ni kawaida mahujaji kutoa pesa taslimu kwa anayekubali dhabihu, kisha baada ya kuchinja huizika nyama[66] hiyo au huibwaga pembeni, kulingana na wingi wa dhabihu wachinjwao na kukosekana wenye kuwahitajia.

Nami katika vitabu nilivyosoma sikuona hata fakihi mmoja aliyepinga uhalali wa hilo, au aliyekataza, licha ya kuwepo haja kubwa ya kutaka kujua hukmu yake na dalili yake.

Na katika mwaka 1949 Mahujaji wa kimisri walikiuliza Chuo Kikuu cha Azhar, wakataka kujua fatwa juu ya jambo hilo, na wakataka wapate idhini ya kutoa thamani ya wanyama wa dhabihu kwa wahitaji; mheshimiwa Sheikh Mahmud Shaltut akatoa fatwa katika Toleo la Nnne la Juzuu ya Kwanza ya jarida la *Risalatul-Islam*, ambalo lilitolewa na *Darut-Taqrib* huko Cairo, Misri, ambapo katika fatwa hiyo aliwajibisha kuchinja hata kama kutalazimu kuiteketeza nyama kwa moto na kuizika.

66 Sayyid Al-Hakim amesema: "Inapokuwa vigumu kutoa sadaka kwa nyama ya dhabihu hufutika ulazima wake. Na kama fukara hatakubali sadaka hiyo ila apewe pesa haitapasa."

Mimi binafsi nilipinga fatwa yake hiyo katika maelezo marefu yaliyochapishwa katika matoleo mawili mfululizo katika jarida hilo hilo tulilolitaja hapo juu katika mwaka 1950. Na wakati Shirika la *Darul-llmi Lilmalayin* liliporudia kukichapisha kitabu *Al-Islam Maal-Hayat* makala hayo niliyaingiza humo kwa anwani ' *Hal Taabbudunash-sharia Bilhadyi Fi halin Yatruk Fihil Fasda? (J*e sharia inatulazimisha tufanye ibada ya kuchinja dhabihu katika hali ya kusababisha ufisadi)?

Nilimalizia makala yangu kwa kusema kuwa, ni wajibu kuchinja dhabihu wakati wanapopatikana walaji, au unapopatikana uwezekano wa kunufaika na nyama hiyo, kama vile kuikausha au kuisindika kwa njia za kileo kwa namna ambayo itafaa kwa kuliwa baadaye. Ama nyama hiyo ya dhabihu inapoishia katika uharibifu, kama vile kuichoma moto au kuizika, basi huko kujuzu kwake, na ndivyo hasa ilivyo, itafaa kuchunguzwe. Na yeyote anayependa kusoma habari hizo kwa kirefu na kikamilifu ili aijue dalili yangu ya kupinga hilo, arejee kitabu *Al-Islam Maal Hayat* chapa ya pili.

Baadaye nilidhihirikiwa na Hadith iliyomo katika kitabu *Al-Wasail* inayounga mkono madai yetu, kwani mwenye kitabu *Al-Wasail* amenukuu katika suala la nyama ya Udhuhiya chini ya anwani hiyo, katika mlango unaokokoteza kusunniwa kwa Udhuhiya, riwaya iliyopokelewa na Ja'far as-Sadiq, kutoka kwa baba zake, nao wamemnukuu Mtume ﷺ kuwa amesema: "Kwa hakika si jenginelo bali hii Udhuhiya imewekwa kwa ajili ya kuwashibisha (kuwalisha) masikini wenu kwa nyama hiyo, basi walisheni." Na Hadith hii, hata kama ilihusu hasa nyama ya Udhuhiya iliyo ya Sunna, lakini inaangaza mwangaza wake katika nyama ya dhabihu ya wajibu pia.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 351 2/1/2017 3:51:59 PM

# KATI YA MAKKA NA MINA

Tumetangulia kusema kwamba tendo la kwanza kabisa linalotendwa huko Mina mnamo siku ya kumi ya Dhulhijja ni kutupa vijiwe, na la pili ni kuchinja dhabihu, ama la tatu ni kunyoa nywele au kupunguza nywele, ambapo tumeonyesha hukmu ya kutanguliza kunyoa au kupunguza kabla ya kuchinja, chini ya anwani isemayo, "Mina' anayetaka kupata maelezo kamili na azirudie sehemu hizi mbili.

Na anayehiji akishamaliza ibada zake Mina mnamo siku ya Idd, kuanzia kutupa vijiwe na kuchinja atarejea Makka akaitufu Al-Kaaba Twawafu ya Ziyara, kisha ataswali rakaa mbili za Twawafu hiyo, akimaliza atakwenda kusai baina ya Swafa na Marwa.

Na kwa mujibu wa madhehebu manne, atarejea Mina baada ya Twawafu hii ya Ziyara, na akimaliza huwa amehalalikiwa na kila kitu (kilichokuwa haramu kwake baada ya kuhirimia) hata wanawake.

Na kwa Maimamiyya, atatufu Twawafu nyingine nayo ni Twawafu Nisaa, kisha ataswali rakaa zake mbili. Na kwao Maimamiyya wanawake hawawi halali hadi awe ametufu Twawafu hii. Na maelezo yake kirefu tumekwisha yasema huko nyuma.

## KULALA MINA:

Amalizapo kutufu huwa ni wajibu kwake kurudi tena Mina katika ile mikesha ya *Tashriq*, nayo ni usiku wa mwezi kumi na moja, wa kumi na mbili na wa kumi na tatu, isipokuwa atakapofanya haraka aka-ondoka baada ya kukengeuka jua na kabla ya kuchwa jua la mwezi kumi na mbili, hatalazimika chochote juu yake. Na hali ni kama hivi mnamo siku ya tatu, kama alivyosema Mwenyezi Mungu (s.w.t.); "Lakini afanyaye haraka katika siku mbili (akarejea) basi si dhambi juu yake." (Al-Baqarah: 203).



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 352 2/1/2017 3:51:59 PM

Abu Hanifa amesema: "Kulala Mina ni Sunna si wajibu." Na wanaosema kuwa ni wajibu kulala Mina wameafikiana kuwa huko kulala Mina ni miongoni mwa matendo ya wajibu katika Hijja na wala si nguzo, kisha wamekhitilafiana kuhusu wajibu wa kutoa kafara kwa mtu aliyeacha kulala Mina.

Ibn Hanbal amesema: "Halazimiki kutoa chochote." Shafi amesema: "Hulazimika kutoa kafara ya kibaba cha chakula." (Kitabu *At-Tadhikra*, *Al-Mughni* na *Fiqh Sunna)*. Maliki amesema: "Hulazimika kuchinja." Sharh ya Az-Zarqani kwenye *Muwatau* ya Imam Malik).

Maimamiyya wamesema: "Kama alilala mahali pengine pasipokuwa Mina; kama alikesha Makka huku akifanya ibada hadi asubuhi, hatalazimika kutoa fidia. Lakini kama alilala mahali pasipokuwa Makka, hata kama hapo alipolala alikesha akifanya ibada, ni wajibu kwake kutoa fidia ya mbuzi mmoja kwa ajili ya kila usiku, hata kama alifanya hivyo kwa kusahau au kwa kutojua." (M*anahijun-Nasikin* cha Sayyid Al-Hakim).

Na katika nyusiku anazokuwepo hapo Mina hakuna amali iliyo wajibu kufanywa hapo, bali husunniwa kuswali Tahajud na ibada nyinginezo.

## KUTUPA VIJIWE KATIKA SIKU ZA *TASHRIQ*:

Katika siku tatu za *Tashriq*, mwenye kuhiji Hijja *Tamattui*, *Qiran* au *Mufrada* hapana tendo lolote jingine analotakikana kulifanya zaidi ya kutupa vijiwe vitatu katika kila siku, kwa itifaki ya mafakihi. Ama idadi ya vijiwe na yote yanayofungamana nayo ni kama ilivyokwisha tangulia kuelezwa katika Jamaratul-Aqaba ambayo hupigwa vijiwe katika siku ya Idd.

Maimamiyya wamesema: "Wakati wa kutupa vijiwe katika kila siku ya kutupa, huanza tangu kuchomoza kwa jua hadi kuzama

kwake, katika siku zote tatu." Mafakihi wa madhehebu manne wamesema: "Huanza tangu kukengeuka kwa jua hadi kuzama kwake, na kama atatupa kabla ya kukengeuka kwa jua atarudia tena." Juu ya hilo Maimamiyya wamesema: "Kutupa katika wakati huo wa kukengeuka jua ni bora zaidi."

Abu Hanifa amejuzisha kutupa vijiwe kabla ya kukengeuka jua katika siku ya tatu tu. Na hujuzu kuchelewesha kutupa hadi baada ya kuzama upatikanapo udhuru wa hakika."

Nasi twamshukuru Mwenyezi Mungu (s.w.t.) kwa kuwafikiana mafakihi wote katika suala zima la kutupa vijiwe hivi katika idadi yake na jinsi ya kutupa kwenye siku tatu hizo. Na kunakofuata, tutataja sura halisi ya kutupa vijiwe kama ilivyoandikwa katika kitabu *At-Tadhikrah* na *Al-Mughni*.

Anayehiji, katika kila siku miongoni mwa siku tatu atatupa jumla ya vikokoto ishirini na moja kwa mikupuo mitatu, kila mkupuo mmoja atatupa vikokoto saba. Ataanza na Jamarat ya kwanza (imeshatajwa huko nyuma), nayo ndiyo Jamarat iliyo mbali zaidi na Makka, na ndiyo iliyo karibu na Masjidul Khaif, nayo yasunniwa aipige vijiwe hivyo kwa namna inayoitwa *Hadhfan*[67] kwa upande wa kushoto wa Jamarat, kutokea upande wa Batnul-Musil. Aipige vijiwe saba, na apige Takbira na aombe dua kila aipigapo kijiwe.

Kisha aende katika Jamarat ya pili, ambayo huitwa *Jamaratul-Wustwa*, asimame upande wa kushotoni wa njia, aelekee Kibla, amuhimidi Mwenyezi Mungu na amsifu kwa sifa zake njema, kisha amuombee rehema Mtume ﷺ kisha asogee mbele kidogo aombe dua, kisha aipige vijiwe. Afanye kama alivyofanya wakati wa kuipiga Jamarat ya kwanza. Asimame baadaye na kuomba dua baada ya kutupa kijiwe cha mwisho.

[67] *Hadhf* ni kukiweka kijiwe juu ya tumbo la dole gumba na akitupe kwa msukumo wa kidole cha shahada.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 354 2/1/2017 3:51:59 PM

Kisha atakwenda kwenye Jamarat ya tatu, ambayo nayo pia huitwa *Jamaratul-Aqaba,* aipige vijiwe kama alivyofanya katika zilizotangulia, na wala asisimame baada ya kumaliza. Na kwa Jamarat hiyo atakuwa amemaliza kupiga vijiwe.[68] Hivyo jumla ya vijiwe atakavyotupa katika siku zote tatu huko Mina ni 63 kama atalala Mina usiku wa mwezi kumi na tatu, kila siku ni vijiwe 21, kuongezea vile alivyovitupa siku ya Idd vitatimia sabini.

Mwenye kitabu *at-Tadhkirah* baada ya kunukuu maneno haya alisema: "Sisi hatujui ikhtilfu katika maelezo haya." Na mwenye kitabu *Al-Mughni* amesema: "Na kamwe hatuelewi kuwepo ikhtilafu katika maelezo yote tuliyoeleza isipokuwa Malik, ambaye amekhalifu wenzake kuhusu kuinua mikono miwili." Na maneno aliyosema mwenye kitabu *Al-Mughni* ni sawa kabisa na aliyoyataja mwenye kitabu *At-Tadhikrah* au yanakurubiana sana.

Na kwa maelezo hayo basi imebainika wazi kuwa kila moja katika hizo mara tatu za kutupa vijiwe, ina mahali pake halisi pa kutupia katika hiyo Mina, ambapo haijuzu kuiruka (kutoka nje yake).

Kisha wote wameafikiana kwa pamoja isipokuwa Abu Hanifa, wajibu wa kufuata mpangilio katika Jamarat hizi, na kama atatanguliza Jamarat ya nyuma kabla ya ile ambayo ilikuwa itangulizwe, ni wajibu kwake kurudia na afuate mpangilio. Abu Hanifa amesema: "Si wajibu kufuata mpangilio kamwe." (*At-Tadhikrah* na *Al-Mughni)*.

Hujuzu kutupa vijiwe hivyo katika hali ya kuwa juu ya mnyama au kwa miguu, na kuwa uko katika hali ya kusimama na miguu ni bora zaidi. Na kwa mwenye udhuru hujuzu kutupiwa na mwenzake. Na kama ataacha kupiga takbira, kuomba dua au kusimama baada ya kutupa kwa pili, hatakuwa na chochote juu yake.

[68] Sayyid Al-Hakim amesema: "Hiyo mara ya tatu inafaa atupe katika hali ya kukipa mgongo Kibla." Na katika *Al-Mughni* atatupa katika hali ya kuelekea Kibla.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 355 2/1/2017 3:51:59 PM

Na kama atachelewesha kutupa vijiwe hadi siku ya pili yake kwa makusudi, au kwa kutojua au kwa kusahau. Au kama atachelewesha mpaka siku ya mwisho ya siku za *Tashriq,* akatupa vijiwe vyote katika siku moja, hatalazimikiwa na chochote kwa mujibu wa madhehebu ya Shafi na Maliki.

Abu Hanifa amesema: "Anapoacha kijiwe kimoja au viwili au vitatu hadi kesho, atavitupa kesho yake, naye kwa ajili ya kila kijiwe kimoja atalazimika alishe masikini chakula. Na kama ataacha vinne atavitupa kesho yake, na atalazimika kuchinja mnyama."

Na mafakihi wa madhehebu manne wameafikiana kuwa mtu ambaye hakuzipiga Jamarat vijiwe hadi siku za *Tashriq* zikapita, si wajibu kwake kuzipiga tena vijiwe. Kisha wamekhitilafiana kuhusu kutoa kafara yake. Maliki wamesema: "Anayeacha kuipiga Jamarat vijiwe mara zote au baadhi yake, ijapokuwa ni mara moja tu, itamlazimu kuchinja mnyama."

Mahanafi wamesema: "Anayeacha basi atapaswa kuchinja, na anayeacha mara moja na kuendelea, basi badala ya kila kijiwe kimoja alichoacha kutupa atalisha masikini."

Mashafi wamesema: "Anayeacha kuipiga Jamarat kijiwe kimoja atalisha kibaba cha chakula, vijiwe viwili atalisha vibaba viwili, na vijiwe vitatu atachinja." (Kitabu *Bidaya* Ibn Rushd na *Al-Mughni*).

Maimamiyya wamesema: "Kama atasahau kuipiga Jamarat vijiwe vyote au baadhi ya vijiwe, atarudia kesho yake maadamu tu bado ni ndani ya siku za *Tashriq*. Lakini kama atasahau kuipiga kabisa Jamarat vijiwe, hadi akawasili Makka, ni wajibu kwake kurejea Mina akaipige vijiwe hivyo kama siku za *Tashriq* zingalipo, na kama zimekwisha basi mwaka unaofuata, yeye mwenyewe binafsi au naibu wake ataipiga vijiwe, na wala hakuna kafara juu yake." (Kitabu *At-Tadhkirah*).



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 356 2/1/2017 3:51:59 PM

Na hili linawafikiana na fatwa ya Masayyid wawili al-Hakim na al-Khui, isipokuwa huyo wa mwanzo ameusifia wajibu wa kulipa kuwa ni wajibu wenye nguvu. Na wameafikiana kwamba anayeacha kuipiga Jamarat vijiwe kwa makusudi, Hijja yake haibatiliki.

Na huko nyuma tumeonyesha kuafikiana kwa madhehebu, kuwa anayehiji anaweza kutosheka na siku mbili tu katika siku za *Tashriq,* hivyo anaweza kuondoka Mina kabla ya kuzama jua la siku ya kumi na mbili. Lakini kama litazama ilihali yeye bado angalipo Mina, ni wajibu kulala hapo na kuipiga Jamarat vijiwe katika siku ya kumi na tatu, lakini Maimamiyya wamesema: "Kwa hakika yajuzu kutoka Mina na kufanya haraka, kwa yule aliyejizuia na mawindo na wanawake katika ihram yake, la sivyo basi ni wajibu kwake kulala usiku wa mwezi kumi na tatu pia."

Na husunniwa kuswali katika msikiti wa Khaif huko Mina, na katika kila jabali ambalo huitwa Khaif. (*At-Tadhkirah)*.

Anayehiji atakaporudi Makka baada ya kumaliza amali za Mina, husunniwa atufu Twawafu ya kuaga kwa mujibu wa madhehebu ya Imamiyya na Maliki.

Mahanafi na Mahanbali wamesema: "Kutufu Twawafu ya kuaga ni wajibu kwa mtu asiyekuwa mkaazi wa Makka, na kwa mtu asiyetaka kukaa Makka baada ya kurudi kutoka Mina."

Na kama mwanamke atazukiwa na damu ya hedhi kabla ya kutufu Twawafu ya kuaga, atatoka wala hataaga, na wala hatatoa fidia kwa mujibu wa wale waliowajibisha kuaga kwa asiyekuwa na hedhi, lakini husunniwa akaage karibu sana na mlango wowote miongoni mwa milango ya msikiti, lakini asiingie ndani.

Na kwa Twawafu hii anayehiji huwa amemaliza amali zake za Hijja. Na katika kifungu kijacho tutaeleza namna ya Hijja kama ilivyo katika madhehebu yote.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 357 2/1/2017 3:51:59 PM

# SURA YA HIJA

Kwa ajili ya kutaka kumfafanulia na kumsahilishia msomaji ibada hii ya Hijja, tumeonelea katika kifungu hiki tuzungumzie ilivyo sura ya Hijja kwa mfumo uliokusanya matendo yote ya Hijja, kufuatana na mpangilio uliowekwa na sharia katika ibada hii:

Mtu anayehiji ambaye ametoka nchi iliyo mbali na Makka atahirimia kwenye *Miqati* ambayo atapitia, au iliyo usawa mmoja na njia anayopitia, na ataanza kuleta *Talbiya.*[69] Na katika kufanya hivyo hakuna tofauti kati ya mwenye kufanya Umra *Mafrada*, *Tamattui* au *Qiran*.

Ama wakazi wa Haram watahirimia kutoka majumbani mwao.[70]

Atakapoiona al-Kaaba atapiga Takbira na Tahlil, hii ni mustahabu. Atakapoingia Makka ataoga, hii pia ni Sunna. Kisha ataingia Baitul-Haram akaliguse jiwe jeusi, na akiweza alibusu, na akishindwa kuligusa ataliasharia kwa mkono wake. Kisha atufu Twawafu ya kuwasili Makka, ambayo ni Sunna kama alikuwa anahiji *Ifrad* au *Qiran*.[71]

Kisha ataswali rakaa mbili za Twawafu, kisha ataligusa jiwe jeusi akiweza na atoke nje, kisha atabaki hapo Makka akiwa na ihram yake.

---

[69] Talbiya kwa Imamiyya, Hanafiyya na Malikiyya ni wajibu. Na kwa Hanbaliyya ni Sunna. Na wakati wake ni baada ya kuhirimia.

[70] Imamiyya huwajibisha Hijja ya *Tamattui* kwa asiyekuwa mkaazi wa Makka wanamuhiarisha ajiamulie kati ya kufanya *Qiran* au *Ifrad*. Na madhehebu manne hayakutofautisha baina ya mkaazi wa Makka na mwenginewe, katika kujiamulia namna anayotaka, isipokuwa Abu Hanifa amekirihisha kwa mkaazi wa Makka kuhiji *Tamattui* na *Qiran*.

[71] Twawaf ya kuwasili Makka ni Sunna kwa madhehebu yote, isipokuwa Malik alisema ni wajibu.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 358 2/1/2017 3:51:59 PM

Itakapofika siku ya Tarwiya, nayo ni mwezi nane ya Dhulhijja ataondoka Makka kwenda Arafah, na akipenda ataweza kuondoka kabla ya kuingia Tarwiya kwa siku moja.

Kama alikuwa anafanya Umra *Mufrada* au anahiji Hijja *Tamattui* itamlazimu atufu, kisha aswali rakaa mbili za Twawafu, kisha atasai baina ya Swafa na Marwa, kisha atanyoa nywele au kuzipunguza,[72] na wakati huo huhalalikiwa katika ihram yake na kila kitu hata wanawake.[73]

Kisha anayefanya *Tamattui* atahirimia tena ihram kwa mara ya pili, hapo hapo Makka katika wakati ambao utayumkinika kuwahi kwenda kusimama Arafah, wakati wa kukengeuka jua mnamo siku ya tisa ya mwezi wa Dhulhijja. Na iliyo bora ni kuhirimia katika siku ya Tarwiya, nayo ni siku ya nane ya Dhulhijja, na kuhirimia huko kufanywe chini ya *Mizab*.

Kisha anayehiji *Tamattui*, *Qiran* au *Mufrada* ataelekea Makka kupitia Mina, na wakati wa kusimama Arafah huanza mara tu baada ya kukengeuka jua la siku ya tisa hadi alfajiri ya siku ya kumi, kwa mujibu wa madhehebu ya Mahanafi, Mashafi na Maliki. Na kwa Mahanbali ni tangu alfajiri ya siku ya tisa hadi alfajiri ya siku ya

---

[72] Imamiyya wamesema: "Anahiarishwa baina ya kunyoa na kupunguza kama anafanya Umra *Mufrada*, ama kama anafanya *Tamattui* basi anawajibika kupunguza. Kama ambavyo wamewajibisha juu ya mwenye kufanya Umra *Mufrada* atufu mara ya pili twawaf ya wanawake baada ya kunyoa au kupunguza nywele na wala hawamuhalalikii wanawake baada ya twawaf hii. Madhehebu manne yamesema: "Ana hiari baina ya kunyoa na kupunguza kwa wawili, wala hawakuwajibisha kutufu twawafu ya wanawake kwa yeyote kwa afanyaye Umra wala anayehiji. Kama ilivyo kwa Malik kutowajibisha kunyoa wala kupunguza nywele kwa anayefanya Umra *Mufrada*."

[73] Imamiyya wamesema: "Huwa halali kwa mwenye kufanya twawaf anapopunguza hata kama ana dhabihu ambayo ameichagua kuipeleka Makka wakati wa kuhirimia." Wasiokuwa wao: "Anayefanya Tamattui ambaye amehirimia Umra kwenye Miqat huhalalikiwa anaponyoa au kupunguza nywele kama hakuwa na dhabihu, na kama ana dhabinu atabaki kuwa katika Ihram. Ama anayefanya Tamattui ya Umra Mufrada basi huhalalikiwa moja kwa moja, ni sawa alikuwa na dhabihu au hakuwa naye. Mwenye *Al-mughni* alipokwisha kusema hivi, alisema; "Hatujuui kuwepo ikhtilafu."



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 359 2/1/2017 3:51:59 PM

kumi. Na kwa Maimamiyya ni tangu kukengeuka jua katika siku ya tisa hadi kuzama kwa jua la siku hiyo, na kwa mwenye dharura ni hadi alfajiri ya siku ya kumi.[74]

Anayehiji ataomba dua hapo Arafah, na yasunniwa atopee katika kuomba dua, kisha ataondoka kuelekea Muzdalifa, ataswali hapo Swala ya Maghribi na Isha usiku wa Idd akizikusanya mbili hizo, kukusanya huko ni mustahabu kwa itifaki ya wanavyuoni.

Na ni wajibu kulala usiku huu hapo Muzdalifa kwa Mahanafi, Mashafi na Mahanbali. Ama kwa Maimamiyya na Maliki si wajibu lakini ni bora zaidi.

Na katika usiku huu hulazimika kusimama Mash'aril Haram baada ya kuingia alfajiri kwa mujibu wa madhehebu ya Imamiyya na Hanafi, na kwa wasiokuwa wao ni Sunna.

Na kutoka hapo Muzdalifa anayehiji ataokota vijiwe sabini - hii ni Sunna - ili akavitumie katika kuipiga Jamarat, kisha ataelekea Mina kabla ya kuchomoza jua la siku ya Idd, akaipige vijiwe *Jamaratul Aqaba*, sawa awe anahiji Hijja *Tamattui*, *Qiran* au *Ifrad,* na ataipiga Jamarat vijiwe muda uliopo kati ya kuchomoza jua na kuzama kwake, na atapiga Takbira na kumsabihi Mwenyezi Mungu wakati wa kuipiga Jamarat vijiwe, hii ni Sunna.

Kisha atachinja kama anahiji Hijja *Tamattui* na si mkaazi wa Makka, hii ni kwa itifaki. Wala si wajibu kwa anayehiji Hijja *Ifrad* kwa itifaki ya madhehebu zote, bali husunniwa.

Ama anayehiji Hijja *Qiran* ni wajibu kwake kuchinja kwa mujibu wa madhehebu mengine manne, bali si wajibu kwa mujibu wa

---

[74] Hupasa kusimama Arafah katika wakati wote uliowekwa kwa dhehebu la Imamiyya. Na wasiokuwa wao hutosha kusimama hata mara moja (muda mchache). Na madhehebu yote yamekubaliana katika kusunniwa kuswali jam'u kati ya Swala mbili, kwa kuwa Mtume ﷺ alifanya hivyo Arafah.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 360 2/1/2017 3:51:59 PM

madhehebu ya Imamiyya, isipokuwa pale anapokuwa ameambatana na mnyama wa dhabiha wakati wa kuhirimia. Na mkaazi wa Makka anapohiji Hijja *Tamattui* hulazimika kuchinja kwa mujibu wa madhehebu ya Imamiyya, na si wajibu kwa mujibu wa madhehebu yaliyobaki.

Kisha atanyoa au kupunguza nywele, sawa awe ni mwenye kuhiji Hijja *Tamattui* au *Qiran* au *Ifrad*, na kwa kunyoa au kupunguza nywele huhalalikiwa na mambo yaliyokuwa haramu juu yake alipohirimia, isipokuwa wanawake kwa Mahanbali, Mashafi na Mahanafi; na isipokuwa wanawake na manukato kwa Maimamiyya na Maliki.

Kisha atarudi hadi Makka siku hiyo hiyo ya Idd, atatufu Twawafu ya Ziyara na ataswali rakaa mbili, sawa awe ni mwenye kuhiji Hijja *Tamattui*, *Qiran* au *Ifrad*, na hapo huhalalikiwa na kila kitu hata wanawake, katika madhehebu manne.

Kisha atasai baina ya Swafa na Marwa awapo ni mwenye kuhiji Hijja *Tamattui*, hii ni kwa itifaki ya madhehebu zote. Na kama ni *Ifrad* au *Qiran* basi ni wajibu kwake kusai baina ya Swafa na Marwa kwa hali yoyote ile baada ya kutufu Twawafu ya ziyara, hii ni kwa Maimamiyya. Na kwa wasiokuwa wao si wajibu juu yake kusai iwapo ameshasai baada ya Twawafu ya kuwasili Makka (Qudum), kinyume na hivyo ni wajibu kwake kusai.

Na kwa Maimamiyya ni wajibu atufu Twawafu nyingine baada ya kusai, sawa awe ni mwenye kuhiji Hijja *Tamattui, Qiran* au *Ifrad,* na hii ndiyo Twawafu Nisaa, kwao Maimamiyya tendo la ndoa haliwi halali kwake ila kwa kutufu Twawafu hii.

Kisha anayehiji atarudi Mina katika siku hiyo hiyo ya kumi, akalale huko usiku wa kumi na moja, na azipige vijiwe Jamarat tatu wakati wa kukengeuka jua hadi kuzama kwake, kuanzia siku



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 361 2/1/2017 3:51:59 PM

ya kumi na moja, kwa itifaki ya mafakihi wote. Na Maimamiyya wamejuzisha kuipiga Jamarat vijiwe baada ya kuchomoza jua na kabla ya kukengeuka jua.

Kisha katika siku ya kumi na mbili atafanya kama alivyofanya jana yake. Na anatakiwa aiache Mina kabla ya kuzama jua la siku hii, kwa itifaki ya mafahiki. Na kama magharibi itaingia hali ya kuwa yupo hapo Mina, ni wajibu kwake kulala hapo usiku wa mwezi kumi na tatu, na azipige Jamarat vijiwe katika siku ya kumi na tatu. Na baada ya kumaliza kuzipiga Jamarat vijiwe atarejea hadi Makka kabla au baada ya kukengeuka jua akipenda.

Na anapoingia Makka atatufu Twawafu ya kuaga, hii ni Sunna kwa Maimamiyya na Maliki; na ni wajibu kwa mkaazi wa Makka kwa wasiokuwa Maimamiyya na Maliki. Hapa tumehitimisha kuelezea amali za Hijja.

Rehema za Mwenyezi Mungu zimshukie (Mtume) Muhammad na jamaa zake.

## MWEZI MWANDAMO WA DHULHIJA

Katika miaka mingi imetokea kuthubutu kuandama kwa mwezi wa mfunguo tatu (Dhulhija) kwa hukmu isiyokuwa ya Kiimamiya, na kwa hiyo serikali inayotawala Haram mbili (ya Saudi Arabia) huwalazimisha mahujaji kufanya amali ya Hijja bila kuthibitishwa mwandamo huo na Mujtahid wa Kiimamiya, sasa basi, hujaji wa Kiimamiyya atafanya nini wakati wa kusimama Arafah, na wakati wa matendo mengineyo ambayo yana muda na wakati maalum, inapokuwa hawezi kutenda amali hiyo kwa kufuata hukmu ya madhehebu yake? Na je, Hijja yake itabatilika kama atasimama pamoja na watu wengine na kufanya pamoja nao matendo yote mengine ambayo hufanywa na wao katika wakati wao wafanyao vitendo vyao?



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 362 2/1/2017 3:51:59 PM

Sayyid al-Hakim katika Kitabu *Manahijul-Hajj* uk. 91 chapa ya 1381 A.H. amesema: "Anapohukumu hakimu (kadhi, kiongozi) asiyekuwa wa Kiimamiyya kuandama kwa mwezi, na wakawa wamesimama Arafah tarehe nane ya mwezi wa Dhulhija, na hivyo ikawa watasimama Mash'ari (Muzdalifa) tarehe tisa, itapasa kufanya Taqiyya kwa kuwa na hofu ya kupata madhara na atasimama nao, kwa dhahiri kabisa ni kuwa kusimama kwake kutaswihi, na ataondokewa na dhima kwa kusimama huko.

Na hukmu ni kama hiyo hiyo anapokuwa ni naibu wa mtu ambaye alikuwa na dhima ya Hijja ya wajibu, au inapokuwa Hijja hiyo ni ya Sunna, ni yake mwenyewe au ni ya mtu mwingine. Kamwe hapana tofauti kati ya anapojua kuwa hukmu imekhalifu uhalisia au hakujua hilo."

Sayyid al-Khui katika kitabu *Manasikul Hajj* uk. 80 chapa ya mwaka 1380 A.H. amesema: "Unapothibiti mwandamo wa mwezi kupitia kwa kadhi asiyekuwa wa kishia, na akahukumu kuonekana kwake, ilihali mwandamo huo haujathibiti kwa Shia, lakini kukawa na matumaini ya hukmu hiyo kuoana na uhalisia, hapo ni wajibu kuwafuata, na kusimama Arafah pamoja nao, na Hijja hii kwa udhahiri kabisa itakuwa imetosheleza. Na atakayekwenda kinyume na Taqiya inavyomtaka, yaani akaacha kuhofia madhara, na nafsi yake ikamwelekeza kuwa tahadhari iliyo bora ni kuwakhalifu wao, basi atakuwa amefanya jambo lililo haramu na Hijja yake itakuwa imebatilika."[75]

[75] Ustadh wetu Sayyid al-Khui ameweka sharti kuwa kujuzu kwa Hijja hii na kutosheka kwayo ni pale anapokuwa hajui kinyume chake. Ama Sayyid Al-Hakim yeye amejumuisha hukmu hii wakati wa kujua na kutokujua. Nasi tuko pamoja na Sayyid al-Hakim; kwani tunafahamu kuwa miongoni mwa dalili za kujuzu Taqiya ni kuwa, bila shaka siku ya tisa ni sharti la kusimama Arafah pale tu panapokuwepo na imani na kutokuwepo hofu ya kupata madhara, ama pakiwepo hofu ya kudhurika au inapokosekana amani, sharti hili (la siku ya tisa kuwa ndio siku ya kusimama Arafah) hufutika kikamilifu, ni kama ilivyo katika Swala, kwamba kusujudu juu ya kisicholiwa au kuvaliwa, bila ya



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 363 2/1/2017 3:51:59 PM

Hapana shaka kabisa kuwa Mwenyezi Mungu anawatakia wepesi waja wake, wala hawatakii uzito na huko kuirudia Hijja mara ya pili ni dhiki hata kwa mtu mwenye uwezo wa kwenda Hijja zaidi ya mara moja, kama maelezo haya yatakuwa sahihi.

Sasa ndugu huyo masikini atafanya nini iwapo atarudia Hijja hiyo mwakani na ikatokea hali kama ile ile iliyotokea hapo kabla. Je itakuwa wajibu kwake kuirudia Hijja tena na tena kwa mara ya tatu na ya nne, na aendelee hivyo hivyo hadi asadifu hukmu ya madhehebu yake?

Rehema na amani zimshukie Amirul Muuminina kwa msemo wake aliosema: "Kwa hakika Mwenyezi Mungu ameweka taklifu katika (mambo yaliyo) mepesi, wala hakukalifisha katika (mambo yaliyo) mazito, na hutoa kwa tendo moja (malipo) ya wingi."

Tukiongezea hili ni kwamba, sisi tunajua fika kuwa hali kama hii ilishatokea katika nyakati za Maimamu wetu watwaharifu na wala haikupokewa hata mara moja kuwa, mmoja kati yao aliwaamuru wafuasi wake wairudie Hijja. Ziwashukie rehema na amani watu wa nyumbani kwa Mtume. Na kwa ajili hii ndiyo maana Sayyid al-Hakim katika kitabu *Dalilun-Nasik* akasema: "Hujuzu kutenda kutokana na hukmu ya kadhi asiyekuwa wa Kiimamiyya. Na sira yakinifu iliyokuweko wakati wa Maimamu عليه السلام inalazimu kuwafuata (makadhi hao) katika kisimamo (cha siku ya Arafah), bila ya kuingilia chochote katika suala hilo."

---

shaka hilo huwa ni sharti wakati panapokosekana hofu ya kudhurika, ama ikiwepo hofu huwa si sharti tena, na huwa inajuzu kwake kusujudu juu ya kinacholiwa au kuvaliwa panapokosekana amani.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 364 2/1/2017 3:52:00 PM

# KUMZURU MTUKUFU MTUME ﷺ

Husuniwa kumzuru Mtukufu Mtume ﷺ, ni Sunna iliyosisitizwa, kwani imethibiti kuwa amesema: "Anayelizuru kaburi langu baada ya kufa kwangu, ni kama aliyehama kunifuata wakati wa uhai wangu." Akasema tena Mtume ﷺ: "Swala moja tu katika msikiti wangu ni sawa na Swala elfu ziswaliwazo katika misikiti mingine yote isipokuwa Masjidul Haram, kwani Swala moja katika msikiti huo ni kama Swala elfu katika msikiti wangu."

Na yakokotezwa kuswali katika msikiti wa Mtume na sana kuswali eneo lililopo baina ya kaburi yake na mimbari yake, kwani mahali hapo ni kiwanja katika viwanja vya peponi. Kama ilivyothibiti katika Hadith.

Na yasunniwa kuiendea misikiti yote iliyoko Madina kama vile Masjid Quba, Mashrabatu Ummu Ibrahim, Masjidul Ahzab na mingineyo.

Aidha, husunniwa kuyazuru makaburi ya mashahidi wote, hasa kaburi la Hamza عليه السلام lililoko Uhud. Na pia yasunniwa kuzuru makaburi ya maimamu waliozikwa Bakii, nao ni Imam Hasan, Imamu Zainul Abidin, Imam al-Baqir na Imam Ja'far a-Sadiq عليهم السلام.

Ama kumzuru Fatima mama wa Hasan na Husein, ni sawa na kuzuru kaburi la baba yake, kwa kuwa yeye ni sehemu kutoka kwake Mtume. Na kauli zimekuwa nyingi zinazohusu mahali palipo kaburi lake tukufu, na kauli iliyo karibu na inayoelekea kuswibu uhakika ni kwamba amezikwa ndani ya nyumba yake ambayo ilikuwa jirani na msikiti wa baba yake. Na wakati viongozi wa Kibani Umayya walipoupanua msikiti kaburi hilo likawa sehemu ya msikiti huo. Na ni kwa ajili hii ndiyo maana Ibn Babawayh akasema: "Kwa hakika tunasema kuwa, kauli hiyo ndiyo iliyo karibu sana (na uhakika) kwa



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 365 2/1/2017 3:52:00 PM

kuwa haiko mbali na riwaya inayosema kwamba kaburi lake lipo eneo lililopo baina ya kaburi la Mtume na mimbari yake (Rawdha)." Na ni Mungu pekee Ndiye ajuaye kwa uhakika.

## HISTORIA YA KUJENGWA HARAM MBILI TAKATIFU

Ni nyumba ya awali iliyo na uongofu na iliyobarikiwa ambayo waliwekewa watu (kwa kufanyia ibada). Na ndiyo nyumba takatifu iliyo ya kale zaidi katika Mashariki ya Kati, nayo kwa yakini ilijengwa na babu wa Manabii wa Mungu, Nabii Ibrahim ﵇ pamoja na mwanawe Ismail ﵇. Amesema Mwenyezi Mungu (s.w.t.):

وَإِذۡ يَرۡفَعُ إِبۡرَٰهِـۧمُ ٱلۡقَوَاعِدَ مِنَ ٱلۡبَيۡتِ وَإِسۡمَٰعِيلُ رَبَّنَا تَقَبَّلۡ مِنَّآۖ إِنَّكَ أَنتَ ٱلسَّمِيعُ ٱلۡعَلِيمُ ١٢٧

**"Na (kumbukeni) Ibrahim alipoinua msingi wa ile nyumba (al-Ka'aba) na Ismail (wakaomba): "Ee Mola Wetu! Tutakabalie (amali yetu hii). Hakika Wewe ndiye Msikizi, Mjuzi." (al-Baqarah; 2:127).**

Ismail ﵇ alikuwa akileta mawe na Ibrahim ﵇ akijenga, hata ukuta ulipoinuka kufikia urefu wa kimo cha mtu lililetwa jiwe jeusi na akaliweka mahali pake.

Riwaya zinaeleza kwamba, kwa yakini nyumba hiyo ya kale; wakati alipoijenga Ibrahim urefu wake ulikuwa ni dhiraa tisa, na mapana yanayofikia dhiraa ishirni kwa dhiraa thelathini, na kwamba ilikuwa na milango miwili na wala haikusakafiwa juu.

Ama hilo jiwe jeusi, husemwa kwamba jiwe hilo alikuja nalo Jibril



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 366 2/1/2017 3:52:00 PM

عليه السلام kutoka mbinguni, na ikasemwa kuwa, bali jiwe hilo lilikuwa pamoja na Adam عليه السلام muda alipoteremshwa ardhini, na kwamba lilikuwa jeupe lenye kung'aa, kisha likawa jeusi kutokana na madhambi ya watu. Na kumesemwa maneno mengi kuhusiana na jiwe hilo yasiyokuwa hayo.

Ama sisi, hakuna ubaya juu yetu iwapo hatutakubali hata moja katika kauli hizo na zilizo katika mfano wake. Na wala kamwe sisi hatulazimiki kufanya utafiti wa kupata ukweli wa kauli hizo. Aidha wala hatulazimiki kutafiti kujua asili ya jiwe hilo na sababu ya kuletwa kwake. Ndiyo, sisi twalitukuza na inatosha; kwa kuwa Mtume صلى الله عليه وآله alilitukuza na alikuwa akilipa taadhima, na tunapoulizwa siri ya Mtume kulitukuza jiwe hilo tutasema: "Mwenyezi Mungu na Mtume Wake ndio wajuao."

Pia riwaya zimeeleza kwamba: "al-Kaaba ilibaki katika mjengo alioujenga Ibrahim na Ismail عليه السلام hadi pindi Quswayyi bin Kilab babu wa tano wa Mtume Mtukufu صلى الله عليه وآله alipoijenga upya. Na kwamba mjengo huo wa Quswayyi uliendelea hadi Mtume صلى الله عليه وآله alipofikia umri wa miaka thelathini na mitano. Kukazuka mafuriko makubwa yaliyosababisha kubomolewa na kusombwa sehemu za kuta za al-Kaaba.

Makuraishi wakarekebisha kuta za jengo lake na wakati wa kuliweka jiwe jeusi mahali pake, makabila yalitofautiana na kukazuka kutokuelewana kuhusiana na ni nani ambaye atapata fahari ya kuliweka mahali pake? Ilikuwa karibu patokee vita vikali kati yao kama wasingempata Muhammad kuwa hakimu wao.

Mtume صلى الله عليه وآله aliitandika chini shuka yake, akalinyanyua jiwe kwa mikono yake na akaliweka juu yake kisha akasema: "Mkuu wa kila kabila ashike kipembe cha nguo hiyo." Kisha wakaliinua wote kwa pamoja hadi lilipofika kuelekeana sawa sawa na mahali pake.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 367 2/1/2017 3:52:00 PM

Mtume Muhammad ﷺ akaliinua kwa mikono yake akaliweka mahali pake.

Rehema za Allah ziwe juu yako ewe Mtume wa rehema… ulilinua jiwe jeusi kwa mikono yako mitukufu mwanzoni, kutoka ardhini., kisha mara ya pili ukaliweka mahali pake kwa mikono yako, ukamridhisha Mwenyezi Mungu na ukawaridhisha watu. Na hilo lilitosha kwako wewe kuwa ni dalili iliyohukumu wazi kuwa wewe uko juu zaidi kuliko wote. Na imedhihirisha wazi kwamba wewe umeletwa ukiwa ni rehema kwa walimwengu wote kabla ya kupewa utume na baada yake. Aidha hiyo tu imetosha kuwa ni ishara dhahiri iliyofikisha hoja kamili kuwa wewe ni mchukuzi wa ujumbe wa Mwenyezi Mungu, na kwamba wale ambao wamekukanusha ni wenye kupinga na kuikataa haki na utu (ubinadamu).

al-Kaaba ilidumu katika hali hiyo aliyoirekebisha Mtume ﷺ pamoja na Makureish hadi utawala wa Waislamu uliposhikiliwa na Yazid bin Muawiya, na ukatokea ugomvi wa kuporwa utawala huo baina yake na Ibn Zubeir, Mfalme wa Hijjaz. Yazid akasimamisha wapiga teo wake juu ya majabali ya Makka wakaipiga al-Kaaba kwa kutumia teo hiyo hadi mawe elfu kumi. Akaiwasha moto na hatimaye ikavunjika. Ibn Zubeir akarudia kuifanyia marekebisho ya kuijenga tena katika hali yake ile ile iliyokuwa awali bila ya kubadilisha chochote na kando yake akakita boma la mbao.

Wakati utawala uliposhikwa na Abdul Malik bin Marwan, Hajjaj alimzingira Ibn Zubeir na akamuua baada ya kuwa amevunja sehemu fulani katika al-Kaaba, na Hajjaj akajenga tena sehemu iliyovunjwa au kupasuka, akazigeuza kuta za al-Kaaba katika mjengo usiokuwa wa mwanzo, na mlango mmoja uliokuwa upande wa Magharibi akaufunga.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 368 2/1/2017 3:52:00 PM

al-Kaaba ilibaki katika marekebisho hayo yaliyofanywa na Hajjaj hadi ulipofikia mwaka 1040 A.H. Kukanyesha mvua kubwa iliyosababisha kuporomoka kuta za al-Kaaba. Waislamu wa pembe zote wakakusanyika kuijenga upya na wakakusanya michango ya misaada itakayogharimia ujenzi huo kutoka katika nchi mbalimbali za Kiislamu na ikajengwa katika hali ilivyo hivi sasa.

**MSIKITI WA MTUME ﷺ:**

Mtume ﷺ aliingia Madina akiwa aliyehama kutoka Makka akiwa hana chochote alichomiliki humo Madina. Akajenga msikiti wa mwanzo kujengwa mjini hapo, kisha akajenga nyumba yake kando ya msikiti huo. Msitiki huo ulikuwa na ukubwa wa mita 35 kwa 30, kisha Mtume akauzidisha ukubwa wake akaufanya mita 57 kwa 50.

Hamkuwa na mimbari ndani ya msikiti huo wakati Mtume ﷺ alipoujenga, na wakati wa kuhutubia alikuwa akiegemea kiguzo cha mtende kilichokuwa nguzo mojawapo ya nguzo za msikiti huo. Kisha Maswahaba zake wakamfanyia mimbari ya mbao iliyoundwa na vidaraja viwili.

Alipotawala ukhalifa, Umar bin Al-Khattab aliupanua msikiti huo kwa kuongeza mita 5 kwa upande wa Kusini, na mita 5 kwa upande wa Magharibi, na mita 15 upande wa Kaskazini. Upande wa Mashariki hakuuongeza kwa sababu upande huo kulikuwepo na nyumba za wake za Mtume ﷺ.

Aliposhika ukhalifa Uthman bin Affan aliuvunja msikiti huo, akauzidisha lakini akaacha nyumba za wake wa Mtume zikiwa nje ya msikiti kama alivyofanya Umar. Msikiti huo ulibaki katika mjengo alioujenga Uthman hadi alipokuja kutawala Walid bin Abdul Malik. Yeye akauvunja na akazidisha katika kila upande. Nyumba za wake wa Mtume akaziingiza ndani ya msikiti, ikiwemo nyumba ya



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 369 2/1/2017 3:52:00 PM

Bibi Aisha, na hapo ndipo kaburi tukufu la Mtume ﷺ likawa ndani ya msikiti huo.

Mjengo huo wa Walid ulibaki hivyo hadi mwaka 266A.H. wakati Mahdi al-Abbassiy alipoongeza sehemu kubwa upande wa Kaskazini. Ulibaki hivyo hadi mwaka 654 A.H. ulipoungua moto na mimbari ya Mtume, milango na vifaa vinginevyo vikateketea na sakafu ikaanguka.

Baada ya miaka sita Dhwahir Baibaris alitawala kazi ya kuujenga msikiti huo na ukarejea katika hali yake ile ile ulivyokuwa kabla ya kuungua moto.

Katika mwaka 885 A.H. kulitokea kimbunga kikali kilichovamia msikiti huo, ukabomoka na hakuna kilichosalia isipokuwa chumba cha Mtume na kuba lililokuwa ndani ya msikiti huo. Mfalme Ashraf alirudia kuujenga katika mjengo mzuri zaidi kuliko ulivyokuwa kabla haujaungua.

Katika karne ya kumi Hijiriya, Sultani Salim al-Uthmaniy aliupamba kweli kweli na akajenga Mihrabu ambayo iko hadi leo hii, nayo iko upande wa Magharibi ya mimbari ya Mtume.

Mnamo karne ya kumi na tatu Hijriya, Sultani Mahmud Al-Uthmaniy alijenga kuba la kijani ndani yake. Na katika mwishoni mwa karne hiyo msikiti huu ulihitaji kuimarishwa, na Sultan al-Uthmaniy akaamuru lifanyike hilo, na wahandisi walikuwa wakivunja sehemu moja ya msikiti na kujenga sehemu itakayochukua mahali pake, kisha wanavunja sehemu nyingine na kusimamisha ukuta mwingine badala yake, hadi ukakamilika uimarishaji huo mnamo mwaka 1277 A.H.

Rehema za Mwenyezi Mungu zimshukie Muhammad na jamaa zake walio watoharifu, na tuarifishe kati yetu na kati yao (ewe Allah),

na uturuzuku shafaa yao siku ya kukutana Nawe, Ewe unayeyageuza maovu ukayafanya mema, na kuyaongezea mema wema zaidi … Hakika Wewe ni Mwenye fadhila kubwa.



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 371 2/1/2017 3:52:00 PM

# ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. i) Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
   ii) Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (a.s.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudhar
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 372 2/1/2017 3:52:00 PM

27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua kwa Mujibu wa Ahlulbayt (a.s)
33. Udhuu kwa Mtazamo wa Qur'ani na Sunna
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Qur'ani na Kuhifadhiwa Kwake
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya Sala Mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an Yatoa Changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu

58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Dhana ya Ndoa ya Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raj'ah)
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 374 2/1/2017 3:52:00 PM

89. Adabu za Sokoni Na Njiani
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali (AT- TAWASSUL)
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Maimamu wa Ahlul Bait – Ujumbe na Jihadi
100. Idi Al-Ghadir
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunna za Nabii Muhammad (saww)
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Mwanamke Na Sharia
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Ndoa ya Mutaa
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne

120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Mkutano wa Maulamaa wa Baghdad
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Elimu ya Ghaibu ya Maimamu
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali (ʻa) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali (ʻa) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul l'Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu
135. Adhana ni Ndoto au ni Wahyi?
136. Tabaruku
137. Saada Kamili – Kitabu cha Kiada cha Maadili
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mjadala wa Kiitikadi
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 376 2/1/2017 3:52:00 PM

151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Shia na Qur'ani – Majibu na Maelezo
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Je, Kufunga Mikono
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. as-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 377 2/1/2017 3:52:00 PM

182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Maswali Ya Uchunguzi Kuhusu Uislam
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Historia maana na lengo la Usalafi
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Upotoshaji Dhahiri katika (Turathi) Hazina ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina (as) na Makhalifa
197. Tawheed Na Shirki
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu za vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni waKisunni na Kishia (Al- Muraja'aat)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Imam Husain ni Mfumo wa Marekebisho na Mageuzi
206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii
210. Maadili ya Ashura
211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi
212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 378 2/1/2017 3:52:00 PM

213. Imam Ali na Mambo ya Umma
214. Imam Ali na Mfumo wa Usawa
215. Uimamu na Tamko la Kutawazwa
216. Mfumo wa Wilaya
217. Vipi Tutaishinda Hofu?
218. Kumswalia Mtume ni Ufunguo wa Utatuzi wa Matatizo
219. Maeneo ya Umma na Mali Zake
220. Nahju 'L-Balagha– Majmua ya Khutba, Amri, Barua, Risala, Mawaidha na Semi za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (a.s.)
221. Mukhtar – Shujaa aliyelipiza kisasi dhidi ya wauaji wa Imam Husein (as) hapo Karbala
222. Mazingatio Katika Swala
223. Imam Hasan na Mfumo wa Kujenga Jamii
224. Vyakula Na Vinywaji
225. Kuelewa Rehema ya Mwenyezi Mungu
226. Imam Mahdi na Bishara ya Matumaini
227. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
228. Shia Na Sahaba - Majibu na Maelezo
229. Majanga Na Jukumu la Jamii
230. Shia Na Hadith - Majibu na Maelezo
231. Upotofu Ndani ya Kitabu cha Mitaala kwa Shule za Sekondari
232. Ugaidi Wa Kifikra Katika Medani Ya Kidini
233. Yafaayo kijamii
234. Uswalihina Dhahiri Na Batini Yake
235. Mkakati wa Kupambana na Ufakiri
236. Mwanamke Katika Harakati Za Mageuzi
237. Jihadi
238. Hija Katika Maneno Na Ujumbe Wa Imam Khomeini (R.A)
239. Tiba Ya Maradhi Ya Kimaadili
240. Yusuf Mkweli
241. Taqiyya Kwa Mujibu Wa Sheria Ya KIISLAMU



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 379 2/1/2017 3:52:00 PM

242. Imam Mahdi (A.S) Imam Wa Zama Hizi Na Kiongozi Wa Dunia
243. Talaka Tatu
244. Safari Ya Kuelekea Kwa Mwenyezi Mungu
245. Hotuba Za Kiislamu Juu Ya Haki Za Binadamu
246. Mashairi Ya Kijamii
247. Ngano Ya Kwamba Qur'ani Imebadilishwa
248. Wito Kwa Waumini: "Enyi Mlioamini"
249. Imam Husain (a.s) ni Utu na Kadhia
250. Imam Husain ni Kielelezo cha Kujitoa Muhanga na Fidia
251. Imam Mahdi ni Tumaini la Mataifa
252. Kuchagua Mchumba
253. Mazungumzo ya Umoja – Ukosoaji na Usahihishaji
254. Utamaduni wa Mwamko wa Kijamii
255. Hekima za kina za Swala
256. Kanuni za Sharia za Kiislamu
257. Utamaduni kufuatana na Qur'ani na Utekelezaji wa Kivitendo (Sehemu ya Kwanza)
258. Kauli sahihi zaidi katika kufafanua Hadithi

## KOPI ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba' Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n;amavuko by;ubushiya
4. Shiya na Hadithi
5. Kor'ani Nziranenge

6. Kwigisha Mu Buryo Bw'incamake Uka Salat Ikotwa

7. Iduwa ya Kumayili

## ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION KWA LUGHA YA KIFARANSA

1. Livre Islamique



21_16_Fiqhi kwa Mujibu wa Madhehebu_2_Feb_2017.indd 381 2/1/2017 3:52:00 PM